

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 2 Mei, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:**Waheshimiwa Tukae, Katibu.

**NDG.ATHUMANI HUSSEIN –KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. OMARI A. KIGODA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo naMaji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE.JOYCE B. SOKOMBI K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI:**

Taarifa ya Msemadi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**MWENYEKITI:**Ahsante sana, Katibu tuendelee.

**NDG. ATHUMANI HUSSEN - KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swal lake.

Na. 154

**Hitaji la Jokofu la Kuhifadhi Maiti Hospitali ya Wilaya ya Kilwa**

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE (K.n.y. MHE. SELEMANI S. BUNGARA)** aliliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Kilwa haina Jokofu la kuhifadhi maiti na pia majengo yake mengi ni chakavu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua jokofu jipya sambamba na kukarabati majengo ya hospitali hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE.MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,TAMISEMI, naomba kujibu swal i

Mheshimiwa Selemani Saidi Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga)ni miongoni mwa Hospitali Kongwe za Wilaya hapa nchini na imekuwepo tangu mwaka 1965. Kwa kutambua umuhimu wa Hospitali hiyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekua ikifanya ukarabati na upanuzi wa majengo mbalimbali ya kutolea huduma kama ifuatavyo:-

Mwaka wa Fedha 1996/1997, ukarabati wa miundombini mbalimbali ya hospitali ulifanyika pamoja na ujenzi wa kliniki ya Mama na Mtoto; Mwaka 2010 ulifanyika ujenzi wa Jengo la Huduma za UKIMWI (*CTC*); Mwaka 2012 ulifanyika ujenzi wa jengo la wazazi; na Mwaka 2017 ulifanyika ujenzi wa jengo la mama ngojea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Kilwa ina jokofu moja la kuhifadhia maiti liililonunuliwa mwaka 1996. Hata hivyo, jokofu hilo lina uwezo wa kuhifadhi mwili mmoja tu. Serikali inaendelea nautaratibu wa kukamilisha hatua za kuanza ujenzi wa jengo jipya la kuhifadhia maiti kwenye hospitali hiyo sambamba na ununuzi wa jokofu jipya la kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kukarabati miundombini ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha utakavyokuwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ngombale.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, jokofu hilo la Hospitali ya Kinyonga halifanyi kazkwa sasa na Hospitali hii ya Kinyonga ipo sambamba kuelekea Mikoa ya Kusini. Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga jengo hilo kwa haraka sambamba na kuleta jokofu lenye uwezo la kuhifadhi zaidi

ya mwili mmoja ili kuendana na chochote kinachowez  
kutokea ili kukidhi haja hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, je, Serikali  
inampango gani kukarabati Kituo cha Afya Njinjo ambacho  
halii yake kwa sasa ni mbaya sana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali  
hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA  
SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa  
Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa  
Ngombale Vedasto,kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtaarifu  
Mheshimiwa Mbunge, leo asubuhi kabla sijaingia hapa  
Bungeni nimefanya utaratibu wa kuwasiliana na Halmashauri  
na nina taarifa njema, naomba nimhakikishie Mheshimiwa  
Mbunge leo tarehe 2 Mei, halmashauri inaingia mkataba na  
mdau wa *Pan Africaambao* wamekubali kujenga jengo la  
kisasa kwa ajili ya chumba cha kuhifadhi maiti, lakini kwa  
makubaliano kwamba na halmashauri nao watatununua  
jokofu la kisasa ili liweze kumudu halii ya uhitaji wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii lake la pili  
anaomba ukarabati waKituo cha Afya cha Njinjo, naomba  
nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge azma ya Serikali ni  
kuhakikisha kwamba tunafanya ukarabati katika vituo vyote  
vya afya vile vile vilivyojengwa zamani, ili viwe na mwonekano  
wa sasa. Naye atakiri kwamba, katika nafasi aliyopata  
kutembelea vituo vya afya ambavyo tunavijenga sasa hivi  
tumevijenga vizuri, halii kadhalika hata hospitali za wilaya za  
zamani tungependa zikarabatiwe ziwe na muonekano wa  
kisasa kama kwa Hospitali ya Kilwa ya mwaka 1965, kwa  
vyovypote vile hata halii yake hailingani na hadhi ya hospitali  
ya Wilaya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Mndolwa,  
atafuatiwa naMheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hospitali ya rufaa ya Temeke haina mashine ya kufulia nguo, hadi kupelekea mashuka ya wagonjwa kupelekwa katika Hospitali ya Muhimbili ili kuweza kufuliwa. Je, Serikali itapeleka lini mashine ya kufulia nguo katika Hospitali ya Rufaa ya Temeke?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na Hospitali ya Rufaa ya Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoju Hospitali yetu ya Rufaa ya Temeke inamashine ya kufulia, inawezekana katika kipindi hiki cha karibuni imeharibika na niombe tu baada ya kikao hiki cha Bunge nitafuatilia. Vile vile tumekuwa na utaratibu mbadala katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Muhimbili ina mashine kubwa za kuweza kufulia na mara nyingi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa katika Mkoa wa Dar es Salaam wanapopata tatizo basi huwa tunatumia Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kama mbadala. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, baada ya kikao nitafuatilia kuhakikisha mashine hiyo inafanya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naishukuru Serikali kwa kutujengea Kituo cha Afya Hirbadawna kukarabati Kituo cha Afya cha Simbay, Iakini ilituahidi kwamba itatusaidia kukamilisha Kituo cha Afya cha Bassotuna Endasak. Naomba jibu ili wananchi wa Hanang waweze kufurahi. Ahsantesana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Nagu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nipokee pongezi, ye ye mwenyewe anakiri kwamba imefanyika kazi nzuri ya ukarabati wa vituo vya afya viwili kwake na ahadi yetu ya kukamilisha ukarabati wa ujenzi wa vituo vya afya kila kata iko pale pale.

Naomba Mheshimiwa Mbunge awaambie wananchi wawe na subira, lakini ni vizuri na wao wakaanza kujitokeza kwa zile kazi ambazo wanaweza kuanza kufanya ambavyo wananchi wake wamekuwa na mwitikio mkubwa waendelee kufanya na nasisi tutaunga mkono, lakini azma ni kuhakikisha kwamba hivyo vituo viwili navyo vinafanyiwa ukarabati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ungando.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wananchi wa Bungu wanashida kubwa ya Kituo cha Afya na wenyewe walishaanza kujenga majengo. Je, Serikali ina mpango wa kuunga mkono Kata ile ya Bungu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fursa ya kwenda Kibiti na tukaenda kutembelea mpaka Kituo cha Afya Mbwera, kituo cha afya ambacho kipo ndani kweli kweli unaenda *delta* kule, kama mtu anataka kuona jinsi ambavyo Serikali ya CCM inafanya kazi ni pamoja na kwenda maeneo kama *delta*, naomba nimhakikishie Mbunge na ye ye mwenyewe ni shuhuda kazi nzuri ambayo inafanyika, hakika hata huko kituo cha afya ambacho hakijafanyiwa ukarabati kwa kadri fedha zitakazopatikana, tutaenda kukikarabati.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Ofisi hiyo hiyo ya TAMISEMI, Mheshimiwa Yosepha Komba, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 155

**Uhaba wa Watumishi na Vitendea kazi Idara ya Ardhi na Maliasili Wilaya ya Muheza**

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA** aliuliza:-

Kuna uhaba wa watumishi na vitendea kazi katika Idara ya Ardhi na Maliasili – Wilaya ya Muheza kunakosababisha kuazima watumishi na vifaa kutoka Halmashauri nydingine:-

(a) Je, ni lini Serikali itaa jiri watumishi na kununua vitendea kazi katika Idara hiyo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwawekea wananchi Wanasheria ili kusaidia kutatua migogoro ya ardhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ardhi na Maliasili katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza inao watumishi 12 kati ya 20 wanaohitajika. Halmashauri imeendelea kuomba vibali kwa ajili ya kuajiri watumishi hao. Hata hivyo, ili kukabiliana na upungufu huo Halmashauri imeajiri watumishi watatu (3) wa Ardhi kwa mkataba ili kutatua changamoto mbalimbali za ardhi. Vile vile katika mwaka wa fedha 2017/

2018, kupitia mapato yake ya ndani Halmashauri ilinunua *GPS-RTK* (*Real time Kinematic*) kwa ajili ya upimaji ardhi kwa gharama ya shilingi milioni 37. Aidha, Halmashauri imetoa gari Toyota *Land Cruiser* kwa ajili ya Idara ya Ardhi na Maliasili. Halmashauri itaendelea kununua vitendea kazi kwa awamu kadri ya upatikanaji wa Fedha.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inao mfumo wa kisheria wa utatuzi wa Migogoro ya Ardhi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao umeainishwa katika Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Na. 2 ya mwaka 2002 na Kanuni zake. Migogoro ya ardhi iliyopo Wilayani Muheza imegawanyika kwenye makundi makuu matatu; migogoro ya kiwilaya ambayo inahusisha mipaka ya vijiji vya Wilaya ya Muheza na Tanga Jiji pamoja na Vijiji vya Muheza na Pangani. Migogoro hii inashughlikwa katika ngazi ya Mkoa na itapatiwa ufumbuzi wakati wowote.

Kundi la pili la migogoro ni migogoro ya mipaka ya vijiji iliyotokana na zoezi la upimaji wa mipaka nchi nzima uliofanyika mwaka 2007. Vikao kwa ajili ya kumaliza migogoro hii vinaendelea na vimefikiwa hatua nzuri. Migogoro mingine ni migogoro ya viwanja ambayo hupokelewa na kutatuliwa kwa utaratibu wa kawaida wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Suluhisho la kudumu kwa aina hii ya migogoro ni kukamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi, kupima viwanja na kurasimisha makazi ambapo mpaka sasa makazi 4,768 yamerasimisha Wilayani Muheza. Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, kurasimisha makazi, kupima viwanja na mashamba ili kumaliza migogoro ya ardhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yosepher.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Waziri wakati anajibu, nafahamu Wilaya ya Muheza ni moja kati ya wilaya ambayo iliyofutiwa hati mashamba zaidi ya sita toka wawekezaji ambao mengi yao yalikuwa mashamba ya mikonge. Kutokana na hilo kumekuwa na tatizo kubwa sana la migogoro, sasa naomba

niulize kuhusu kwanza watumishi, Serikali imejiendaaje hasa kwa mwaka huu inatuambia nini wananchi wa Muheza kwenye suala la watumishi, tutawaongezea watumishi wangapi ukizingatia tatizo la watumishi linatuathiri sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Rais alipokuwa anaenda kuzindua bomba la mafuta kule Tanga alipopita Muheza aliahidi na aliwaambia wananchi watagawiwa maeneo bure walime na kuyaendeleza, lakini wananchi wa Muheza hawakuamini hivyo, wamekuwa wanalipishwa gharama za upimaji na wamekubali. Hata hivyo, kuna migogoro mikubwa sanasana, wafanyakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wanaohusika na ardhi wamekuwa wanauzu maeneo ya wananchi kwa watu tofauti ambao siyo wakazi wa Muheza. Nataka nipate kauli ya Serikali, je, wapo tayari kutuma timu maalum iende Muheza ikasimamie masuala ya ugawaji wamashamba na viwanja hasa katika maeneo haya sita ambayo yamefutiwa hati? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri katika swali lake la msingi, lakini naomba njiblu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yosepher kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watumishi nadhani hata kipindi kilichopita Bunge liliopita tulilizungumzia kwamba baada ya watumishi sasa kuelekezwa kwenye Wizara ya Ardhi, tayari tulikuwa tunafanya utaratibu wa kupata ikama yao na kujua wanataaluma tulionao ni kiasi gani ili waweze kusambazwa katika Halmashauri kulingana na uhitaji na kazi hiyo inafanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMIkwa sababu suala la uhamisho litasimamiwa na Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika suala zima la ugawaji wa mashamba na wakati tumeenda kwenye ziara ya Kamati ya Ardhi suala hilo tulilikuta, lakini tayari Ofisi ya

Halmashauri pale Muheza walikuwa wameshaanza kugawa hekari tatu tatu kwa wananchi katika yale mashamba yaliyorejeshwa na suala la kulipishwa katika suala la upimaji ni makubaliano ya Halmashauri yenyewe ambayo walikaa wakakubaliana na kiasi cha wao kuchangia na ndicho hicho kilichofanyika. Kwa hiyo suala linalofanyika linafanyika kutegemeana na mamlaka zenyewe za upangaji na matumizi bora ya ardhi. Kwahiylo hilo ni suala ambalo lipo chini ya halmashauri na Serikali inalisimamia kulingana na makubaliano ambayo yanakuwa yamefikiwa, hakuna migogoro ambayo itaendelea kwa sababu kila kitu kinasimamiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Migogoro ya ardhi katika nchi hii ipo katika kila wilaya na kila mkoa, lakini katika Mkoa wetu wa Songwe mpaka sasa hivi hatujapata Baraza la Ardhi la Wilaya na Wilaya zetu za lleje Mombasa na maeneo mengine zinakwenda Mbeya Mjini. Je, ni lini Serikali sasa itaanizisha Baraza la Ardhi la Wilaya katika Mkoa wetu wa Songwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Meshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakajoka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ambayo Serikali inatakiwa kufanya kazi kila wilaya inapaswa kuwa na Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya na tayari tulishasema na kutoa majibu tuna mabaraza 97 ambayo tayari yalikwishaanzishwa na sasa hivi yote yatakwenda kufanya kazi kwa maana ya kwamba tumepata baadhi ya watumishi ambao wanakwenda. Hata hivyo, kufungua Baraza la Ardhi katika eneo inategemeana pia na idadi ya kesi na namna ambavyo

wilaya yenyewe imejiandaa katika kutupa ofisi, kwa sababu katika maeneo ambayo tunafanya kazi hiyo, Wizara hajengi ofisi bali Halmashauri na mkoa husika wanatupa majengo, sisi tunapeleka watumishi pamoja na vitendea kazi, kwa maana ya thamani. Kwahiyu kama watakuwa tayari, basi tunaweza tukafika katika eneo hilo, lakini pia tunazingatia takwimu na migogoro iliyopo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi. Naipongeza Serikali kwa upande wa Morogoro kwa kuanza upimaji wa ardhi hasa kwa upande wa Wilaya za Malinyi, Kilombero na Ulanga, lakini upimaji unakuta migogoro bado inaendelea kwenye Wilaya nyingine, lakini ni matatizo kweli kwa vifaa vya upimaji kwa sababu vinanunuliwa kwa bel ghalli na halmashauri zingine hazina uwezo wa kununua hivyo vifaa. Je, Serikali inasemaje kwa kusaidia hizo Halmashauri ambazo haziwezi kununua hivyo vifaa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ishengoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipokee shukrani zake kwa Serikali kwa kazi inayofanya katika Wilaya ya Malinyi, Ulanga na Kilombelo, kwa kupima ardhi yote katika maeneo yale na niwashukuru wananchi wa maeneo hayo kwa sababu wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumaliza migogoro hiyo kama ambavyo tumeanza ile ni kama *pilot area*, lakini tayari tutakuwa na *resource persons* wengi kutokana na wananchi wenyewe kwa sababu pia watakuwa wamepata ujuzi mzuri wa kuweza kufanya *scale up* kwenye maeneo

mengine na lengo la Wizara ni kuhakikisha maeneo yote yanapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa vya upimaji, napenda nitoe rai kwa halmashauri zetu zote, Wizara ilikwishatoa vifaa katika maeneo yote ya kanda zetu nane, lakini halmashaurihaziendi kuomba vifaa vile. Bahati nzuri kwa kuwa ameuliza hili swali, basi nitatayarisha takwimu niletahapa baada ya kuwa tumeshapata vifaa, ni halmashauri ngapi zimeomba. Halmashauri nyngi hawaendi kuchukua vifaa, lakini wana-opt kutafuta vifaa vya kukodi wakati kuna vifaa vya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa halmashauri zetu, watumie vifaa hivyo ambavyo Wizara ilishafundisha watumishi wawili, wawili kutoka kila halmashauri kwa nchi nzima ambao wana Wapima kwa ajili ya kuweza kutumia vile vifaa. Matokeo yake wamefundishwa, hawaleti maombi na vifaa vimekaa *idle*, halafu Wabunge wanalamikia suala la upimaji. Naomba usimamizi katika halmashauri, watumie vifaa ambavyo tayari Wizara imegharamia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sanakwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Lupembe katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe haina Afisa Ardhi Mteule na tuna mpango wa kupima ardhi katika maeneo yetu.

Je, ni lini Serikali italeta mtaalam kwa maana ya Afisa Ardhi Mteule ili kuweza kusaidia kupima ardhi lakini pia kutatua migogoro iliyopo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hongoli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati najibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Yosepher, nimesema utaratibu unafanyika sasa tutaweza kuwatawanya wataalam wetu kama walivyo, lakini kwa sasa naomba tu waendelee kumtumia huyo Afisa Ardhi Mteule ambaye alikuwa kazi yote kutoka kwenye halmashauri jirani ya jimbo lake ili tuweze kuendelea. Hii kazi itakamiliaka muda si mrefu, naomba tu Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane kwa sababu kazi ya kuwapanga itachukua muda kwa sababu yakutaka kujua taaluma zao na uhitaji wa kila halmashauri.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi. Sasa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua Mbunge wa Masasi sasa aulize swalii lake.

Na. 156

### **Serikali kuboresha Mazingira ya Kazi kwa Askari Polisi**

**MHE. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Jeshi la Polisi limekuwa likifanya kazi katika mazingira magumu sana kutohana na uchakavu wa vitendea kazi pamoja na kukosekana kwa magari ya kutosha:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia magari Askari Polisi wa Wilaya ya Masasi kutohana na kutokuwa na magari ya kutosha?

(b) Je, ni lini Serikali itarekebisha utaratibu uliopo ambapo askari wanalahizimika kutoa pesa zao za mfukoni kuwapa chakula mahabusu?

(c) Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za askari katika Wilaya ya Masasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhaba wa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na uchache wa magari. Kwa sasa Wilaya ya Masasi imeshapatiwa gari moja aina ya *Leyland Ashok*, hivyo kufanya kuwepo kwa magari matatu ambayo ni *PT 1865, Toyota Landcruiser, PT 4011 Grand Tiger na Leyland Ashok*. Gari hili jipya litatumika kwa shughuli mbalimbali kama doria na operesheni kubwa. Aidha, kutokana na jiografia ya Wilaya ya Masasi, Jeshi la Polisi litalongezea Wilaya ya Masasi magari kwa kadri yatakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utaratibu wa Askari Polisi kutoa pesa zao mfukoni kwa ajili ya chakula cha mahabusu, bali utaratibu uliopo ni kwamba Serikali kuitia Jeshi la Polisi lina wajibu wa kuwapatia chakula mahabusu waliopokorokoroni ingawa pia ndugu za mahabusu wanaruhusiwa kuwapelekea chakula jamaa zao walioko korokoroni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Masasi ina nyumba za makazi ya askari zipatazo 15 ambazo zinaishi familia za askari 30, ingawa ni kweli askari wengine wapatao 154 bado wanaishi uraiani. Hata hivyo, Serikali itaendelea kujenga nyumba za makazi ya Askari kwa awamu kwa kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa gari alizozitaja *Toyota Land Cruiser* na *Grand Tiger* ni gari mbovu sana ambazo hazifai kufanya kazi katika kipindi hiki ambacho Polisi wana majukumu makubwa. Pia gari la *Leyland* ambalo amelitaja siyo la kazi ngumu kwa sababu kwanza halina hata *four-wheel drive*. Je, Serikali haionti sasa kuna umuhimu wa kufanya jambo hili ni la dharura kwa askari wetu wa Jeshi la Polisi waishio Masasi ili waweze kupata gari haraka iwekekanavyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa hali ya nyumba za Askari Polisi waishio Masasi ni mbaya sana maana zimejengwa tangu enzi ya mkoloni. Je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami hadi Masasi baada ya Bunge hili ili akashuhudie hizo anazoiita nyumba 15 zilizopo? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja ya umuhimu wa kupeleka magari mengine katika Jimbo la Masasi ni muhimu na nilieleza hivyo kwenye jibu langu la msingi tunaamini kwamba kuna haja ya kupeleka magari Masasi. Kwa hiyo, tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba magari yaliyopo hayatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli magari yale mawili ni ya zamani ingawa yakinengenezwa yatasaidia. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa tunatambua umuhimu wa Wilaya ya Masasi kuwa na magari ya ziada, kwa sasa hivi hatuna magari mapya lakini pale ambapo yatapatikana katika maeneo ambayo tutayaangalia kwa jicho la karibu moja ni Wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili nimthibitishie kwamba niko tayari kwenda pamoja naye katika Jimbo la Masasi kwa mara nyingine tena. Niliwahi kufika Masasi na nayaafahamu mazingira ya Masasi lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge anahisi kuna haja ya kuambatana naye kwa mara nyingine tena basi tutafanya hivyo ili kwa pamoja mimi na yeye tuweze kuona jinsi gani tunaweza tukakabiliana na changamoto mbalimbali zinazohusu vyombo vyetu vya usalama vilivyopo pale hususan Jeshi la Polisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul halafu Mheshimiwa Maftah.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru umenipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Wizara ya Mambo ya Ndani kutupatia fedha kujenga nyumba sita za askari pale Babati Mjini, kwenye Mtaa wa Bagala Ziwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la *RPC* katika Mkoa wetu wa Manyara liko Mtaa wa Komoto. Tangu mwaka 2006 liko kwenye lenta, miaka 13 sasa Wizara hamjatuletea fedha. Mmeweza kutuletea shilingi milioni 150 kazi inaendelea, ni lini sasa mtatuletea fedha kwa ajili ya kukamilisha jengo la *RPC* pale Babati Mjini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Babati Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa kwamba jengo hilo linahitaji kukamilika. Tunayo majengo kadhaa nchi nzima ambayo yanahitaji kukamilishwa, siyo tu kwa Jeshi la Polisi, kwa upande wa Jimbo lake la Babati, nadhani

atakubaliana nami hata jengo la Uhamiaji nalo linahitaji kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si dhamira ya Serikali kuona majengo haya yanafikia robo ama nusu kukamilika. Dhamira ya Serikali ni kuona majengo haya ambayo yametumia fedha nydingi na yana umuhimu mkubwa kwa ajili ya vyombo vyetu yakamilike haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambayo inatukabili ni fedha kwamba bajeti haitoshi kukamilisha majengo yote kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira, pale ambapo hali ya kibajeti itakaa vizuri tutakamilisha majengo yote mawili ikiwemo la Polisi na Uhamiaji katika Jimbo lake pamoja na majengo mengine ambayo yanashubiri kukamilishwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kiasi ambazo zitaendelea kutatua changamoto hiyo. Kadri miaka inavyokwenda na hasa tukitilia maanani uchumi wa nchi yetu unakwenda vizuri sasa kutokana na kazi kubwa ya Serikali ya Awamu ya Tano, chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, naamini kabisa miaka ya mbele tutakuwa na fedha za kutosha kuweza kukamilisha majengo yote ambayo hayajakamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mtwara kimejengwa enzi ya Mkoloni na hivi sasa ukiingia mle ndani kinakaribia kubomoka, kinauliza kabisa niue nikuache, niue nikuache? Kila mwaka tunazungumza ndani ya Bunge na Serikali inasema imetenga bajeti. Kwa nini mpaka leo Serikali haileti fedha kwa ajili ya kukarabati kituo hiki ambacho hivi sasa kinatarajia kubomoka? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yatakuwa ni yale yale tu kwamba vituo vinavyohitaji kukarabatiwa ni vingi ikiwemo hiki cha Mtwara Mjini. Hata hivyo, kwa sababu kituo hiki nakifahamu na gharama zake za ukarabati si kubwa sana pengine mimi na Mheshimiwa Mbunge wakati tukisubiri hali ya bajeti ikae vizuri tushauriane ikiwezekana hata kwenda pamoja jinsi ya kutafuta njia zingine mbalimbali za kusaidia kukiweka vizuri kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya hivyo katika maeneo mbalimbali nchini kwa kutumia rasilimali nyingine nje ya kibajeti. Nina hakika kwa gharama ndogo za ujenzi zinazohitajika katika kituo hicho tunaweza tukafanikiwa tukashirikiana. Naamini Mheshimiwa Maftaha ni mchakapazi kwa hiyo, hata nikimshawishi na yeye kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo achomoe kidogo halafu tushirikiane kutafuta wadau basi tutaweza kikitendea haki kituo hiki.

**MWENYEKITI:** Swalii letu la mwisho litaulizwa na Mheshimiwa Issa Ally Mangungu, Mbunge wa Mbagala. Kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Mtalea.

Na. 157

**Hitaji la Kituo cha Polisi - Wilaya ya Mbagala**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y. MHE. ISSA A. MANGUNGU)** aliuliza:-

Serikali ilianzisha Kanda Maalum ya Kipolisi Dar es Salaam na kufanya Wilaya ya Temeke kuwa Mkoa wa Kipolisi; tangu Temeke iwe Mkoa wa Kipolisi kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu hasa maeneo ya Jimbo la Mbagala:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kituo cha Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mbala?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Vituo vya Polisi na kuviongezea askari, vitendea kazi na kujenga nyumba za askari katika maeneo ya Jimbo la Mbagala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mbagala ni Wilaya mpya ya Kipolisi iliyopo katika Mkoa wa Kipolisi wa Temeke. Kama ilivyo kwa wilaya nyingine katika Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Wilaya ya Mbagala inahitaji kujengewa Kituo cha Polisi chenye hadhi ya Wilaya. Kwa sasa wananchi wa Mbagala wanahudumiwa katika Kituo cha Polisi cha Mbagala Kizuiani ambacho miundombinu yake haitoshelezi. Aidha, hali kibajeti itakaporuhusu, Serikali itaweka mpango wa kuwajengea wananchi wa Mbagala Kituo kipywa cha Polisi, nyumba za makazi ya askari na ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kukabiliana na uhalifu, Wilaya ya Kipolisi Mbagala imepata mgao wa magari matatu (3) aina ya *Leyland Ashock Stile* yenye Na. PT 3779; PT 3881 na PT 3891 na kufanya jumla ya magari yote katika Wilaya ya Mbagala kuwa tisa ambayo yanatumika kwa shughuli za doria, upelelezi na operesheni mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha usalama katika Wilaya ya Mbagala.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mt Olea halafu Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Swali lwa kwanza, kama ambavyo Serikali inakiri umuhimu wa kituo hiki lakini ni muda mrefu sasa majibu yamekuwa ni haya haya kwamba bajeti itakaporuhusu, bajeti itakaporuhusu. Juzi tumepitisha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani na ujenzi wa kituo hiki haupo kwenye bajeti hiyo. Sasa nataka kujuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anavyotuambia tusubiri bajeti itakaporuhusu ni bajeti ipi anayoizungumzia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wamekuwa wakijitahidi kujenga vituo vya polisi lakini vingi havifanyi kazi kwa saa 24 yaani havipewi hadhi ya kufanya kazi saa 24. Kwa mfano, Kituo cha Polisi cha Buza ambacho wananchi wamekijenga kwa kiwango cha hali ya juu lakini mpaka leo ni miaka mitano bado kinafanya kazi kwa saa 12 tu. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari sasa kutoa amri kituo hicho kianze kufanya kazi kwa saa 24?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtalea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikijibu swali lake la kwanza kwamba bajeti ya mwaka huu haikuhusisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Mbagala. Hata hivyo, si Kituo cha Polisi Mbagala tu, vituo vya polisi vingi havikuhusishwa sababu ni kama nilivyozungumza mwanzo kwamba hatuwezi tukategemea bajeti ya mwaka mmoja itatue changamoto ya vituo vyote au maeneo yote. Kwa hiyo, kazi hii itaenda kwa awamu na kituo hiki kama hakijaweza kupata fursa katika bajeti hii basi kinaweza kupata fursa katika bajeti zinazokuja. Cha muhimu atambue Serikali inathamini na inatambua juu ya umuhimu wa ujenzi wa kituo hiki hasa ukililia maanani changamoto za usalama katika Mkoa wa Kipolisi Temeke na Wilaya ya Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili, kwanza niwapongeze yeye pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kipolisi Temeke kwa ujumla wao kwa jitihada zao kubwa ambazo wanachukua katika kusaidiana na Serikali kupunguza changamoto ya vituo vya polisi. Nami ni shahidi kwani nimeshiriki katika programu mbalimbali ikiwemo programu ya uchangishaji fedha wa kituo cha Chamanzi, ambapo sasa kipo katika hatua nzuri ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nimhakikishie kwamba tutakopomala kujenga vituo hivi madhumuni yake ni vitumike kama ilivyokusudiwa. Hoja ya kutumika saa 24 inategemea na aina ya kituo. Kwa mujibu wa *PGO* kuna *Class A, B* na *C*. Kuna vituo ambavyo vinapaswa vitumike kulingana na *category* ya *class* ya kituo hicho kwa muda wa saa 24 na viko ambavyo havipaswi kutumika kwa muda wa saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo ambacho amekizungumza ni *Class C*, kwa hiyo, hakiwezi kutumika kwa saa 24. Si kwa sababu labda hatuna askari wa kupeleka ama tumekitelekeza au hatuoni umuhimu huo lakini ni kwa sababu ya aina ya kituo na utaratibu ambao tumejiwekea kwa mujibu wa *PGO*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Jimbo la Mbagala limekuwa na ongezeko kubwa la watu hali ambayo inachangia sana kuwa na ongezeko kubwa la uhalifu lakini mazingira ya Kituo cha Polisi Mbagala Kizuiani ni mabaya sana pamoja na makazi ya polisi. Pamoja na hayo, Serikali imeeleza wazi kwamba utaratibu wa kujenga kituo hiki kwa sasa haupo. Je, Serikali ina mkakati gani basi wa kuwaboreshea angalau makazi ya askari wale jamani, hali mbaya, nyumba zile haziendani na eneo lile? Mbagala sasa

imekua, mabasi ya mwendokasi yanakuja, zile nyumba za Polisi pale zinatisha. Je, Serikali mna mkakati gani wa kufanya angalau maboresho ya eneo lile? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyeekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, changamoto ya uchakavu wa nyumba za askari katika eneo la Mbagala Kizuiiani tunaifahamu. Nichukue fursa hii kumpongeza kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo na kutupatia fedha ambazo tunatarajia kujenga takriban nyumba 400 nchi nzima. Katika maeneo ambayo nyumba hizo zitajengwa ni Kanda Maalum ya Dar es Salaam ikiwemo Mkoa wa Kipolisi wa Temeke. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na nimpongeze kwa *concern* na huruma aliyokuwa nayo kwa askari wetu, Serikali inalitambua na tunaendelea kulitatua hatua kwa hatua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Muda wetu wa maswali kwa siku ya leo umekwisha, sasa naanza kutangaza matangazo yaliyopo, kwanza tutaanza kutangaza wageni waliopo Bungeni siku ya leo.

Wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wa Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Maji ambaao ni viongozi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, wakiongozwa na Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Katibu Mkuu; *Engineer Emmanuel Kalobel*, Naibu Katibu Mkuu; Mheshimiwa Balozi Job Lusinde, Mwenyeekiti wa Bodi ya *DUWASA*; Jenerali Davis Mwamunyange, Mwenyeekiti wa Bodi ya *DAWASA*; Ndugu Fadhil Manongi, Kaimu Mwenyeekiti wa Bodi ya *EWURA*; Ndugu Nzinyangwa Mchany, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji *EWURA*; Ndugu Shija Kazumba, Mkuu wa Chuo cha Maji na Ndugu Barnabas Nduguru Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu. Karibuni sana. (*Makof*)

Pia wapo Wakurugenzi 27 wa Mamlaka za Maji za Mikoa nchini; Wakurugenzi wanane wa Miradi ya Maji ya Kitaifa; Wakurugenzi Watendaji tisa wa Mabonde ya Maji nchini pamoja na wakurugenzi wa Wizara na maafisa wa Wizara hii ya Maji. Karibuni sana, maafisa wetu na Wakurugenzi wa Wizara ya Maji. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Waheshimiwa Wabunge ambapo tuna wageni wawili ya Mheshimiwa Abdallah Ulega, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuu ambao ni wapiga kura wake kutoka Mkuranga Mkoani Pwani, Ndugu Yahya Kassim na Ustaadh Abdallah Msangi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni nane wa Mheshimiwa Goodluck Mlinga kutoka Shirika la *Women Action Towards Economic Development*, wakiongozwa na Ndugu Maria Matui. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Maulid Mtulia ambao ni wapiga kura wake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Omary Kimbau, Ndugu Abdallah Kambi, Ndugu Barton Msemwa. Karibuni wote. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ambaye ni baba yake mdogo kutoka Nandembo, Mkoa wa Mtwara ndugu Daimu Rashid Chuachua. Karibu sana Mzee Chuachua. (*Makofi*)

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM, Mkoa wa Arusha, Ndugu Hussein Abdullah. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia hapa tuna tangazo la mchezo, tunaambiwa jana timu yetu ya *Bunge Sports Club* ilicheza na vijana wa Polisi. Matokeo *Bunge Sports Club* magoli 2 na Polisi goli moja. Wafungaji wa magoli ya Bunge ni Mheshimiwa Chumi na Mheshimiwa Yussuf Kaiza. Mchezaji bora wa mchezo ni Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. (*Makofi*)

Katibu, tuendelee.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maji na  
Umwagiliaji**

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mwongozo.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) nikiwa naomba mwongozo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi wakati naingia ndani ya viwanja hivi vya Bunge, nikiwa kama Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini, nimepigiwa simu na wananchi wengi sana kutoka Mtwara Mjini wakinieleza kwamba hivi sasa Mtwara Mjini kuna tataruki kubwa sana ambayo inaenda kujitokeza kutokana na barua ambayo imeandikwa na Mkurugenzi wa Manispaa ya Mtwara Mikindani kwamba matawi ya Chama cha Wananchi - CUF yaliyojengwa maeneo ya Mkanaledi na Chipuputa yaweze kubomolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu suala hili limeleta tataruki kubwa sana. Kama likiendelea hivi kwamba watu wa chama fulani wanamtumia Mkurugenzi kwa ajili ya kubomoa matawi ya Chama cha Wananchi CUF maana yake kutakuwa na tataruki kubwa sana na wanachama wa Chama cha Wananchi CUF Mtwara Mjini ambao ndiyo wengi Manispaa ya Mtwara, hawatakulali, kwa hiyo, itapelekea kuwa na machafuko na hali ya amani kuweza kutoweka kabisa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba mwongozo wako kwa nini viongozi walioteuliwa na Serikali waliopo Mtwara Mjini, Wilaya Mtwara na Mkoa wa Mtwara wanashawishi Mkurugenzi alete hali ya taharuki ambayo inaweza kutupelekea kurudi kule tulikotoka mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwangozo wako viongozi waliteuliwa na Serikali waliopo Mtwara Mjini, Wilaya ya Mtwara na Mkoa wa Mtwara wanashawishi Mkurugenzi alete hali ya taaruki na baadaye ambayo inaweza kutupelekea kurudi kule tulikotoka mwaka 2013. Naomba mwongozo wako. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Maftaha naamini Serikali wanallijua hilo, kama lipo na limetokea kwa sababu lipo mkononi kwako na kitengo husika kitawezeka kufanya kazi hiyo. Katibu tunaendelea sasa na Waziri wa Maji ili aweze kuwasilisha hoja yake.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Maji na  
Umwagiliaji**

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyikiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifungo na Maji naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea nakujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka fedha 2018/2019. Aidha naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyikiti, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutuwezesha kukutana tena kujadili Bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyikiti, napenda kwa dhati kabisa kuishukuru kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa Mbunge wa Mufindi Kaskazini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuingoza Wizara, ushauri na maelekezo yao mazuri yaliwezesha Wizara kusahihisha dosari mbalimbali na kuboresha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyikiti, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuniamini na kunteua kuwa Waziri wa Maji Wizara yenye mchango mkubwa katika maisha ya watu maendeleo ya kiuchumi na kijamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyikiti, ninapenda kumuahidi Mheshimiwa Rais pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa, mimi na wenzangu katika Wizara ya Maji tutafanya kazi kwa bidii maarifa na uadilifu mkubwa ili ukufikia malengo ya tuliojivekea kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na rasilimali za maji za kutosha na kwamba wananchi wetu wanapata maji safi na salama na ya kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyikiti, kwa namna ya kipekee ninaomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya walichaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mwaka fedha unaoushia. Wabunge hao Mheshimiwa Thomas Paul Mzava kupitia Jimbo la Korogwe viji, Mheshimiwa Mwita Waitara kupitia Jimbo la Ukonga, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer kupitia Jimbo la Monduli, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka kupitia Jimbo la Liwawe, Mheshimiwa Christopher Chiza kupita Jimbo la Buyungwa, Mheshimiwa Marwa Chacha kupita Jimbo la Serengeti na Mheshimiwa Abdallah Mtalea kupitia Jimbo la Temeke ninawataenia kheri na mafaniko makubwa Wabunge

hao katika utekezaji wa majukumu yao ya kuwaaletea wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyikiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kasim Majaliwa Majaliwa kwa hotuba yake aliyowasilisha hapa Bungeni ambayo imetoa dira na muongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali ninawapongeza pia Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyikiti, Wizara ilipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha aliyekuwa Mbunge la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Steven Ngonyani alikuwa Mbunge wa Jimbo la Korongwe Vijijiini ninatoa pole kwako, ninatoa pole kwa Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu , familia ya marehemu ndugu na wananchi wa jimbo la Korogwe vijijiini. Vile vile ninatoa pole za dhati kwa wananchi walipoteza ndugu zao na mali kutoka na ajali ya kivuko cha MV Nyerere iliyookena katika Ziwa Victoria tarehe 18 Septemba mwaka jana. Mwenyenzi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi Amen. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyikiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi ninaomba kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya Wizra ya maji yenye maeneo matatu makubwa maeneo haya ni kama ifuatavyo:

- (i) Mabadiliko ya kimfumo katika uendeshaji wa sekta ya maji nchini;
- (ii) Hali ya sekta ya maji nchini na;
- (iii) Utekelezaji wa bajeti wa mwaka 2018/2019 na malengo ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabadiliko ya Kimfumo Katika Uendeshaji wa Sekta ya Maji, Katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi na kupunguza mwingiliano wa majukumu baina ya idara na vitengo vilivyo katika Wizara Serikali ilifanya

mabadiliko madogo ya Muundo wa Wizara. Aidha, katika kuimarisha uajibikaji na usimamizi wa sekta ya maji Bunge lako Tukufu lilitunga sheria mpya ya huduma za maji na usafi wa mzingira sheria namba tano ya mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekitii, Marekebisho ya Muundo wa Wizara, Serikali imefanya madadiliko ya Muundo wa Wizara ya Maji ambapo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliyokuwa ikisimamiwa na Wizara Maji imehamishiwa Wizara ya Kilimo. Vilevile Idara ya Maji Vijijini na Idara ya Maji Mjini zimeunganishwa na kuwa idara moja ya usambazaji maji na usafi wa mazingira ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji safi na salama hapa nchini. Aidha, katika kuhakikisha miradi ya maji inakuwa endelevu na ubora unatakiwa Wizara imekiongezea Kitengo cha Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji chenye jukumu la kupita taarifa za usanifu wa miradi zinazoandaliwa na wataalam wa shauri.

Mheshimiwa Mwenyikiti, kutungwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Mazingira, Sheria Na. 5 ya Mwaka 2019, katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alioitoa tarehe 10 Mei, 2018 yenye lengo la kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa watumishi katika sekta ya maji Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Sheria Na. 5 ya Mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyikiti, pamoja na mambo mengine sheria hiyo imeanzisha wakala wa usambazi wa maji na usafi wa mzingira vijijini ambao utakuwa na jukumu la kusimamia miradi ya utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Sekta ya Maji Nchini, hali ya rasilimali za maji. Rasilimali za maji nchini hutegemea kiasi ya mvua kinachopatika katika vipindi viwili vy'a masika na vuli, maeneo mengi ya nchi yanapata mvua mara mbili kwa mwaka katika miezi ya Oktoba, Disemba na Machi hadi

Mei. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya nchi yetu yanapata nchi yetu yanapata mvua mara moja kwa mwaka kuanzia mwezi Disemba hadi Aprili. Kiwango cha wastani wa mvua kwa mwaka katika maeneo mengi nchini ni milimita 900 hadi 1200. Wakati wa wastani wa mvua katika maeneo kame ya katikati ya nchi yetu ni kati ya milimita 400 hadi 550 kwa mwaka. Kwa upande wa maeneo yenye mvua nyingi kama vile Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya Milima ya Usambara ni wastani wa 2200 mpaka 2500 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyikiti, inakadiriwa kuwa rasilimali za maji zinatafaa kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa mita za ujazo ni milioni 126 kwa mwaka. Kiwango hicho kimegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni maji juu ya ardhi ambayo ni mita za ujazo milioni 105 na maji chini ya ardhi mita za ujazo milioni 21 kwa mwaka. Hifadhi hiyo ya maji inaonyesha kuwa kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu ni takribani wastani wa mita za ujazo mita 2300.

Mheshimiwa Mwenyikiti, mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile majumbani, umwagiliaji, viwandani n.k. ni wastani wa mita za ujazo bilioni 40 kwa mwaka, wakati mita za ujazo kati ya mita za ujazo bilioni 126 kwa mwaka zilizopo. Hali hiyo inaonyesha nchi yetu kuwa nchi yetu itandelea kuwa na rasilimali za maji za kutosha kwa ajili shughuliza maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya huduma ya ubora za maji, ufuatiliaji na utafiti wa ubora wa maji uliofanyika nchini inaonyesha ubora wa maji kutofautiana katika eneo moja hadi nyingine kutofautiana huko huko kunatoka na miamba ya asili. shughuli za kibidamu. jiografia ya eneo na mbadiliko ya tabia ya nchi. Changamoto zilizobainishwa katika utafiti huo ni pamoja na kuwepo kwa viwango kikubwa vya *Nitrogen Phosphorous na tope (turbidity)* kwenye maji ya ardhi vinavyosabishwa na shughuli za kibidamu kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa upande wa maji chini ya ardhi changamoto ni uwepo wa kiwango kikubwa

cha chumvi chumvi na *Nitrate* madini ya *Fluoride*, Chuma, Manganese na Chloride. Pamoja na changamoto hizo hali ya ubora wa maji katika vyanzo inaridhisha na vinaweza kuendelezwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali baada ya kutibitwa na kuwa salama kulinga na matumzi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyikiti, hali ya upatikanaji za maji usafi wa mazingira, huduma za maji vijijini. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza miradi ya maji vijiji kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye mkazi yao. Lengo ni kufikia 85% ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2020. Hadi mwezi Aprili mwaka huu jumla ya miradi 1659 vyenye vituo vya kuchotea maji 131,370 imejengwa kati ya vituo hivyo vilijengwa vituo 86,780 vinafanya kazi na vina uwezo wa kuhudumia watanzania wapatao 25,359,290 sawa na 64.8% ya wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyikiti, huduma ya maji mijini, huduma ya maji mijini katika meneo ya mijini hutolewa na mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayo hudumiwa na miradi ya kitaifa. Malengo ya Serikali ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma maji katika miji mikuu ya mikoa kufikia 95% na miji mikuu ya wilay, miji midogo na miradi ya kitaifa kufikia 90% ifikapo mwaka 2020. Kwa upande wa huduma ya uondoaji wa maji taka, lengo la Serikali ni kuongeza huduma hiyo kufikia 30% ikifakapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyikiti, hadi mwenzi Aprili mwaka huu hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya mikoa ni 80% na kwa miji Mikuu ya Wilaya. Miji midogo na miradi kitaifa upatikanaji wa huduma hiyo ni 64%. Aidha, kwa upande wa huduma ya uondoaji maji taka katika maeneo ya mijini hadi mwezi

Aprilii mwaka huu huduma hiyo imefikia wastani 20% kwenye miji ya mitandao wa maji taka .

Mheshimiwa Mwenyikiti, utekelezaji wa bajeti wa mwaka 2018/2019 na malengo ya mwaka 2019/2020 upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2019/2020 Fungu namba 49 Wazara ya Maji iliidhinishwa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 697.57 na kati fedha hizo shilingi bilioni 24.363 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 673.214 zilikuwa fedha za maendeleo hadi mwezi Aprilii mwaka huu jumla shilingi bilioni 16.653 sawa na 68% za matumizi ya kawaida zilipokelewa na kati hizo, shilingi bilioni 2.95 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi bilioni13.747 ni fedha za mishahara. Shilingi bilioni 343.486 sawa na 51% ni fedha za maendeleo ambazo zilipokelea.

Mheshimiwa Mwenyikiti, utekelezaji wa miradi na program mbalimbali katika mwaka wa fedha 2018/2019 na malengo ya mwaka 2019/2010. Katika mwaka 2018/2019 sekta ya maji imeendelea kutekeleza miradi na pragamu mbalimbali zinazolenga kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji wa rasilimali za maji ufuatuliaji wa ubora wa maji, kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini na kutekeleza masuala mtambuka utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 na mpango wa mwaka 2019/2020 umeelezwa kwa kina kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyikiti, kwanza usimamizi na uendelezaji wa rasilimali maji. Jukumu la Wizara ni kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini, utekelezaji wa majukumu hayo ni kama ifuatavyo: kwanza mwenendo wa rasimlimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyikiti, upatikanaji wa takwimu sahihi na za muda mrefu za rasilimali za maji ni muhimu katika kuwezesha Serikali katika kutoa taarifa sahihi za hali ya maji nchini. Kuchua taahadhalii juu majanga ya ukame na mafuriko pamoja na kuibua na kusanifu miradi mbalimbali ya kiuchumi na kujamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Aprili mwaka huu Wizara kuptitia Bodi za Maji za Mabonde imeendelea kukusanya takwimu za rasilimali za maji nchini kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Kutokana na takwimu hizo zilizokusanya katika mwaka wa kihaidrolojia kuanzia mwezi Novemba mwaka 2017 hadi Oktoba, 2018 hali ya maji katika Maziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa, Rukwa, mabwawa ya Mtera Kihansi, Kidatu, Nyumba ya Mungu na Mindu na Mito ya Pangani, Ruvuma Malagarasi, Wami, Ruvu, Rufiji, Mara na Kagera ilikuwa juu ya wastani ikilinganishwa na mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa mazingira na vyanzo vya maji, uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira unatokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu umekuwa ni changamoto katika kulinda na kuhifadhi vyanzo hivyo vya maji nchini. Katika kukabiliana na changamoto hilo hadi mwezi Aprili mwaka huu Wizara imeweeka mipaka kwenye vyanzo mbalimbali na kupanda miti kwenye vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji, katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, Wizara hufanya ukaguzi wa uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji na ubora wa maji taka yanayotiririshwa kwenye vyanzo hivyo. Hadi mwezi Aprili mwaka huu Wizara imefanya ukaguzi katika viwanda saba na Migodi minne ya dhahabu na vyanzo vya maji katika mabwawa ya Igombe na Kazima yanayotoa huduma ya maji katika Manispaa ya Tabora. Katika maeneo yaliyokaguliwa matokeo yameonesha kuwa maji taka yanayorudishwa kwenye baadhi ya vyanzo vya maji yanakidhi viwango. Wizara inaendelea na jitihada za kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi bora ya rasilimali za maji na udhibiti wa migogoro. Katika kuhakikisha matumizi ya maji yanayoratibiwa hadi mwezi Aprili mwaka huu, bodi za maji za Bonde zimeta vibali kumi na sita, vya matumizi ya maji. Vilevile ukaguzi wa vibali vya kutumia maji ulifanyika ambapo watumiaji 350 walibainika kutokuwa na vibali. Katika

kudhibiti hali hiyo, watumiaji walipewa elimu kuhusu matumizi bora ya maji yanayozingatia Sheria, Taratibu, Kanuni za rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji wa vyanzo vipyta vya maji, Wizara kuititia Bodi za maji za Bonde kwa kushirikiana na halmashauri mbalimbali nchini, imeendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji, yakiwemo maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa. Lengo ni kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019. Wizara ilifanya utafiti na kubaini maeneo mapya 91 yanayofaa kwa uchimbaji wa visima. Ujenzi wa mabwawa ya Kimkakati, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji nchini. Serikali imepanga kujenga mabwawa ya Kimkakati kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa maji katika kipindi chote cha mwaka, mabwawa hayo yamepangwa kujengwa ni Farkwa, ambalo liko huko Chemba, Kidunda Morogoro na Ndembera huko Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Farkwa, litakuwa kwa ajili ya usambazaji wa maji katika mji wa Dodoma, na Wilaya za Chemba na Bahi pamoja na Kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango Shirikikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Uandaaji wa Mpango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, ni hitaji la Kisheria linalolenga kusimamia rasilimali za maji kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Kwa sasa, Mipango shirikishi ya Mabonde ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Mto Rufiji na Bonde la Kati imekamilika. Kati ya Mabonde hayo, bonde la Mto Rufiji imekamilisha tathmini ya Kimkakati ya kimazingira na kijamii na kuanza utekelezaji wake. Kwa mabonde yaliyobaki taratibu za kuanza kufanya tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ubora na usafi wa maji, ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji maji nchini na mijini ni muhimu katika kulinda afya ya jamii pamoja na mifumo ya ikolojia. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ilipanga kukusanya na kuchunguza sampuli 10,000 za maji kwa matumizi mbalimbali na sampuli 1,500 za maji taka, hadi mwezi Aprili mwaka huu. Jumla ya sampuli 4,713 za maji safi, na sampuli 226 za maji taka zilikusanywa na kuchunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji kwa matumizi ya nyumbani sampuli 4,165 zilifanyiwa uchunguzi na matokeo yalionesha kuwa sampuli 3,776 za maji sawa na asilimia 91 zilikidhi viwango vinylvokubalika na sampuli 389 sawa na asilimia 9 hazikukidhi viwango. Aidha, sampuli 201 zilichunguzwa kwa ajili ya matumizi ya viwandani, ambapo sampuli 199 sawa na asilimia 99 zilikidhi vigezo. Vilevile sampuli 36 za maji kwa ajili ya ujenzi, sampuli 31 kwa ajili ya utafiti na sampuli 38 kwa ajili ya umwagilaji zilichunguzwa na zote zilikidhi viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubora wa Dawa za Kusafisha na Kutibu Maji; udhibiti wa ubora wa madawa yanayotumika kusafisha na kutibu maji, kabla ya matumizi ni muhimu, katika kulinda afya za wananchi na usalama wa maji kwa ujumla. Hadi mwezi Aprili mwaka huu jumla ya sampuli 31 za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Taasisi 31 zilichunguza ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yamebaini kuwa sampuli zote za madawa zilikidhi viwango vinylvokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya *Fluoride* katika Maji; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza mkakati wa uondoaji wa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwenye mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo kwa kusambaza na kufuatilia ufanisi wa mitambo ya kuondolea madini ya *fluoride*; Kutoa elimu kuhusu madhara ya madini hayo; Kuongeza uzalishaji wa malighafi ya kuondoa madini ya *fluoride* pamoja na kufanya utafiti wa *fluoride* katika

vyanzo vya maji kwenye maeneo mbalimbali, hadi mwezi Aprili mwaka huu, jumla ya mitambo 220 ya kuondoa madini ya *fluoride* katika ngazi ya kaya na mitambo minne katika ngazi ya jamii imesambazwa kwenye maeneo yaliyoathiriwa na madini ya *fluoride* na jumla ya wananchi wapatao 1,760 wananaufaika na teknolojia hiyo. Ili kuhakikisha teknolojia hiyo inakuwa endelevu, Wizara imeendelea kufuatilia ufanisi wa mitambo iliyosambazwa ambazo mitambo 40 ya ngazi za kaya na mitambo minane ya ngazi za jumuiya ilikaguliwa na ushauri ulitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imepanga kutengeneza na kusambaza mitambo midogo 1,000 ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji katika ngazi ya kaya. Huduma za usambazaji maji vijijiini, katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Disemba, 2018 jumla ya miradi 168 yenye vituo vya kuchotea maji 4,719 imekamilika na ina wanufaisha wananchi wapatao 1,252,731 waishio vijijiini. Aidha, miradi 653 inaendelea kutekelezwa na ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha miradi ya maji vijijiini inakuwa endelevu Serikali inaendelea kutekeleza programu mbili ambazo ni mfumo wa malipo kwa matokeo na matumizi ya teknolojia ya nishati jadidifu. Lengo la programu hizo ni kuimarisha uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijiini. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la maendeleo la Kimataifa *DFID*, inatekeleza Mpango wa mfumo wa malipo kwa matokeo, ambao una lengo la kuimarisha uendelevu wa miradi ya maji, hadi mwezi Aprili, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya pili ya programu hiyo imekamilika, ambapo Halmashauri 95 zilifuzu na kupewa shilingi bilioni 8.55 kati ya shilingi bilioni 53.6 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, awamu ya tatu ya programu inayoendelea na uhuishaji Halmashauri 181 ambazo zitapewa fedha kwa vigezo vya idadi ya vituo vilivyojengwa na kutoa maji. Kupitia program hiyo paundi 300 hutolewa kwa kila kituo kilichohakikiwa na kinafanya kazi na

paundi 1,500 hutolewa kituo kipyta kitakachojengwa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, jumla ya paundi milioni kumi zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza program hiyo kwenye halmashauri zote nchini. Hadi mwezi Aprili mwaka huu, fedha zilizolipwa katika awamu ya tatu ni paundi milioni 8.7, sawa na shilingi bilioni 25.43 katika mwaka wa fedha 2019/2020. Shilingi bilioni 46.47 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Same, Mwanga na Korogwe, mradi umegawanyika katika awamu mbili, utekelezaji wa awamu ya kwanza, umegawanyika katika vipande vine. Hadi mwezi Aprili mwaka huu, utekelezaji wa kipande cha kwanza umefikia asilimia 79 na kipande cha tatu asilimia 15 na ujenzi wa kipande cha nne umefikia asilimia 55. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha pilli. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi bilioni 29.28 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo. Mradi utakapokamiliika utawanufaisha Watanzania wapatao 556,931 wa Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyomo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya ya Same, Mwanga na Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Viji 100 vilivyoko kandokando ya Bomba Kuu la *KASHWASA*; Mradi huu kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga, unaendelea kutekelezwa chini ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Kahama, Shinyanga (*KASHWASA*). Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo itahusisha vijiji 40 ambapo vijiji 33 vimefanyiwa usanifu. Kati ya vijiji vilivyoofanyiwa usanifu, ujenzi wa miradi kwenye vijiji 14 umekamiliika na kunufaisha Watanzania wapatao 36,348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Aprili mwaka huu, utekelezaji wa mradi katika vijiji vilivyobakia vya Mwasekagi na Mwakatole umefikia asilimia 90 na wananchi wanapata huduma ya maji safi. Vilevile ujenzi wa mradi unalenga kwenye Viji vya Mwakuzukuna, Kabondo, Zuga, Isese, Igenge na kadhalika, ambapo utekelezaji wake

umefikia asilimia 40. Kukamilika kwa mradi huo, kutawanufaisha Watanzania wapatao 26,573 wa vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Ntomoko; Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliunda Tume ya wataalam kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina wa Mradi wa Maji Ntomoko. Timu hiyo ilibaini kuwa chanzo cha Ntomoko kina uwezo wa kuhudumia vijiji vitatu tu kati ya vijiji kumi na nane vilivyokuwa katika mpango. Baada ya Timu kubaini upungufu huo, utafiti ulifanyika na kubaini uwezekano wa kujenga bwawa kubwa litakalokidhi mahitaji ya vijiji vilivyobaki na usanifu wa bwawa hilo umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa muda mfupi, Wizara kuititia *DUWASA* inakarabati miundombini ya maji katika Viji<sup>j</sup>i vya Ntomoko, Pahi na Makirinya vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya Kondoa na Viji<sup>j</sup>i vya Kinkima na Lusangi vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, ambavyo kwa muda vitapata chanzo cha maji cha Ntomoko. Mradi huo unagharimu shilingi bilioni 2.27 na mwezi Februari mwaka huu *DUWASA* ilisaini Mkataba na Mkandarasi ambaye ameanza utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukarabati wa mabwawa, katika kukubaliana na changamoto ya uhaba wa maji katika maeneo kame, Serikali imeendelea kujenga mabwawa mapya na kukarabati mabwawa yaliyopo ili wananchi waweze kunufaika na huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Aprili mwaka huu ujenzi wa bwawa la Mwanjoro lilitopo Wilaya ya Meatu ambalo linatoa huduma ya maji kwa wananchi 13,859 wa Viji<sup>j</sup>i vitatu vya Mwanjoro, Jinamo na Mbushi vilivyopo katika Halmashauri ya Meatu umekamilika. Ujenzi wa bwawa la Wanging'ombe lilitopo Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoani Njombe, ambalo linahudumia vijiji tisa, ujenzi umefikia asilimia 75, ujenzi wa Bwawa la Nse-kwa lilitopo Wilaya ya Mlele, Mkoani Katavi unaendelea na umefikia asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, usanifu kwa mabwawa mengine unaendelea ili kutatuta tatizo la maji katika maeneo hayo. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali itaendelea kufanya utafiti wa maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa mapya. Kujenga na kufanya ukarabati wa mabwawa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi bilioni 10.3 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ya mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji katika Vijiji Vilivymo Pembezoni mwa Maziwa; katika kuhakikisha rasllimali za maji yetu yanawanufaisha wananchi wetu. Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji katika maeneo ya pembezoni mwa Maziwa Makuu, ya Tanganyika, Nyasa na Victoria. Kwa upande wa Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika, Mtaalamu Mshauri amekamilisha na kuwasilisha taarifa ya upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za mazingira na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inayofuata ni kufanya usanifu wa kina wa mradi, kwa upande wa mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa, Mtaalam Mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu na anaendelea na tathmini ya athari za mazingira ya kijamii. Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa Mradi wa Kutoa Maji kutoka Ziwa Victoria katika vijiji vitakavyonufaika na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo mwezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Utekelezaji wa Mradi wa Maji Vijiji; katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji vijiji inayoendelea kutekelezwa na kuanza ujenzi wa miradi mipyä katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Jumla ya shilingi bilioni 301.25 zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 224.03 na fedha za nje ni shilingi bilioni 77.22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini; katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji

wa huduma ya maji mijini kwa kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya maji safi na maji taka. Hatua hiyo, iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi ya Kutoa Maji Ziwa Victoria kupeleka katika Miji Mbalimbali; Miji ya Isaka na Kagongwa; Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Isaka na Kagongwa umegawanyika katika vipande viwili, hadi mwezi Aprili mwaka huu utekelezaji wa kipande cha kwanza umefikia asilimia 94 na kipande cha pili umefikia asilimia 87. Mradi utakapokamilika utahudumia wakazi wapatao 115,000 wa Mji wa Isaka na Kagongwa. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga shilingi bilioni nne kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui; Mradi wa Kutoa Maji kutoka Bomba Kuu la *KASHWASA* kupeleka Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya na Uyui imegawanyika katika vipande vitatu. Hadi mwezi Aprili mwaka huu kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 68.5 na unatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha ujao 2019/2020. Mradi utakapokamilika utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji hiyo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Mwanza na Miji la Lamadi, Magu na Misungwi; Mradi wa Uboreshaji wa Maji wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa. Hadi mwezi Aprili mwaka huu utekelezaji umefikia asilimia 75 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao 105,649 wanaoishi maeneo mbalimbali ya milimani ya Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi; utekelezaji wa miradi hadi mwezi Aprili mwaka huu umefikia asilimia 87 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei mwaka huu. Kukamilika kwa mradi huo

kutawanufaisha wakazi 23,515 wa Misungwi Mjini na Kijiji cha Nyehita, wakazi wa 45,340 wa Magu Mjini na Vijiji vya Ilunga na Kipeja na wakazi 23,540 wa Lamadi Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Kigoma; utekelezaji wa mradi ulitarajiwa kukamilika mwezi Novemba mwaka 2017, lakini haukukamilika kutokana na uwezo mdogo wa Mkandarasi. Kutokana na hali hiyo Serikali imechukua hatua ya kuvunja Mkataba na Mkandarasi huyo mwezi Oktoba mwaka jana. Hadi kuvunjwa kwa Mkataba, utekelezaji wa Mradi ulikuwa umefikia asilimia 87 na mradi umeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Kufuatia kuvunjwa kwa Mkataba na Mkandarasi aliyekuwepo, Wizara imeajiri Wakandarasi wengine wa kujenga chanzo cha maji na kumalizia kazi zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Arusha, utekelezaji wa mradi huu, hadi mwezi Aprili mwaka huu ulifikia asilimia 30 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2020. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 kwa siku hadi lita milioni mia mbili kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Lindi; mradi huo ulitarajiwa kukamilika mwezi Novemba mwaka 2017, lakini haukukamilika kutokana na uwezo mdogo wa kiutendaji wa Mkandarasi, hivyo Serikali ilichukua hatua ya kuvunja Mkataba na Mkandarasi huyo mwezi Oktoba mwaka jana, ambapo utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 92.3 na unatoa huduma ya maji kwa wakazi wapatao 81,343 wa Mji wa Lindi. Kufuatia kwa kuvunjwa kwa Mkataba na Mkandarasi wa awali, Serikali imeajiri Mkandarasi mwingine atakayemalizia kazi zilizobaki na anatarajiwa kuanza kazi mwezi Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Geita; hadi mwezi Aprili mwaka huu, utekelezaji wa mradi umekamilika na upo katika hatua ya makabidhiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Njombe; katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji

katika Mji wa Njombe, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Chemchemi ya Kibena ambao umeboresha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. Mradi huo umeongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Njombe kutoka asilimia 68 mwaka 2016 hadi asilimia 87 za sasa. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili kuboresha huduma ya maji katika mji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji ya Vwawa na Mlowo; hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Mji ya Vwawa umefikia asilimia 90. Kukamilika kwa mradi huo, kutawanufaisha wakazi wapatao 10,171. Kwa upande wa mji wa Mlowo mradi umekamilika na wakazi wapatao 9,154 wanapata huduma ya maji. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji katika miji hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji Mikuu ya Wilaya na Mji midogo; Mji wa Orkesumet; Serikali inatekeleza Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Salama katika Mji wa Orkesumet. Utekelezaji wa mradi huo, umegawanyika katika vipande viwili ambapo kipande cha kwanza utekelezaji wake, uko katika hatua za awali na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020 na kwa kipande cha pili, utekelezaji wake umefikia asilimia 68 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2019/2020. Mradi utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa maji katika mji huo kutoka asilimia 48 hadi asilimia 82 na kuwanufaisha wakazi wapatao 52,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Longido; Mradi wa Maji katika Mji wa Longido unalenga kuboresha huduma ya maji katika mji huo pamoja na Kijiji cha Engikaret. Mradi huo umegawanyika katika vipande vinne ambapo hadi mwezi Aprili mwaka huu utekelezaji wa kipande cha kwanza, cha tatu na cha nne umekamilika. Kipande cha pili kinachohusisha kazi za ulazaji bomba la kusafirisha maji kutoka Longido Mjini hadi Kijiji cha Engikaret na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji utekelezaji wake umefikia asilimia 95.

Kukamilika kwa Mradi wa Longido kumewezesha wananchi wapatao 16,712 wa Longido Mjini na wananchi wapatao 1,294 wa Kijiji cha Engikaret kupata huduma ya maji na salama. Katika mwaka wa fedha 2019/2020. Serikali imetenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa kipande kilichobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoro. Mradi wa Visima virefu vya Kimbiji na Mpera; Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa Visima virefu 20 vya Kimbiji na Mpera. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu visima 19 vimechimbwa na sasa viko katika hatua mbalimbali za uendelezaji. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya uendelezaji wa visima vitano vya Kimbiji ambapo mamlaka iko kwenye hatua ya mwisho ya kumpata Mkandarasi kwa ajili kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi; Serikali imekamilisha mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza maji safi katika maeneo ya Tegeta hadi Mpiji, Mpiji hadi Bagamoyo na Mbezi hadi Kiluvya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa uimarishaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, ambapo utagharimu dola za kimarekani milioni 86. Mradi huu pamoja na mambo mengine utahusisha ujenzi wa matanki na kupanua mtandao wa kusambaza wa maji wenye urefu wa kilomita 1,440 na kuunganisha wateja 64,000 katika maeneo yote ya mradi. Hadi mwezi Aprili mwaka huu, Mkandarasi wa mradi huo amepatikana na ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Bwawa la Kidunda; Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda lenye mita za ujazo milioni 190 ambao unatarajiwa kugharimu dola za Kimarekani milioni 215. Lengo la mradi huo ni kuhakikisha maji katika Mto Ruvu ambao ni

chanzo kikubwa cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo yanapatikana kwa kipindi chote cha mwaka. Kazi za usanifu wa bwawa pamoja na ulipaji wa fidia kwa wakazi watakaopisha ujenzi wa bwawa hilo umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuboresha Miundombinu ya Uondoaji Majitaka; Serikali inatekeleza miradi ya uondoaji maji taka, miradi hiyo itawezesha kufikia lengo la kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya uondoaji maji taka kutoka asilimia 10 hadi asilimia 30 ifikapo 2020. Miradi hiyo inatarajiwu kujengwa katika maeneo matatu kwanza Jangwani, Kurasini na *Mbezi Beach*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Dodoma; Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika Jiji la Dodoma ili kuendana na uhitaji mkubwa wa maji uliopo kwa sasa. Miradi inayotekelizwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ujenzi wa Mradi wa Maji katika Mji Mpya wa Serikali. Serikali inatekeleza mradi wa maji katika Mji Mpya wa Serikali uliopo eneo la Mtumba Jijini Dodoma. Utekelezaji wa mradi huo umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza iliyogharimu shilingi bilioni 3.6 imekamilika na awamu ya pili ya mradi inayogharimu shilingi milioni 508 inaendelea na hadi kufikia Aprili, 2019, utekelezaji wa awamu hiyo umefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kusambaza maji kwenye maeneo yasiyo na huduma. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma inaendelea na taratibu za kupata mkopo wa shilingi bilioni 1.5 kupitia utaratibu wa Mfuko *wa Investment Financing Facilities – Output Based Aid (IFF-OBA)* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*). Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji kwenye maeneo yasiyo na huduma ya mafi safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bwawa la Farkwa. Serikali imeweka mkakati wa muda mrefu wa kuwapatia huduma ya maji ya uhakika wakazi wa Jiji la Dodoma kwa kujenga Bwawa la Farkwa katika Wilaya ya Chemba. Bwawa hilo litakuwa chanzo kikuu cha maji kwa Jiji la Dodoma, Wilaya Bahi na Chemba. Mradi huu utaongeza uzalishaji wa maji wa Jiji la Dodoma kwa zaidi ya ujazo wa lita milioni 120 kwa siku. Hadi Aprili, 2019, tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi imekamilika na inatarajiwa kuanza kulipwa katika mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Majisafi katika Jiji la Dodoma na Chamwino. Serikali imeajiri Mtaalamu Mshauri anayefanya upembuzi yakinifu, tathmini ya athari za kimazingira na kijamii na usanifu wa kina wa mradi wa kuboresha huduma za maji safi katika Jiji la Dodoma na Chamwino. Kwa sasa Mtaalam huyo anaendelea na kazi hiyo inayotarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi huu. Aidha, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma inaendelea na taratibu za kupata mkopo wa shilingi bilioni 1.5 kwa mradi wa kusambaza maji kwenye maeneo yasiyo na huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Maji Safi katika Miji mbalimbali. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Miradi inayotarajiwa kutekelezwa ni miradi wa maji katika Miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi, Morogoro Mjini, Mtwara na Babati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika Miji 29 kupitia mkopo wa masharti ya nafuu kutoka Serikali ya India ambaao utagharimu Dola za Kimarekani Milioni 500. Miji hiyo ni Muheza, Wanging'ombe, Makambako, Kayanga, Songea, HTM, Njombe, Mugumu, Kilwa Masoko, Geita, Chunya, Makonde, Manyoni, Sikonge, Kasulu, Rujewa, Chato, Singida Mjini, Kiomboi, Mpanda, Chemba, Mafinga, Urambo-Kaliua, Pangani, Ifakara, Rarya/Tarime, Chamwino na Nanyumbu. Mtaalamu Mshauri ambaye atapitia usanifu na kutayarisha

makabrasha ya zabuni tayari ameshapatikana. Kwa sasa mkataba kwa ajili ya kazi hiyo uko ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi. Wakati wowote kuanzia sasa mkataba huo utasainiwa na kazi hiyo kuanza mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama. Mradi huo utagharimu takriban shilingi bilioni 30.69. Kwa sasa Wizara iko katika hatua ya mwisho ya kumpata mkandarasi ambaye atatekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji mijini inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya shilingi bilioni 248.42 zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni shilingi bilioni 100.42 na fedha za nje ni shilingi bilioni 148.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu katika taasisi zilizo chini ya Wizara. Mfuko wa Maji. Lengo la Mfuko wa Taifa ya Maji ni kuwekeza kwenye miradi ya huduma za maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidaka maji. Kipaumbele ikiwa ni kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa huduma ya maji safi na salama hususan maeneo ya vijijiini. Maelezo ya kina kuhusu Mfuko wa Maji yanapatika kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kutoka ukurasa wa 93.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa. Katika mwaka 2018/2019, Wizara kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa iliendelea kutekeleza majukumu ya kuchimba visima, kujenga mabwawa, kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na kuchunguza ubora wa udongo kwa ajili ya shughuli za ujenzi nchini. Maelezo ya kina kuhusu Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa yanapatika kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kutoka ukurasa wa 94-95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati. Wizara inaendelea kuisimamia *EWURA* ili iweze kutekeleza majukumu yake ya udhibiti katika sekta za maji na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini. Maeleo ya kina ya utekezaji kazi mbambali za *EWURA* zinapatikana kwenye kitabu cha hotuba ukurasa wa 96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maji. Mafunzo mbalimbali yanayotolewa na chuo katika ngazi ya Stashahada na shahada. Maeleo ya kina kuhusu Chuo cha Maji yanapatikana kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kutoka ukurasa wa 94-95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka. Masuala Mtambuka yamezungumzwa kwa kina kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 100 - 104.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2018/2019 na hatua zilizochukuliwa. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, punguzeni sauti.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo na jinsi Wizara inavyoipanga kukabiliana nazo zimeelezwa kwa kina kwenye kitabu cha hotuba ya bajeti kutoka ukurasa wa 106 - 112.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Napenda kuwashukuru sana viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mhe. Jumaa Hamidu Aweso, Naibu Waziri wa Maji; Prof.

Kitila Alexander Mkumbo, Katibu Mkuu; Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelio, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, wataalam na watumishi wote wa Wizara ya Maji pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na watumishi wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji pia na Wenyeviti wote wa Mamlaka za Maji kwa ushirikiano mkubwa walionipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kuwashukuru washirika mbalimbali wa maendeleo ambao wametoa michango yao kwa namna moja au nyingine katika kuendeleza sekta za Maji. Washirika hao ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (AFD), Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (KfW), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*), Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GIZ), *Global Environment Facility (GEF)*, *Green Climate Fund*, Shirika la Afya Duniani (*WHO*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*). Vilevile, nashukuru sana Mashirika na Taasisi za Kidini na Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki kwa ukamilifu katika kuendeleza sekta ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2019/2020. Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.634,196,197,530 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni Sh.23,726,309,000 ambapo Sh. 6,266,714,000 sawa na asilimia 24 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (*OC*) na Sh.17,459,555,000 sawa na asilimia 76 ni kwa ajili ya kulipa mishahara (*PE*) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya

maendeleo ya Sh.610,469,888,530 ambapo kati ya fedha hizo, Sh.349,449,000,000 sawa na asilimia 57 ni fedha za ndani na Sh.261,020,888,530 sawa na asilimia 43 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, sasa naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI, MHE. PROF. MAKAME  
MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA  
MWAKA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, leo hii Bunge lako Tukufu limepokea taarifa ya Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini**, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Maji. Ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/2020.

**2. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kwa dhati kabisa kuishukuru **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji** kwa ushauri, maoni na maelekezo iliyoyatao wakati nilipowasilisha Taarifa ya Utekelezaji ya mwaka 2018/2019 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara kwa mwaka 2019/2020. Ninapenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

**3. Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Rais wa Jamhuri ya**

**Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli**, kwa kuniamini na kunteua kuwa Waziri wa Maji, Wizara yenye mchango mkubwa katika maisha ya watu na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ninapenda kumuahidi Mheshimiwa Rais pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa nitafanya kazi kwa bidii, maarifa na uadilifu mkubwa ili kufikia malengo tuliojiwekea yatakayowezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, ninaomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka wa fedha unaoisha. Wabunge hao ni **Mhe. Timotheo Paul Mnzava** kupitia Jimbo la Korogwe Vijijini, **Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara** kupitia Jimbo la Ukonga, **Mhe. Julius Kalanga Laizer** kupitia Jimbo la Monduli, **Mhe. Zuberi Mohamedi Kuchauka** kupitia Jimbo la Liwale, **Mhe. Christopher Kajoro Chiza** kupitia Jimbo la Buyungu, **Mhe. Marwa Ryoba Chacha** kupitia Jimbo la Serengeti na **Mhe. Abdallah Ally Mtolea** kupitia Jimbo la Temeke. Ninawatakia kheri na mafanikio Wabunge hao katika utekelezaji wa majukumu yao ya kuwaleta wananchi maendeleo.

5. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kumpongeza **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Ninawapongeza pia Mawaziri wenzangu walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

6. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Stephen Ngonyani** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Ninatoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa Jimbo la Korogwe Vijijini. Vilevile, ninatoa pole za dhati kwa wananchi waliopoteza ndugu zao na mali kutokana na ajali ya kivuko cha MV Nyerere iliyotokea katika Ziwa Victoria

tarehe 19/09/2018. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. **Amin.**

**7. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji yenye maeneo makuu matano, ambayo ni mabadiliko ya kimfumo katika uendeshaji wa sekta ya maji; hali ya sekta ya maji nichini; utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 na malengo ya mwaka 2019/2020; changamoto na hatua zinazochukuliwa; na maombi ya fedha kwa mwaka 2019/2020. Muundo na Mfumo wa bajeti hiyo umeongozwa na kuzingatia Malengo Endelevu ya Dunia (*Sustainable Development Goals – SDGs*) hususan Lengo Na. 6; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (*Five Year Development Plan – FYDP*); Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2019/2020; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP II*).

**2. MABADILIKO YA KIMFUMO KATIKA UENDESHAJI WA SEKTA YA MAJI**

**8. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi na kupunguza muingiliano wa majukumu baina ya Idara na Vitengo vilivypopo katika Wizara ya Maji, Serikali ilifanya mabadiliko madogo ya muundo wa Wizara. Aidha, katika kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa Sekta ya Maji, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019. Muhtasari wa maudhui ya mabadiliko ya kimfumo na Sheria mpya ni kama ifuatavyo:-

**2.1. Marekebisho ya Muundo wa Wizara**

**9. Mheshimiwa Spika**, Serikali imefanya mabadiliko ya Muundo wa Wizara ya Maji ambapo Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliyokuwa ikisimamiwa na Wizara ya Maji imehamishiwa Wizara ya Kilimo. Vilevile, Idara ya Maji Vijijini na Idara ya Maji Mijini zimeunganishwa kuwa Idara moja ya

Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira. Aidha, Kitengo cha Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kimeongezewa jukumu la kuandaa miradi ya maji, lengo likiwa ni kuweka msisitizo zaidi kwenye eneo la uandaaji wa miradi ambalo limekuwa na changamoto kwa kipindi kirefu.

**2.2. *Kutungwa kwa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019***

**10. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maelekezo ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, **Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli** aliyojatoa tarehe 10/05/2018 yenye lengo la kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa watumishi katika sekta ya maji, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019. Pamoja na mambo mengine, Sheria hiyo imeanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Authority – RUWASA*) ambaao utakuwa na jukumu la kusimamia utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini. Vilevile, Sheria mpya imeendelea kuzitambua Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira na Mfuko wa Taifa wa Maji. Aidha, muundo wa Vyombo vyta Watumiaji Maji Vijijini umefanyiwa mabadiliko na kuimarishwa zaidi katika Sheria hiyo.

**3. HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI**

**11. Mheshimiwa Spika**, Azimio Namba 64/292 la mwaka 2010 la Umoja wa Mataifa linatamka kuwa huduma ya maji na usafi wa mazingira ni haki ya msingi ya binadamu. Vilevile, lengo namba sita la Malengo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2015-2030 linaweka msisitizo wa upatikanaji wa huduma za maji safi na salama na usafi wa mazingira kwa wote. Uwepo wa rasilimali za maji za kutosha; miundombinu ya usambazaji maji na usafi wa mazingira; na uwezo wa kiuchumi wa kuwekeza na kuendesha huduma za maji ni masuala ya msingi na muhimu katika kufikia lengo hilo. Taarifa ya Maendeleo ya Maji Duniani iliyotolewa na Umoja wa Mataifa (*The United Nations World Water Development Report - 2019*) inaonesha kuwa zaidi ya watu **bilionti 2** duniani

wanaishi katika maeneo yenyе uhaba mkubwa wa maji. Vilevile, wakati mahitaji ya maji yanaongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, maeneo kame yameendelea kuwa kame zaidi na matukio ya mafuriko yanaongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na hali hiyo, zaidi ya watu **bilion 2.1** duniani hawapati maji safi na salama na kati ya hao, watu **milioni 844** hawapati huduma za msingi za maji ya kunywa.

**12. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Umoja wa Afrika (*The African Water Resources Priority Action Programme, 2016 - 2025*) ya mwaka 2016, katika Bara la Afrika zaidi ya watu **milioni 340** bado wanakosa huduma ya msingi ya maji ya kunywa na zaidi ya watu **milioni 547** hawana huduma za usafi wa mazingira. Hali hiyo inaonesha jitihada zaidi zinahitajika katika kuwekeza na kuendesha mindombinu ya huduma za maji kwa ajili ya kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma za majisafi na usafi wa mazingira ili kuendana na kasi ya mahitaji ya maji na malengo ya nchi na ya Umoja wa Mataifa.

### **3.1. HALI YA RASILIMALI ZA MAJI**

**13. Mheshimiwa Spika**, rasilimali za maji nchini hutegemea kiasi cha mvua kinachopatikana katika vipindi viwili vya masika na vuli. Maeneo mengi ya nchi yanapata mvua mara mbili kwa mwaka katika miezi ya Oktoba – Desemba na Machi - Mei. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya nchi yanapata mvua mara moja kwa mwaka kuanzia mwezi Desemba hadi Aprili. Kiwango cha wastani wa mvua kwa mwaka katika maeneo mengi nchini ni **milimita 900** hadi **milimita 1,200** wakati wastani wa mvua katika maeneo kame ya katikati ya nchi ni kati ya **milimita 400** hadi **milimita 550** kwa mwaka. Kwa upande wa maeneo yenyе mvua nyingi kama vile Nyanda za Juu Kusini na maeneo ya milima ya Usambara, kiasi cha mvua ni wastani wa **milimita 2,200** hadi **milimita 2,500** kwa mwaka.

**14. Mheshimiwa Spika**, kupitia taftishi zilizofanywa na Wizara wakati wa kuandaa Mipango Shirikishi ya Usimamizi

na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji nchini, inakadiriwa kuwa rasilimali za maji zinazofaa kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa **mita za ujazo bilioni 126** kwa mwaka. Kiwango hicho kinagawanyika katika sehemu kuu mbili, ambazo ni maji juu ya ardhi (**mita za ujazo bilioni 105**) na maji chini ya ardhi (**mita za ujazo bilioni 21**) kwa mwaka. Hifadhi hiyo ya maji inaonesha kuwa kiwango cha maji kilichopo kwa kila mtu kwa mwaka ni takribani wastani wa **mita za ujazo 2,300** ukilinganisha na wastani wa **mita za ujazo 1,700** ambacho ni kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa. Historia imeonesha kwamba kiasi cha maji kwa mtu kwa mwaka kimeendelea kupungua kutoka wastani wa **mita za ujazo 7,862** mwaka 1962 wakati nchi ikiwa na idadi ya watu **milioni 10.6** hadi kufikia wastani wa mita za ujazo **2,300** mwaka 2018 nchi ikiwa na idadi ya watu wapatao **milioni 54**. Hali hiyo imeonesha kuwa nchi yetu ipo juu ya mstari wa uhaba wa maji (*water stress*). Hivyo, hatua madhubuti zinahitajika kuchukuliwa ili nchi yetu isifikie kwenye hali ya uhaba wa maji.

**15. Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama vile majumbani, umwagiliaji, viwanda na mazingira ni wastani wa **mita za ujazo bilioni 40** kwa mwaka kati ya **mita za ujazo bilioni 126** kwa mwaka zilizopo. Vilevile, makadirio yameonesha kuwa mahitaji ya maji yataongezeka kufikia wastani wa **mita za ujazo bilioni 57** kwa mwaka ifikapo mwaka 2035. Hali hiyo inaonesha kuwa nchi yetu itaendelea kuwa na rasilimali za maji za kutosha kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, kutokana na mwenendo wa kuongezeka kwa mahitaji ya maji nchini, ni muhimu nchi yetu ikaendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maji ili Taifa lisikumbwe na uhaba wa maji katika siku za usoni.

### **3.2. HALI YA HUDUMA ZA UBORA WA MAJI**

**16. Mheshimiwa Spika**, maji safi na salama ni hitaji muhimu kwa maisha ya viumbe hai na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika kutekeleza Sera ya Maji ya Taifa ya mwaka 2002, Wizara ina jukumu la kuhakiki ubora na usalama wa

maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya kusambaza maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira. Uhakiki wa ubora wa maji hufanyika kupitia maabara 16 za ubora wa maji zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini. Lengo ni kubaini hali halisi ya mwenendo wa ubora maji na kuchukua hatua stahiki pale ambapo ubora wa maji utabainika kutokidhi viwango. Maabara hizo huhakiki ubora wa maji kwa kufanya uchunguzi wa kibaiolojia, kikemia pamoja na kifizikia katika maji.

**17. Mheshimiwa Spika**, ufuatiliaji na utafiti wa ubora wa maji uliofanyika nchini unaonesha hali ya ubora wa maji kutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Kutofautiana huko kunatokana na hali ya miamba ya asili, shughuli za kibinadamu, jiografia ya eneo na mabadiliko ya tabianchi. Changamoto zilizobainishwa katika utafiti huo ni pamoja na kuwepo kwa viwango vikubwa vya *Nitrogen*, *Phosphorous* na tope (*turbidity*) kwenye maji juu ya ardhi vinavyosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji. Vilevile, kwa upande wa maji chini ya ardhi changamoto ni uwepo wa kiwango kikubwa cha chumvichumvi, *Nitrate*, madini ya *Flouride*, Chuma, *Manganese* na *Chloride*. Pamoja na changamoto hizo, hali ya ubora wa maji katika vyanzo inaridhisha na vyanzo hivi vinaweza kuendelezwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali baada ya kutibiwa na kuwa salama kulingana na matumizi yaliyokusudiwa.

### **3.3. HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA**

**18. Mheshimiwa Spika**, hali ya huduma ya maji nchini huangaliwa kwa kuzingatia miundombinu ya maji iliyopo na idadi ya watu wanaopata huduma ya maji. Kwa upande wa vijijini, kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama hukokotolewa kwa kuangalia idadi ya vituo vya kuchotea maji vinavyofanya kazi. Kwa maeneo ya mijini, kiwango hicho hukokotolewa kwa kuangalia idadi ya wateja walionunganishwa kwenye mtandao wa maji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Hali halisi ya huduma za

usambazaji maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini ni kama ifuatavyo:-

### *3.3.1. Huduma ya Maji Vijijini*

**19.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza miradi ya maji vijijini kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao. Lengo ni kufikia **asilimia 85** ya wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2020. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya miradi ya maji **1,659** yenyе vituo vya kuchotea maji **131,370** imejengwa. Kati ya vituo vilivyojengwa, vituo **86,780** vinafanya kazi na vina uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **25,359,290** sawa na **asilimia 64.8** ya wananchi waishio vijijini.

### *3.3.2. Huduma ya Maji Mijini*

**20.** **Mheshimiwa Spika**, huduma ya maji katika maeneo ya mijini hutolewa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa. Mamlaka hizo zimeendelea kutekeleza miradi ya maji kwa kujenga, kukarabati na kufanya upanuzi wa miundombinu ya majisafi katika maeneo ya miji hiyo. Malengo ya Serikali ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa kufikia **asilimia 95**; na Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa kufikia **asilimia 90** ifikapo mwaka 2020. Kwa upande wa huduma ya uondoaji wa majitaka, lengo la Serikali ni kuongeza huduma hiyo kufikia **asilimia 30** ifikapo mwaka 2020.

**21.** **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa ni **asilimia 80** na kwa Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa upatikanaji wa huduma hiyo ni **asilimia 64. Kiambatisho Na.**

1 kinaonesha hali ya huduma ya maji inayotolewa na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini.

22. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa huduma ya uondoaji majitaka katika maeneo ya mijini, hadi mwezi Aprili 2019, huduma hiyo imefikia wastani wa **asilimia 20** kwenye miji yenye mtandao wa majitaka. Miji hiyo ni Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa. Katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao huo, huduma ya majitaka hutolewa na magari maalum ya majitaka na kuyatirisha kwenye mabwawa ya majitaka.

#### **3.4. UWEZO WA KITAASISI**

23. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kujenga uwezo wake wa kitaasisi pamoja na Taasisi zinazotekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika kutekeleza jukumu hilo Wizara hutoa mafunzo, vitendea kazi pamoja na kujenga ofisi. Kwa upande wa rasilimali watu, sekta ya maji ina watumishi **6,377** ambaao wamejiriwa katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde na Makao Makuu ya Wizara.

### **4. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2018/2019 NA MALENGO YA MWAKA 2019/2020**

#### **4.1. UPATIKANAJI WA FEDHA**

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Fungu 49 – Wizara ya Maji iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 697,577,902,677** na katи ya fedha hizo **Shilingi 24,363,869,000** zilikuwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 673,214,033,677** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya **Shilingi 16,653,542,964.15** sawa na **asilimia 68** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na katи ya hizo, **Shilingi 2,905,702,353.15** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi 13,747,840,611** ni fedha za mishahara. Vilevile, **Shilingi**

**343,486,935,592.46** sawa na **asilimia 51** ya fedha za maendeleo zilipokelewa.

**4.2. UTEKELEZAJI WA MIRADI NA PROGRAMU MBALIMBALI KATIKA MWAKA 2018/2019 NA MALENGO YA MWAKA 2019/2020**

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, sekta ya maji imeendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali zinazolenga kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; ufuutiliaji wa ubora wa maji; kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini; na kutekeleza masuala mtambuka. Utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 na mpango wa mwaka 2019/2020 umeelezwa kwa kina kama ifuatavyo:-

**4.2.1. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**26. Mheshimiwa Spika**, Wizara ina jukumu la kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini kupitia Bodi za Maji za Mabonde. Rasilimali hizo zinajumuisha maji yaliyomo ndani ya nchi na maji shirikishi (*transboundary waters*) ambayo usimamizi wake unafanyika kwa kushirikiana na nchi na Taasisi mbalimbali za kikanda na kimataifa. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji umegawanyika katika maeneo ya tathmini na ufuutiliaji wa rasilimali za maji; ugawaji wa maji kwa matumizi mbalimbali; uhifadhi na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji; uendelezaji wa rasilimali za maji; na ushirikiano katika usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi. Hatua zilizofikiwa katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji ni kama ifuatavyo:-

**4.2.1.1. Tathmini na Ufuutiliaji wa Rasilimali za Maji**

**(a) Mwenendo wa Rasilimali za Maji**

**27. Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa takwimu sahihi na za muda mrefu za rasilimali za maji ni muhimu katika kuiwezesha Serikali kutoa taarifa sahihi za hali ya maji nchini; kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya ukame na mafuriko;

pamoja na kuibua na kusanifu miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Wizara imeendelea kuratibu na kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji kwa kutumia mifumo ya ukusanyaji wa takwimu. Takwimu hizo husaidia kutambua wingi na ubora wa rasilimali za maji zilizopo kwa sasa na baadaye ili kuzisimamia na kuziendezea kwa ufanisi.

**28. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde imeendelea kukusanya takwimu za mvua, hali ya hewa, mtiririko wa maji katika mito; kina cha maji katika maziwa na mabwawa; kiasi cha tope (*sediment*) katika mito, maji chini ya ardhi na ubora wa maji kupitia mifumo mbalimbali. Vilevile, Wizara imefanya tathmini ya hali ya mtandao wa vituo vya kukusanya takwimu za mwenendo wa maji; pamoja na kujenga kituo **kimoja** cha kufuatilia mwenendo wa maji mitoni katika Bonde la Mto Pangani; kukarabati vituo **vitatu** katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini na vituo **vitatu** katika Bonde la Rufiji; na kufunga mfumo wa kukusanya takwimu unaojiendesha wenyewe (*data loggers*) katika vituo **vinane** kwenye Bonde la Mto Rufiji na vituo **viwili** Bonde la Mto Pangani.

**29. Mheshimiwa Spika**, kutokana na takwimu zilizokusanya katika mwaka wa kihaidrolojia; Novemba 2017 – Oktoba 2018, hali ya maji katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika, Nyasa na Rukwa; mabwawa ya Mtera, Kihansi, Kidatu, Nyumba ya Mungu na Mindu; na mito ya Pangani, Ruvuma, Malagarasi, Wami, Ruvu, Rufiji, Mara na Kagera ilikuwa juu ya wastani ikilinganishwa na mwaka uliopita (**Kiambatisho Na. 2** kinaonesha kiwango cha maji katika maziwa, mito na mabwawa mbalimbali nchini). Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya kukusanya takwimu za rasilimali za maji ili kupata takwimu sahihi na kwa wakati ikiwemo kutoa taarifa za uhakika za hali ya rasilimali za maji na tahadhari ya mafuriko (*Flood Early Warning System*) nchini.

**(b) Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima**

**30. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchimbaji holela wa visima vya maji, Wizara huratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima. Vilevile, Bodi za Maji za Mabonde zimepewa mamlaka ya kuratibu na kutoa vibali vya uchimbaji wa visima katika maeneo mbalimbali nchini. Lengo ni kuhakikisha misingi ya kitaalam inafuatwa katika uchimbaji wa visima kwenye maeneo husika. Hadi mwezi Aprili 2019, leseni mpya **13** za uchimbaji visima zimetolewa na leseni **29** zimehuishwa. Aidha, vibali **827** vya kuchimba visima vya maji katika maeneo mbalimbali nchini vilitolewa ambapo visima **105** vimechimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na visima **812** vimechimbwa na kampuni binafsi. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kusimamia udhibiti wa uchimbaji holela wa visima vya maji na kutoa vibali stahiki.

**(c) Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji na Udhibiti wa Migogoro**

**31. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde ina jukumu la kusimamia ugawaji wa maji kwa uwiano sahihi kwa watumiaji kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Kanuni za rasilimali za maji. Kufuatia ongezeko la idadi ya watu na kukua kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, mahitaji ya maji yameongezeka, hivyo ni muhimu ugawaji wa rasilimali hiyo ukaratibiwa. Uratibu huo hutekelezwa kwa kutumia mfumo madhubuti unaowezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani na sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, viwanda, mazingira, madini, utalii, uvuvi na mifugo.

**32. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Bodi hizo kwa kushirikiana na Jumuiya za Watumiaji Maji zimekuwa zikidhibiti migogoro ya matumizi ya maji katika maeneo yao. Katika mwaka 2018/2019, Bodi za Maji za Mabonde zimetoa vibali **116** vya matumizi ya maji. Aidha, ukaguzi wa vibali vya kutumia maji ulifanyika ambapo watumia maji **350** walibainika kutokuwa na vibali. Vilevile, elimu kuhusu matumizi bora ya maji yanayozingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za rasilimali za maji

ilitolewa kwa watumiaji hao. Utoaji wa elimu hiyo umeleta matokeo chanya ambapo maombi **851** ya vibali vyatatu za matumizi ya maji vimepokelewa na viro katika hatua mbalimbali za kupewa vibali. Aidha, jumla ya migogoro **22** ya matumizi ya maji imeripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini ambapo migogoro **11** imetatuliwa na utatuzi wa migogoro mingine **11** upo katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde ili kuziwezesha kutoa vibali **600** vyatatu za matumizi ya maji na kudhibiti migogoro ya maji.

#### **4.2.1.2. Uhifadhi na Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji**

##### **(a) Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji**

**33. Mheshimiwa Spika**, uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira unaotokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu umekuwa ni changamoto katika kulinda na kuhifadhi vyanzo hivyo vya maji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, hadi mwezi Aprili 2019, Wizara imeweeka mipaka kwenye vyanzo vya maji **sita** katika Bodi za Maji za Mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini chanzo **kimoja**; Wami-Ruvu (**kimoja**), Rufiji (**viwili**) na Pangani vyanzo **viwili**. Aidha, katika Bonde la Mto Pangani, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilianisha vyanzo **227** kwa ajili ya uhifadhi. Vyanzo **10** kati ya hivyo viliwekwa katika mpango wa kuwekewa mpaka na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Kati ya hivyo, vyanzo **vitatu** vyachemchemi za Teema, Magadirisho na eneo la Tindiga - Kiwawa, viliwekewa mipaka ya nguzo na kupandwa miti **3,000**. Vilevile, katika Bonde la Ruvuma, chanzo cha maji cha Magumichila ambacho kinahudumia Mji wa Masasi kiliwekewa mipaka. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imepanga kutangaza vyanzo **45** kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji.

**34. Mheshimiwa Spika**, aidha, Wizara imeendelea na jitihada za kuishirikisha jamii katika kuhifadhi vyanzo vya maji kwa kuziimarisha Jumuia za Watumiaji Maji kuititia mafunzo mbalimbali ya kuzijengea uwezo kwa vitendo na warsha. Hadi

mwezi Aprili 2019, Jumuiya za Mgolole, Ngerengere Juu B, Mbezi, Ngerengere Chini, Miyombo, JUWABOMA na JUWAMURU kutoka Bodi ya Maji Bonde la Wami-Ruvu; na Lumeme Kaskazini na Lumeme Kusini katika Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Pangani zilijengewa uwezo kwa kupewa mafunzo kuhusu Sera ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009. Vilevile, Wizara imetoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa wananchi wa vijiji vya Gawaye na Chihanga ambavyo vinapakana na chanzo cha maji cha Makutupora ambacho ni chanzo muhimu cha maji kwa Jiji la Dodoma.

**(b) Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyano vya Maji**

**35. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchafuzi wa vyano vya maji, Wizara hufanya ukaguzi wa uharibifu wa mazingira katika vyano vya maji na ubora wa majitaka yanayotirishwa kwenye vyanzo hivyo. Hadi mwezi Aprili 2019, Wizara imefanya ukaguzi katika viwanda **vitano** katika Bonde la Pangani, viwanda **viwili** katika Bonde la Kati, migodi **miwili** ya dhahabu na viwanda **viwili** katika Bonde la Rukwa. Vilevile, ukaguzi na udhibiti wa uchafuzi wa vyano vya maji umefanyika katika mgodi **mmoja** Mkoani Geita na mgodi **mmoja** Mkoani Mara. Aidha, ukaguzi wa vyano vya maji katika Bonde la Ziwa Tanganyika ulifanyika katika mabwawa ya Igombe na Kazima yanayotoa huduma ya maji katika Manispaa ya Tabora. Katika maeneo yaliyokaguliwa, matokeo yameonesha kuwa majitaka yanayorudishwa kwenye baadhi ya vyano vya maji yanakidhi viwango. Katika maeneo mengine ambayo matokeo ya ukaguzi yaliyoonesha kuwa na uchafuzi wa mazingira; watusika walipewa elimu na maelekezo ya kufanya shughuli za kibinadamu nje ya eneo la hifadhi ya vyano vya maji.

Vilevile, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde imetoa vibali vya muda **11** vya kutiririsha majitaka na kusajili maombi **manane** ya vibali vya kutiririsha majitaka ambayo yako katika hatua mbalimbali za kupewa vibali. Ili kuhakikisha uhifadhi wa vyano vya maji, Wizara kupitia Bodi ya Maji ya Bonde la Wami-Ruvu iliendesha warsha kuhusu usimamizi wa majitaka

kwa Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania. Katika warsha hiyo, pamoja na mambo mengine, Wizara iliwaelekeza wamiliki wa viwanda kuwa na vibali vya kutiririsha majitaka na viwanda visivyokuwa na vibali hivyo viwasilishe maombi ya vibali. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea na jitihada za kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

**(c) Mradi wa Kunusuru Vyanzo vya Maji Kupitia  
Mpango Endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi  
Katika Mabonde Madogo ya Mto Zigi na Mto Ruvu**

**36. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kuhifadhi vyanzo vya maji katika Mabonde ya Wami-Ruvu na Pangani unaolenga kuzijengea uwezo Taasisi kwa ajili ya kuboresha shughuli za kuratibu rasilimali za maji. Katika Bonde la Wami-Ruvu, mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Morogoro na Mvomero na unalenga kuhifadhi mazingira ya Mto Ruvu. Kwa upande wa Bonde la Pangani mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Muheza, Mkinga, Korogwe na Jiji la Tanga katika Mto Zigi. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) pamoja na Mfuko wa Mazingira Duniani (*Global Environment Facility - GEF*) kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 27.65**. Hadi mwezi Aprili 2019, **vituo viwili (2)** vya kukusanya taarifa za hali ya hewa vimejengwa kwenye Bonde Dogo la Mto Zigi. Vilevile, Halmashauri za Wilaya tano ambazo ni Muheza, Mkinga, Korogwe, Morogoro na Mvomero zimewezeshwa kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi na kujengewa uwezo katika utekelezaji wa mipango hiyo na uandaaji wa mipango mingine. Aidha, klabu **36** za uhifadhi wa mazingira zimeanzishwa katika shule za msingi na sekondari.

**37. Mheshimiwa Spika,** vilevile, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga, Ofisi ya Bodi ya Maji ya Bonde la Mto Pangani na Wilaya ya Muheza mradi umekamilisha ujenzi wa mtandao wa kusambaza maji wenye urefu wa **kilomita 6** katika vijiji **vitatu** vya Mashewa, Shembekeza na Kimbo unaowanufaisha wananchi wapatao

5,400; ujenzi wa banio (*intake*) la kuchukulia maji kutoka kwenye chanzo na kusambazwa kwenye vijiji vya Tangeni na Mnyanza katika Wilaya ya Mvomero; na ujenzi wa mabirika **matatu** ya kunyweshea mifugo katika Wilaya za Muheza, Mkinga na Tanga Jiji. Aidha, utekelezaji wa mradi huo umesaidia kupungua kwa tope katika Bonde dogo la Mto Ruvu na Mto Zigi; kuhifadhi **hekta 353** katika Wilaya ya Muheza na Morogoro; pamoja na kurejesha uoto wa asili katika vyanzo vya maji baada ya kutenga ardhi kwa ajili ya kilimo, malisho na mapito ya mifugo.

**38. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi kwa kuunda na kuziimarisha Jumuiya **11** za Watumiaji Maji; kuziwezesha Jumuiya **mbili** za Watumiaji Maji kujenga ofisi, kutoa mafunzo na vitendea kazi; kununua vifaa vya kupima mwenendo wa maji na hali ya hewa; kuweka mipaka kwenye eneo la Bwawa la Mabayani; kuanza ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika vijiji vya Mnyanza na Tangeni; kujenga miundombinu ya kuvuna maji ya mvua katika Shule ya Msingi Ubiri iliyopo Wilayani Korogwe; kutoa elimu na kuanzisha mashamba darasa kwa wakulima; kujenga mabirika **matatu** ya kunyweshea mifugo katika Wilaya za Mvomero na Morogoro; na ununuzi wa ng'ombe **20** wa maziwa na madume bora **20** kwa ajili ya uzalishaji.

#### *4.2.1.3. Uendelezaji wa Rasilimali za Maji*

##### **(a) Utafutaji wa Vyanzo Vipya vya Maji**

**39. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde na Halmashauri mbalimbali nchini imeendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji yakiwemo maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa. Lengo ni kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma ya maji nchini. Katika mwaka 2018/2019, Wizara ilifanya utafiti kwenye maeneo **91** yanayofaa kuchimbwa visima katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini **31**, Ziwa Victoria maeneo **22**, Rufiji **10**, na Bonde la Kati maeneo **28**.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Oman itachimba visima **100** kwa ajili ya kusambaza maji katika shule za sekondari na msingi. Katika kufikia azma hiyo, maeneo **98** katika shule za msingi **58** na sekondari **40** yalifanyiwa utafiti kwa ajili ya kuchimba visima. Idadi ya maeneo hayo katika Bodi za Maji za Mabonde ni: Ruvuma na Pwani ya Kusini maeneo **12**, Wami-Ruvu (**10**), Ziwa Victoria (**19**), Bonde la Kati (**16**), Ziwa Tanganyika (**15**), Rufiji (**10**), Ziwa Nyasa (**1**), Ziwa Rukwa (**9**) na Pangani maeneo **nane (8)**. Maeneo hayo yako katika Mikoa **23** na Halmashauri **96** nchini. Aidha, maeneo **mawili (2)** yaliyoko katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini ambayo utafiti haukuonesha uwezekano wa kuwa na maji chini ya ardhi, itajengwa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua. Gharama zilizokadiriwa kwa kazi ya kuchimba visima ni **Shilingi bilioni 2.73**. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuvitambua vyanzo vya maji na kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo mengi zaidi ili kuongeza upatikanaji wa maji nchini.

**(b) Ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati**

**40. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa maji nchini, Serikali imepanga kujenga mabwawa ya kimkakati kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa maji katika kipindi chote cha mwaka. Mabwawa hayo yanayopangwa kujengwa ni Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro) na Ndembera (Iringa). Bwawa la Farkwa litatumika kwa ajili ya usambazaji maji katika Jiji la Dodoma na Wilaya za Chemba na Bahi; pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Bwawa la Kidunda litatumika kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruvu unakuwa na maji katika kipindi chote cha mwaka; kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa umeme; na Bwawa la Ndembera litatumika kwa ajili ya kuhakikisha Mto Ruaha unakuwa na maji katika kipindi chote cha mwaka na uzalishaji wa umeme. Hadi mwezi Aprili 2019, usanifu wa barabara ya mchepuko kutoka Dodoma kuelekea Kwa Mtoro – Kondoa kupisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa na Tathmini ya Athari za Kijamii na Kimazingira imefanyika. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa mabwawa hayo ikiwa ni pamoja na fedha kwa ajili ya

ukarabati wa mabwawa mengine ya kimkakati ya Itobo wilayani Nzega na Enguikumet II wilayani Monduli.

**(c) Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**41. Mheshimiwa Spika**, uandaaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji (*Integrated Water Resources Management and Development Plans – IWMDP*) ni hitaji la kisheria linalolenga kusimamia rasilimali za maji kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Kwa sasa, mipango shirkishi ya Mabonde ya Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Mto Rufiji na Bonde la Kati imekamilika. Kati ya mabonde hayo, Bonde la Mto Rufiji limekamilisha Tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii (*Strategic Environmental and Social Assessment-SESA*) na kuanza utekelezaji wake. Kwa mabonde yaliyobaki, taratibu za kuanza kufanya SESA zinaendelea. Aidha, uandaaji wa Mpango katika Bonde la Wami-Ruvu unaendelea na Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya kazi (*interim report*). Kwa upande wa Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Victoria na Mto Pangani, Wizara inaendelea na hatua za awali za maandalizi ya mipango hiyo. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuanza kufanya Tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii, kukamilisha Mpango wa Bonde la Wami-Ruvu na kuanza uandaaji wa mipango hiyo katika Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Victoria na Mto Pangani.

**(d) Uanzishwaji wa Majukwaa ya Wadau wa Maji**

**42. Mheshimiwa Spika**, usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji unahitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali ambao ndio watumia maji na wasimamizi wa kwanza wa rasilimali hizo. Kwa kutambua umuhimu huo, katika mwaka 2016, Wizara ilianzisha Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa Sekta Mtambuka katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji (*National Multi-Sectoral Water Resources Management Forum*) ambalo linajumuisha Wataalam wa Maji, Taasisi za Maji za Umma na Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti, Bodi za Maji za Mabonde, Wizara za Kisekta, Washirika wa Maendeleo na Waandishi wa Habari.

Aidha, katika mwaka 2018/2019, majukwaa mapya yalianzishwa katika Bodi za Maji za Mabonde ya Wami-Ruvu, Ziwa Victoria na Mto Rufiji pamoja na Vidaka Maji vya Mto Songwe, Mto Lwiche, na Mto Katuma katika Bonde la Ziwa Rukwa; Mto Kiwira na Mto Ruhuhu katika Bonde la Ziwa Nyasa. Malengo ya majukwaa hayo ni kujadili na kuzitafutia ufumbuzi changamoto za usimamizi wa rasilimali za maji zikiwemo mgawanyo wa rasilimali za maji, uhifadhi wa vyano vya maji, mabadiliko ya tabianchi na migogoro ya maji pamoja na kuhamasisha wadau kushiriki katika utekelezaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Mapendekezo yanayotolewa katika majukwaa hayo, huchukuliwa na Wizara na yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuanzisha majukwaa ya wadau katika ngazi za Bodi za Maji za Mabonde na Vidaka Maji.

#### *4.2.1.4. Uimarishaji wa Taasisi zinazosimamia Rasilimali za Maji*

##### **(a) Kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde**

43. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Bodi za Maji za Mabonde zinasimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini kwa ufanisi, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Bodi hizo kwa kujenga na kukarabati ofisi, ununuzi wa vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi. Hadi mwezi Aprili 2019, ujenzi wa ofisi za Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini umefikia **asilimia 90**, Ziwa Rukwa (**65**); Ziwa Nyasa - ofisi ndogo za Songea na Njombe (**50**); na Bonde la Kati umefikia **asilimia 95**. Vilevile, ujenzi wa ofisi ya Bodi ya Maji, Bonde la Wami-Ruvu na ofisi ya Jumuiya ya Watumiaji Maji Msowero; pamoja na ukarabati wa ofisi ndogo za Wami-Ruvu zilizoko Dodoma umeanza; ukarabati wa ofisi ya Bodi ya Maji, Bonde la Mto Rufiji na ujenzi wa ofisi za Jumuiya za Watumiaji Maji Kimani na Mkoji upo katika hatua za awali. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (*USAID*) wanaotekeleza mradi wa Mpango Jumuishi wa Uendelezaji wa Rasilimali za Maji (*Water Resources Integration Development Initiative-WARIDI*) katika Mabonde ya Mto Rufiji

na Wami-Ruvu imetoa vifaa vya upimaji wa rasilimali za maji kwa Mabonde hayo vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 2.35**.

**44. Mheshimiwa Spika**, Aidha, Wizara imeunda Bodi mpya za usimamizi (*Executive Boards*) katika Bodi za Maji za Mabonde ya Mto Pangani, Mto Wami-Ruvu, Mto Rufiji, Mto Ruvuma, Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Bonde la Kati ambazo zilimaliza muda wake. Vilevile, Wizara imeunda Bodi mpya ya Taifa ya Maji baada ya Bodii iliyokuwepo kumaliza muda wake. Bodi hiyo mpya pamoja na zile za Mabonde zilizoundwa zimejengewa uwezo ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde kwa kuzipatia mafunzo na vitendea kazi.

**(b) Mradi wa Kuimarisha Taasisi Zinazosimamia Rasilimali za Maji**

**45. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji katika Bodi za Maji za Mabonde, Serikali inatekeleza mradi wa kutunza na kuendeleza vyanzo vya maji kuititia mradi wa *Water Sector Support Project - WSSP II* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 50**. Mradi huo unatekelezwa katika Mabonde ya Wami-Ruvu, Rufiji na Pangani. Hadi mwezi Aprili 2019, Bodi ya Maji ya Bonde la Wami-Ruvu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imetenga maeneo **matatu** kwa ajili ya kujenga mabirika **matano** ya kunyweshea mifugo ili kuzuia mifugo kuharibu vyanzo vya maji; pamoja na uundaji na uelimishaji wa vikundi vya wafugaji. Vilevile, kuititia mradi huo, Bonde la Wami-Ruvu lilifanya tathmini ya mahitaji ya kuanzisha Jumuiya za Watumia Maji **10** ambapo kazi inayoendelea kwa sasa ni uundaji wa Jumuiya **nne** ambazo ni Jumuiya za Watumia Maji za Mgeta Juu A, Mgeta Juu B, Mgeta Chini na Mtombozi.

**(c) Ukusanyaji wa Maduhuli**

**46. Mheshimiwa Spika**, maduhuli yanayokusanywa na Bodi za Maji za Mabonde kutokana na ada za maombi ya

vibali mbalimbali na matumizi ya maji pamoja na faini hutumika kwa ajili ya kusimamia, kutunza na kuendeleza rasilimali za maji katika mabonde husika. Lengo ni kuzimarissha Bodii hizou ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hadi mwezi Aprili 2019, **Shilingi bilioni 3.69** zilikusanywa ambazo ni sawa na **asilimia 83** ya lengo la **Shilingi bilioni 4.44** zilizopangwa kukusanywa katika mwaka 2018/2019. Katika mwaka 2019/2020, Bodii za Maji za Mabonde zimepanga kukusanya **Shilingi bilioni 5.4** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato. **Kiambatisho Na. 3** kinaonesha mchanganuo wa maduhuli yaliyokusanywa na Bodii za Maji za Mabonde kwa mwaka 2018/2019 na makadirio ya mwaka 2019/2020. Katika kuendeleza usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji, Wizara imefanya taftishi ya namna ya kuongeza vyanzo vya mapato (*study on financing options for water resources management interventions*). Taarifa ya mwisho imeshawasillshwa na utekelezaji wake utaanza mwaka 2019/2020.

#### **4.2.1.5. Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi**

**47. Mheshimiwa Spika**, kihaidrolojia, nchi yetu ni sehemu ya mabonde matatu makubwa ya maji katika Bara la Afrika, ambayo ni Bonde la Mto Nile unaoanza Ziwa Victoria na kumwaga maji katika Bahari ya Mediterania; Bonde la Mto Zambezi unaomwaga maji Bahari ya Hindi; na Bonde la Mto Kongo unaomwaga maji Bahari ya Atlantiki. Vilevile, mabonde saba kati ya tisa yaliyopo nchini ni ya maji shirkishi; mabonde hayo ni Pangani, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Nyasa, Rukwa, Tanganyika, Bonde la Kati na Victoria. Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa takriban **asilimia 43.4** ya rasilimali za maji nchini ni za majishirikishi na zinajumuisha maziwa ya Tanganyika, Victoria, Nyasa, Natron, Chala na Jipe pamoja na mito ya Kagera, Mara, Malagarasi, Momba, Mwiruzi, Umba, Ruvuma na Songwe.

**48. Mheshimiwa Spika**, usimamizi wa rasilimali za majishirikishi una changamoto zinazotokana na masuala ya siasa za maji (*hydro - politics*) na matumizi yasiyowiana ya majishirikishi. Hali hiyo inahitaji maelewano na makubaliano baina ya nchi

washirika katika kushirikiana kusimamia rasilimali za majishirikishi. Ushirikiano huo unahusisha nchi nane majirani ambazo ni Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Uganda, Malawi, Msumbiji na Zambia. Nchi nyingine tunazoshirikiana nazo ni Angola, Botswana, Ethiopia, Misri, Namibia, Sudan, Sudan Kusini, Zimbabwe na nchi ya Eritrea ambaye ni mtazamaji chini ya ushirikiano wa nchi zilizo katika Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*).

**49.** **Mheshimiwa Spika**, ushirikiano wa usimamizi wa rasilimali za majishirikishi unahusisha kuunda na kuendesha Taasisi za kikanda na kimataifa za kusimamia rasilimali za maji. Ushirikiano wa kitaasisi na nchi hizo unatekelezwa kama ifuatavyo:-

(a) **Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria**

**50.** **Mheshimiwa Spika**, Tanzania inashirikiana na nchi za Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda katika kuandaa Awamu ya Tatu ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Project – LVEMP*). Hadi mwezi Aprili 2019, kazi zilizotekelozwa ni pamoja na kuandaa andiko la mradi; kufanya tafiti mbalimbali za kusaidia maandalizi ya mradi; kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Taasisi na wananchi watakaonufaika; kuainisha kazi zitakazotekelozwa na mradi; na kukamilisha machapisho na miongozo mbalimbali ya mradi.

**51.** **Mheshimiwa Spika**, mradi unalenga kusimamia na kulinda mazingira ya Ziwa Victoria hususan katika kuimarisha Taasisi za usimamizi wa rasilimali za ziwa ikiwemo maji na samaki; ukusanyaji wa takwimu za mazingira, kubuni na kutekeleza hatua mbalimbali za kuzuia uchafuzi katika ziwa ikiwemo kupanua mifumo ya majitaka mijini, kuzuia uchafuzi toka maeneo ya kilimo na mifugo, kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kudhibiti na kuondoa gugumaji katika Ziwa Victoria, kufanya utafiti wa aina mbalimbali katika maeneo muhimu ya mazingira na kutekeleza miradi ya kijamii inayolenga kuongeza kipato na kuhifadhi mazingira katika eneo la Mto Simiyu na maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria. Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na utagharimu

**Dola za Marekani milioni 60.** Mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa baada ya taratibu za kupata fedha kukamilika.

**(b) Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe**

52. **Mheshimiwa Spika**, nchi za Malawi na Tanzania ziliridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe (*Songwe Convention*) ulioanza kutekelezwa mwezi Julai, 2018. Kamisheni inayosimamia programu ya kuendeleza Bonde hilo ilizinduliwa tarehe 11 Machi, 2019. Miradi itakayotekelawa kuititia Kamisheni hiyo ni pamoja na ujenzi wa mabwawa makubwa matatu; miundombinu ya umwagiliaji na ya kusambaza maji; na kupunguza athari za mafuriko. Serikali za Tanzania na Malawi zinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. Aidha, mradi wa utunzaji wa mazingira ya Mto Songwe utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 6.4** ambazo zitatolewa na *Global Environment Facility (GEF)* upo katika hatua za awali za maandalizi. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kushirikiana na Serikali ya Malawi kwa ajili ya kuimarisha Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe na kutekeleza miradi iliyopangwa.

**(c) Bonde la Mto Zambezi**

53. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mwanachama wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM*) ambayo ina jukumu la kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji za Bonde la Mto Zambezi. Nchi nyingine wanachama ni Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zambia na Zimbabwe. Katika mwaka 2018/2019, Tanzania imeshiriki katika uandaaji wa Mpango Mkakati wa Bonde la Mto Zambezi wa mwaka 2019 – 2030 ambapo nchi yetu inanufaika na miradi ya kusambaza maji iliyopo mpakanii na nchi za Malawi na Zambia katika miji ya Nakonde (Zambia), Tunduma (Tanzania), Kasumulu (Tanzania) na Songwe (Malawi). Aidha, katika kipindi cha mwezi Februari 2018 hadi mwezi Februari 2019, Tanzania ilikuwa mwenyekiti wa ZAMCOM na mwenyeji wa mkutano wa sita wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa ZAMCOM uliofanyika tarehe 28 Februari, 2019 Jijini Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulipitisha

mpango mkakati wa bonde hilo na Tanzania ilikabidhi uenyekiti kwa nchi ya Zambia. Vilevile, mfumo wa kanzidata utakaotumika kuhifadhi takwimu za rasilimali za maji na kufanya utabiri wa hali ya maji umekamilika na umeanza kutumika katika Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa.

(d) **Mkutano wa Kamati ya Mawaziri wa Utangamano wa Uchumi wa Kikanda wa Nchi za SADC**

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 19 wa Kamati ya Mawaziri wa Utangamano wa Uchumi wa Kikanda wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*Southern African Development Community- SADC*) uliofanyika Jijini Pretoria nchini Afrika ya Kusini tarehe 18 hadi 23 Julai 2018. Kupitia mukutano huo, hali halisi ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya miundombinu ikiwemo ya maji ilijadiliwa. Katika mukutano huo, jumla ya miradi **44** ya miundombinu itakayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika ilipitishwa na kati ya hiyo, Tanzania itanufaika na Mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi; Mradi wa Umwagiliaji wa Bonde la Mto Ruhuhu (Tanzania); Mradi wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Makonde (Tanzania na Msumbiji); na Mradi wa Usambazaji wa Maji wa Nakonde - Tunduma (Tanzania na Zambia). Vilevile, kupitia Idara ya Maji ya *SADC*, Wizara itanufaika na Awamu ya Nne ya Mradi wa Ufutiliaji wa Taarifa za Maji (*Hydrological Cycle Observing System – HYCOS/M*). Lengo la mradi huo ni kutoa taarifa za maji na mafuriko kwa wakati.

(e) **Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (AMCOW)**

55. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri 55 wa Maji wa Afrika (*African Ministers' Council on Water - AMCOW*) ambalo lina jukumu la kushughulikia masuala ya maji katika nchi za Afrika. Katika kipindi cha mwaka 2016 hadi 2018, Tanzania ilikuwa mwenyekiti wa *AMCOW*na ilishiriki katika Mkutano wa 11 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika na Wiki ya Maji ya Afrika iliyo fanyika Libreville, Gabon mwezi Oktoba 2018. Hata hivyo, mukutano huo

haukukamilika na uliendelea tena mwezi Februari, 2019 Jijini Kigali, Rwanda. Katika mkutano huo, pamoja na masuala mengine yallyojadiliwa, ulipitisha Mkakati wa Maji wa *AMCOW* wa mwaka 2018 – 2030. Mkakati huo unalenga kuisaidia *AMCOW* kufikia malengo yake ya kuhakikisha utu wa Mwfrika unaheshimika kwa kuwa na huduma za uhakika za majisafi na usafi wa mazingira; na kuendeleza, kusimamia na kutumia rasilimali za maji kwa ajili ya uhakika na usalama wa chakula na nishati Barani Afrika. Kuanzia mwezi Februari 2019, Tanzania imekuwa mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Maji wa Afrika (*African Water Facility - AWF*) ambao umeanzishwa na *AMCOW* kwa lengo la kugharamia miradi ya maji na usafi wa mazingira barani Afrika. Mfuko huo unasimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank - AfDB*).

(f) **Mikutano ya Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile**

**56. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 26 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile (*Nile Council of Ministers - NILECOM*) uliofanyika Bujumbura-Burundi tarehe 13 Agosti 2018. Wizara pia ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 21 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Bonde la Mto Nile Ukanda wa Maziwa Makuu (*Nile Equatorial Lakes Council of Ministers' - NELCOM*) uliofanyika tarehe 22 Novemba, 2018 Jijini Dar es Salaam. Mikutano hiyo ilisisitiza nchi wanachama kuongeza ushirikiano katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kama vile mradi wa kufua umeme kwa nguvu za maji wa Rusumo ambao unajumuisha nchi za Burundi, Rwanda na Tanzania. Mradi huo utazalisha **megawati 80** za umeme ambapo Tanzania itapata **megawati 27** zitakazoongezwa kwenye Gridi ya Taifa. Umeme huo utawanufaisha wakazi wapatao **450,000** katika Wilaya za Ngara, Karagwe na Biharamulo. Faida nyingine ambazo Tanzania itapata kupitia utekelezaji wa mradi wa Rusumo ni pamoja na kuboresha maisha ya watu takribani **100,000** katika Wilaya ya Ngara na watu **323,000** katika Wilaya ya Biharamulo kupitia shughuli za kiuchumi zitakazoanzishwa. Vilevile, miradi midogo ya

kusambaza maji na afya itakayowahudumia takribani watu **50,000** itaanzishwa.

**(g) Bonde la Mto Mara**

**57. Mheshimiwa Spika**, kupitia Jumuia ya Afrika Mashariki na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, nchi yetu inashirikiana na Jamhuri ya Kenya katika uhifadhi na kusimamia Bonde la Mto Mara. Ushirikiano huo unafanyika kupitia Hati ya Makubaliano (*Memorandum of Understanding*) ya mwaka 2015 ya kusimamia kwa pamoja rasilimali za maji za bonde hilo. Utekelezaji wa makubaliano hayo unaratibiwa na Kamati ya Pamoja ya Wataalamu (*Joint Technical Committee*) na Kamati ya Pamoja ya Maamuzi ya Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya Utunzaji wa Rasilimali za Maji ya Bonde la Mto Mara (*Joint Steering Committee*) ambayo ni ngazi ya Makatibu Wakuu kutoka katika sekta za maji, mazingira, maliasili na utalii, uvuvi, misitu pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - TAMISEMI.

**58. Mheshimiwa Spika**, pamoja na ushirikiano wa Serikali hizo, taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Mradi wa Mto Mara katika Bonde la Mto Nile ukanda wa Maziwa Makuu zinashiriki katika uhifadhi wa bonde hilo. Kupitia ushirikiano huo, Wizara inashirikiana na Taasisi ya *Sustainable Water Partnership (SWP)* kutekeleza mpango wa miaka mitatu wa kuhakikisha upatikanaji wa maji katika Bonde la Mto Mara. Malengo ya mpango huo ni kuimarisha usalama wa maji, kuboresha hali ya maisha ya jamii, kukuza uchumi na kupunguza umaskini pamoja na kuimarisha mahusiano.

**59. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Kenya imeandaa mpango wa matumizi ya maji ya Bonde la Mto Mara (*Mara River Basin Water Allocation Plan-WAP*). Utekelezaji wa mpango huo unatarajia kuboresha uhifadhi wa mazingira, kuratibu mgawanyo wa maji, kupunguza majanga ya kimazingira, kuboresha afya na maisha ya wananchi wa Bonde la Mto Mara. Vilevile, Wizara imehakikisha kuwa mpango huo

unalinda maslahi ya nchi katika matumizi ya maji ya Mto Mara ambayo ni muhimu kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na matumizi mengine lkiwemo miradi ya umwagiliaji. Aidha, Tanzania ilishiriki katika maadhimisho ya nane ya Siku ya Mto Mara (*Mara Day*) yaliyofanyika MJINI Kilgoris nchini Kenya mwezi Septemba, 2018. Maadhimisho hayo yalisaidia kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya Bonde la Mto Mara pamoja na kuongeza ushirikiano.

**60. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kikanda na kimataifa pamoja na kuimarisha ushirikiano katika usimamizi na uendelezaji wa majishirikishi kwa manufaa ya nchi yetu.

#### *4.2.2. Huduma za Ubora na Usafi wa Maji*

**61. Mheshimiwa Spika**, ufuatiliaji wa ubora wa maji katika vyanzo na mifumo ya usambazaji maji vijijini na mijini ni muhimu katika kulinda afya ya jamii pamoja na mifumo ya ikolojia. Wizara kupitia maabara za ubora wa maji imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora na usalama wa maji ili kuhakikisha maji yanatotumika kwa shughuli za kijamii na kiuchumi yanakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

**62. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara ilipanga kukusanya na kuchunguza sampuli **10,000** za maji kwa matumizi mbalimbali na sampuli **1,500** za majitaka. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya sampuli **4,713** za maji na sampuli **226** za majitaka zilikusanywa na kuchunguzwa. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizo na hali ya ubora wa maji kwa matumizi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

##### *4.2.2.1. Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani*

**63. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayosambazwa katika Halmashauri, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Taasisi pamoja na vyanzo vya maji vinavyomilikiwa na watu

binafsi. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya sampuli **4,165** zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi yalibaini kuwa sampuli **3,776** sawa na **asilimia 91** zilikidhi viwango vinavyokubalika na sampuli **389** sawa na **asilimia 9** hazikukidhi viwango. Maji kutokidhi viwango kumetokana na uwepo wa vimelea vya vijidudu na kiwango kikubwa cha madini. Madini hayo ni *Nitrate* katika maeneo ya Chamwino na Bahi; *Manganese* (Kakonko, Kibondo, Kasulu, Buhigwe, Kigoma, Kaliua, Iramba na Mkalama); Chuma (Kasulu, Uvinza, Buhigwe, Kigoma, Kaliua, Nsimbo, Nkasi, Mlele na Sumbawanga); *Fluoride* (Magugu, Babati, Singida, Manyoni na Arusha); na madini ya chumvichumvi katika maeneo ya Mbande, Hombolo, Bahi na Singida. Ushauri stahiki ultolewa na watusika walishauriwa kutafuta vyanzo mbadala au kutumia teknolojia zilizopo za kuondoa madini hayo ili kudhibiti athari ambazo zingeweza kutokea kutokana na matumizi ya maji yasiyo salama.

#### **4.2.2.2. Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda, Ujenzi na Umwagiliaji**

**64. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakiki na kufuatilia ubora wa maji yanayotumika viwandani, kwenye shughuli za ujenzi na umwagiliaji ili kuhakikisha maji hayo yanakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya sampuli **306** zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli **201** zilichunguzwa kwa ajili ya matumizi ya viwandani ambapo sampuli **199** sawa na **asilimia 99** zilikidhi viwango. Vilevile, sampuli **36** za maji kwa ajili ya ujenzi, **31** kwa ajili ya tafiti na sampuli **38** kwa ajili ya umwagiliaji zilichunguzwa na zote zilikidhi viwango.

#### **4.2.2.3. Mwenendo wa Ubora wa Maji Katika Vyanzo**

**65. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kufuatilia hali ya ubora wa maji katika vyanzo kwenye mabonde yote tisa nchini. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya sampuli **171** kutoka Bodi za Maji za Mabonde zilikusanywa na kuchunguzwa ili kutoa takwimu zinazotumika katika kutoa maamuzi kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Matokeo ya

uchunguzi yalionesha maji kuwa na ubora unaokidhi vigezo vya ustawi wa viumbe hai na kuendelezwa kwa matumizi mbalimbali. Aidha, kwa vyanzo vilivybainika kuathiriwa na uchafuzi, ushauri stahiki ultolewa kwa bodi za maji za mabonde ili kukabiliana na changamoto za uchafuzi.

#### ***4.2.2.4. Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa Kwenye Mazingira***

**66. Mheshimiwa Spika**, udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira ni muhimu katika kuhakikisha vyanzo hivyo vinakuwa endelevu. Wizara kuitia maabara za maji imeendelea kufuatilia ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira kutoka majumbani, viwandani na katika taasisi mbalimbali ili kulinda vyanzo vya maji na mazingira. Hadi mwezi Aprili, 2019, jumla ya sampuli **226** za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilihakikiwa ubora wake. Matokeo ya uhakiki yalibaini kuwa sampuli **94** sawa na **asilimia 39** hazikukidhi viwango vya ubora unaokubalika. Matokeo hayo yanaashiria kuwepo kwa uchafuzi wa mazingira. Kutokana na hali hiyo, Wizara imetoa ushauri wa kitaalam katika miji, viwanda na taasisi mbalimbali kuhusu uboreshaji wa mifumo ya kusafisha majitaka.

**67. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa maji yanayosambazwa kwa matumizi ya majumbani, viwandani, umwagiliaji na matumizi mengine na kuhakiki ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira kutoka viwandani, majumbani na katika taasisi ili kuhakikisha maji hayo yanakidhi viwango vya ubora unaokubalika.

#### ***4.2.2.5. Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji***

**68. Mheshimiwa Spika**, udhibiti wa ubora wa madawa yanayotumika kusafisha na kutibu maji kabla ya matumizi ni muhimu katika kulinda afya za wananchi na usalama wa maji kwa ujumla. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya sampuli **31** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Taasisi **11** zilichunguzwa ubora wake. Sampuli hizo ni za dawa aina ya

*Aluminium Sulphate* (Shabu) sampuli **15**, *Polymerblend* (**4**), *Algal Floc* (**3**), *Dew Floc* (**1**), *Polyaluminium chloride* sampuli **1** kwa ajili ya kusafisha maji; na *Calcium Hypochlorite* sampuli **7** kwa ajili ya kutibu maji. Matokeo ya uchunguzi yamebaini kuwa sampuli zote za madawa zilikidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya kusafisha na kutibu maji. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kuendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira.

#### **4.2.2.6. Utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji**

**69. Mheshimiwa Spika**, Mipango ya Usalama wa Maji (*Water Safety Plan*) inahusu ufuatiliaji wa mfumo wa usambazaji maji kutoka kwenye chanzo hadi kwa mtumiaji kwa kuainisha vihatarishi vinavyoweza kusababisha utoaji wa huduma haffiu na kuweka vidhibiti vya kuzuia vihatarishi hivyo. Lengo la mipango hiyo ni kuhakikisha maji yanayosambazwa kwa jamii ni salama.

**70. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji, Wizara imeweka masuala ya usalama wa maji kama mojawapo ya kiashiria cha ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira. Vilevile, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa mipango hiyo inayoendana na mabadiliko ya tabianchi (*Climate Resilient Water Safety Plans*) kwa kufanya majoribio katika Jumuia ya Watumiaji Maji Mbande. Katika mwaka 2018/2019, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Serikali ya Uingereza (*Department for International Development - DFID*) kupitia Shirika la Afya Duniani limetoa jumla ya **Shilingi milioni 125** kwa ajili ya kutafuta vyanzo zaidi vya maji ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Kijiji cha Mbande. Zoezi la kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji linaendela ambapo hadi mwezi Aprili 2019 kisima kirefu chenye uwezo wa kuzalisha maji **lita 18,000** kwa saa kilichimbwa katika kijiji hicho. Hata hivyo, kisima hicho hakikuendeleza kwa kuwa maji yake hayakukidhi viwango vinavyokubalika. Aidha, katika kuhakikisha mpango huo unatekelezwa katika Mamlaka zote za maji nchini, Wizara

imeweka masuala ya usalama wa maji kama mojawapo ya kiashiria cha ufanisi wa utendaji kazi wa Mamlaka hizo.

#### ***4.2.2.7. Utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufutiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa***

**71.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi na ufutiliaji wa ubora wa maji, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Ufutiliaji wa Ubora wa Maji ya Kunywa na utoaji wa Taarifa (*National Guidelines for Monitoring Drinking Water Quality and Reporting*). Lengo la Mwongozo huo ni kuhakikisha watoa huduma ya maji ya kunywa wanazingatia viwango vya ubora vinavyokubalika ili kulinda afya za wananchi. Katika mwaka 2018/2019, Wahandisi Washauri wa Maji wa mikoa na Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na wataalam wa maabara zote za maji wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo kuhusu utekelezaji wa Mwongozo huo. Aidha, mafunzo hayo yalilenga kuandaa timu ya walimu wa walimu (*Training of Trainers*) ambapo timu hizo zitatumika kujenga uwezo kwa wadau wa maji katika ngazi zote kuanzia Halmashauri za Wilaya hadi ngazi ya kijiji. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na UNICEF imechapisha nakala **500** za Mwongozo huo na kuzisambaza kwa watekelezaji katika mikoa yote. Katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mwongozo huo kwa mikoa yote.

#### ***4.2.2.8. Utekelezaji wa Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride Katika Maji***

**72.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Uondoaji wa Madini ya Fluoride katika maji ya kunywa na kupikia kwenye mikoa iliyoathirika zaidi na madini hayo (*fluoride belt*) kwa kusambaza na kufuatilia ufanisi wa mitambo ya kuondoa madini ya fluoride, kutoa elimu kuhusu madhara ya madini hayo, kuongeza uzalishaji wa malighafi ya kuondoa madini ya fluoride pamoja na kufanya utafiti wa fluoride katika vyanzo vya maji kwenye maeneo mbalimbali nchini. Hadi

mwezi Aprili 2019, jumla ya mitambo **220** ya kuondoa madini ya *fluoride* katika ngazi ya kaya na mitambo **minne** katika ngazi ya jamii imesambazwa kwenye maeneo yaliyoathiriwa na madini ya *fluoride* na jumla ya wananchi wapatao **1,760** wananaufaika na teknolojia hiyo. Ili kuhakikisha teknolojia hiyo inakuwa endelevu, Wizara imeendelea kufuatilia ufanisi wa mitambo iliyosambazwa ambapo mitambo **40** ya ngazi ya kaya (*Household Defluoridation Unit*) na mitambo **nane** ya ngazi ya jamii (*Community Defluoridation System*) ilikaguliwa na ushauri ulitolewa.

Aidha, Wizara ilifanya uchunguzi wa kiwango cha madini ya *fluoride* kwenye vyanzo **105** vya maji Mkoani Geita. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha madini ya *fluoride* katika vyanzo **100** yalikuwa katika kiwango kinachokubalika na vyanzo **vitano (5)** vilibainika kuwa na kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride*. Wananchi katika maeneo yaliyobainika kuwa na kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride* walipewa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya maji yenye kiwango kikubwa cha madini hayo na namna ya kuyaondoa kwa kutumia teknolojia ya mkaa wa mifupa ya ng'ombe.

Katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kutengeneza na kusambaza mitambo midogo **1,000** ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji katika ngazi ya kaya.

#### **4.2.2.9. Maabara za Maji Kupata Ithibati (Accreditation)**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo maabara za maji nchini ili ziweze kupata ithibati (*accreditation*) na kuziwezesha kutoa takwimu zitakazotambulika kimataifa. Lengo ni kuongeza idadi ya maabara zenyte ithibati kutoka **moja** iliyopo hadi maabara **tano** ifikapo mwaka 2021/2022. Katika kufikia lengo hilo, mafunzo yametolewa kuhusu Mwongozo mpya wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Maabara za Uchunguzi (*ISO 17025:2017*) kwa maabara za maji za Mwanza, Tanga, Iringa, Kigoma na maabara kuu Dar es Salaam. Vilevile, katika kujenga uwezo, Wizara imekarabati na kujenga majengo ya maabara yanayokidhi vigezo vya maabara za uchunguzi;

kununua vifaa vya kufanya uchunguzi pamoja na kuziwezesha maabara zote 16 kushiriki katika mazoezi ya kujipima uwezo (*Proficiency Test*) ambavyo ni kigezo katika mchakato wa kupata ithibati.

**74. Mheshimiwa Spika**, matokeo ya zoezi la kujipima uwezo wa utendaji kazi katika kufanya uchunguzi wa viashiria vya kikemikali na kibakteriolojia kwa kila maabara yanaonesha kuwa maabara zimeendelea kufanya vizuri katika upimaji wa viashiria hivyo kwenye maji. Vilevile, matokeo hayo yanaonesha kuwa maabara za maji zimeimarika katika utoaji wa takwimu sahihi zinazotumika kwenye maamuzi ya uendelezaji wa miradi na utoaji wa huduma za maji. Aidha, katika mwaka 2018, Maabara ya Ubora wa Maji Mwanza ambayo ina ithibati ilifanyiwa ukaguzi mara mbili na wataalam wa *Southern African Development Accreditation Service Board (SADCAS)*. Matokeo ya ukaguzi yalionesha kuwa maabara hiyo imeendelea kuzingatia vigezo vya ithibati. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kuziwezesha maabara zote kushiriki mazoezi ya kujipima uwezo na itaendelea na taratibu za kutafuta ithibati kwa maabara za Tanga, Iringa, Kigoma na maabara kuu Dar es Salaam.

#### **4.2.2.10. *Ujenzi na Ukarabati wa Maabara za Maji***

**75. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuboresha mazingira ya kazi, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati maabara za ubora wa maji nchini ili kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya Mwongozo wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Maabara za Uchunguzi (ISO 17025:2017). Katika mwaka 2018/2019, Wizara imekamilisha ujenzi wa Maabara ya ya Maji Bukoba na kuendelea na ujenzi wa majengo ya maabara za Singida ambaao umefikia **asilimia 96**, Sumbawanga (**asilimia 87**), Mbeya (**asilimia 80**), Shinyanga (**asilimia 98**) na Mtwara (**asilimia 85**). Vilevile, upanuzi na ukarabati wa majengo ya maabara za maji unaendelea katika maabara ya Dar es Salaam ambaao umefikia **asilimia 99** na maabara ya Songea umefikia **asilimia 65**. Katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kukarabati na kukamilisha ujenzi wa

majengo ya maabara unaoendelea pamoja na kuanza ujenzi wa Maabara ya Maji Morogoro.

#### *4.2.3. Huduma za Usambazaji Maji Vijijini*

**76. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini kwa kujenga miradi mipya, kukarabati na kupanua miradi iliyopo kwa kutumia vyanzo vya maji vya visima virefu na vifupi; mabwawa, chemchemi, mito na maziwa. Katika kipindi cha mwezi Julai 2018 hadi mwezi Desemba 2018, jumla ya miradi **198** yenye vituo vya kuchotea maji **4,719** imekamilika na inawanufaisha wananchi wapataao **1,252,731** waishio vijijini. Aidha, miradi **653** inaendelea kutekelezwa na ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vilevile, Serikali inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji vijijini pamoja na kutekeleza programu mbalimbali za kuimarisha uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo ili iwe endelevu. Utekelezaji wa miradi ya maji vijijini pamoja na programu mbalimbali umeainishwa kama ifuatavyo:-

##### *4.2.3.1. Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini*

**77. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini umefikia hatua mbalimbali. Utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

###### **(a) Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe**

**78. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na *BADEA, OFID, Saudi Fund na Kuwait Fund* inatekeleza mradi wa maji Same - Mwanga – Korogwe wenyе lengo la kuwapatia huduma ya maji wakazi wa miji ya Same na Mwanga, pamoja na vijiji **38** vilivyopo kandokando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo unatekelezwa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji maji pamoja na miundombinu ya kusambaza maji katika miji ya Same, Mwanga na vijiji **tisa** vilivyopo kandokando ya bomba kuu. Awamu ya pili itahusu kusambaza maji katika vijiji **29** vilivyobaki

ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa awamu hiyo.

**79. Mheshimiwa Spika**, awamu ya kwanza ya mradi umegawanywa katika vipande vinne. Kipande cha kwanza kinachogharimu **Dola za Marekani milioni 41.36** kinahusu ujenzi wa miundombinu ya kuzalisha maji, ulazaji wa bomba kuu la kusafirisha maji hadi kwenye tanki la kuhifadhi maji, mtambo wa kusafisha maji pamoja na ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 79**. Kipande cha pili kinahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika vijiji **tisa** vya Ruu Mferejini, Ruu Jiungeni, Handeni, Lang'ata Bora, Lang'ata Kagongo, Nyabinda, Kiti cha Mungu, Njia Panda na Kirya. Ujenzi wa kipande hicho haujaanza na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kipande hicho.

**80. Mheshimiwa Spika**, kipande cha tatu kinachogharimu **Dola za Marekani milioni 36.70** kinahusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Mji wa Mwanga. Hadi mwezi Aprili 2019, ujenzi wa kipande hicho umefikia **asilimia 15**. Aidha, kipande cha nne kinachohusu ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika Mji wa Same kinatekelezwa kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 35.25** na hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 55**.

**81. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji Same - Mwanga - Korogwe utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuzalisha maji **lita milioni 103.7** kwa siku ambapo mahitaji ya maji kwa sasa ni **lita milioni 78.4** kwa siku. Vilevile, mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wananchi **438,931** wa Wilaya za Same **(246,793)** na Mwanga **(177,085)** katika Mkoa wa Kilimanjaro; na wananchi **15,053** wa Wilaya ya Korogwe katika Mkoa wa Tanga. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 29.28** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo.

(b) Mradi wa Maji Masoko

82. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa Masoko uliopo Wilaya ya Rungwe Mkoani Mbeya ambao unahusisha ulazaji wa mtandao wa mabomba, ujenzi wa vidakio vya maji, matanki ya maji na vituo vya kuchotea maji. Hatua za utekelezaji wa mradi zimegawanyika katika vipande vitano. Kipande cha kwanza kinachogharimu **Shilingi milioni 552.2** kinahusisha ujenzi wa kidakio cha maji katika Mto Mbaka, tanki la ujazo wa **lita 90,000**; vituo vitano vya kuchotea maji, ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 12.6** na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 370,000**. Hadi mwezi Aprili, 2019 utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 65**.

83. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa kipande cha pili kinachogharimu **Shilingi milioni 851.6** unahusisha ujenzi wa kidakio cha maji, ujenzi wa chujio la maji, ujenzi wa vituo **40** vya kuchotea maji, ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 19.1** na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 290,000**. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 70**. Kwa upande wa kipande cha tatu kinachogharimu **Shilingi bilioni 1.26**, utekelezaji wake unahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 600,000**, ujenzi wa vituo **112** vya kuchotea maji na ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 61.9**. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho cha tatu umefikia **asilimia 90**.

84. **Mheshimiwa Spika**, kipande cha nne kinahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 550,000**, ujenzi wa vituo **111** vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 80.6**. Kipande hicho kinagharimu **Shilingi bilioni 2.4** na hadi mwezi Aprili 2019, ujenzi umefikia **asilimia 30**. Hata hivyo, utekelezaji wa kipande hicho umesimama baada ya Mkandarasi kusimamishwa kazi kwa kutokidhi matakwa ya mkataba. Wizara kupitia wataalam wake wa ndani itakamilisha kazi zilizobaki. Kwa kipande cha tano kinachogharimu **Shilingi milioni 552.4**, utekelezaji wake unahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 90,000**, ujenzi wa vituo **67** vya kuchotea maji na ulazaji wa mabomba yenye

urefu wa **kilomita 30.5**. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande cha tano umefikia **asilimia 70**.

**85. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji Masoko utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao **19,624** wanaoishi katika vijiji vya Bulongwe, Ngaseke, Igembe, Ntandabala, Lupando, Bujesi, Lufumbi, Nsyasa, Ikama, Itagata, Busisywa, Mbaka, Isabula, Lwifa na Nsanga.

**(c) Mradi wa Maji wa Vijiji 100 Vilivyopo Kando ya Bomba Kuu la KASHWASA**

**86. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa vijiji 100 vilivyopo kandokando ya bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga unaendelea kutekelezwa chini ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Kahama - Shinyanga (KASHWASA). Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo itahusisha vijiji **40** ambapo vijiji **33** vimefanyiwa usanifu. Kati ya vijiji vilivyofanyiwa usanifu, ujenzi wa miradi kwenye vijiji **14** umekamilika na kunufaisha wananchi wapatao **38,348**. Vijiji hivyo ni Runele, Gatuli, Nyashimbi, Magobeko, Kakulu, Butegwa, Nyang'homango, Ng'homango, Jimondoli, Kadoto, Lyabusalu, Mwajiji, Ichongo na Bukamba.

**87. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi katika vijiji vilivybaki vya Mwasekagi na Mwakatola umefikia **asilimia 90** na wananchi wanapata huduma ya maji. Vilevile, ujenzi wa mradi unaendelea kwenye vijiji vya Mwakuzukana na Kabondo ambapo utekelezaji umefikia **asilimia 35**; na vijiji vya Izuga, Isesa, Igenge na Mbarika, utekelezaji umefikia **asilimia 40**. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapatao **26,573** wa vijiji hivyo.

**(d) Mradi wa Maji Ntomoko**

**88. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliunda Timu ya Wataalam kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu wa kina wa mradi wa maji Ntomoko. Timu hiyo ilibaini kuwa chanzo cha Ntomoko kina

uwezo wa kuhudumia vijiji vitatu tu kati ya vijiji 18 vilivyopo katika mpango. Baada ya Timu kubaini upungufu huo, utafiti ulifanyika na kubaini uwezekano wa kujenga bwawa kubwa litakalokidhi mahitaji ya vijiji vilivyobaki na usanifu wa bwawa hilo umekamilika.

**89. Mheshimiwa Spika**, katika mipango ya muda mfupi, Wizara kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (*DUWASA*) itakarabati miundombinu ya maji katika vijiji vya Ntomoko - Fai na Makirinya vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na vijiji vya Kinkima na Lusangi vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ambavyo kwa muda vitatumia chanzo cha maji cha Ntomoko. Mradi huo utagharimu **Shilingi bilioni 2.27**. Mwezi Februari 2019, *DUWASA* ilisaini mkataba na Mkandarasi ambaye ameanza maandalizi ya utekelezaji wa mradi. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa matanki matatu katika vijiji vya Makirinya (**lita 45,000**), Kinkima (**lita 90,000**) na Lusangi (**lita 90,000**); ununuzi wa pampu; ulazaji wa mabomba ya kusafirisha maji pamoja na ujenzi wa chemba.

**90. Mheshimiwa Spika**, kwa vijiji **11** vilivyobaki vya Mtakuja, Igunga, Goima, Songolo, Jinjo, Jangalo, Mlongia, Jenjeluse, Chandama, Itolwa, na Mapango, vitapata maji kupitia mradi mkubwa wa bwawa unaotarajiwa kutekelezwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2019/2020.

**(e) Mradi wa Maji Chiwambo**

**91. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa maji Chiwambo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ulioharimu **Shilingi bilioni 4.49** ulikamilika mwezi Mei, 2018. Mradi huo unahudumia vijiji **30** vilivyopo Kata za Lulindi, Lupumbulu, Namalenga, Chiungutwa, Sindano, Mchauru na Mbonyuni. Utekelezaji wa mradi huo ulihusisha ukarabati wa matanki na miundombinu ya maji iliyochakaa, ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji, upanuzi wa miundombinu ya kusambaza maji na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji.

Kukamilika kwa mradi huo kumeboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wapatao **84,082** wa vijiji hivyo.

**(f) Mradi wa Maji wa Pamoja na Mgodi wa Bulyanhulu**

**92. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni inayomiliki Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu (ACACIA) inatekeleza mradi wa maji wa Bulyanhulu unaogharimu **Shilingi bilioni 13.86** na utahusisha vijiji **14** katika Halmashauri za Wilaya ya Shinyanga na Msalala kwa Mkoa wa Shinyanga na Halmashauri ya Wilaya ya Nyangh'wale kwa Mkoa wa Geita. Mradi huo utachepusha maji kutoka bomba kuu la *KASHWASA* na utanufaisha vijiji vya Mwenge, Nyugwa, Kharumwa, Mwamakiliga, Izunya, Kafita, Lushimba, Lwabakanga, Kakola Namba 9, Bushing'we, Kakola, Bugarama, Igudija na Ilogi.

**93. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, Mkandarasi amekamilisha kazi za ujenzi wa ofisi za mradi, uchimbaji wa mtaro wenye umbali wa **kilomita 15** na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 8.94**. Aidha, Mkandarasi anaendelea na kazi zilizobaki za uchimbaji na ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 56** pamoja na ufungaji wa viungio vya mabomba. Mradi unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2019/2020.

**(g) Ujenzi na Ukarabati wa Mabwawa**

**94. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji katika maeneo kame, Serikali imeendelea kujenga mabwawa mapya na kukarabati mabwawa yaliyopo ili wananchi waweze kunufaika na huduma ya maji. Hadi mwezi Aprili 2019, hatua iliyofikiwa katika ujenzi na ukarabati wa mabwawa ni kama ifuatavyo:-

**(i) Bwawa la Dongo**

Bwawa la Dongo liliopo katika Wilaya ya Kiteto, linalenga kuhudumia jumla ya vijiji **19** vilivyopo katika Wilaya za Kiteto, Kongwa na Gairo. Vijiji vitakavyohudumiwa na bwawa hilo

ni Dongo, Logoit, Chang'ombe, Laiser, Ndotoi, Engusero Sidan na Nhati katika Wilaya ya Kiteto; vijiji vya Njoge, Ngomai, Manyata, Hembahemba, Pandambili, Silwa, Lobilo na Lenjulu (Wilaya ya Kongwa); na Mji Mdogo wa Gairo pamoja na vijiji vya Letegunya, Majawanga, Mishugi na Mkalama (Wilaya ya Gairo). Hadi mwezi Aprili 2019, upembuzi yakinifu umekamilika na kazi inayoendelea ni usanifu wa mradi. Ujenzi wa bwawa hilo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2019/2020.

**(ii) Bwawa la Nsenkwa**

Serikali imeanza ujenzi wa Bwawa la Nsenkwa liliopo katika Wilaya ya Mlele, Mkoani Katavi. Bwawa hilo litahudumia Kata za Nsekwa, Kamsisi, Utende Ilala na Mji mdogo wa Inyonga. Kazi zinazoendelea ni uchimbaji na ujenzi wa utoro wa maji ambapo hadi mwezi Aprili 2019, ujenzi wa bwawa hilo umefikia **asilimia 15**.

**(iii) Bwawa la Wanging'ombe**

Bwawa la Wanging'ombe liliopo katika Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoani Njombe, litahudumia vijiji tisa vya Wanging'ombe, Utiga, Itandula, Ufwala, Mbembe, Litunda, Mayale, Katenge na Mng'elenge. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tuta na utoro wa maji na hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kazi hizo umefikia **asilimia 75**.

**(iv) Bwawa la Mwanjoro**

**95. Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha ujenzi wa bwawa la Mwanjoro liliopo Wilayani Meatu ambao umegharimu **Shilingi bilioni 1.79**. Bwawa hilo linatoa huduma ya maji kwa wananchi **13,859** wa vijiji **vitatu** vya Mwanjoro, Jinamo na Mbushi vilivyopo katika Halmashauri ya Meatu.

**(v) Mabwawa ya Kudhibiti Mafuriko Katika Mto Kinyasungwe**

**96. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji ikishirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI iliunda timu ya pamoja kwa ajili ya

kukusanya taarifa za usanifu wa mabwawa yatakayojengwa maeneo ya Kimagai (Mpwapwa), Hombolo (Dodoma Mjini), Ikowa (Chamwino), Dabalo (Chamwino), Kidete (Kilosa) na Buigiri (Chamwino). Pamoja na matumizi mengine, mabwawa hayo yatatumika kuzuia mafuriko yanayotokana na kiwango kikubwa cha maji kwenye Mto Kinyasungwe (*Kinyasungwe Flood Control Dams*). Hadi mwezi Aprili 2019, taarifa ya usanifu na uainishaji wa namna za kudhibiti mafuriko kwenye Mto Kinyasungwe imekamilika na kuwasilishwa Wizarani kwa mapitio na hatua zaidi.

**97. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kufanya utafiti wa maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa mapya, kujenga na kufanya ukarabati wa mabwawa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 10.3** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ya mabwawa.

#### *4.2.3.2. Programu za Kuimarisha Uendelevu wa Huduma ya Maji Vijiini*

**98. Mheshimiwa Spika**, miradi ya maji vijiini inapokamiliika hukabidhiwa kwa wananchi husika kupitia Vyombo vya Watumiaji Maji (CBWSOs) ambavyo husimamia na kuendesha miradi hiyo. Vyombo hivyo vimepewa jukumu la kusimamia miradi ya maji kwa ufanisi. Hivyo, Serikali imeandaa programu mbalimbali zenye lengo la kuhakikisha miradi inayokabidhiwa kwa vyombo hivyo inakuwa endelevu na wananchi wanapata huduma iliyotarajiwa. Utekelezaji wa Programu hizo umeelezwa kwa kina kama ifuatavyo:-

(h) **Matumizi ya Teknolojia ya Nishati Jadidifu (Renewable Energy)**

**99. Mheshimiwa Spika**, katika kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji vijiini, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza programu ya kubadilisha teknolojia ya uendeshaji wa miradi ya maji vijiini inayotumia mafuta ya dizeli ili iweze kutumia teknolojia nafuu ya nishati ya juu. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali kwa kushirikiana na

*Ohio State University – OSU*chini ya ufadhili wa Taasisi ya Kiraia (*Water Development Alliance–WADA*) inaendelea na utekelezaji wa miradi miwili ya majaribio ya matumizi ya nishati jadidifu katika vijiji vya Ghalunyangu na Mughangha katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida. Miradi hiyo inahusisha ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji; kuongeza vyanzo vya maji na kufunga mfumo wa umeme jua. Hadi mwezi Aprili 2019, kazi za ukarabati wa miundombinu ya kusambaza maji na uchimbaji wa visima zimekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukarabati wa nyumba ya mitambo na ufungaji wa mfumo wa umeme jua. Kufanikiwa kwa mradi huo kutawezesha kuanza kwa utekelezaji wa miradi mingine kwenye vijiji **36** vilivyo poto katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mara, Mwanza na Kilimanjaro.

**100. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia utaratibu wa *Global Partnership on Output Based Aid (GPOBA)* inaandaa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa matumizi ya umeme jua (*Accelerating Solar Water Pumping Project via Innovative Financing*) utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 4.2**. Mradi huo utahusisha pia ufungaji wa dira za maji za mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*pre-paid water meter*). Awamu hiyo itaanza kwa majaribio kwenye vijiji **280** katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Mtwara, Rukwa, Singida, Tabora, Arusha na Manyara. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi ya teknolojia hiyo pamoja na kuzihamasisha Halmashauri zote nchini kukusanya takwimu za miradi ambayo itabdalilishiwa teknolojia inayotumika.

**101. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, kazi iliyokamilika ni kukusanya takwimu katika mikoa ya Tabora, Dodoma, Singida, Mtwara na Shinyanga. Kazi inayoendelea ni kuwapata wakandarasi kwa ajili ya kununua, kufunga na kufanya matengenezo ya mitambo ya mfumo wa umeme jua katika Mikoa ya Dodoma na Singida ambapo miradi **43** kutoka Mkoa wa Singida na miradi **39** kutoka Mkoa wa Dodoma itafungwa mitambo ya umeme jua. Katika mwaka 2019/2020, kazi ya ufungaji wa mitambo ya umeme jua

itatekelezwa katika mikoa hiyo. Vilevile, taratibu za kuwapata wakandarasi wa kununua, kufunga dira za maji za mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*pre-paid water meter*) zinaendelea na dira hizo zinatarajiwa kufungwa kwenye miradi itakayotekerezwa katika mikoa ya Dodoma na Singida.

(a) **Mpango wa Kuimarisha Uendelevu wa Huduma ya Maji Vijiji Kupitia Mfumo wa Malipo Kwa Matokeo**  
**(Payment by Results - PbR)**

102. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuhakikisha miradi ya maji vijiji inakuwa endelevu, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimatalifa (*DFID*) inatekeleza Mpango wa Mfumo wa Malipo kwa Matokeo (*Payment by Results – PbR*) ambao una lengo la kuimarisha uendelevu wa miradi ya maji vijiji. Hadi mwezi Aprili 2019, awamu ya pilii ya programu hiyo imekamilika ambapo Halmashauri **95** zilifuzu na kupewa **Shilingi bilioni 8.55** kati ya **Shilingi bilioni 53.6** zilizotengwa katika mwaka 2017/2018. Aidha, awamu ya tatu ya programu inaendelea na inahusisha Halmashauri **181** ambazo zitapewa fedha kwa vigezo vya idadi ya vituo vilivyojengwa na kutoa maji. Kupitia *PbR*, **Paundi 300** hutolewa kwa kila kituo kilichohakikiwa na kinachofanya kazi na **Paundi 1,500** hutolewa kwa kituo kipya kitakachojengwa. Katika mwaka 2018/2019, jumla ya **Paundi milioni 10** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza programu hiyo kwenye Halmashauri zote nchini. Hadi mwezi Aprili 2019, fedha zilizolipwa katika awamu ya tatu ni **Paundi milioni 8.7** sawa na **Shilingi bilioni 25.43**. Katika mwaka 2019/2020, **Shilingi bilioni 46.47** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo.

#### **4.2.3.3. Uvunaji wa Maji ya Mvua**

103. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maji, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi na taasisi mbalimbali kuhusu umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya majengo. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali imetoe maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kutunga sheria ndogo zenye

kuzitaka Taasisi za kijamii, asasi na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao. Sheria hizo zinalenga kuhakikisha kuwa michoro ya majengo yote yanayojengwa inajumuisha mifumo ya kuvuna maji ya mvua kabla ya ujenzi wa majengo hayo kuidhinishwa. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuvuna maji ya mvua kupitia mapaa ya majengo. Vilevile, Serikali inaendelea kuzisisitza Halmashauri zote nchini kutunga na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo zinazohusu ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye mapaa ya majengo.

#### **4.2.3.4. *Miradi Mingine ya Maji Vijiji Inayotarajiwa Kutekelezwa***

##### **(a) Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira Mkoani Kigoma**

**104. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji itatekeleza mradi wa maji na usafi wa mazingira Kigoma katika vijiji **26** vya Halmashauri za Mkoa wa Kigoma. Mradi huo unatarajiwa kugharimu **Euro milioni 8.8** na kati ya fedha hizo, Serikali ya Ubelgiji itatoa **Euro milioni 8** na Serikali ya Tanzania itatoa **Euro 800,000**. Hadi mwezi Aprili 2019, Meneja wa mradi ameajiriwa na ameanza kazi. Aidha, zabuni za kuwapata Wataalam Washauri watakaofanya kazi ya uhamasishaji, uanzishwaji na kujenga uwezo kwa Jumuiya za Watumiaji Maji pamoja na Wataalam Washauri watakaosimamia ujenzi wa miradi zimetangazwa. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao **200,000** wa vijiji hivyo.

##### **(b) Mradi wa Maji Isimani**

**105. Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa maji Isimani unaotarajiwa kugharimu **Shilingi bilioni 2.8**. Mradi huo unatarajiwa kuhudumia vijiji 29 vya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri ameajiriwa na anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wananchi wapatao **56,000** wa vijiji hivyo.

(c) Mradi wa Maji Lukululu

106. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Hispania imepanga kutekeleza mradi wa maji Lukululu utakaohusisha vijiji vya Lukululu, Mbewe, Mlangali, Shomola, Shaji na Ndolezi katika Kata ya Mlangali na vijiji vya Igunda, Mahenje, Mbulu, Myovizi, Ichesa na Ivugula vilivyopo katika Halmashauri ya Mbozi. Gharama za kutekeleza mradi huo zinakadiriwa kufikia **Shilingi bilioni 5**. Mkataba kati ya Wizara na Mtaalam Mshauri ulisainiwa mwezi Desemba, 2018 na Mtaalam huyo anaendelea na usanifu wa mradi unaotarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Mradi huo utakapotekelezwa utawanufaisha wananchi wapatao **35,277** wa vijiji hivyo.

(d) Miradi ya Maji Katika Viji Viliwyomo Pembezoni mwa Maziwa Makuu

107. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha rasilimali za nchi yetu zinawanufaisha wananchi, Serikali imepanga kutekeleza miradi ya maji katika maeneo ya pembezoni mwa Maziwa Makuu ya Tanganyika, Nyasa na Victoria. Lengo ni kuwapatia wananchi wa maeneo hayo huduma ya maji ya uhakika. Utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Tanganyika

108. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Tanganyika utakaohudumia wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri amekamilisha na kuwasilisha taarifa ya upembuzi yakinifu na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii. Kazi itakayofuata ni kufanya usanifu wa kina wa mradi. Mradi huo utatekelezwa katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa na Katavi na utahusisha vijiji **73** vya Halmashauri za Wilaya za Kigoma, Uvinza, Nkasi, Kalambo, Mpimbwe na Mpanda.

**(ii) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Nyasa**

**109.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Nyasa utakaohudumia wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu na anaendelea na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii. Mradi huo utatekelezwa katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma na utahusisha vijiji **41** vya Halmashauri za Wilaya za Ludewa na Nyasa.

**(iii) Mradi wa Kutoa Maji Ziwa Victoria**

**110.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria utakaohudumia wananchi waishio maeneo ya pembezoni mwa ziwa hilo. Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa mradi katika vijiji vitakavyonufaika na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo mwezi Mei, 2019. Usanifu utakapokamiliika, ujenzi wa mradi utaanza na utanufaisha jumla ya vijiji **301** vilivyopo pembezoni mwa Ziwa Victoria katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Simiyu.

**4.2.3.5. Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini**

**111.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji vijijini inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 301.25** zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 224.03** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 77.22**. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini katika mwaka 2019/2020 umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 4**.

**4.2.4. Huduma za Usambazaji Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini**

**112.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma

ya maji mijini kwa kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji Mijini. Miradi hiyo inatekelezwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kuwapatia wananchi wengi zaidi wa maeneo ya mijini huduma bora na endelevu ya majisafi na usafi wa mazingira. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

**4.2.4.1. *Miradi ya Kutoa Maji Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali***

**(a) Miji ya Isaka na Kagongwa**

113. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka katika miji ya Isaka na Kagongwa umegawanywa katika vipande viwili. Kipande cha kwanza kinachogharimu **Shilingi bilioni 11.91** kinahusu ujenzi wa chemba na ulazaji wa bomba kuu kutoka Kinaga hadi Kagongwa lenye urefu wa **kilomita 52.8**. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 94**. Kipande cha pili kinachogharimu **Shilingi bilioni 12.81** kinahusu ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenyе urefu wa **kilomita 24** katika Mji wa Kagongwa na **kilomita 23** katika Mji wa Isaka pamoja na ujenzi wa matanki mawili ya chuma kwa kila miji pamoja na ujenzi wa vituo **16** vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 87**. Mradi utakapokamilika utahudumia wakazi wapataao **115,000** wa miji ya Isaka na Kagongwa. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 4** kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

**(b) Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui**

114. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa kutoa maji kutoka bomba kuu la *KASHWASA* kupeleka katika Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na Wilaya ya Uyui unatekelezwa kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 268.35**, fedha ambazo ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Lengo la mradi huo ni kuwapatia huduma ya maji ya uhakika wananchi wapataao **milioni 1.1** wa miji ya Tabora, Igunga,

Nzega na Wilaya ya Uyui pamoja na vijiji **110** vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka bomba kuu la *KASHWASA*. Utekelezaji wa mradi umegawanywa katika vipande vitatu ambapo kipande cha kwanza kinahusu ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 93.4** kutoka Kijiji cha Solwa (kilichopopo katika Wilaya ya Shinyanga) hadi Mji wa Nzega. Kipande cha pili kinahusu ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 103.8** kutoka Nzega Mjini hadi Manispaa ya Tabora kupitia Wilaya ya Uyui; na kipande cha tatu kinahusu ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 80** kutoka Nzega Mjini hadi Igunga Mjini. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 68.5.** na unatarajiwu kukamilika katika mwaka 2019/2020. Mradi utakapokamilika utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji hiyo hadi kufikia **asilimia 100.**

**(c) Jiji la Mwanza na Miji ya Lamadi, Magu na Misungwi**

**115. Mheshimiwa Spika**, mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB*) pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) kwa gharama ya **Euro milioni 104.5.** Kwa upande wa Jiji la Mwanza, kazi zinazotekelizwa ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa matanki katika eneo la Kitangiri, Nyasaka Mjimwema/ Nyakabungo, Nyegezi na Bugarika; kubadilisha mabomba ya zamani yaliyochakaa katika maeneo ya barabara ya Kenyata, Makongoro na Nyakato yenye urefu wa **kilomita 15.77**; na ujenzi wa mtambo wa kutibu maji katika eneo la Capripoint. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji umefikia **asilimia 75** na unatarajiwu kukamilika mwezi Aprili, 2019. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **105,649** wanaoishi maeneo ya milimani ambayo ni Nyasaka, Bugarika, Nyegezi, Capripoint, Mjimwema, Nyakabungo na Kitangiri. Aidha, kwa upande wa huduma ya usafi wa mazingira, Serikali imekamilisha mradi wa ujenzi wa mfumo rahisi wa uondoaji majitaka katika maeneo ya milimani na

kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika maeneo hayo.

**116. Mheshimiwa Spika**, katika Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi, utekelezaji wa mradi unahusu kujenga mifumo mipyaya kusafisha na kutibu maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa matanki; vituo vya kuchotea maji na ununuzi wa vitendea kazi (magari na pipipiki). Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 87** na unatarajiwaa kukamilika mwezi Mei, 2019. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi **23,315** wa Misungwi Mjini na Kijiji cha Nyahiti; wakazi **45,340** wa Magu Mjini na vijiji vya llungu na Kipeja; na wakazi **23,540** wa Lamadi Mjini.

#### *4.2.4.2. Kuboresha Huduma ya Maji Katika Miji Mikuu ya Mikoa*

##### **(a) Manispaa ya Kigoma**

**117. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza mradi wa usambazaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Kigoma kwa gharama ya **Euro milioni 16.32**. Utekelezaji wa mradi huo ulitarajiwaa kukamilika mwezi Novemba 2017 lakini haukukamilika kutokana na uwezo mdogo wa Mkandarasi. Kutokana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua ya kuvunja Mkataba na Mkandarasi huyo mwezi Oktoba 2018. Hadi kuvunjwa kwa mkataba, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 87** na mradi ulikuwa umeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Aidha, wakati mkataba huo unavunjwa, huduma ya maji ilikuwa imesimama kutokana na kuharibika kwa pampu kwenye kidakio na pia kwenye baadhi ya maeneo ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji ulikuwa haujakamilika.

**118. Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, Wizara imechukua jitihada za kuhakikisha huduma iliyokuwa ikitolewa kwa wakazi wa Mji wa Kigoma inarejeshwa kwa kuajiri mkandarasi wa kuweka mitambo ya muda ya

kusukuma maji. Vilevile, Serikali imeingia mkataba na Mkandarasi mwingine atakayemilisha sehemu ya kazi ya ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo yanayopata huduma. Kazi zinatarajwa kukamilika mwezi Juni 2019. Aidha, kutokana na changamoto za kidakio kilichopo, Wizara imeajiri Mtaalam Mshauri anayefanya usanifu wa ujenzi wa kidakio kipya. Baada ya usanifu huo kukamilika, Wizara itamwajiri Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kidakio hicho.

(b) **Jiji la Arusha**

**119. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika Jiji la Arusha kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 233.9**. Kazi zinazotekelawa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu **56**; ujenzi wa matanki **10**; ujenzi wa mtambo wa kutibu na kusafisha maji; upanuzi na ukarabati wa mtandao wa mabomba ya majisafi; upanuzi na ukarabati wa mtandao wa majitaka, ujenzi wa mabwawa mapya **18** ya majitaka; ujenzi wa ofisi ya Mamlaka; ununuzi wa vitendea kazi na kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 30** na unatarajiwaa kukamilika mwaka 2020. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 200** kwa siku. Vilevile, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi utaongezeka kutoka wastani wa **saa 12** za sasa kwa siku hadi **saa 24** pamoja na kuongeza huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**.

(c) **Manispaa ya Lindi**

**120. Mheshimiwa Spika**, mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Lindi unaogharimu **Euro milioni 11.7**, unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Serikali ya Ujerumani pamoja na Umoja wa Ulaya. Mradi ulitarajiwaa kukamilika mwezi Novemba, 2017 lakini haukukamilika kutokana na uwezo mdogo wa kiutendaji wa Mkandarasi.

Hivyo, Serikali ilichukua hatua ya kuvunja Mkataba na Mkandarasi huyo mwezi Oktoba 2018 ambapo utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 92.3** na unatoa huduma ya maji kwa wakazi wapatao **81,343** wa Mji wa Lindi. Kazi zilizobaki ni kufunga mfumo wa angalizi wa uzalishaji maji, ununuzi wa gari la uondoaji majitaka na kurekebisha maeneo yenye mapungufu katika mradi huo. Serikali imeajiri Mkandarasi mwingine atakayekamilisha kazi zilizobaki. Kukamilika kwa mradi huo kutapunguza kero ya uhaba wa huduma ya maji iliyokuwa ikiwakabili wakazi wa Mji wa Lindi.

**(d) Mji wa Geita**

121. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LVWATSAN II*) katika Mji wa Geita unatekelezwa kwa ushirikiano katika Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.67**. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 98**. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 3.8** kwa siku hadi **lita milioni 5.7** kwa siku na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 35** hadi **asilimia 70** kwa wakazi wapatao **135,359** wa Mji wa Geita. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi umekamilika na upo katika hatua za makabidhiano. Kwa upande wa usafi wa mazingira, kazi zinazoendelea ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka ambaao umefikia **asilimia 90** na ujenzi wa dampo la kisasa la kutupa taka ngumu kwenye eneo la Usindakwe ambaao umefikia **asilimia 70**. Kukamilika kwa mabwawa hayo kutapunguza uchafuzi wa mazingira unaotokana na umwagaji wa majitaka usiozingatia taratibu za utunzaji wa mazingira.

**(e) Mji wa Njombe**

122. **Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa muda mfupi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Njombe, Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa chemchemi ya Kibena uliogharimu **Shilingi bilioni 1.1**. Mradi huo ulihusisha

ujenzi wa kidakio cha maji, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 2.2** na ufungaji wa pampu mbili za kusukuma maji zenye uwezo wa kuzalisha **lita 72,000** kwa saa. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 480,000** hadi **lita 864,000** kwa siku na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Hospitali ya Kibena, Chuo cha Uuguzi, maeneo ya Nyamyuya, Ofisi za Mkoa na Mgendela. Mradi huo umeongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Njombe kutoka **asilimia 69** mwaka 2016 hadi **asilimia 87** za sasa. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji huo.

Katika mpango wa muda mrefu wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Njombe, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Hagafilo unaotarajiwaa kutekelezwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India.

**(f) Miji ya Vwawa na Mlowo**

**123. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuhakikisha Miji ya Vwawa na Mlowo inapata huduma ya maji ya uhakika, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi kwenye miji hiyo. Kwa Mji wa Vwawa, utekelezaji wa mradi unahusisha ujenzi wa kidakio cha maji kwenye Mto Mantengu, ufungaji wa mitambo ya kutibu maji, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 1.71**, ulazaji wa mtandao wa kusambaza maji wenyewe urefu wa **kilomita 12.6** na ununuzi wa dira za maji **1,200**. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi huo unaogharimu **Shilingi bilioni 1.56** umefikia **asilimia 90**. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapataao **10,171** wa Mji wa Vwawa. Kwa upande wa Mji wa Mlowo, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji huo unaogharimu **Shilingi milioni 586** umekamilika na wakazi wapataao **9,154** wa mji huo wanapata huduma ya maji. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji katika mji hiyo.

#### 4.2.4.3. Kuboresha Huduma ya Maji Katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo

##### (a) Mji wa Orkesumet

124. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (*BADEA*) na Mfuko wa Nchi zinazozalisha mafuta kwa Maendeleo ya Kimataifa (*OPEC Fund for International Development - OFID*) inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Mji wa Orkesumet. Utekelezaji wa mradi umegawanyika katika vipande viwili ambapo kipande cha kwanza kinagharimu **Shilingi bilioni 12.99** na kinahusisha ujenzi wa kidakio cha maji na mtambo wa kutibu na kusafisha maji. Utekelezaji wa kipande hicho upo katika hatua za awali na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2019/2020. Kipande cha pili kinachogharimu **Shilingi bilioni 25.02** kinahusisha ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa vituo vya kuchotea maji; na miundombinu ya kunyweshea mifugo. Utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 68** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2019/2020. Mradi utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kutoka **asilimia 48** hadi **asilimia 82** na kuwanufaisha wakazi wapatao 52,000 wa Mji wa Orkesument pamoja na mifugo yao.

##### (b) Mji wa Longido

125. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji katika Mji wa Longido unalenga kuboresha huduma ya maji katika mji huo pamoja na kijiji cha Engikaret. Mradi huo umegawanyika katika vipande vinne ambapo kipande cha kwanza kinagharimu **Shilingi bilioni 10.89** na kinahusisha ujenzi wa chanzo katika Mto Simba; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 63.02** kutoka Mto Simba hadi kwenye tanki la Longido Mjini; na ujenzi wa chemba nne za kupunguza msukumo wa maji. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umekamilika. Kipande cha pili kinagharimu **Shilingi bilioni 2.54** na kazi zinazotekelze wa ni pamoja na ulazaji wa bomba la kusafirisha maji kutoka Longido Mjini hadi

Kijiji cha Engikaret na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 95.**

**126. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelawa katika kipande cha tatu ni ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji katika Mji wa Longido lenye ujazo wa lita 450,000, ukarabati wa matanki matatu, ukarabati wa miundombinu ya kunyweshea mifugo na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika Kijiji cha Engikaret. Kipande hicho kinagharimu **Shilingi milioni 276.36** na utekelezaji wa kipande hicho umekamilika. Kipande cha nne kinahusu ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika Mji wa Longido kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2.09** ambapo utekelezaji wa kipande hicho umekamilika. Kukamilika kwa mradi wa Longido kumewezesha wananchi wapatao **16,712** wa Longido Mjini na wananchi wapatao **1,294** wa kijiji cha Engikaret kupata huduma ya maji safi na salama hivyo kuzuia magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa majisafi na salama. Aidha, Serikali itajenga mabirika ya kunyweshea mifugo katika maeneo linapopita bomba kuu linalotoa maji kutoka Mto Simba kwenda katika Mji wa Longido. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya ujenzi wa mabirika ya kunyweshea mifugo, kukamilisha kazi za kipande cha pili na kulipa hati za madai ya Wakandarasi ambazo hazijalipwa.

Utekelezaji wa miradi mingine ya uboreshaji wa upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo pamoja na fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya matokeo ya haraka (quickwins) ili kuboresha huduma ya maji katika miji midogo umeainishwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. 5.**

#### **4.2.4.4. Uboreshaji wa Huduma ya Maji Katika Maeneo Yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa**

##### **(a) Mradi wa Maji Chalinze**

**127. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa maji Chalinze baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza na ya pili.

Awamu hiyo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 41.3**. Mradi huo unahusisha upanuzi wa kidakio cha maji kwenye Mto Wami kitakachoongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5** kwa siku hadi **lita milioni 9**; ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji katika vijiji **20**; ulazaji wa bomba kuu na upanuzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji yenyе urefu wa **kilomita 921.7**; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 2** katika Mlima Mazizi; na ujenzi wa vituo **496** vya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na huduma ya maji wakati wa ujenzi wa awamu ya kwanza na ya pili ya mradi. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 79.5**. Hata hivyo, Mkandarasi ameshindwa kuendelea na kazi hivyo, Serikali imeamua kuvunja mkataba na Mkandarasi huyo. Serikali inaendelea na taratibu za kuajiri Mkandarasi mwingine atakayekamilisha kazi zilizobaki. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufalsha wananchi wapatao **397,384** wanaohudumiwa na mradi wa kitaifa wa maji Chalinze. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 4.5** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze.

**(b) Mradi wa Maji Mugango - Kiabakari**

**128. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development - SFD*) inatekeleza mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari. Mradi huo unaogharimu **Dola za Marekani milioni 30.69** unalenga kuboresha huduma ya maji katika maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama. Hadi mwezi Aprili 2019, usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni umekamilika na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na upanuzi wa kidakio cha maji katika Ziwa Victoria; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji iliyopo Kiabakari; ujenzi wa matanki matatu katika maeneo ya Mugango, Kiabakari na Butiama; ulazaji wa bomba kuu kutoka Mugango kwenda Kiabakari hadi Butiama lenye urefu wa **kilomita 32**; na ulazaji wa mabomba

ya kusambaza maji Butiama na Bisarye. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao **80,000** walipo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya **kilomita 12** kutoka eneo la bomba kuu. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 8.5** kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

**(c) Mradi wa Maji Maswa**

**129. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Maswa unaogharimu **Shilingi bilioni 3.35** unaendelea kutekelezwa kwa kujenga mtambo wa kusafisha na kutibu maji katika Bwawa la New Sola. Hadi mwezi Aprili 2019, ujenzi wa mradi huo umefikia **asilimia 90**. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5.9** hadi **lita milioni 10.37** na hivyo, kuwahakikishia wananchi kupata huduma ya maji safi na salama katika Mji wa Maswa na vijiji vya Zanzui, Malita, Bayubi, Dodoma, Hinduki, Mwasita, Mwabayanda, Ng'wigwa, Iyogelo, Mwadila na Mwabujiku.

**(d) Mradi wa Maji Wanging'ombe**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo yanayohudumiwa na mradi wa kitaifa wa maji Wanging'ombe kwa ghamra ya **Shilingi bilioni 1.93**. Hadi mwezi Aprili 2019, ukarabati wa matanki **44** ya kuhifadhi maji na mabirika **59** ya kunyweshea mifugo umekamilika na kazi inayoendelea ni ukarabati wa chanzo cha Mbukwa. Kwa ujumla ukarabati wa mradi umefikia **asilimia 85**. Kukamilika kwa ukarabati huo kutapunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia 76** za mwaka 2016 hadi **asilimia 61** mwaka 2019. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mradi huo.

(e) Mradi wa Maji Masasi - Nachingwea

131. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara imekamilisha kazi ya upanuzi wa mtandao wa kusambaza maji katika baadhi ya maeneo yanayohudumiwa na mradi wa kitaifa wa maji Masasi – Nachingwea ambazo zimegharimu **Shilingi milioni 870.74**. Kukamilika kwa kazi hizo kumewanufaisha wananchi wapatao **24,077** wa vijiji nya Mtepeche, Magereza, Mailisita, Mkotokuyana na Naipanga vilivypo Wilayani Nachingwea; vijiji nya Chiyapi, Nandanga, Ipingo, Lucheregwa, Mbecha na Litama vilivypo Wilayani Ruangwa; na Kijiji cha Chikunja kilichopo katika Halmashauri ya Mji wa Masasi. Aidha, katika kuwapatia huduma ya majisafi na salama wakazi wa Masasi na Nachingwea, Serikali itajenga mtambo wa kutibu na kusafisha maji katika chemchemi ya Mbwinji ambapo Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu amepatikana na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo mwezi Juni 2019. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma ya maji kwenye maeneo yanayohudumiwa na mradi huo.

*4.2.4.5. Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira  
Katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na  
Bagamoyo*

132. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam pamoja na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Miradi inayotekeliza na iliyopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Visima Virefu nya Kimbiji na Mpera

133. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa visima nya Kimbiji na Mpera unaohusisha uchimbaji wa visima virefu **20** kwa gharama ya **Shilingi bilioni 18** na hadi mwezi Aprili 2019, visima **19** vimechimbwa. Kukamilika kwa mradi wa visima nya Mpera kutawanufaisha wakazi wa maeneo ya Gongo la Mboto, Chanika, Luzando,

Pugu, Mpera, Chamazi, Kitunda, Ukonga, Kinyerezi na Uwanja wa Ndege; na visima vya Kimbiji vitawanufaisha wakazi wa maeneo ya Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Tandika, Keko na Chang'ombe. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 3** kwa ajili ya kuanza uendelezaji wa miundombinu ya kusambaza maji kwa visima **vitano** vya Kimbiji ambapo zabuni kwa ajili ya uendelezaji wa visima hivyo imetangazwa. Serikali inaendea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha uendelezaji wa miundombinu ya kusambaza maji kwa mradi huo.

**(b)      Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

**134.      Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza majisafi katika maeneo ya Tegeta hadi Mpiji, Mpiji hadi Bagamoyo na Mbezi hadi Kiluvya kwa fedha za mkopo kiasi cha **Dola za Marekani milioni 32.93** kutoka Serikali ya India. Kazi zilizotekelizwa ni pamoja na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 511.6**; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa **lita milioni 5** katika eneo la Salasala; na ujenzi wa matanki manne yenye ujazo wa **lita milioni 6** kila moja katika maeneo ya Changanyikeni, Wazo, Bunju na Bagamoyo. Mradi huo unawanufaisha wakazi wa Mji wa Bagamoyo na vitongoji vyake, eneo la uwekezaji la Bagamoyo (*EPZ*), Mpiji, Bunju, Mabwepande, Boko, Mbweni, Tegeta, Ununio, Wazo, Madale, Mivumoni, Salasala, Kinzudi, Matosa, Mbezi Juu, Goba, Changanyikeni, Makongo, Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Msakuzi, Makabe, Malamba Mawili na Msigani.

**135.      Mheshimiwa Spika**, Serikali imepata **Dola za Marekani milioni 86** kutoka Benki ya Dunia; kat i ya fedha hizo, **Dola za Marekani milioni 56** ni kwa ajili ya ujenzi wa matanki na kupanua mtandao wa kusambaza maji wenye urefu wa **kilomita 1,440** na kuunganisha wateja **64,000** katika maeneo yote ya mradi, **Dola za Marekani milioni 20** ni kwa ajili ya mradi wa kupunguza upotevu wa maji katika Jiji la Dar es Salaam

na **Dola za marekani milioni 10** ni kwa ajili ya ununuzi wa dira za maji **50,000** na vifaa vya uboreshaji wa huduma ya maji. Hadi mwezi Aprili 2019, Mkandarasi wa mradi huo amepatikana na ujenzi wa mradi huo unatarajija kuanza katika mwaka 2019/2020.

**(c) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

136. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa bwawa la Kidunda unaotarajija kugharimu **Dola za Marekani milioni 215**. Lengo la mradi huo ni kuhakikisha maji katika Mto Ruvu ambaao ni chanzo kikubwa cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka. Kazi ya usanifu wa bwawa pamoja na ulipaji wa fidia kwa wakazi watakaopisha ujenzi wa bwawa hilo imekamilika. Mradi utajumuisha ujenzi wa bwawa lenye **mita za ujazo milioni 190** kwa ajili ya kuhifadhi maji yatakayowezesha mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini kupata maji ya kutosha katika kipindi chote cha mwaka; ujenzi wa kituo cha kufua umeme **Megawati 20**; ujenzi wa njia ya msongo mkubwa wa umeme kutoka Kidunda hadi Chalinze; na ujenzi wa barabara yenye urefu wa **kilomita 76** kutoka Ngerengere hadi Kidunda. Ujenzi wa mradi utaanza baada ya fedha kupatikana.

**(d) Kuboresha Miundombinu ya Uondoaji Majitaka**

137. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaboresha huduma ya usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam kwa kutekeleza miradi ya uondoaji majitaka. Miradi hiyo itawezesha kufikia lengo la kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya uondoaji majitaka kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 30** ifikapo mwaka 2020. Miradi hiyo inatarajija kujengwa katika maeneo matatu ya Jangwani, Kurasini na Mbezi Beach kama inavyoelezwa hapa chini: -

**(i) Eneo la Jangwani**

138. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka kwa kushirikiana

na Serikali ya Korea Kusini utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 90.09**. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri atakayesimamia mradi huo amepatikana na ameanza kazi ya mapitio ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni. Mradi huo utahusisha ujenzi wa mfumo wa majitaka wa mabomba yenye urefu wa **kilomita 376** kutoka maeneo ya katikati ya Jiji, Ubungo, Kinondoni, Magomeni, Mwananyamala, Msasani na Ilala hadi kwenye mtambo wa kusafisha majitaka utakaojengwa eneo la Jangwani. Mtambo huo utakuwa na uwezo wa kusafisha **lita milioni 200** za majitaka kwa siku. Vilevile, ujenzi wa mradi utahusisha kubadili mwelekeo wa bomba linalomwaga majitaka baharini na kuyapeleka kwenye mtambo wa Jangwani. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka 2019/2020 na Serikali imetenga **Shilingi bilioni 10** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**(ii) Eneo la Kurasini**

**139. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika eneo la Kurasini utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 100** ambapo majadiliano ya mkataba wa kifedha yanaendelea. Mradi utahusisha ujenzi wa mtambo wenye uwezo wa kusafisha majitaka **lita milioni 11** kwa siku na ujenzi wa mfumo wa mabomba ya majitaka yenye urefu wa **kilomita 90** katika maeneo ya Keko, Chang'ombe, Kurasini, Temeke na Uwanja wa Taifa. Hadi mwezi Aprili 2019, Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wakazi watakaopisha upanuzi wa eneo la mradi na taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayefanya upembizi yakinifu wa mradi zinaendelea.

**(iii) Eneo la Mbezi Beach**

**140. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika maeneo ya Mbezi Beach, Kawe na Kilongawima utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 65** utatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Mradi huo utahusisha ujenzi wa mtambo mpya utakaojengwa

eneo la Mbezi Beach utakaokuwa na uwezo wa kusafisha **lita milioni 16** kwa siku pamoja na ujenzi wa mfumo wa mabomba ya majitaka yenyeye urefu wa **kilomita 97**. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri atakayesimamia mradi na kufanya mapitio ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni amepatikana. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 11** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

#### **4.2.4.6. Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Katika Jiji la Dodoma**

**141. Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Dodoma ili kuendana na uhitaji mkubwa wa maji uliopo kwa sasa. Miradi inayotekeliza ni kama ifuatavyo:-

**(a) Ujenzi wa Mradi wa Maji Katika Mji Mpya wa Serikali – Ihumwa, Dodoma**

**142. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatekeleza mradi wa maji katika Mji Mpya wa Serikali uliopo eneo la Ihumwa. Utekelezaji wa mradi huo umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza iliyogharimu **Shilingi bilioni 3.6** imekamilika na ilihuisha kazi za upimaji wa maji chini ya ardhi, ujenzi wa tanki la kukusanya maji lenye ujazo wa **lita 200,000**; tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa **lita milioni 1**; uchimbaji wa visima **saba**, ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 4.5** kutoka kwenye tanki la kukusanya maji hadi kwenye tanki la kuhifadhi maji; ununuzi wa pampu **nane**; ujenzi wa nyumba za mitambo; kufunga transfoma pamoja na kupeleka umeme kwenye visima.

**143. Mheshimiwa Spika,** awamu ya pili ya mradi inayogharimu **Shilingi milioni 508** inahusisha ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenyeye urefu wa **kilomita 11.2** na ujenzi wa chemba **27** za maji. Hadi mwezi Aprili 2019, utekelezaji wa awamu hiyo umefikia **asilimia 80**. Mradi huo utawezesha upatikanaji wa huduma ya maji ya uhakika

katika Mji wa Serikali hususan katika maeneo yote ya majengo ya Wizara mbalimbali za Serikali.

**(b) Miradi ya Kusambaza Maji Kwenye Maeneo Yasiyo na Huduma**

**144. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma inaendelea na taratibu za kupata mkopo wa **Shilingi bilioni 1.5** kuitia utaratibu wa Mfuko wa *Investment Financing Facilities – Output Based Aid (IFF-OBA)* unaofadhliliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (KfW). Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza maji kwenye maeneo yasiyo na huduma ya Chidachi, Ndachi, Nzuguni, Njedengwa/Medeli, Kizota na Mwangaza. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mara baada ya kupata fedha hizo za mkopo.

**(c) Mradi wa Bwawa la Farkwa**

**145. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeweka mkakati wa muda mrefu wa kuwapatia huduma ya maji ya uhakika wakazi wa Mji wa Dodoma kwa kujenga bwawa la Farkwa katika Wilaya ya Chemba. Bwawa hilo litakuwa chanzo kikuu cha maji kwa Mji wa Dodoma na litaongeza uzalishaji wa maji kwa zaidi ya ujazo wa **lita milioni 120** kwa siku, kiasi ambacho kitatosheleza mahitaji ya maji ya watu zaidi ya **milioni 1** wa Mji huo. Hadi mwezi Aprili 2019, tathmini ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi imekamilika.

**(d) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma za Majisafi na Uondoaji Majitaka Katika Jiji la Dodoma na Chamwino**

**146. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeajiri Mtaalamu Mshauri anayefanya upembuzi yakinifu, tathmini ya athari za kimazingira na kijamii na usanifu wa kina wa mradi wa kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira Jijini Dodoma na Chamwino. Pamoja na kazi hizo, Mtaalam huyo atafanya kazi ya kutafuta vyanzo vingine vya maji kwenye maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dodoma. Lengo ni kutambua mahitaji halisi ya majisafi na huduma ya uondoaji

wa majitaka. Kwa sasa Mtaalam huyo anaendelea na kazi hiyo inayotarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019.

**(e) Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Uondoaji Majitaka**

**147. Mheshimiwa Spika,** Serikali imepanga kuboresha huduma za uondoaji majitaka katika Jiji la Dodoma kwa kujenga miundombinu ya uondoaji wa majitaka kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 56**. Hadi mwezi Aprili 2019, eneo kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kusafisha majitaka limepatikana katika eneo la Nzuguni. Aidha, mitandao ya kukusanya majitaka itajengwa kwenye maeneo ya Area A, Chadulu, Chinangali, Kikuyu, Makole, Ipagala, Urban Renewal East and West, Viwandani, Mlimani, Medeli, Ilazo, Kisasa, NCC na Nkuhungu. Vilevile, ukarabati wa mtandao wa majitaka utafanyika kwenye maeneo ya Area C na Area D. Katika mwaka 2019/2020, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

**4.2.4.7. Miradi ya Maji Mijini Inayotarajiwa Kutekelezwa Katika Maeneo Mbalimbali**

**(a) Mradi wa Kutoa Maji Mto Malagarasi Kwenda Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka**

**148. Mheshimiwa Spika,** mpango wa awali ulikuwa ni kuchukua maji kutoka Mto Malagalasi kupeleka katika miji ya Urambo na Kaliua. Hata hivyo, kutokana na gharama kubwa za kutekeleza mpango huo, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mji wa Tabora ambao utapata maji kutoka bomba kuu la *KASHWASA* na kupeleka katika miji hiyo. Mradi huo utatekelezwa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Mradi utakapokamilika utahudumia wakazi 607,086 wa miji hiyo.

**(b) Mradi wa Maji Katika Miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi**

**149.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana Benki ya Maendeleo ya Ujeruman (KfW) pamoja na *Green Climate Fund (GCF)* itatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi. Mradi huo utatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ya mradi inatarajiwa kugharimu **Euro milioni 127.7**, ambapo **Euro milioni 25** zitatolewa na KfW na **Euro milioni 102.7** zitatolewa na *Green Climate Fund (GCF)*. Awamu hiyo itahusisha miji ya Nyashimo, Bariadi, Lagangabilili pamoja na vijiji **253** vilivypopo ndani ya Kilomita 12 kutoka bomba kuu. Awamu ya pili ya mradi huo itahusisha miji ya Mwanhuzi na Maswa ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa awamu hiyo. Aidha, Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kina wa mradi na anatarajia kukamilisha kazi hiyo mwezi Aprili, 2019. Mradi unatarajiwa kuwanufaisha wakazi wapatao **834,204** katika maeneo utakapotekelezwa mradi huo. Katika mwaka 2019/2020, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 19.51** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**(c) Mradi wa Maji katika Mji wa Morogoro**

**150.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na upungufu wa maji katika Manispaa ya Morogoro, Serikali kwa kushirikana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa gharama ya **Euro milioni 70**. Lengo la mradi ni kuongeza urefu wa tuta la Bwawa la Mindu kwa mita 2.5 ili kuongeza ujazo wa maji kutoka **lita bilioni 12** hadi **lita bilioni 20** pamoja na ujenzi wa miundombinu ya majitaka. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu na Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii. Vilevile, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri atakayeandaa Mpango Kabambe wa Hali ya Rasilimali za Maji (*Water Resource Master Plan*) katika Manispaa ya Morogoro pamoja na kuijengea uwezo Mamlaka zinaendelea.

(d) **Mradi wa Maji katika Miji ya Mtwara na Babati**

151. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya itatekeleza mradi wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya Mtwara na Babati kwa gharama ya **Euro milioni 18.9**. Hadi mwezi Aprili 2019, Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa mradi na ujenzi wa mradi utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu huo.

(e) **Miradi ya Usafi wa Mazingira katika Miji ya Musoma na Bukoba**

152. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency - AFD*) itatekeleza miradi ya usafi wa mazingira katika Manispaa ya Musoma na Bukoba ambayo itagharimu **Shilingi bilioni 24.87**. Kwa upande wa Manispaa ya Musoma, Mkandarasi amepatikana na kazi zitakazotekelzwa ni pamoja na ujenzi wa mtandao wa majitaka wenye urefu wa **kilomita 50**, ufungaji wa pampu **nne** za kusukuma majitaka, ujenzi wa vyoo **58** katika shule na vyoo **tisa** katika maeneo ya jamii. Mradi huo ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuunganisha wateja **1,200** na kuwanufaisha wakazi wapatao **200,000** ifikapo mwaka 2025. Katika Manispaa ya Bukoba taratibu za kuajiri Mtaalam Mshauri atakayefanya usanifu pamoja na usimamizi wa ujenzi zinaendelea.

(f) **Mradi wa Maji katika Miji 29**

153. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India, itatekeleza miradi ya uboreshaji wa huduma ya maji katika miji **29** ikiwemo Zanzibar. Gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ni **Dola za Marekani milioni 500**. Taratibu za kupata Wataalamu Washauri watakaofanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni zinaendelea. Ujenzi wa miradi katika miji hiyo unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2019/2020. **Kiambatisho Na. 6** kinaonesha miji itakayonufaika na fedha hizo.

#### **4.2.4.8. *Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini***

**154.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Mpanda na ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Maji Geita umefikia **asilimia 92**. Aidha, ujenzi wa ofisi unaendelea katika Mamlaka ya Jiji la Arusha ambao umefikia **asilimia 5** pamoja na miji ya Tabora (**asilimia 40**), Igunga (**asilimia 96**), Nzega (**asilimia 62**) na *KASHWASA* ujenzi umefikia **asilimia 79**. Kukamilika kwa ofisi hizo kutaziwezesha Mamlaka za Maji kuweza kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ili kuongezea ujuzi katika utendaji kazi.

#### **4.2.4.9. *Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Mijini***

**155.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kukamilisha miradi ya maji mijini inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini. Jumla ya **Shilingi bilioni 248.42** zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 100.42** na fedha za nje ni **Shilingi bilioni 148.00**. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2019/2020 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji mijini umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 7**.

#### **4.2.5. *Utekelezaji wa Majukumu Katika Taasisi Zilizo Chini ya Wizara***

##### **4.2.5.1. *Mfuko wa Taifa wa Maji***

**156.** **Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maji ni Taasisi yenyе jukumu la kutafuta vyanzo vya mapato ya Mfuko, kukusanya mapato, kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi yake. Lengo la Mfuko ni kuwekeza kwenye miradi ya huduma za maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidaka maji, kipaumbele

ikiwa ni kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa huduma ya maji hususan maeneo ya vijijini.

157. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009, imeainisha vyanzo vyaa mapato ya Mfuko ambavyo ni fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Hadi mwezi Aprili 2019, Mfuko wa Maji umepata kiasi cha **Shilingi bilioni 93.66** sawa na **asilimia 59.1** ya makadirio ya mapato ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 91.52** sawa na **asilimia 98** zilipelekwa kwa watekelezaji wa miradi ya maji kwenye maeneo mbalimbali nchini. Kati ya fedha zilizopelekwa kwa watekelezaji, **Shilingi bilioni 47.77** sawa na **asilimia 52** zilitumwa kwenye Halmashauri 120 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini; **Shilingi bilioni 24.05** sawa na **asilimia 26** zilitumwa kwenye Mamlaka 30 za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa ajili kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika maeneo ya pembezoni mwa miji pamoja na miji midogo kwenye mikoa husika; **Shilingi bilioni 17.84** sawa na **asilimia 19** zilitumwa kwenye miradi inayosimamiwa moja kwa moja na Wizara; na **Shilingi bilioni 1.86** sawa na **asilimia 2** alilipwa DDCA kwa ajili ya mikataba ya uchimbaji visima na ujenzi wa mabwawa hususan kwenye maeneo ya vijijini. Mchanganuo wa fedha za Mfuko wa Maji zilizotumwa kwa Watekelezaji mbalimbali umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 8**.

#### 4.2.5.2. *Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)*

158. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wizara kuitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*Drilling and Dam Construction Agency - DDCA*) iliendelea kutekeleza majukumu ya kuchimba visima, kujenga mabwawa, kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi na kuchunguza ubora wa udongo kwa ajili ya shughuli za ujenzi nchini. Hadi mwezi Aprili 2019, *DDCA* imefanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **195** kwa ajili ya uchimbaji wa visima, ukarabati wa visima **21** na kufunga pampu **saba**

za mkono na umeme. Vilevile, Wakala huo umeendelea kutekeleza mikataba ya kuchimba visima virefu **102** katika maeneo mbalimbali nchini.

**159. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, Wakala umekamilisha mikataba ya ujenzi wa mabwawa ya ujazo wa kati ya Mwamapalala na Nhocola yaliyopo Wilayani Itilima Mkoani Simiyu. Vilevile, mikataba wa ujenzi wa bwawa la Mbangala liliopo Wilaya ya Songwe Mkoani Songwe unaendelea na utekelezaji wake umefikia **asilimia 35**. Aidha, uchunguzi wa udongo katika maeneo **matatu**, kujenga mfumo wa kusambaza maji katika maeneo **mawili** na kupima ubora wa mabomba ya kusambaza maji katika miradi **mitano** umefanyika. Vilevile, Wakala umeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu katika usanifu wa mabwawa **matano** ya Namasogo, Mkangaula, Chilunda, Nangomba na Maratani yatakayojengwa katika Wilaya ya Nanyumbu Mkoani Mtwara.

**160. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wakala umepanga kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **400**, kuchimba visima **400**, kukarabati visima **50**, kufunga pampu za maji **55**, kujenga bwawa **moja** la ujazo wa kati, kujenga bwawa **moja** dogo, kukarabati mabwawa ya ujazo wa kati **manne**, kujenga mifumo ya kusambaza maji kwenye maeneo **manne** na kufanya uchunguzi wa udongo kwa ajili ya shughuli za ujenzi katika maeneo **35**.

#### *4.2.5.3. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA)*

**161. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kuisimamia EWURA ili iweze kutekeleza majukumu yake ya udhibiti katika sekta za maji na nishati. Majukumu hayo ni pamoja na kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao.

**162. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa sekta ya maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini. Hadi mwezi Aprili 2019, *EWURA* ilitoa leseni **mbili** za kutoa huduma ya majisafi na majitaka kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji ya Vwawa-Mlowo na Karatu. Vilevile, *EWURA* ilitathmini na kuidhinisha bei mpya za huduma ya maji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira **26**. Aidha, *EWURA* ilipitisha Mipango-Biashara kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira **15** na kuidhinisha mikataba **mitano** ya huduma kwa mteja. Pia, *EWURA* imetoa taarifa za utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka 2017/18, ambazo zinatoa mwelekeo wa mamlaka za maji nchini na kuweza kusaidia Wizara pamoja na wadau wa sekta ya maji katika kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira.

**163. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Mamlaka hizo zinaendelea kutoa huduma ya maji iliyo bora na endelevu, *EWURA* ilikagua miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na majitaka katika Mamlaka **57** na kuzishauri kuhusu taratibu bora za uendeshaji, matengenezo, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu kwa huduma endelevu. Vilevile, *EWURA* ilifanya uhakiki wa ubora wa majisafi katika Mamlaka **48** na uhakiki wa ubora wa majitaka yanayotoka katika mabwawa ya kusafisha majitaka katika Mamlaka **saba** ili kujiridhisha kama majitaka hayo yanakidhi viwango vya ubora unaokubalika kurudishwa kwenye mazingira. Matokeo ya ukaguzi huo yanaisaidia *EWURA* kutoa maelekezo na ushauri kwa mamlaka husika katika kuboresha huduma na kutunza mazingira.

**164. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020 *EWURA* itaendeleza ushirikiano wa karibu kwa kupokea na kutekeleza miongozo inayotolewa na Wizara zinazosimamia sekta za maji na nishati kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

#### 4.2.5.4. *Chuo cha Maji*

**165.** **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Maji ni Wakala unaosimamiwa na Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Maji. Chuo hicho kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuandaa wataalam, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalam unaohitajika katika sekta za maji na umwagiliaji. Utekelezaji wa majukumu hayo unazingatia Sera na miongozo ya Wizara pamoja na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundı (*NACTE*). Mafunzo yanayotolewa na Chuo katika ngazi ya Stashahada ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*), Haidrolojia na Hali ya Hewa (*Hydrology and Meteorology*), Haidrojolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*), Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*), pamoja na Teknolojia ya Maabara na Ubora wa Maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada, Chuo kinatoa fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation Engineering*). Vilevile, Chuo kinatoa mafunzo ya muda mfupi kulingana na mahitaji ya wadau wa sekta za maji na umwagiliaji.

**166.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/2019, jumla ya wanafunzi **652** walidahiliwa na kati ya hao, wanafunzi **495** ni wa stashahada (*water technicians*) na wanafunzi **157** ni wa shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor in Water Resources and Irrigation Engineering*). Udhahili huo umeongeza idadi ya wanafunzi kutoka **2,027** mwaka 2017/2018 hadi **2,151** mwaka 2018/2019. Kati ya hao, wanafunzi **1,543** ni wa ngazi ya Stashahada na wanafunzi **608** ni wa ngazi ya Shahada ya kwanza. Vilevile, Mfuko wa Mafundi Sanifu (*Water Technicians Fund*) ulifadhili jumla ya wanafunzi **79** na kati yao wanafunzi **40** ni wanafunzi wa kike. Hii imewezesha kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike Chuoni kutoka **547** mwaka 2017/2018 hadi **635** mwaka 2018/2019 sawa na **asilimia 29** ya wanafunzi wote. Aidha, jumla ya wanafunzi **309** walihitimu mafunzo yao na kati yao, wanafunzi **98** ni wa Shahada na **211** wa Stashahada.

167. **Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo kwa wanafunzi, Chuo kimeingia mkataba kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Chuo pamoja na ununuzi wa vifaa vya maabara ya *Hydraulics*. Aidha, katika kuhakikisha Chuo kinatoa taaluma bora, kimepanga kuwaendeleza watumishi kimasomo ambapo jumla ya watumishi **17** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao watumishi **16** wako katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*) na mtumishi **mmoja** ni wa shahada ya pili (*Masters*).

168. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Chuo kimepanga kudahili wanafunzi **1,200**. Vilevile, Chuo kitaendelea kuboresha mazingira ya kazi na ya kutoa mafunzo kwa kufanya ukarabati wa majengo, ikiwemo zilizokuwa ofisi za Wizara ya Maji – Ubungo, madarasa, karakana za mafunzo na mifumo ya majisafi na majitaka. Aidha, Chuo kitaongeza vifaa vya kufundishia katika maabara, kununua vitabu mbalimbali vya rejea pamoja na kuwapatia watumishi mafunzo ya muda mrefu na ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo.

#### 4.2.6. *Masuala Mtambuka*

##### 4.2.6.1. *Sheria*

169. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 umekuwa ukisimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na.11** ya mwaka 2009; Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009; na Sheria ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam **Na. 20** ya mwaka 2001. Wizara imeendelea kutoa elimu ya sheria hizo kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji na Vyombo vya Watumiaji Maji kupitia warsha, mikutano, semina, mafunzo, makongamano na vyombo vya habari. Wizara pia inaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria za maji na hatua za kuchukua dhidi ya wale wanaokiuka. Sheria hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Bunge ([www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz)) na kanuni za Sheria za Maji

zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Maji ([www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)).

**170. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2019, Wizara imekamilisha maandalizi ya Sheria Mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019 (*The Water Supply and Sanitation Act 2019*) ambayo imetungwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu tarehe 31 Januari, 2019. Vilevile, Wizara inaendelea kukusanya maoni ya wadau mbalimbali ili kuifanyia mapitio Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na.11 ya mwaka 2009 (*The Water Resources Management Act*). Aidha, Amri ya kulifuta Shirika la DAWASCO (*DAWASCO dis-establishment Order*) iliandaliwa na kusainiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Julai, 2018 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 414 la tarehe 10 Agosti, 2018. Kutokana na Amri hiyo, kwa sasa imebaki Taasisi moja ambayo ni DAWASA inayowajibika kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani.

**171. Mheshimiwa Spika**, Ili kuimarisha mfumo na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji, Wizara imekamilisha kuandaa kanuni **sita** ambazo ni:

(a) *Water Resources Management (Water Resources Classification System) Regulations, GN 156 ya tarehe 20/04/2018;*

(b) *Water Resources Management (Control And Management of Storm Water) Regulations, GN 153 ya tarehe 20/04/2018;*

(c) *Transfer of Water Use, Discharge and Groundwater Permits Regulations, GN 157 ya tarehe 20/04/2018;*

(d) *Water Resources Management (Water Well Quality Monitoring) Regulations, GN 155 ya tarehe 20/04/2018;*

(e) *Water Supply and Sanitation (Licensing Board) Regulations, GN 154 ya tarehe 20/04/2018; na*

(f) *The National Water Investment Fund Regulations, GN 253 ya tarehe 08/06/2018.*

Vilevile, Notisi **nne** za kutangaza Mamlaka za Maji za Miji Midogo na Makao Makuu ya Wilaya zimeandaliwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.Oda na Notisi hizo ni:

(a) *Water Supply and Sanitation (Mbeya Urban Water Supply and Sanitation Authority)(Extension of Service Area) Notice, GN 250 ya tarehe 01/06/2018;*

(b) *Water Supply and Sanitation (Arusha Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area) Notice, 2018; GN 490 ya tarehe 07/09/2018;*

(c) *Water Supply and Sanitation (Moshi Urban Water Supply and Sanitation Authority) (Extension of Service Area) Notice, 2018; GN 573 ya tarehe 5/10/2018; na*

(d) *Water Supply and Sanitation (Establishment of Mbambabay, Madaba, Newala, Tandahimba, Mahuta na Nanyamba Water Supply and Sanitation Authorities) Notice, 2018; GN. No. 67 ya tarehe 3/03/2018.*

**172. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea na utayarishaji wa Kanuni za Sheria Mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 na kuendelea kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria na miongozo mbalimbali ya kisheria kwa wadau wa sekta ya maji kadri itakavyohitajika.

#### **4.2.6.2. Maendeleo ya Rasilimali Watu**

**173. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2019, jumla ya watumishi

**1,069** wamepata mafunzo na kati yao watumishi **tisa** walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi, watumishi **54** walipata mafunzo ya muda mfupi njie ya nchi na watumishi **1,006** walipata mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Aidha, katika mwaka 2018/2019, mahitaji ya watumishi kwa mujibu ya ikama iliyoidhinishwa ni nafasi **1,322** ambapo kibali cha kuajiri watumishi wapya **67** kimepatikana.

#### **4.2.6.3. Ujenzi wa Majengo ya Ofisi za Wizara**

**174.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi, Wizara imeendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi yaliyopo Makao Makuu ya nchi, Dodoma. Hadi mwezi Aprili 2019, ukarabati wa jengo la ofisi (Maji House) lilitopo maeneo ya Posta, Dodoma umefikia **asilimia 60** na ujenzi wa jengo la ofisi lilitopo kwenye Mji wa Serikali, Ihumwa umekamilika.

#### **4.2.6.4. Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**175.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu (*National Anti-Corruption Strategy and Action Plan - NACSAP III*) kwa lengo la kupambana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Vilevile, Wizara iliunda Kamati ya Uongozi na Usimamizi pamoja na Kamati ya Uadilifu kwa ajili ya kusimamia mapambano dhidi ya rushwa ngazi ya Wizara na Taasisi zake. Tangu kuundwa kwa Kamati hizo, malalamiko dhidi ya viashiria vya rushwa yamepungua kwenye manunuza ya wakandarasi na huduma zinazotolewa.

#### **4.2.6.5. UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY)**

**176.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Mwongozo wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa kutoa elimu kuhusu magonjwa hayo kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake. Hadi mwezi Aprili 2019, mafunzo kwa watumishi kuhusu kujikinga na magonjwa hayo yametolewa, na posho kwa ajili ya kununua lishe bora na usafiri kwa

watumishi **nane** wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kutolewa. Katika mwaka 2019/2020 Wizara itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha watumishi wake kuendelea kupima afya zao na kujikinga dhidi ya magonjwa hayo.

#### **4.2.6.6. Jinsia**

**177. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia katika Taasisi zake. Uwiano huo ni muhimu kwenye vyombo vya maamuzi, usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa miradi nchini. Suala hilo huzingatiwa katika uteuzi wa viongozi wa ngazi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zake kulingana na mpango wa kurithishana madaraka. Vilevile, uteuzi wa kamati na vikosi kazi mbalimbali huzingatia jinsia ili kuhakikisha watumishi wote wanashiriki kikamilifu katika kutekeleza majukumu yao bila kujali jinsia zao.

#### **5. CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2018/2019 NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

**178. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa kuzikabili ni kama ifuatavyo:-

##### **5.1. *Upatikanaji Mdogo wa Fedha za Kutekeleza Miradi ya Maji***

**179. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza miradi ya majisafi na usafi wa mazingira, Wizara imekuwa ikitabili na changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira. Fedha zinazopatikana zimekuwa hazitoshelezi mahitaji ya uwekezaji kwenye miradi ya maendeleo. Mathalani, katika mwaka 2018/2019, Wizara ilikasimiwa **Shilingi bilioni 673,214,033,677** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hata hivyo, hadi mwezi Aprili 2019, ni kiasi cha **Shilingi bilioni 343,486,935,592.46** kimepokelewa sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyoidhinishwa.

Kutopatikana kwa fedha za kutosha na kwa wakati kumesababisha baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati na mingine kushindwa kutekelezwa.

**180. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi ya sekta ya maji, Serikali ilianzisha Mfuko wa Taifa wa Maji ambao unatumika kama chanzo cha uhakika cha fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira na katika mwaka 2018/2019, Mfuko wa Taifa wa Maji umeidhinishiwa kiasi cha **Shilingi bilioni 158.5**. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo zaidi yya fedha ili kuongeza uwezo wa Mfuko katika kugharamia miradi ya maji nchini.

**181. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ili kupunguza nakisi ya bajeti Serikali iliona upo umuhimu wa kuihusisha sekta binafsi kuchangia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kugharamia miradi hiyo na kuiendesha. Ili kuweka mazingira mazuri kwa sekta binafsi kutekeleza jukumu hilo, Serikali ilianda miongozo mbalimbali ikiwemo Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, Sera ya Taifa ya Ubria baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*) ya mwaka 2009, Sheria ya Ubria baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 na Mkakati wa Ubria baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2012. Pamoja na kuwepo kwa miongozo hiyo, bado sekta binafsi hajahamasika ipasavyo kutekeleza miradi katika sekta ya maji. Vilevile, Serikali inaendelea kuboresha mfumo wa *PPP* ikiwa ni pamoja na kupitia Sheria na Kanuni zake ili kuweka mazingira mazuri zaidi kwa ajili ya sekta binafsi kuwekeza kwenye miradi ya ubia.

**182. Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi, Wizara itaendelea kujadiliana na wadau mbalimbali ikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi Zisizo za Kiserikali ili kuweka mikakati madhubuti ya kupata fedha za kutekeleza miradi ya maji.

**5.2. Uwezo Mdogo Katika Utekelezaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Miradi ya Maji**

**183. Mheshimiwa Spika**, baadhi ya miradi ya maji inayotekelawa imeshindwa kutoa huduma ya maji iliyotarajiwa kutokana na miradi hiyo kutokamilika kwa wakati na mingine kujengwa chini ya kiwango. Hali hiyo inasababishwa na baadhi ya Wataalam Washauri na Wakandarasi kuwa na uwezo mdogo katika kutekeleza miradi ya maji. Baadhi ya wakandarasi wamekuwa siyo wakweli wakati wa kuwasilisha taarifa zao kipindi cha manunuzi hususan taarifa za fedha, vifaa na wataalam. Katika kukabiliana na changamoto ya wakandarasi na wataalam washauri wasiokidhi matakwa ya mkataba, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali zikiwemo kuwapa onyo, kuwatoza riba ya kuchelewesha kazi (*liquidated damages*) na wakati mwininge kuvunja mikataba.

**184. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara ina upungufu wa wataalam kwa ajili ya usimamizi wa miradi inayotekelawa hivyo sehemu kubwa ya kazi kubaki chini ya Wataalam Washauri na wakandarasi. Mfano, mahitaji halisi ya watumishi kwa sekta ya maji ni **10,287** lakini waliopo ni **6,377** tu hivyo kuwa na upungufu wa watumishi **3,910**. Hali hiyo imesababisha baadhi ya miradi kukosa usimamizi thabitii na hivyo kutokamilika kwa wakati na wakati mwininge kujengwa chini ya kiwango. Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa wataalam katika sekta ya maji, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kupata kibali cha kuajiri watumishi watakaokidhi mahitaji. Aidha, Wizara inaendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo stahiki ya muda mfupi na muda mrefu ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**185. Mheshimiwa Spika**, aidha, miradi ya maji vijijini inapokamilika hukabidhiwa kwa wananchi kwa ajili ya kuiendesha kupitia Vyombo vya Watumiaji Maji (CBWSOs). Uendeshaji na usimamizi wa miradi hiyo umekuwa na

changamoto katika maeneo mengi ya vijijini kutokana na wananchi kutokuwa na ujuzi na taaluma za maji; uwezo wa kusimamia makusanyo ya fedha kutoka kwenye huduma za maji; kugharamia uendeshaji miradi hiyo; na kufanya matengenezo pindi miradi inapoharibika. Hali hiyo imesababisha, miradi mingi vijijini kutokuwa endelevu hivyo wananchi kukosa huduma iliyotarajija. Katika kukabiliana na changamoto za uendeshaji wa miradi ya maji, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo na kutoa miongozo kwa Vyombo vya Watumiaji Maji ili viweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Vilevile, Serikali imeboresha Sheria ya huduma za maji ambapo Sheria Mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 imeanzisha Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*RUWASA*) ambao utasimamia utoaji wa huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini. Aidha, muundo wa Vyombo vya Watumiaji Maji Vijijini umefanyiwa mabadiliko na kuimarishwa zaidi katika Sheria hiyo.

### **5.3. *Changamoto Katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji***

**186. Mheshimiwa Spika**, mgawanyiko wa rasilimali za maji nchini hauko sawa, yapo maeneo yenye rasilimali nyingi za maji na maeneo mengine yana uhaba wa rasilimali hiyo. Serikali imegawanya usimamizi wa rasilimali za maji katika Bodi za Maji za Mabonde **tisa** ambazo zina majukumu ya kuhakikisha rasilimali za maji zinatunzwa, zinahifadhiwa, zinaendelezwa na zinagawanywa kwa matumizi mbalimbali. Vilevile, kunahitajika usimamizi madhubuti utakaohakikisha rasilimali za maji zinagawanywa kwa uwiano sawia unaotokana na kuanzisha na kuimarisha Taasisi zinazosimamia rasilimali hiyo zikiwemo Kamati za Vidaka Maji na Jumuiya za Watumia Maji. Kukamilika na kuimarika kwa mfumo wa kitaasisi kutahakikisha rasilimali za maji zinalindwa, kuhifadhiwa na kuwanufaisha watumiaji wa maji wote.

**187. Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Bodi za Maji za Mabonde zimekuwa na changamoto mbalimbali zinazosababisha zisitekeleze majukumu yake ipasavyo zikiwemo uhaba wa fedha, upungufu wa wataalam na vifaa

vya kazi. Changamoto hizo zimechangia usimamizi usioridhisha wa rasilimali za maji hivyo kusababisha uvamizi katika vyanzo vya maji, migogoro ya matumizi ya maji, uchafuzi wa vyanzo vya maji na matumizi holela ya maji. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara itaimarisha mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa rasilimali za maji kwa ajili ya matumizi endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye. Vilevile, Sheria ya Usimamizi wa Rasimali za Maji Namba 11 ya mwaka 2009 itafanyiwa mapitio ili iweze kusadifu mazingira ya sasa na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji.

#### **5.4. *Kiwango Kikubwa cha Upotevu wa Maji Kinachosababisha Upotevu wa Mapato***

**188. Mheshimiwa Spika**, kiwango kikubwa cha upotevu wa maji ni mielongoni mwa changamoto zinazozikabili Mamlaka za Maji katika miji mikuu ya mikoa, wilaya, miji midogo, miradi ya Kitifa pamoja na miradi ya maji vijijini. Upotevu huo wa maji unasababishwa na miundombunu chakavu na wizi wa maji. Hali hiyo inasababisha kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya maduhuli na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za matengenezo na uendeshaji wa miradi kutokana na uhaba wa fedha. Mathalan makadirio ya kiwango cha maji yasiyolipiwa kwa Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2019 yanaonesha mamlaka hizo kupoteza wastani wa jumla ya **Shilingi bilioni 51** kwa mwaka sawa na asilimia **33** ya upotevu wa maji. Kwa upande wa DAWASA, wastani wa upotevu wa maji kwa kipindi hicho ni asilimia **43** ambapo ni sawa na **Shilingi bilioni 80**.

**189. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekua ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na upotevu wa maji kwa kukarabati miundombini chakavu; na kuhakikisha Mamlaka zake zinaimarisha vitengo vya matengenezo ili viweze kukarabati mitando ya maji kwa wakati pindi mivujo inapojitokeza. Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya wizi wa maji, Mamlaka za Maji kwa kushirikiana na Halmashauri za Majiji/Manispaa/Miji husika zimeweka

mikakati ya kufuutilia wezi wa maji na kuwachukulia hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019.

**5.5. *Uwezo Mdogo wa Uwekezaji na Uendeshaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Unaotokana na Madeni Makubwa ya Ankara za Maji kwa Taasisi za Serikali***

**190. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini zimekuwa zikikabiliwa na changamoto ya Taasisi na Idara za Serikali kutumia huduma za maji bila kulipa gharama za huduma hizo kwa muda mrefu. Hali hiyo imesababishwa na malimbikizo ya madeni makubwa ya Ankara za matumizi ya huduma za maji na hivyo kusababisha Mamlaka za Maji kushindwa kutimiza majukumu yao katika kuendesha, kutengeneza na kuwekeza katika miundombinu ya maji hivyo kutoa huduma isiyokidhi mahitaji kwenye maeneo yao ya huduma. Hadi mwezi Aprili, 2019 madeni yanayodaiwa kwa Taasisi za Serikali ni **Shilingi bilioni 21.84**. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Mamlaka za Maji imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na kukutana na Taasisi husika na kuweka mikakati ya namna bora ya ulipaji wa madeni hayo.

**6. SHUKRANI**

**191. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, ninapenda sasa kuchukua fursa hii kuwatambua na kuwashukuru wadau mbalimbali waliochangia kuiwezesha Wizara ya Maji kufanikisha majukumu yake katika mwaka 2018/2019. Ninakiri kwamba, kufanikiwa huko kunatokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika hao ambao wanajumuisha nchi wahisani, mashirika ya maendeleo ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Ninapenda kuzishukuru nchi wahisani zikiwemo Korea Kusini, China, Uingereza, Marekani, Ujerumani, Japan, Uhlanzi,

Hispania, Ubelgiji, Ufaransa, India, Misri, Saudi Arabia na Kuwait.

**192. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninapenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo na Taasisi za kimataifa za fedha kwa misaada ya kitaalam na fedha katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank-WB*), Benki ya Maendeleo ya Africa (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (*Kuwait Fund*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*), *Global Environment Facility (GEF)*, *Green Climate Fund*, Shirika la Afya Duniani (*WHO*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*).

**193. Mheshimiwa Spika**, Mashirika na Taasisi za Kidini yameendelea kuongeza hamasa katika kuyafikia malengo tuliyojiweke. Hivyo, ninapenda kuyashukuru mashirika na Taasisi hizo ambazo ni *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA)*, *Norwegian Church Aid*, *Livingwater International*, *World Islamic League*, Shirika la Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, *Islamic Foundation*, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (*BAKWATA*), Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania (*KKKT*), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.

**194. Mheshimiwa Spika**, vilevile, nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshiriki katika kuendeleza sekta ya maji. Taasisi hizo ni pamoja na *Association of Tanzanian Water Suppliers (ATAWAS)*, *WaterAid*, *Tanzania Water and Sanitation Network*

(TAWASANET), Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (WAMMA), World Vision; World Wide Fund for Nature (WWF), Water Resources Integration Development Initiatives (WARIDI), Netherlands Volunteers Services (SNV), Plan International, Concern Worldwide, Bill and Melinda Gates Foundation, Water Mission (T), Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (IUCN), African Medical Research Foundation (AMREF) na Clinton HIV Aids Initiative.

**195. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mhe. Juma Hamidu Aweso (Mb), Naibu Waziri wa Maji; Prof. Kitila Alexander Mkumbo, Katibu Mkuu; Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelio, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara ya Maji; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia pamoja na kujituma kwao katika kuhakikisha majukumu ya Wizara ya Maji yanatimizwa. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa upendo, ushirikiano na msaada wao katika kipindi chote na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

## **7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020**

**196. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 634,196,197,530** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 23,726,309,000** ambapo **Shilingi 6,266,714,000** sawa na **asilimia 24** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 17,459,555,000** sawa na **asilimia 76** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 610,469,888,530** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 349,449,000,000** sawa na **asilimia 57** ni fedha za ndani na **Shilingi 261,020,888,530** sawa na **asilimia 43** ni fedha za nje.

**197. Mheshimiwa Spika**, ninaomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz).

**198. Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Maji, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. (*Makofii*)

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya leo hii kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mpandwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya ya kizalendo ya kuwatumikia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii pia kuwatachia kila la kheri Waislamu wote duniani katika Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan utakaoanza hivi karibuni. Ramadhan Karim. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii naomba iingie katika *Hansard* kama ilivyo katika vitabu vya taarifa ya Kamati milzogawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayoiswasilisha inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

- (a) Utekelezaji wa ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji - Fungu 49, kwa mwaka wa fedha 2018/2019;
- (b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2018/2019;
- (c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019;
- (e) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na
- (f) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo yatakayotolewa ni matokeo ya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, majadiliano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelawa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelawa. Baadhi ya ushauri uliotekelawa ni pamoja na uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijiji (Rural – Urban Water and Sanitation Authority - RUWASA) pamoja kukamiliwa kwa taratibu zote za upatikanaji wa fedha za mkopo kutoka Serikali ya India kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika miji 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo ya kutekeleza ushauri wa Kamati kwa lengo la kuimarisha upatikanaji maji safi na salama kwa wananchi. Pamoja na pongezi hizo, ili kuweza kupata matokeo tarajiwa ni vyema Wakala ulioanzishwa ukawezeshwa kwa kupatiwa rasilimali fedha na rasilimali watu ili uweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini pia kuwa baadhi ya ushauri uliotolewa haukutekeleza kikamilifu hususan kwenye ushauri uliohusu kuongeza tozo kwenye mauzo ya mafuta ya dizeli na petroli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia (100) kwa lita ili kutunisha Mfuko wa Maji, uvunaji wa maji ya mvua, upatikanaji wa maji safi na salama mjini na kupunguza ghamama za maji safi na salama miongoni mwa wakazi wa kaya duni mijini. Pendekezo la kuongeza tozo kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli siyo tu ni ushauri wa Kamati lakini pia ni Azimio la Bunge lako Tukufu liliopitishwa kuitia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2017 hadi 2019. Kamati inasisitiza uamuzi wa agizo hili la Bunge lako Tukufu litekelezwe kutokana na kuridhika na mafanikio yaliyofikiwa katika Bajeti ya mwaka 2018/2019 ambapo asilimia 67 ya pesa zilizopatikana na kutumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo maji vijiji zilitokana na makusanyo ya Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Maji na Umwagiliaji - Fungu 49, liliidhinishwa jumla ya Sh. 24,363,869,000. Kati ya fedha

hizo Sh. 6,266,714,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na Sh. 18,097,155,000 ni mishahara. Aidha, kiasi cha Sh. 673,214,033,677 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Sh. 443,214,033,677 sawa na asilimia 66 ni fedha za ndani ambapo kati ya fedha hizo, Sh.158,500,000,000 ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na Sh. 284,714,034,677 ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine vya ndani. Aidha, Sh. 229,999,999,000 sawa na asilimia 34 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2019 Wizara ya Maji - Fungu 49 ilikuwa imepokea fedha za matumizi mengineyo Sh. 2,905,702,353.15 sawa na asilimia 46, na mishahara Sh.13,747,840,611 sawa na asilimia 76 ya kiasi Kilichoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Aprili, 2019 zilikuwa Sh. 343,486,935,529.46 sawa na asilimia 51 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zillzoidhinishwa ambazo zinajumuisha fedha za Mfuko wa Maji na vyanzo vya ndani Sh. 155,096,701,543.56 na fedha za nje Sh.188,390,234,048.90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni kuhusu mwenendo wa utolewaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji - Fungu 49 zilizotolewa sawa na asilimia 51, ikilinganishwa na asilimia 22 ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga asilimia kubwa ya fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, jumla ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Sh.443,214,033,677.00. Kati ya fedha hizi Mfuko wa Maji ni Sh.158,500,000,000 na fedha kutoka vyanzo vingine vya ndani ni Sh.284,714,034,677.00. Hadi mwezi Aprili 2019, fedha za Mfuko wa Maji zilizotolewa ni asilimia 67, ilhali fedha kutokana na vyanzo vingine vya ndani ni asilimia 17 tu. Kamati inasisitiza ushauri iliokwisha utoa kuwa Mfuko wa Taifa wa Maji ndio chanzo cha uhakika cha ndani kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukusanyaji wa maduhuli, kwa upande wa maduhuli mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Maji ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya 5,071,000,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili, 2019 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya 4,127,958,000 sawa na asilimia 81 ya malengo ya ukusanyaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara. Katika ziara hiyo, Kamati ilikagua jumla ya miradi sita kama inavyoonekana katika Taarifa ya Kamati mliyopewa kipengele cha kwanza mpaka cha sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazopatikana katika miradi hiyo;

- (i) Ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini;
- (ii) Kuchelewa kupatikana kwa fedha za utekelezaji;
- (iii) Kukosekana umakini katika usadifu wa miradi;
- (iv) Usanifu na ujenzi wa baadhi ya miradi katika vijiji ambavyo vinapitiwa na miradi;
- (v) Kuchelewa kufanyika kwa mapitio ya usanifu na hivyo kupelekea miradi kuchelewa kukamilika kwa kipindi cha miaka miwili hadi mitano;
- (vi) Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi wa miradi;
- (vii) Ucheleweshaji wa kutoa msamaha wa kodi na ongezeko la thamani(VAT) kwa miradi ya maji;
- (viii) Ucheleweshaji wa vibali vya kazi (*working permit*) kwa wataalam wanaotekeliza miradi ya maji;
- (ix) Uwezo mdogo wa wakandarasi;
- (x) Kushindwa kupunguza maji yanayopotea;

(xi) Miradi ya maji safi kutotekelawa sambamba na mifumo ya uondoaji wa maji taka;

(xii) Ufanisi mdogo wa miradi ya maji vijijini kutokana na umeme kuwa na nguvu ndogo hivyo kushindwa kuendesha visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu miradi ya maendeleo kwa Sekta ya maji;

(i) Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo mapema na kwa kadri mikataba ilivyo ili kuepusha hasara na ghamama za miradi kuongezeka kutokana na ucheleweshaji;

(ii) watendaji wa Serikali kuwa makini wakati wa kufanya usanifu wa miradi kwani kukosekana kwa umakini katika usanifu wa miradi, kunapelekea ongezeko la kazi za miradi ambazo hazikuwa katika mikataba;

(iii) Kamati inatahadhirisha kuwa ni vema utoaji wa zabuni za utekelezaji wa miradi ya maji uzingatie uwezo wa makandarasi pamoja na mionganini mwao utoaji wa zabuni ili kuepusha kutoa miradi mingi kwa mkandarasi mmoja kwani hali hii imedhihirisha kucheleva kwa miradi kikamilifu kwa wakati.

(iv) Kamati inashauri Serikali kuwa na miradi ya maji iliyo vijijini itumie *pump* zinazoendeshwa kwa kutumia umeme wa juu (*Solar power*) ambazo ghamama za uendeshaji wake ni nafuu;

(v) Utekelezaji wa miradi unaofanyika kwa ushirikiano na wataalam wa kigeni ambao kwa mujibu wa Sheria huhitajika kupatikana kwa vibali;

(vi) Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kulipa wakandarasi kadri wanavyokamilisha mikataba yao ya ujenzi na kukabidhi miradi;

(vii) Taasisi ya Serikali kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama wa mazingira

kwa haraka. Kwa mfano kuna mabomba na vifaa vingine vya ujenzi wa visima vya maji vimekwama bandarini, Dar es Salaam toka mwezi Desemba, 2018 kutokana na mlolongo mrefu wa kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Fungu Namba 49. Fedha zilizoombwa kwa ajili matumizi ya kawaida. Ili kutekeleza kazi zillizopangwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Maji inaomba kuidhinisha kiasi cha shilingi 23,326,309,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,266,714,000 sawa na asilimia 24 ni kwa ajili ya gharama ya matumizi mengineyo (*Other Charges, OC*) na shilingi 17,459,595,000 sawa asilimia 76 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji inaomba iihdinishiwe jumla ya shilingi 610,469,888,530 sawa na asilimia 99.26 ya bajeti yote ya maji iliyoombwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 349,449,000,000 sawa na asilimia 57 ni fedha za ndani na shilingi 261,020,888,530 ni sawa na asilimia 43 ya fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Maji imepanga kukusanya shilingi 7,678,502,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Kamati kuhusu malengo ya bajeti na maombi ya fedha ya wizara. Kwa kuzingatia tatizo la upungufu wa maji safi na salama nchini na malengo yaliyowekwa kufikia upatikanaji wa maji safi na salama, asilimia 80 kwa vijiji na asilimia 95 kwa miji ifikapo mwaka 2020. Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji ya mwaka 2019/2020 hayakidhi kufikia malengo yaliyowekwa na kubainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji umeme,

kilimo na umwagiliaji, ufugaji, viwanda, usalama, uchukuzi pamoja na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa, jumla ya fedha za miradi za maendeleo kilichotengwa ni pungufu ya asilimia 9 ya fedha zilizoidhinishwa katika mwaka uliomalizika 2018/2019. Aidha, fedha za ndani zilizoidhinishwa zimepungua kwa asilimia 69 iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia asilimia 57 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo umeongezeka kutoka asilimia 34 kwa bajeti ya 2018/2019 mpaka asilimia 43 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kamati inasikitishwa na kitendo cha Serikali kupunguza fedha za ndani kwenye bajeti ya maendeleo, kwani kwa kutegemea fedha za nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kwa wananchi hakutatoa uhakika wa kuwapatia wananchi maji safi na salama ili kufikia asilimia 85 kwa wananchi wa vijijini na asilimia 95 kwa wananchi waishio mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo ya Kamati, naomba kuwasilisha maoni na ushauri kama ifuatavyo; moja, kuimarisha kitengo cha fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati imebaini kushuka kwa kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maendeleo iliyotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa asilimia 9 ikilinganishwa na bajeti ya 2018/2019. Ili kuwe na uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo, na kuwapatia wananchi maji safi na salama Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utengaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuimarisha makusanyo ya Mfuko wa Taifa wa Maji. Kwa miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuimarisha makusanyo ya Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kuongeza tozo la mafuta kwa kila lita ya mafuta ya petrol na diesel kutoka shilingi 50 hadi shilingi 100. Endapo ushauri huu wa Kamati

utazingatiwa, Kamati inaamini kuwa Mfuko wa Maji utakuwa ndiyo chanzo cha uhakika cha ndani kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijjini. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, mikakati ya uvunaji maji ya mvua kwa ajili ya matumizi. Kamati inashauri Serikali kutekeleza kwa vitendo mkakati wa namna ya kuvuna maji ya mvua nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni ujenzi wa miundombinu ya maji taka katika miji na makao makuu ya mikoa nchini. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji mipango na miradi mbalimbali ya maji taka na safi kwa mazingira na hasa ukizingatia miundombinu ya barabara nyingi imeendelezwa, hivyo ni vyema mifumo ya maji taka ikaenda sambamba na ujenzi wa barabara ili kuondoa gharama za ubomoaji barabara hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuimarisha na kutekeleza mpango mkakati wa kutumia maji kutoka Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina asilimia 41 ya Ziwa Tanganyika lenye ujazo wa maji safi na salama ya kunywa (*fresh water*) kiasi cha kilometa za ujezo 18,900 *cubic* ya kimiminika ambayo ni sawa na asilimia 17 ya maji yote ya kunywa ya kimiminika yaliyoko kwenye uso wa dunia nzima. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Maji kufanya juhudi ya kuanza kuvuna maji hayo mengi na kuyasambaza katika Mikoa yenye uhaba wa maji kama vile Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo majumbani na maendeleo viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kuimarisha tafiti za rasilimali maji na kuboresha mitaala ya elimu kwa umma kuhusu kutunza vyanzo vya maji. Kamati inatoa wito kwa Serikali kuwezesha watafiti nchini wawzeze kufanya tafifi za kina kuhusu wingi na ubora wa rasilimali maji nchini na juu ya ardhi kwenye kila upande wa nchi. Utatifi utakaofanyika

utawezesha kupanga mipango endelevu ya matumizi ya maji na wananchi wataweza kushauriwa ipasavyo kuhusu usimamizi na matumizi endelevu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Prof. Makame Mbarawa, Naibu wake Mhe. Jumaa Aweso, Katibu Mkuu Prof. Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu Kalobelio pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa napenda kushukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyotoa wakati wa kuitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, ndugu Dickson Bisile, Mkurugenzi Msaidizi kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza wajibu wake kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati amba ni Virgil Mtui, Rachel Nyega na msaidizi wake wa Kamati Mwimbe John.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,  
MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA  
WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019  
PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA  
WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2010 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

**1.1 MAJUKUMU YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagilajji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na maoni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvubi. Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Maji – Fungu 49 inahusika.

**1.2 MUUNDO WA TAARIFA**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji - fungu 49, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(b) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na

(e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, maoni na mapendekezo yatakayotolewa ni matokeo ya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa mbele ya Kamati, majadiliano kati ya Kamati na wadau mbalimbali na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelizwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI**

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitekeza katika uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.2 cha Sehemu ya Kwanza.

### **2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo nane (8) ya kipaumbele yafuatayo:-

(a) Mtiririko usioridhisha wa fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge;

(b) Umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo;

(c) Kuongeza tozo ya shilingi hamsini (50) hadi kufikia shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli ili kutunisha Mfuko wa Maji;

(d) Kufanya kazi changamoto zilizojitekeza katika zoezi la kuunganisha Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es salaam (DAWASA) na Shirika la Maji Safi na Maji Taka Dar es salaam (DAWASCO);

(e) Uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini na umuhimu wake katika kuharakisha upatikanaji wa maji vijijini;

(f) Kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama mijini pamoja na kupunguza gharama za maji safi na salama miongoni mwa wakaazi wa kaya duni mijini;

(g) Umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua, kama njia ya kukabiliana na uhaba wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali; na

(h) Kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za mkopo wa India kwa ajili ya miradi ya maji katika miji ishirini na sita (26).

**Mheshimiwa Spika**, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri uliotolewa na Kamati umetekelizwa, Baadhi ya ushauri uliotekelizwa ni pamoja na uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini (*Rural – Urbun Water and Sanitation Authority - RUWASA*) pamoja kukamilika kwa taratibu zote za upatikanaji fedha za mkopo kutoka Serikali ya India kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika miji 26.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo ya kutekeleza ushauri wa Kamati kwa lengo la kuimarisha upatikanaji maji safi na salama kwa wananchi. Pamoja na pongezi hizo, ili kuweza kupata matokeo tarajiwa ni vyema Wakala ulioanzishwa ukawezeshwa kwa kupatiwa rasilimali fedha na rasilimali watu ili uweze kutekeleza majukumu nyake kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia kuwa baadhi ya ushauri uliotolewa haukutekeleza kikamilifu hususan kwenye ushauri uliohusu kuongeza Tozo kwenye mauzo ya mafuta ya dizeli na petroli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia (100) kwa lita ili kutunisha Mfuko wa Maji, uvunaji wa maji ya mvua kama njia ya kukabiliana na uhaba wa maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali, kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na kuimarisha upatikanaji wa maji safi

na salama mijini na kupunguza ghamara za maji safi na salama miongoni mwa wakazi wa kaya duni mijini.

**Mheshimiwa Spika**, kutotekelawa kwa ushauri wa Kamati kikamilifu kumepelekeea athari katika sekta. Kwa mfano: kutoongezwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na diseli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia moja (100) kunaathiri ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji hususan kwa maeneo ya vijijini. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, mfuko ulikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi **158,500,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha za miradi ya maji iliyotolewa hadi mwezi Aprili, 2019 zilikuwa shilingi **106,373,473,916.46** sawa na **asilimia 67** ya fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji zillizoldhlnishwa, ikillinganishwa na fedha za ndani kutoka vyanzo vingine ambazo zimetolewa kiasi cha shilingi **48,723,227,627.10** sawa na **asilimia 17** tu ya fedha zilizotengwa. Kwa takwimu hizi, ni maoni ya Kamati kuwa, Mfuko wa Taifa wa Maji ndio chanzo cha uhakika cha ndani kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, kama tozo hii ingeongezwa maradufu kama ilivyopendekezwa mfuko ungekua na shilingi **billioni 317**, fedha ambazo zingesaidia kukamilisha miradi mingi ya maji Vijiini na hivyo kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wengi zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, pendekezo la kuongeza tozo kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli sio tu ni ushauri wa Kamati, lakini pia ni azimio la Bunge lako Tukufu lililopitishwa kuititia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2017 hadi 2019.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza uamuzi wa agizo hili la Bunge lako Tukufu litekelezwe kutokana na kuridhika na mafanikio yaliyofikiwa katika Bajeti ya Mwaka 2018/2019 ambapo **asilimia 67** ya pesa zilizopatikana na kutumika katika

miradi mbalimbali ya maendeleo maji vijijini zilitokana na makusanyo ya Mfuko wa Maji.

**Mheshimiwa Spika**, kutotekelezwa kwa ushauri wa kuratibu na kusimamia programu za kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi na kutumika katika maeneo yenye ukame kunazorotesha jitihada za kuimarisha upatikanaji maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali katika maeneo kame hususani katika maeneo ya taasisi za umma, asasi za kiraia na watu binafsi ambazo zinakosa miundombinu ya uvunaji maji ya mvua kwenye majengo na maeneo yao.

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa miundombinu ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua katika vituo vya kutolea huduma za afya, taasisi za elimu, mahakama, ofisi zote za Serikali na sekta binafsi ungeweza kuimarisha hali ya upatikanaji maji kwa matumizi mbalimbali. Aidha katika maeneo kame, ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kungeimarisha upatikanaji maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo pamoja na kilimo cha bustani na hivyo kuinua tija katika ufugaji na kilimo biashara.

## **2.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 yalijielekeza katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanya hadi Aprili, 2019.

### **2.2.1 Kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Maji na Umwagiliaji - Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **24,363,869,000**. Kati ya fedha hizo shilingi **6,266,714,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **18,097,155,000** ni mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi **673,214,033,677** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **443,214,033,677** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani

ambapo kati ya fedha hizo, shilingi **158,500,000,000** ni za Mfuko wa Taifa wa Maji na shilingi **284,714,034,677** ni fedha zinazotokana na vyanzo vingine nya ndani. Aidha, shilingi **229,999,999,000** sawa na **asilimia 34** ni fedha za nje.

## **2.2.2 Mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2019 Wizara ya Maji-Fungu 49 ilikuwa imepokea fedha za matumizi mengineyo shilingi **2,905,702,353.15** sawa na **asilimia 46**, na mishahara shilingi **13,747,840,611** sawa na **asilimia 76** ya kiasi kilichoidhinishwa. Aidha, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Aprili, 2019 zilikuwa shilingi **343,486,935,529.46** sawa na **asilimia 51** ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilizoidhinishwa ambazo zinajumuisha fedha za Mfuko wa Maji na vyanzo nya ndani shilingi **155, 096, 701,543.56** na fedha za nje shilingi **188,390,234,048.90**.

## **2.2.3 Maoni kuhusu Mwenendo wa Utolwaji Fedha za miradi ya maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika (2018/2019) fedha za miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Maji - Fungu 49 zilizotolewa ni **asilimia 51**, ikilinganishwa na **asilimia 22** ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga asilimia kubwa ya fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hasa kuimarisha utoaji wa fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mbalimbali ya maji nchini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, jumla ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **shilingi 443,214,033,677.00**. Kati ya fedha hizo Mfuko wa Maji ni shilingi **158,500,000,000** na fedha kutoka vyanzo vingine nya ndani ni shilingi **284,714,034,677.00**. Na kwamba hadi mwezi Aprili 2019, fedha za Mfuko wa Maji zilizotolewa ni **asilimia 67**, ilihali fedha kutokana na vyanzo vingine nya ndani ni **asilimia 17** tu. Hivyo, Kamati inasisitiza ushauri iliokwisha utoa kuwa Mfuko wa Taifa wa Maji ndio chanzo cha uhakika cha ndani kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijijini.

#### **2.2.4 Ukusanyaji wa maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara ya Maji ilipanga kukusanya mapato yenye jumla ya shilingi **5,071,001,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili, 2019, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **4,127,958,527.77** sawa na **asilimia 81** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo hata hivyo, Kamati inaamini hadi mwisho wa Mwaka wa Fedha mwezi Juni, 2019 Wizara itafanikiwa kufikia malengo iliyojiwekea katika ukusanyaji wa maduhuli.

### **2.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaisha (2018/2019). Ili kutekeleza masharti ya kanuni hiyo, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Dar es salaam, Lindi na Mtwara. Katika ziara hiyo, Kamati ilikaguwa jumla ya miradi sita (6) ambayo ni pamoja na: -

- i) Mradi wa Maji Igombe katika Halmashauri ya Manispaa ya Illemela – Mwanza.
- ii) Mradi wa Maji Halmashauri ya Manispaa ya Arusha Mradi wa Maji Loovilukuny na Ngaramtoni – Arusha
- iii) Mradi wa Majisafi Longido - Arusha.
- iv) Ujenzi wa Bomba la Maji la urefu wa kilomita 63 kutoka Mto Simba Wilayani Siha - Kilimanjaro hadi Halmashauri ya Wilaya ya Longido – Arusha.
- v) Mradi wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha na Maeneo ya Wilaya ya Arumeru- Arusha.
- vi) Mradi wa Maji Kilambo na Msanga Mkuu - Mtwara Vijijini.

### **2.3.1 Malengo ya Miradi iliyokaguliwa.**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maji kimsingi unalenga: -

- i) Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wa maeneo ya miradi iliyokaguliwa;
- ii) Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa ajili ya mbauti za kunyweshea mifugo kwa wakazi wa Longido;
- iii) Kuongeza uzalishaji maji kulingana na mahitaji ya maeneo ya miradi;
- iv) Kuondoa kero ya upungufu wa maji safi na uondoaji maji taka katika Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru ili kuendana na kasi ya ukuaji wa Jiji la Arusha;
- v) Kuboresha Huduma ya usambazaji wa majisafi na miundombinu yake kwa kuongeza uzalishaji wa maji;
- vi) Kuboresha huduma ya usafi wa mazingira na miundombinu kwa kuongeza mtandao wa kukusanya majitaka; na
- vii) Kujenga uwezo wa taasisi kwa kusogeza huduma kwa wananchi kwa kujenga ofisi, kununua magari kumi na sita na mitambo mbalimbali ya kuboresha utoaji wa huduma za majisafi na majitaka.

### **2.3.2 Changamoto zinazokabili utekelezaji miradi ya maji iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto zinazofana karibu miradi yote iliyokaguliwa. Changamoto zilizobainika ni pamoja na:-

- i) Ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini;
- ii) Kuchelewa kupatikana kwa fedha za utekelezaji;

- iii) Kukosekana umakini katika usanifu wa mradi na hivyo kupelekea ongezeko la kazi za mradi ambazo hazikuwa katika mkataba wa awali;
- iv) Usanifu na ujenzi wa baadhi ya miradi kuruka vijiji ambavyo vinapitiwa na mradi;
- v) Kuchelewa kufanya mapitio ya usanifu wa mradi na hivyo kupelekea mradi kuchelewa kukamilika kwa kipindi cha miaka miwili hadi miaka mitano;
- vi) Ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi wa miradi;
- vii) Ucheleweshwaji wa kutoa msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa vifaa vya miradi ya maji;
- viii) Ucheleweshaji wa vibali vya kazi (*working permit*) kwa wataalamu wanaotekeleza Mradi wa Huduma ya Maji katika Jiji la Arusha;
- ix) Uwezo mdogo wa mkandarasi kutokana na kuwa na kazi nyingi maeneo mengine ya nchi;
- x) Kushindwa kupunguza maji yanayopotea;
- xi) Miradi ya maji safi kutotekeliza sambamba na mifumo ya uondoaji maji taka; na
- xii) Ufanisi mdogo wa miradi ya maji vijijini kutokana na umeme kuwa na nguvu ndogo na hivyo kushindwa kuendesha visima.

### **2.3.3 Maoni ya jumla kuhusu miradi ya maendeleo kwa sekta ya maji**

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zilizobainika kwenye miradi ya maji iliyokaguliwa imekua ni sababu kubwa ya kutokamilika miradi kwa muda uliopangwa na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa Serikali na kukosesha wananchi huduma ya upatikanaji maji safi kwa muda uliopangwa. Hivyo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

- i) Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha za miradi ya maendeleo mapema na kwa kadiri ya mikataba ili kuepusha hasara kwa gharama za miradi kuongezeka kutokana na ucheleweshaji.
- ii) Watendaji wa Serikali kuwa makini wakati wa kufanya usanifu wa miradi kwani kukosekana kwa umakini katika usanifu wa miradi kunapelekea ongezeko la kazi za mradi ambazo hazikuwa katika mkataba. Aidha, ni muhimu kwa usanifu wa miradi kuzingatia upatikanaji wa maji kwa wakazi wanaopitiwa na miundombinu ya miradi ya maji.
- iii) Kamati inatahadharisha kuwa ni vyema utoaji wa zabuni za utekelezaji miradi ya maji ukazingatia uwezo wa mkandarasi, pamoja na miongozo ya utoaji zabuni ili kuepusha kutoa miradi mingi kwa mkandarasi mmoja kwani hali hii imedhihirisha kuchelewa kwa miradi kukamilika kwa wakati.
- iv) Kutokana na miradi mingi ya maji vijijini kuendeshwa kwa gharama kubwa zitokanazo na matumizi ya mafuta ya dizeli na hivyo kuwa na ufanisi kidogo, Kamati inashauri Serikali kuwa, kwa miradi ya maji iliyovijijini itumie pampu zinazoendeshwa kwa kutumia umeme wa jua (*solar power*) ambazo gharama za uendeshaji ni nafuu. Aidha, kwa miradi mikubwa ya maji isiyoweza kuendeshwa kwa umeme wa jua, ni vema kuwa na mkakati wa kupeleka umeme wa kutosha ili pamoja na shughuli zingine, umeme huo uweze kuendesha miradi ya maji vijijini kwa gharama nafuu.
- v) Utekelezaji wa miradi ya maji unafanyika kwa ushirikiano na wataalamu wa kigeni ambao kwa mujibu wa sheria huitajika kupata vibali vya kufanya kazi nchini. Pamoja na kwamba mikataba inayoingiwa ya utekelezaji wa miradi ya maji imeainisha uhitaji wa wataalamu hao, bado kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa utolewaji wa vibali hivyo kwani vimekuwa vikichukua muda mrefu kupatikana na hivyo kuathiri utekelezaji wa mradi kwa kutopata wataalamu hao kwa muda unaohitajika. Kufatia changamoto hiyo, Kamati inashauri Serikali na Taasisi zake

kufanya kazi kwa ushirikiano na kuharakisha mchakato wa utoaji vibali vya wataalam wageni kufanya kazi nchini.

vi) Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kulipa wakandarasi kadiri wanavyo kamilisha mikataba ya ujenzi na kukabidhi miradi kwani kutolipa wakandarasi kwa wakati na kwa kadiri ya makubalianao kunaathiri wakandarasi kimapato na hivyo kushindwa kukamilisha miradi mingine waliyonayo. Kwa mfano: - Kamati ilikagua mradi ambao umekamilika kwa asilimia 100 tangu mwezi June, 2018, hadi Kamati ilipotembelea mradi huu mwezi Machi, 2019 mkandarasi bado hajalipwa na anaidai Serikali kiasi cha shilingi **56,478,960.00**.

vii) Taasisi za Serikali kufanya kazi kwa ushirikiano ili kufanikisha upatikanaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira kwa haraka. Kwa mfano; Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa Ubreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Arusha na Maeneo ya Wilaya ya Arumeru ilibaini kuwa Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) wa jumla ya Shilingi za Kitanzania zipatazo **bilioni 514 (233.9 mil USD)** fedha ambazo zimeshapatikana na mradi umeanza kutekelezwa tangu Julai 2018. Hata hivyo, mradi umekuwa unasusua kutokana na kuchleweshwa kwa vifaa ikiwemo mabomba kwa ajili ya visima vinavyoendelea kuchimbwa ambapo toka mwezi Desemba 2018, mabomba pamoja na vifaa vingine vimekwama Bandari ya Dar es salaam kutokana na mlolongo mrefu wa kupata msamaha wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa vifaa hivyo. Kukosekana kwa vifaa hivyo kunapunguza kasi ya wakandarsi kukamilisha uchimbaji wa visima lakini pia kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi.

#### **2.4 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020-FUNGU 49**

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 26 na 27 Machi, 2019 Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na

Matumizi umezingatia Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Awamu II), Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV 2025), Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002.

**Mheshimiwa Spika**, Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inaeleza kuwa maji ni bidhaa muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Hivyo, upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mahitaji ya msingi kwa binadamu wote<sup>1</sup>. Kwa kutambua hilo ndio maana swala la maji limewekewa mkazo katika malengo mahususi ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo la sita la maendeleo endelevu linadhamiria kuona kuna upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote ifikapo 2030.

#### **2.4.1 Umuhimu wa Maji kwa Maendeleo ya Nchi**

**Mheshimiwa Spika**, juhudhi zote hizo zinadhahirisha kuwa Maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kwamba kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kwa kiasi kikubwa kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa lakini bado upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini umethibitika kuwa mgumu hususan maeneo ya vijijini ambapo takwimu zinaonyesha ni **asilimia 64.8%** tu ya wakazi wa vijijini ndio wanaopata maji safi na salama, na **asilimia 80%** kwa wakazi wa mjini. Takwimu hizi ni za chini ikilinganishwa na malengo yaliyopo ya kufikia **asilimia 85** vijijini, **asilimia 90** katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo na **asilimia 95** katika Makao Makuu ya Mikoa ifikapo Mwaka 2020.

#### **2.4.2 Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 inatarajiwa kwenda kutekeleza miradi ya vipaumbele vitakayosaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa

---

<sup>1</sup> Sera ya Maji ya Mwaka 2002

maji safi na salama ili kuhakikisha kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Malengo makuu na vipaumbele vya bajeti inayoombwa ni pamoja na: -

- (a) Kuwa na huduma bora ya maji kwa wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025;
- (b) Huduma bora za maji vijijini kwa zaidi ya **asilimia 90** ya wananchi ifikapo mwaka 2025; na
- (c) Kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuivilinda, kuvitunza, kuviedeleza na kutafuta vyanzo vypya vya maji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na vipaumbele hivyo, bajeti inayoombwa pia itatakeleza kazi zifuatazo: -

- i) Kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini;
- ii) Kukamilisha miradi 482 inayoendelea katika Halmashauri mbalimbali na kuanza miradi mipyta ya maji vijijini;
- iii) Kukamilisha miradi inayoendelea na kuanza utekelezaji wa miradi mipyta katika Jiji la Dar es salaam, miradi ya kutoa maji Ziwa Victoria, mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na majitaka katika Jiji la Dodoma na Ikulu Chamwino, kuendelea na ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha, mradi wa kuboresha mfumo wa majitaka katika Miji ya Musoma na Bukoba, Mradi wa kutoa maji mto Kiwira kwenda jiji la Mbeya na miradi mingine ya maji katika Miji midogo, Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya mbalimbali na Miradi ya Maji Kitaifa.
- iv) Kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati ya Farkwa (Dodoma), Kidunda (Morogoro Vijijini) na Ndembera (Iringa) na ukarabati wa mabwawa ya ukubwa wa kati ya Itobo (Nzega) na Enguikment (Monduli).

#### **2.4.3 Fedha zinazoombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Maji - Fungu 49**

inaomba kuidhinishiwa kiasi **cha** shilingi 23,726,309,000 kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha **hizo**, shilingi 6,266,714,000 sawa na asilimia 24 ni kwa ajili ya kugharamia **Matumizi mengineyo (Other Charges)** na shilingi 17,459,595,000 sawa na asilimia 76 ni kwa ajili ya **kulipa mishahara (PE)** ya Watumishi.

#### **2.4.4 Fedha zinazoombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji kupitia Fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 610, 469,888,530**, sawa na **asilimia 96.26** ya bajeti yote ya maji Fungu 49 inayoombwa. Kati ya fedha **hizo**, shilingi **349,449,000,000** sawa na **asilimia 57** ni fedha za ndani na shilingi **261,020,888,530** sawa na **asilimia 43** ni fedha za nje.

#### **2.4.5 Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ya Maji- **Fungu 49** imepanga kukusanya **shilingi 7,678,502,000** itakazozipata kutokana na makadirio ya kukusanya maduhuli yatakayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji visima vya maji na tozo mbalimbali zitakazotozwa kwa wateja watakaopata huduma za maabara za ubora wa maji na vibali vya matumizi ya maji katika mabonde.

#### **2.4.6 Tathimini ya Kamati kuhusu Malengo ya Bajeti na Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Maji - Fungu 49**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia, imechambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020. Malengo haya ni ya msingi na ya kuridhisha. Hata hivyo Kamati inatoa maoni kuwa, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo la upungufu wa maji safi na salama nchini, ambapo upatikanaji kwa sasa ni **asilimia 64.8** vijijini na **asilimia 85** mijini, wakati lengo ni kufikia **asilimia 80** kwa vijijini na **asilimia 95** kwa mijini ifikapo mwaka 2020, Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 hayakidhi mahitaji makubwa ya Maji kama

yalivyoolezwa katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano (Awamu ya I&II) ambao umebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, ufungaji, viwanda, usafirishaji na uchukuzi na kupunguza umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa jumla ya fedha za miradi ya maendeleo kilichotengwa ni pungufu kwa **asilimia 9** ya fedha zilizoidhinishwa katika mwaka unaomalizika 2018/2019. Aidha fedha za ndani zilizoidhinishwa zimepungua kutoka **asilimia 66** iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufikia **asilimia 57** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo umeongezeka kutoka **asilimia 34** kwa bajeti ya 2018/2019 hadi **asilimia 43** kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati imesikitishwa na kitendo cha Serikali kupunguza fedha za ndani kwenye bajeti ya maendeleo, kwani kutegemea fedha za nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kwa wananchi hakutoi uhakika wa kuwapatia wananchi maji safi na salama ili kufikia **asilimia 85** kwa wananchi wa vijiji na **asilimia 95** kwa wakazi wa mijini ifikapo 2020.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2019/2020. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwenye maeneo saba (7) yafuatayo: -

#### **1) KUIMARISHA KUTENGA FEDHA ZA NDANI KWA AJILI YA KUTEKELEZA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kushuka kwa kiasi cha fedha za miradi ya maendeleo iliyotengwa katika bajeti ya

Mwaka 2019/2020 kwa **asilimia 9** ikilinganishwa na bajeti ya 2018/2019. Ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na kuwapatia wananchi maji safi na salama, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha utengaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

**2) KUIMARISHA MAKUSANYO YA MFUKO WA TAIFA WA MAJI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa miaka mitatu sasa Kamati imekua ikiishauri Serikali kuimarisha makusanyo ya Mfuko wa Taifa wa Maji kwa kuongeza tozo ya mafuta kwa kila lita ya petroli na diseli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia moja (100). Kutotekelezwa kwa ushauri huu kunaathiri ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maji hususan kwa maeneo ya vijijini. Endapo ushauri huu wa Kamati utazingatiwa Kamati ina amini kuwa, Mfuko wa Taifa wa Maji utakuwa ni chanzo cha uhakika cha ndani kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijijini. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza ushauri huu.

**3) MIKAKATI YA UVUNAJI WA MAJI YA MVUA KWA AJILI YA MATUMIZI MBALIMBALI**

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kwamba mahitaji ya rasilimali maji yameendelea kuongezeka wakati upatikanaji wake ukiendelea kupungua, kutohana na hali hii Serikali ina jukumu la kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zilizopo nchini zinatunzwa na kuendeleza kwa uwiano ulio sawa kwa sekta zote, ikiwa ni pamoja na kubuni na kujenga miundombinu ya kuongeza upatikanaji wa maji. Kamati ina amini kwamba uvunaji wa maji ya mvua ni njia mojawapo ya upatikanaji wa maji safi na salama na ya gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kutekeleza kwa vitendo mkakati wa namna ya kuvuna maji ya mvua nchi nzima pamoja na kusimamia kikamilifu miongozo iliyopo kuhusu ujenzi wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua katika majengo mbalimbali.

**4) UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJITAKA KATIKA MIJI NA MAKAO MAKUU YA MIKOA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, huduma ya usafi wa mazingira kwa upande wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini hutolewa kwa njia ya uondoaji majitaka pekee. Kwa hapa nchini, huduma hiyo imefikia wastani wa **asilimia 20** kwenye miji yenyne mtandao wa majitaka na kwa maeneo ambayo hayajafikiwa na mtandao huo, huduma ya majitaka hutolewa na magari maalumu ya majitaka na kumwagwa kwenye mabwawa ya majitaka.

**Mheshimiwa Spika**, Miji yenyne mtandao wa Majitaka ni 11 (Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa). Hadi kufikia mwezi Machi 2019 mtandao wa majitaka ni **kilomita 837** wenyne maunganisho **48,882 na** unahudumia wakazi wapatao **511,208** kwa ujumla. Miundombinu hii haitoshelezi na mingi ni chakavu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza mipango na miradi mbalimbali ya majitaka na usafi wa mkazingira.

**5) KUIMARISHA NA KUTEKELEZA MIPANGO NA MIKAKATI YA KUTUMIA MAJI KUTOKA ZIWA TANGANYIKA**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ina **asilimia 41** ya Ziwa Tanganyika lenye ujazo wa maji safi na salaama ya kunywa (*fresh water*) kiasi cha kilomita za **ujazo 18,900 km<sup>3</sup>** ya kimiminika ambayo ni sawa na **asilimia 17 (17%)** ya maji yote ya kunywa ya kimiminika yaliyoko kwenye uso wa dunia nzima.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizaya ya Maji kufanya juhudzi za makusudi za kuanza kuvuna maji hayo mengi na kuyasambaza kwenye mikoa yenyne uhaba wa maji kama vile mikoa iliyo kwenye bonde la maji la katii (*Internal drainage basin* lenye mikoa ya Dodoma, Singida

na Manyara) kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo ya majumbani na maendelo ya viwanda.

**6) KUIMARISHA TAFITI ZA RASILIMALI MAJI NA KUBORESHA  
MITAALA YA ELIMU KWA UMMA KUHUSU KUTUNZA  
VYANZO VYA MAJI.**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa rasilimali ya maji inazidi kupungua hapa nchini kwa sababu ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira pamoja na athari za tabia nchi. Na kwa kuwa matumizi ya maji yanaongezeka siku hadi siku kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu pamoja na shughuli za kiuchumi ambazo zinahitaji maji. Kamati inatoa wito kwa Serikali kuwezesha watafiti nchini waweze kufanya tafiti za kina kuhusu wingi na ubora wa rasilimali ya maji chini na juu ya ardhi kwenye kila kipande cha nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu kwa watafiti kufanya tafiti ili kubaini ni kwa kiasi gani mabadiliko ya tabianchi na uharibifu na uchafuzi wa mazingira pekee huchangia kupungua kwa rasilimali ya maji nchini. Vilevile kuwa na kupanga mipango endelevu ya matumizi ya rasilimali maji na Wananchi wanaweza kushauriwa ipasavyo kuhusu usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali ya maji.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kufanyika kwa tafiti za rasilimali maji, Kamati pia inashauri Serikali kuititia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuboresha mitaala kwa kuhakikisha kuwa elimu kuhusu rasilimali ya maji inafundishwa kuanzia shule ya msingi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kuwa watoto wakifunzwa bado wadogo wataweza kufahamu umuhimu wa kutunza na kuhifadhi vyanzo vya rasilimali maji kwa weledi mpana zaidi. Aidha, ni muhimu kwa Serikali kutoa elimu kwa jamii nzima kuhusu umuhimu wa kutunza na kuhifadhi vyanzo vya rasilimali ya maji pamoja na ufanisi wa kutumia na kusambaza rasilimali hii ya maji.

**7) KUKAMILISHA MIRADI MBALIMBALI YA MAJI  
INAYOTEKELEZWA NCHINI**

**Mheshimiwa Spika**, ufuatiliaji na uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji miradi mbalimbali ya maji nchini umebaini changamoto ya kutokamilika utekelezaji miradi kadiri ya muda wa mikataba uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi uliofanywa na Kamati mwezi machi, 2019 baadhi ya miradi imebainika kuchelewa kati ya miaka 3 hadi miaka 5, miradi hii ni pamoja na Mradi wa Maji Igombe katika Halmahauri ya Manispaa ya Illemela, Mradi wa Maji Halmashauri ya Manispaa ya Arusha Mradi wa Maji Loovilukuny na Ngaramtoni pamoja na Mradi wa maji safi katika Mji wa Longido.

**Mheshimiwa Spika**, kuchelewa kukamilika miradi kwa muda uliopangwa kumekuwa na athari mbaya ikiwa ni pamoja na kuongezeka gharama za miradi pamoja na kukosesha wananchi kupata huduma ya maji kwa muda stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi wa utekelezaji miradi, utoaji wa fedha kwa ajili ya wakandarasi pamoja na kufanya kazi changamoto zinazotajwa kukwamisha miradi ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupata vibali vya msamaha wa kodi kwa ajili ya vifaa, vifaa kuchelewa bandarini na kuchelewa kupata vibali vya wataalamu mahsusni wa miradi kutoka Idara ya uhamiaji.

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mhe. Prof. Makame Mbarawa, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Katibu Mkuu Prof. Kitila Mkumbo, Naibu Katibu Mkuu Eng. Emmanuel Kalobeloo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji

kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Maji.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb "
5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb "
6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb "
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb "
9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "
10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
11. Mhe. Lucy Simon Magereli, "
12. Mhe. Justine Joseph Monko "
13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb "
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb "
15. Mhe. Pascal Yohana Haonga "
16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
18. Mhe. Devotha Mathew Minja, Mb "
19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb "
21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb "
22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb "
23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb "
26. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb "

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Ndg. Athuman Hussein Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge na Ndugu Dickson

Bisile Mkurugenzi Msaidizi kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuhudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa katika hoja ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Mahmoud Hassan Mgimwa, (Mb)  
**MWENYEKITI,**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**  
**YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**  
2 MEI, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji kwa kuwasilisha hoja ya Kamati. Naendelea sasa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, tunamkaribisha Mheshimiwa Devotha Minja kwa niaba ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, karibu. (*Makofii*)

**MHE. DEVOTHA M. MINJA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza hotuba hii, leo asubuhi Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea taarifa za kusikitisha za kufariki kwa mfanyabiashara maarufu, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Makampuni ya IPP, Dkt. Reginald Mengi. Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, tunatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard*. Kwanza kabisa

nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii adhimu kuwapongeza viongozi wangu wa Vyama vyta Upinzani kwa mshikamano mkuu wanaouunesha katika kipindi hiki kigumu sana cha kufanya siasa nje ya CCM ambayo imekuwa ni kosa la jinai. Aidha, nimshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuendelea kuwa na imani na mimi katika majukumu ya kusimamia Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu mkubwa, niwashukuru wanachama wote wa vyama shindani pamoja na wananchi wote kwa kuendelea kutuunga mkono katika mapambano ya kupigania demokrasia ya kweli katika nchi hii hasa uchaguzi ulio huru na haki. Kwani Kambi Rasmi ya Upinzani ina amini kuwa bila haki hakuna demokrasia, pia hakuna amani katika nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo na Mfumo wa Kisekta. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaungana na tamko la kauli mbiu ya kitaifa na kimataifa umuhimu wa maji kama inavyoeleza, Maji ni Haki ya Kibinadamu, Maji ni Uhui, Maji ni Uchumi, Maji ni Msingi wa Amani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa pamoja na kwamba maji ni huduma, vilevile ni biashara. Ni ukweli kwamba kwa sasa hakuna huduma yoyote ya kijamii inayotolewa bure na Serikali, achilia mbali ukweli kwamba kodi zinazotolewa na wananchi wenyewe ndio zinazoitwa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa huduma ya maji, hakuna eneo lolote Tanzania ambalo wanapata maji ya bomba kutoka katika vyanzo safi na salama bila ya malipo ya aina yoyote. Hivyo huduma hii ya maji, iwe ni kwa matumizi

ya majumbani, iwe ni matumizi ya mifugo, iwe ni matumizi ya viwandani au kwa matumizi ya kilimo, vyovoyote vile ni sehemu huduma ya maji ni gharama, hivyo watumiaji wa maji wapatiwe kwa malipo ili kuchangia uzalishaji wa maji safi na salama, lakini kwa kiingereza, tunasema *water has an economic value*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, kama ni biashara, utolewaji wa huduma hiyo lazima uwepo na ushindani wa utumiaji wa huduma hiyo ili wananchi wapate huduma iliyobora kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa maji kwa ajili ya uhai na watu, pamoja na wanyama na mimea, pamoja na mazingira kwa ujumla ni jambo lisilopingika na bila ya maji viumbe vyote vinaweza kupotea na mazingira yanaweza kuwa mfu na maendeleo ya kiuchumi na kijamii yataadumaa. Kutohana na umuhimu wa maji, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha tarehe 21 Desemba, 2016, limeridhia kwa kauli moja kwa miaka kumi ya utekelezaji wa Azimio jipya la Maji kwa Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira ya Maendeleo ya Taifa, pia mipango ya maendeleo kwa miaka ya 2016 - 2021 kwa Tanzania, kuwa ni nchi ya uchumi wa viwanda ifikapo 2015. Azma hii haiwezi kufikiwa endapo changamoto za upatikanaji wa maji kwa matumizi ya majumbani, kwa matumizi ya kilimo na kwa ajili ya viwanda hazitajibwa kikamilifu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa dira imekuwa na malengo ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na ustawi wa kijamii ikiwa ni pamoja na maendeleo yanayogusa moja kwa moja Wizara na Sekta za Maji pamoja na umwagiliaji, baadhi ya malengo muhimu katika muktadha huu ni kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kuwa ni nchi ya uchumi wa katii, ambapo wananchi wake watafurahia amani na umoja wa kimataifa, lengo la pili lilikuwa ni upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wote, ambapo kwa wakazi wa mijini watapata maji kwa asilimia 100 na wakazi

wa vijijini watapata maji safi na salama agalau asilimia 90 ifikapo mwaka 2020 – 2025, na tatu ilikuwa ni kuhakikisha kwamba, rasilimali za maji ni endelevu ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama vijijini na mijini, bado Tanzania inakabiliwa na changamoto nyingi za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Tofauti na nchi nyingi za majirani, nchi ya Tanzania imejaaliwa kuwa na rasilimali ya kutosha ya maji safi na salama, kwa maana ya mito, maziwa na miamba oevu za kutosheleza mahitaji yote kwa sasa kwa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za kitaifa za rasilimali za maji zilizopo zinaonesha kuwa kiasi cha maji kwa sasa kwa kila mtanzania ni wastani wa lita za ujazo 1,952 kwa mwaka. Pamoja na takwimu hizi, ikumbukwe kuwa idadi ya watu imeongezeka kwa kasi katika miaka 25 iliyopita, vilevile matumizi ya maji sio yameongezeka bali yamebadilika kwa kiasi kikubwa kufuatia kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi, kukua kwa miji na mabadiliko ya mfumo wa kilimo pamoja na biashara. Ambapo kilimo kinachukua wastani wa asilimia 89 ya rasilimali za maji na matumizi ya majumbani pamoja na Taasisi zingine zinatumia asilimia kumi ya viwandani na asilimia moja.

Endapo hatua madhubuti za utunzaji wa vyanzo vya maji hazitachukuliwa mapema, kiasi hicho kinatarajiwa kupungua hadi kufikia mita za ujazo 883 kwa mwaka 2020 – 2035 na kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni lita za ujazo 1,700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri hapa kama hatutachukua hatua stahiki muda si mrefu Tanzania inaweza kuwa kwenye tatizo kubwa la maji ambapo ukosefu wa maji linakuwa janga kubwa na hivyo kupelekea rasilimali hiyo kuwekewa utaratibu wa jinsi gani ya kugawanya kwa kila familia, mifugo na kwa matumizi ya viwandani kama ilivyowahi kuwa kwa nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa Tanzania ni Kusaidia Rasilimali za Maji kwa mwaka 2006 na tunatambua umuhimu wa kipekee wa maji katika utendaji kazi wa sekta muhimu za kiuchumi na ustawi wa Watanzania. Mkakati huu unabainisha athari za uwekezaji duni katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni usambazaji wa maji na huduma safi kama hitaji la msingi kwa maisha zalishi na pili uendeshaji wa kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa umeme wa maji kwa ajili ya kuhakikisha unapatikana chakula cha kutosha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati unabainisha namna ya utendaji kazi wa sekta kuu za uchumi (nishati, kilimo, viwanda, mifugo, uchimbaji madini, utalii, na uvuvi) ambavyo vimeathirika kutokana na ukame, mafuriko na usimamizi duni wa rasilimali za maji. Pia, tunasisitiza hoja ya kufanya juhudzi za haraka kupanua uwekezaji katika uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji, ili kuwe na udhibiti mzuri wa rasilimali za maji na ulinzi na uhifadhi wa vyanzo vya maji katika – mito, maziwa na kwenye miamba ya ardhi oevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ushahidi huo ni ukweli kabisa kuwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi yana uhusiano wa moja kwa moja katika upatikanaji wa rasilimali ya maji na utunzaji wa mazingira. Maji ni rasilimali inayomalizika kama haitatunzwa ili kuwa endelevu, hivyo maendeleo ya kilimo, mifugo, viwanda vyote vinategemea upatikanaji wa uhakika wa rasilimali ya maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli pia kuwa mahitaji na matumizi ya maji yanazidi kuongezeka, japokuwa upatikanaji wa maji unazidi kupungua na mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka kutokana na ukweli kuwa idadi ya watu inazidi kuongezeka, kutokuwa na mifumo mizuri ya kuhifadhi maji ya mvua, mabadiliko ya tabianchi pamoja na shughuli za kiuchumi ambazo hazizingatii utunzaji wa mazingira ambayo ndicho chanzo kikuu cha maji mengi ya mito yetu.

Hivyo ni lazima kuwa na mkakati madhubuti wa kuhakikisha maji yaliyopo yanatumiwa kwa uangalifu na uendelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo la maji ni lazima kuifanya rasilimali hii kutumika kwa uangalifu na kwa uendelevu baina ya makundi yote ya kijamii, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa; ni lazima mahitaji kwa kila kundi katika mfumo mzima wa uzalishaji (kilimo,mifugo,viwanda na majumbani) lijulikane siku hadi siku ili kuweze kuwa na mgawanyo sawa wa rasilimali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa vyanzo vya maji nchini unafuata utaratibu za mipango shirikishi ya usimamizi wa rasilimali ya maji kwenye bonde na mabonde tisa yaliyopo nchini, ambapo saba katika hayo yanahuisha maji shirikishi kati ya nchi zetu nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo katika usimamizi wa rasilimali za maji ni kupungua na kuharibika kwa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kibinadamu, suala la uchafuzi wa vyanzo vya maji. Taarifa za uchafuzi kuanzia mwaka 2014, tafiti nyineza za kitaalam ni zile za Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na nyiningezo ambazo zinaonesha athari ya uchafuzi mkubwa hapa na hii tunatoa kwa baadhi ya maeneo yaliyoathirika kwa kiwango kikubwa. Katika maeneo ya vyanzo vya maji na katika misitu ya hifadhi ya maji. Aidha, kupungua kunatokana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo imeathiri shughuli za kijamii na kiuchumi na kusababisha migogoro kwenye vyanzo vya maji. Hifadhi hizi zinaweza kupatikana kwa maji kwa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa mabonde tisa ya maji, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni lazima na muhimu kuhifadhi vyanzo vya maji kwa mabonde hayo bila kusahau umuhimu wa kipekee kwa kuhifadhi vyanzo vya Bonde la Rufiji ambalo ndilo chanzo kikuu cha mabonde ya Kilombero na Ruaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe hapa kwamba, Mto Rufiji hupata maji yake mengi kutoka mito miwili mikuu yaani Kilombero na Ruaha na hasa mto Kilombero, ambao huchangia theluthi mbili ya maji ya Mto Rufiji ambao tunatarajia utapeleka maji kwenye *Stiegler's Gorge*. Hivyo ustawi wa Mto Rufiji unategemea ustawi wa Mto Rufiji; ambao nao pia unategemea kwa asilimia 60 ustawi wa Mto Kilombero; hususan Bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri, uwezekano wa Watanzania kupata umeme wa maji kwa bei nafuu kutoka *Stiegler's Gorge*, ni ndoto inayokaribia kuwa ya kweli endapo Serikali itashindwa kuchukua hatua za makusudi za kuhifadhi Bonde la Mto Kilombero, kwani ustawi wa bonde hilo hivi sasa unasambaratishwa na shughuli za kibinadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam wanakubaliana kwamba, uharibifu wa mazingira ukiongezeka tatizo sasa litaibuka dunia nzima na mabadiliko ya tabianchi vinaashiria kuwa muda si mrefu Bonde la Kilombero linaweza kupoteza sifa yake ya kuwa bonde adhimu la maji baridi ambalo ni kubwa kuliko yote duniani, liliokuwa linajaa maji misimu yote kwa mwaka. Kitu pekee ambacho wataalam hao wanatofautiana, ni muda uliobakia kabla Bonde hilo halijasambaratika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti uliofanywa na *JET* kuhusu hali ya mito kati ya Kihansi na Ifakara, unaonesha kati ya mito 29 iliyokuwepo, sasa imebaki mito mitano tu, huku mito tisa ikiwa na maji yaliyotuama. Miongoni mwa mito hiyo mitano ambayo inatiririsha maji, ni Luipa, Mpanga na Mnyera ndio bado ina maji ya kutosha kwa mwaka mzima. Kwa hivyo, hali ya mito katika Bonde la Kilombero ni mbaya na chanzo kikubwa cha hayo ni uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa maji katika maeneo mengi ya miji midogo na mikubwa sasa inatokana na kutokuwepo kwa taarifa za uhakika tunashindwa kuweka

takwimu za uhaba wa maji kwa kila eneo hadharani ili Serikali iweze kuzifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mto Ngerengere unapokea maji taka kutoka kwenye ukanda wa viwanda wa Morogoro pamoja na mfumo mzima wa maji taka ya mji wa Morogoro, maji taka yanayoingia kwenye mto huo kutoka kwenye viwanda vya nguo na viwanda vya ngozi hayafai kabisa kutumika kwa matumizi ya nyumbani na kwa matumizi ya kilimo kutokana na kuwa na viwango vya juu vya kemikali hatarishi kwa viumbe na wanadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutokuwa na chanzo mbadala cha maji kwa wakazi zaidi ya 5,000 waishio kwenye maeneo ya Kipera, Kingolwira, Bomba la Zambia na Sanga Sanga wanalahazimika kutumia maji ya mto huo kwa matumizi ya nyumbani na mashambani na hivyo bila kuwa na dawa jambo hilo linaweza kuwa hatarishi kwa usalama wa afya zao. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli kuhusiana na uchafuzi huo wa chanzo kikuu cha maji kwa mamilioni ya wakazi wa Dar es Salaam sambamba na wale wa jamii tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia randama ya Wizara inaonesha kuwa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili ukamilike unahitaji kiasi cha dola za Kimarekani milioni 215. Kwa mwaka 2018/2019, mradi wa Bwawa la Kidunda uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni tatu, lakini haikutoka hata shilingi na mwaka 2019/2020 cha kushangaza imeombwa tena shilingi bilioni tatu kwa mradi wa Mpera na Kimbiji na mwaka 2018/2019 ziliidhinishwa Sh.14,109,999,000.00 lakini hazikutoka hata shilingi, mwaka 2019/2020 zimeombwa tena shilingi bilioni tatu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Serikali haina uhakika na nini inataka kifanyike katika huo Mradi wa Mpera na Kimbiji kwani tofauti ya maombi ya mwaka jana na mwaka huu ni kubwa sana na ukiangalia hali halisi ya thamani ya shilingi kwa dola ya Kimarekani. Hii inapelekea kushindwa kufanya tathmini ya thamani ya fedha iliyotumika na kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumetangulia kusema, kuwa hakuna huduma ya bure na hivyo ukiangalia mwongozo wa biashara kwa mradi huo inajulikana wanufaikaji ni wangapi na kwa muda gani uwekezaji huo utakuwa umerejesha fedha hizo kwa kiasi gani. Kwa mantiki hiyo basi kushindwa kumalizika kwa mradi huo ambaao kwa sasa umeshachukua takriban miaka zaidi ya nane (8) na wakati huo huo thamani ya shilingi yetu dhidi ya dola inazidi kuporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo huo wa Serikali maana yake ni kwamba miradi mingi ya huduma za maji haitakuja kukamilika kwa miaka ya hivi karibuni hadi hapo tutakapopata watu wenyewe maono wa kibiashara watakao kuwa kwenye madaraka katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017 - 2019 ukurasa wa 44 hadi ule wa 49 kuna miradi ya maji iliyofanyiwa usanifu na mingine inaendelea na mingine imekamilika. Mradi wa Same - Mwanga - Korogwe, Mradi Mkoa wa Kigoma, Mradi wa Maji wa Ntomoko, Mradi wa Chiwambo, Mradi wa ujenzi wa Mabwawa, Mradi wa Maji wa Lukululu na kadhalika) mingi haifanyiki na kazi ni kutumia fedha nyingi na imelazimu Wizara itoe maelekezo kuwa miradi mingine isitekelezwe na Halmashauri kutokana na sababu zao na hivyo Mamlaka za Maji za Mikoa ziruhusiwe katika utekelezaji wake. Lakini hoja ya msingi ni je ikishatekelezwa ni mamlaka ipi itakuwa inaiendesha miradi hiyo? Hapa ndipo pa kutupia mpira kunapoanzia, kwani waendeshaji wasema hawakujenga kwa kiwango kinachohitaji na visingizo vingi vitaendelea kuwepo Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo sio uwezo mdogo wa Halmashauri, tatizo linaanza Serikali Kuu ambaao ndio waratibu na wasimamizi wa walipaji. Hapa lipi tatizo la msingi la kutokuwa na vipaumbele vinavyogusa moja kwa moja maisha ya Watanzania na maeneo yenye mchango mkubwa wa haraka kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Wimbo wa Serikali inayodhamiria kujenga uchumi wa viwanda

utaendelea kuimbwa bila mafanikio ikiwa mwelekeo huu hautabadiili na kuwekeza kwenye miradi yenye kuchochea maendeleo halisi ya uchumi wetu kama kwenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa miradi mikubwa Serikali inaweza kuingia katika ubia na Sekta binafsi na miradi kutekelezwa kwa utaratibu wa Kujenga mradi na kuuendesha na baadaye kuurudisha Serikalini. Utaratibu huu kwa mazingira yetu ambayo Serikali imeshindwa kupata mikopo ya masharti nafuu ndio utaratibu utakaokuwa suluhisho katika miradi ya maendeleo. Katika hili ujenzi wa mradi kwa njia ya ubia nao ndio utakuwa uendeshaji wa fedha ambao kwa mujibu wa mkataba Serikali itakayoingia siyo miradi itakayoleta faida kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasilitiza mikataba kuwa wazi na yenye tija baina ya wabia watakaohusika katika utekelezaji na usimamizi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, aliyoitao hapa Bungeni mwezi Mei, 2018 katika ukurasa wake wa nane na aya ya 16 imetoa takwimu za kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji kwa kipindi cha mwezi Machi, 2017 hadi Machi, 2018, ikionesha ongezeko la maji dhidi ya mahitaji kwa maeneo ya mijini. Hivyo imetulazimu kuchambua takwimu hizo kama ifuatavyo ili kuonesha hali halisi ya upatikanaji wa maji kwa maeneo ya mijini ukilinganisha na takwimu zilizopo ambazo zimetolewa na Waziri

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo liliowekwa na llani ya Chama cha Mapinduzi iliyoiingiza madarakani Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais Magufuli ni kuwa hadi 2020 Dar es Salaam iwe na upatikanaji wa maji kwa asilimia 95 na miji mingine iwe ni asilimia 90. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je, kwa mwendo huu wa hali halisi ya maji itafikia malengo yanayosemwa na Chama cha Mapinduzi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maji unachangiwa kwa makato ya watumiaji wa bidhaa ya

mafuta ya petroli kwa Sh.50 kwa kila lita moja ili kuwa endelevu. Taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2018/2019, inaonesha kuwa Mfuko umepata jumla ya shilingi bilioni 93.661 sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mapato ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lilikuwa ni kumtua mama ndoo ya maji lakini kwa makusanyo hayo maana yake kuna tatizo sehemu fulani na kwa nini mapato hayakukamilika angalau kwa asilimia 90? Hata hivyo, makato hayo hayawezi kuwa ya milele bila kuwepo kwa ukomo kuwa Mfuko unaoweza kujidesha wenyewe, kama ni hivyo basi, sio Mfuko bali ni kitu kingine mbadala kinachohitajika kusaidia katika sekta hii. Kwa dhana endelevu ni lazima upatikanaji wa fedha zilizokuwa zimepangwa zifikie angalau asilimia 75 na kufikia asilimia 100, sasa makusanyo ni asilimia 59 na chini yake maana yake makato yataendelea kwa miongo kadhaa ijayo na watumiaji wa mafuta wataendelea kupata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kutokukamilika kwa lengo angalau kwa asilimia 90 ni kutokana na msinyao wa uchumi unaoendelea kuikumba nchi yetu, jambo linaloendelea kuleta matumizi ya mafuta hasa petroli na dizeli kushuka. Dhana hiyo ya mfuko, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuititia Mfuko huo kuingia ubia na sekta binafsi ili kuendesha miradi mikubwa ya maji kama vile miradi ya umwagiliaji, miradi ya malambo kwa ajili ya ufugaji na miradi ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Kwa njia hii ni dhahiri Mfuko utazidi kuwa endelevu na hivyo kupunguza kilio cha kila siku kuwa Serikali haina fedha. Ni ukweli kuwa maji ni huduma lakini vile vile ni biashara, pia suala hapa ni Serikali kuacha undumilakuwili na kuifanya kazi Sera ya PPPkwa vitendo kwa maeneo yenye uhitaji mkubwa wa maji ya shughuli za kibashara kama kilimo cha umwagiliaji na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasilitiza uhusishwaji wa Sekta binafsi katika hatua zote za utoaji wa huduma za msingi hasa katika miradi ya maji. Kutokana na historia ya matumizi ya Serikali inaonesha kuwa

sekte ya maji imetumia fedha nyingi sana lakini upatikanaji wa maji hauakisi thamani halisi ya fedha zilizokwisha kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa tangu mwaka 2006- *WSDP*-i ilipoanza jumla ya miradi 1,810 ilipangwa kutekelezwa, lakini mpaka sasa ni miradi 1,493 ndio imekamilika na miradi 366 inaendelea kujengwa. Aidha, vituo vya kuchotea maji 123,888 vilijengwa, lakini vinavyofanya kazi kwa sasa ni vituo 85,000 na vituo 38,602 havifanyi kazi kabisa, sawa na asilimia 31. Huu ni udhaifu mkubwa sana ambao ni lazima utafutiwe ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi hiyo yote na kuwa fedha zilikwishatolewa lakini matokeo yake wananchi wanaendelea kukosa maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka wasimamizi wa miradi hiyo ikiwemo Serikali kuhakikisha inakamilisha matumizi hayo ya maji na kuhakikisha wananchi wote wanaendelea kupata maji kwa uwiano unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba licha ya jitihada hizo za kutafuta mikopo, lakini bado tuna tatizo la uendelevu wa miradi, kama ilivyo shauriwa kwa muafaka sasa *PPP* itakayohusisha *BOT* ndilo litakalokuwa suluhisho la uendelevu kwa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka huu wa Fedha 2018/2019, Bunge liliombwa kuidhinisha fedha za miradi ya maendeleo yenye jumla ya shilingi bilioni 673.2. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 443.2 sawa na asilimia 66 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 230 sawa na asilimia 34 zilikuwa ni fedha za nje. Hadi Mwezi February 2019 jumla ya shilingi sawa na asilimia 15 ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 95. 3 sawa na asilimia 22 ya fedha za ndani. Fedha za nje zilizotolewa ni shilingi bilioni 4.7 tu sawa na asilimia 2.06 ya fedha za nje. Takwimu hizi zinaonesha kuwa fedha za maendeleo zinazotolewa zinakuwa zikipungua kila

mwaka hii ni dhahiri kuwa maji sio kipaumbele kwa Serikali hii ya CCM. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara inaomba fedha za maendeleo jumla ya shilingi bilioni 610.5; fedha za ndani ni shilingi bilioni 261.021. Katika Bajeti ya maendeleo upungufu ukilinganisha na ile ya mwaka 2018/2019 ni shilingi bilioni 62.7, sawa na asilimia 9.32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo inakosa fedha na iliyopatiwa fedha ni dhahiri kwamba tunachokipanga na kukipitisha hapa Bungeni, hakiendani na hali halisi. Hapa kuna miradi ambayo toka imeanza kuandikwa kwenye vitabu vya bajeti ni zaidi ya miaka saba sasa na bado haioneshi kama inamalizika, kama Miradi ya Bwawa la Kidunda, Mpera na Kimbiji. Madhara yake ni kwamba gharama zinazidi kuongezeka kila kukicha kutokana na ukweli kwamba thamani ya shilingi yetu dhidi ya dola ya Kimarekani inazidi kuporomoka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni muda muafaka sasa kwa Serikali kabla ya kuanzisha miradi mipyä tumalize miradi iliyopo tayari, kinyume cha hapo ni kuendelea kupoteza fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Randama ya mwaka 2018/19, ukurasa wa 51, kifungu cha 3.4.2.4, ukarabati na ujenzi wa majengo ya Wizara, ni ukweli hili linatusumbua kwani, ujenzi wa *Maji House Dar es Salaam*, jengo lenye ghorofa 13, pale pale kuna ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara ambayo ni Dodoma, jengo la Dar es Salaam ni kwa ajili ya watu gani? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni muhimu kwa uhai wa binadamu na viumbe vingine na yanatakiwa kusimamiwa vizuri. Pia maji ni mahitaji muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na hivyo wananchi wanayo haki ya kupata maji safi na salama na kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba magonjwa yatokanayo na maji machafu yanababisha vifo vingi kuliko vile vitokanavyo na vita na machafuko mengine ya kijamii duniani, kwa muktadha huo tutajikita katika uhifadhi endelevu wa vyanzo

vya maji, na hili litafanyika kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutahakikisha ubia imara kati ya sekta ya umma na binafsi katika kuwekeza kwenye miradi ya maji kwa mfumo wa Anzisha, Endesha na Hamisha Umiliki (*Build, Operate and Transfer*). Mfumo huu utatoa hakikisho la upatikanaji wa maji ya kutosha kwa matumizi ya majumbani, viwandani, wakulima, wanyama wafugwao na wale wa porini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hivi sasa kuangalia upya jinsi ya kufanya mgawanyo wa maji, kuhakikisha kila mwananchi anaendelea kupata huduma ya maji kama walivyooleza kwenye llani yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KUHUSU  
MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019  
NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA  
MWAKA WA FEDHA 2019/20 - KAMA YALIVYOWASILISHWA  
MEZANI**

(*Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9),  
Toleo la Mwaka 2016*)

## **1.0      UTANGULIZI**

1.      **Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii.

2.      **Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii adhimu kuwapongeza viongozi wakuu wa vyama

vyo Upinzani kwa mshikamano mkuu wanaouunesha katika kipindi hiki kigumu sana ambacho kufanya siasa nje ya CCM imekuwa ni kosa la jinali. Aidha, nimshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuendelea kuwa na imani na mimi katika majukumu ya kusimamia Wizara hii muhimu sana kwa maisha ya watanzania.

3. **Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu mkubwa niwashukuru wanachama wote wa vyama shindani pamoja na wananchi wote kwa kuendelea kutuunga mkono katika mapambano ya kupigania demokrasia ya kweli katika nchi hii hasa uchaguzi ulio huru na haki. Kwani Kambi Rasmi ya Upinzani ina amini kuwa bila haki hakuna demokrasia, pia hakuna amani katika nchi.

## 2.0 MUUNDO NA MFUMO WA KISEKTA

4. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaungana na tamko la kaulimbiu za kitaifa na kimataifa kuhusu umuhimu wa maji. Kaulimbiu hizi ni kwamba; "*Maji ni Haki ya Kibinaadamu, Maji ni Uhai, Maji ni Uchumi; Maji ni Msingi wa Amani*".

5. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba pamoja na kwamba maji ni huduma vile vile ni biashara. Ukweli ni kwamba kwa sasa hakuna huduma yoyote ya kijamii inayotolewa bure na Serikali, achilia mbali ukweli kwamba kodi zinazotolewa na wananchi wenyewe ndio zinaitwa fedha za Serikali. Pamoja na kodi bado Bunge limeidhinisha tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta kwa ajili ya uwekezaji kwenye maji.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa "huduma ya maji" hakuna eneo lolote katika Tanzania ambalo wanapata maji ya bomba au kutoka katika vyanzo vyao maji safi na salama bila ya malipo ya aina yoyote. Hivyo huduma hii ya maji, iwe ni kwa matumizi ya majumbani, matumizi ya mifugo, matumizi ya viwandani au kwa matumizi ya kilimo, hiyo yote ni sehemu ya huduma ya maji ni gharama hivyo watumiaji wa maji hupatiwa kwa malipo ili kuchangia uzalishaji wa maji

safi na salama. Lakini kwa kiingereza, tunasema water has an economic value.

**7. Mheshimiwa Spika**, Hivyo basi, kama ni biashara utolewaji wa huduma hiyo lazima kuwepo na ushindani ili mtumiaji wa huduma hiyo apate huduma iliyo bora zaidi. Kwa muktadha huo, sekta binafsi ni mdau muhimu sana katika utoaji wa huduma hii kwa wananchi.

**8. Mheshimiwa Spika**, umuhimu wa maji kwa ajili ya uhai wa watu, wanyama, mimea na mazingira kwa ujumla ni jambo lisilopingika. Bila ya maji, viumbe vyote vitapotea, mazingira yatakuwa mfu, na maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii yatadumaa. Kutokana na umuhimu wa maji, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha tarehe 21 Desemba 2016 limeridhia kwa kauli moja miaka kumi ya utekelezaji wa **Azimio jipya la Maji kwa Maendeleo Endelevu (Interational Decade (2018-2028) for Action- Water for Sustainable Development)**.

**9. Mheshimiwa Spika**, Dira ya Maendeleo ya Taifa (Tanzania Development Vision 2025) Pia Mpango wa pili wa Maendeleo wamiaka mitano 2016-2021 wa Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda ifikapo 2015, azma hii haiwezi kufikiwa iwapo changamoto za upatikanaji wa maji kwa matumizi ya nyumbani,kilimo na kwa ajili ya viwandani hazitajipiwa kikamilifu. Japokuwa dira imeweka malengo ya maendeleo ya kiuchumi, kisasa na ustawi jamii ikiwa ni pamoja na malengo yanayogusa moja kwa moja Wizara na Sekta ya Maji na Umwagiliaji. Baadhi ya malengo muhimu katika muktadha huu ni kama ifuatavyo:-

- i. Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati, ambapo wananchi wake wanafurahia amani na umoja wa kitaifa
- ii. Upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wote. Ambapo kwa wakazi wa mijini watapata maji kwa asilimia 100 na kwa wakazi wa vijijini watapata maji safi na salama kwa angalau asilimia 90 ifikapo 2025.

iii. Kuhakikisha kwamba rasilimali za maji ni endelevu ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii.

### **3.0 HALI YA MAJI KWA NCHI YETU**

**10. Mheshimiwa Spika**, pamoja na upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama vijijini na mijini, bado Tanzania inakabiliwa na changamoto nydingi za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Tofauti na nchi nydingi majirani, nchi ya Tanzania imeaaliwa kuwa na rasilimali za kutosha za maji safi – mito, maziwa, maji ya kwenye miamba, na ardhioevu – za kutosheleza mahitaji yake yote ya sasa ya maji.

**11. Mheshimiwa Spika**, Takwimu za kitaifa za rasilimali za maji zilizopo zinaonesha kuwa kiasi cha maji kwa sasa kwa kila mtanzania ni wastani wa **mita za ujazo 1,952** kwa mwaka. Pamoja na takwimu hizi ikumbukwe kuwa idadi ya watu imeongezeka kwa kasi katika miaka 25 iliyopita, vile vile matumizi ya maji sio tu yameongezeka bali yamebadilika kwa kiasi kikubwa kufuatia kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi,kukua kwa miji,mabadiliko ya mfumo wa kilimo,biashara na viwanda. AMBAPO kilimo kinachukua wastani wa asilimia 89 ya rasilimali za maji,matumizi ya majumbani na ya taasisi ni asilimia 10 na viwandani ni asilimia 1 . Endapo hatua madhubuti za utunzaji wa vyanzo vya maji hazitachukuliwa mapema, kiasi hicho kinatarajiwu kupungua hadi kufikia **mita za ujazo 883** mwaka 2035. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni **mita za ujazo 1,700**

**12. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri hapa kama hatutachukua hatua stahiki si muda mrefu Tanzania inaweza kuwa kwenye tatizo kubwa la maji ambapo ukosefu wa maji linakuwa janga kubwa na hivyo kupelekea rasilimali hiyo kuwekewa utaratibu wa jinsi gani ya kugawanywa kwa kila familia, mifugo na kwa matumizi ya viwandani kama ilivyowahi kuwa kwa nishati ya umeme.

- 13.** **Mheshimiwa Spika**, Mkakati wa Tanzania wa Kusaidia Rasilimali za Maji wa Mwaka 2006 unatambua umuhimu wa kipekee wa maji katika utendaji kazi wa sekta muhimu za kiuchumi na ustawi wa Watanzania. Mkakati huu unabainisha athari za uwekezaji duni katika: (a) usambazaji wa maji na huduma za usafi kama hitaji la msingi kwa maisha zalishi (b) uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji na uzalishaji wa umeme wa maji kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa chakula na nishati ya kutosha.
- 14.** **Mheshimiwa Spika**, Mkakati huu unabainisha namna utendaji kazi wa sekta kuu za uchumi (nishati, kilimo, viwanda, mifugo, uchimbaji madini, utalii, na uvuvi) zinavyoathirika kutokana na ukame, mafuriko, na usimamizi duni wa rasilimali za maji. Pia, unasisitizia haja ya kufanya juhudzi za haraka za kupanua uwekezaji katika uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji, udhibiti mzuri wa rasilimali za maji, na ulinzi na uhifadhi wa vyanzo muhimu vya maji – mito, maziwa, maji ya kwenye miamba, na ardhioevu.
- 15.** **Mheshimiwa Spika**, hivyo basi, ushahidi huo ni ukweli kabisa kuwa Maendeleo ya kijamii na kiuchumi yana uhusiano wa moja kwa moja katika upatikanaji wa rasilimali ya maji na utunzaji wa mazingira. Maji ni rasilimali inayomalizika kama haikutunzwa ili kuwa endelevu, hivyo maendeleo ya kilimo, mifugo, viwanda vyote vinatagemea upatikanaji wa uhakika wa rasilimali ya maji.
- 16.** **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli pia kuwa mahitaji ya matumizi ya maji yanazidi kuongezeka, japokuwa upatikanaji wa maji unazidi kupungua na mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka kutokana na ukweli kuwa idadi ya watu inazidi kuongezeka, kutokuwa na mifumo mizuri ya kuhifadhi maji ya mvua (Inadequate rain-water storage), mabadiliko ya tabianchi pamoja na shughuli za kiuchumi ambazo hazizingatii utunzaji wa mazingira ambayo ndicho chanzo kikuu cha maji mengi ya mito yetu. Hivyo ni lazima kuwa na mkakati madhubuti wa kuhakikisha maji yaliyopo yanatumiwa kwa uangalifu na uendelevu.

17. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na tatizo la maji ni lazima kuifanya rasilimali hii kutumika kwa uangalifu na kwa uendelevu baina ya makundi yote ya kijamii, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa; ni lazima mahitaji kwa kila kundi katika mfumo mzima wa uzalishaji(kilimo,mifugo,viwandani na majumbani) lijulikane mahitaji yake (water demand) kwa siku ni lita ngapi, hapo ndipo tunapoweza kupanga mgawanyo wa uendelevu; lazima kuwa na mipango ya muda mfupi,kati na muda mrefu ya kuvuna maji na matumizi yake.

#### 4.0 UHIFADHI WA VYANZO VYA MAJI

18. **Mheshimiwa Spika**, Usimamizi wa vyanzo vya maji nchini unafuata taratibu za mipango shirkishi ya usimamizi wa rasilimali za maji kwenye Bodi za Maji za mabonde tisa yaliyopo nchini, ambapo **saba** katika hayo yanahusisha maji shirkishi kati ya nchi yetu na nchi jirani.

19. **Mheshimiwa Spika**, Changamoto kubwa iliyopo kwenye usimamizi wa rasilimali za maji ni kupungua na kuharibika kwa vyanzo vya maji kutokana na shughuli za kibinadamu, suala la uchafuzi wa vyanzo vya maji.Taarifa za uchafuzi kuanzia mwaka 2014(Joint Water Sector Review)na tafiti nyingine za kitaalam kama zile za Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na nyinginezo zinaonesha athari za uchafuzi mkubwa na hapa tunatoa baadhi ya maeneo yaliyoathirika kwa kiwango kikubwa. Katika maeneo ya vyanzo vya maji na katika misitu ya hifadhi ya maji (*catchments forests and wetlands*). Aidha, kupungua huko kunatokana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kumeathiri shughuli za kijamii na kiuchumi na na kusababisha migogoro kwenye vyanzo vya maji. Hifadhi hizi zinawezesha upatikanaji wa maji juu na chini ya ardhi.

20. **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa mabonde tisa ya maji, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni lazima na muhimu kuhifadhi vyanzo vya maji kwa mabonde hayo bila kusahau umuhimu wa kipekee wa uhifadhi wa vyanzo vya bonde la

Rufiji ambalo chanzo chake ni mabonde ya Kilombero na Ruaha.

**21. Mheshimiwa Spika**, Ikumbukwe hapa kwamba, Mto Rufiji hupata maji yake mengi kutoka mito miwili mikuu—Kilombero na Ruaha Mkuu—na hasa Mto Kilombero, ambao huchangia theluthi mbili ya maji ya Mto Rufiji kabla hayajafika *Stiegler's Gorge*. Hivyo ustawi wa Mto Rufiji unategemea ustawi wa Mto Rufiji; ambao nao pia unategemea (kwa asilimia 60) ustawi wa Mto Kilombero; hususan Bonde la Mto Kilombero.

**22. Mheshimiwa Spika**, Ni dhahiri, kwamba uwezekano wa Watanzania kupata umeme wa maji wa bei nafuu kutoka *Stiegler's Gorge*, ni ndoto inayokaribia kuwa ya kweli endapo Serikali itashindwa kuchukua hatua za makusudi za kuhifadhi (conservation measures) Bonde la Mto Kilombero, kwani ustawi wa bonde hilo hivi sasa unasambaratishwa na shughuli za kibinadamu.

**23. Mheshimiwa Spika**, Wataalamu wanakubaliana kwamba, uharibifu wa mazingira ukiongeza na tatizo la sasa linaloikumba dunia nzima—mabadiliko ya tabianchi (*climate change*), vinaashiria kuwa muda si mrefu Bonde la Kilombero linaweza kupoteza sifa yake ya kuwa bonde adhimu la maji baridi ambalo ni kubwa kuliko yote duniani, lililokuwa linajaa maji misimu yote.

**24. Mheshimiwa Spika**, kitu pekee ambacho wataalamu hao wanatofautiana, ni muda uliobakia kabla Bonde hilo halijasambaratika kabisa. Ni muhimu Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge kuhusu hali halisi ya Bwawa la Ngapemba lililopo katika Kata ya Utengule na lile la Kibasila ambayo ni makubwa na yamekuwepo kwa miaka mingi likiwa ni chanzo kikuu cha shughuli za kiuchumi kwa wanavijiji wanaozunguka Bonde la Kilombero. Bwawa hilo Ngapemba lililokuwa na ukubwa wa eka za mraba 1,000 na lililokuwa na hekaheka nyingi za uvuvi, sasa limenyauka na kusinyaa na kubakia eka chache sana za mraba.

**25. Mheshimiwa Spika**, Utafiti uliofanywa na JET kuhusu hali ya mito kati ya Kihansi na Ifakara, unaonyesha kati ya mito 29 iliyokuwepo, sasa imebaki mito mitano tu, huku mito tisa ikiwa na maji yaliyotuama. Mionganoni mwa mito hiyo mitano ambayo inatiririsha maji, ni Luipa, Mpanga na Mnyera ndio bado ina maji ya kutosha mwaka mzima. Kwa hiyo, hali ya mito katika Bonde la Kilombero ni mbaya, na chanzo kikubwa cha hali hiyo ni uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi.

**26. Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo ni kwa vipi uzalishaji wa umeme wa maji kwa mradi wa Stiegler's Gorge utakuwa endelevu?

#### **5.0 UHABA WA MAJI NA UCHAFUZI WA VYANZO VYA MAJI**

**27. Mheshimiwa Spika**, uhaba wa maji katika maeneo mengi ya miji na miji midogo ni mkubwa sana ila kutokana na kutokuwepo kwa taarifa za uhakika tunashindwa kuweka takwimu za uhaba kwa kila eneo hadharani ili Serikali iweze kuzifanya kazi. Lakini kwa taarifa za Uhakika tulizozikusanya na kuzithibitisha kutoka kwa Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, na viongozi wa Chadema kwenye kata zote sita(6) na Mitaa 45 iliyopo Jimbo la Kibamba imebainika kwamba;

**28. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Usambazaji wa Maji unaofanywa na JAIL IRRIGATION haujakamilika mpaka leo mbali na Naibu Waziri kueleza ulikamilika 2016. Maeneo ya Kwa Mwakatundu, Kwa Nyembele, Kwafungo na Kwa Mndeme katika barabara ya Makabe na kwa Mangara barabara ya Mpiji MAGOE bomba kubwa la Inchi 10 halijaunganishwa mpaka hii leo.

**29. Mheshimiwa Spika**, hakuna Ujenzi wa TENKI ulioanza wala unaoendelea katika eneo la MSAKUZI (Kwa Paulo)kata ya MBEZI na MARAMBA MAWILI (Maarufu kama Manzese) kata ya MSIGANI na mbaya zaidi wananchi waliopaswa kuachia ardhi kwaajili ya Ujenzi huo wa Matenki hawajalipwa fidia hadi leo japokuwa maeneo yao yalifanyiwa uthamini Februari 2018. Baadhi ya wananchi waliounganishiwa

huduma ya maji miezi 3 iliyopita katika mitaa ya Luis, Msakuzi Kusini Kata ya Mbezi mpaka leo hawajapata maji.

**30. Mheshimiwa Spika**, kuna maeneo yasiyo na maji kabisa katika kata zote sita (6) za jimbo la Kibamba. Mbezi katika Mitaa 8 ya kata ya Mbezi, Mitaa ya Mpiji Magoe, Msumi, Makabe na Msakuzi hakuna kabisa Mtandao wa Maji wananchi hununua maji kati ya 18,000 hadi 20,000 kwa lita 1000. Katika Mtaa wa Luis eneo la Upendo, Furaha, kwa Mkome na Maeneo ya Uzunguni hakuna kabisa Miundombinu.

**31. Mheshimiwa Spika**, kata Goba-katika mitaa 8 iliyopo kata hiyo, mtaa wa Muungano, Tegeta A, Matosa na Kibururu hakuna kabisa maji ya bomba. Mtaa wa Kunguru 45% wanapata maji lakini maeneo ya Kitongwa, Kontena B na Kwa Ndambi Kiswani hakuna maji kwa sababu presha ya maji ni ndogo sana na haiwezekani kuunganishiwa wateja wapya. Mtaa wa Kulangwa ambao unategemea maji kutoka Kisauke maji hutoaka mara 1 hadi 2 ndani ya mwezi mmoja na maeneo ya Jipe moyo, Mtambani, Mwishehe na Kimambo hakuna mtandao kabisa.

**32. Mheshimiwa Spika**, kata ya KWEMBE Katika mitaa 10 iliyopo kata ya Kwembe, Mitaa ya Kisopwa, Mpakani na Kingazi A hakuna mabomba kabisa. Mitaa ya Njeteni, Mloganzila maji hupatikana maeneo machache yasiyofika robo ya eneo la mtaa na maeneo maji yanatoka hutoka mara chache. Mtaa wa Msakuzi Miundombinu ni michache na haijawahi kutoa maji kabisa.

**33. Mheshimiwa Spika**, kata ya MSIGANI Katika Mitaa 5 iliyopo katika kata hiyo; Mtaa wa Msingwa, Maramba Mawili hakuna kabisa Mtandao wa Maji na Kwa Yusufu hakuna MAJI KABISA lakini mabomba yamesambazwa Mnarani na Mchungwani wakati Njeteni, Kwamakofia na Mbezi Hill hakuna hata miundombinu kabisa. Mtaa Temboni Kanisa la Udongo hakuna maji.

**34. Mheshimiwa Spika**, kata ya KIBAMBA-Katika Mitaa 5 ya kata hiyo; maeneo ya Magengeni - uwanjani, uwanjan kwenda shule ya msingi, mbuyuni kwenda malonga na msakati hayana Maji wala mtandao.

**35. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kulieleza Bunge ni lini wananchi hao ambao wanaishi kandokando ya Bomba kuu linalosambaza maji kutoka Ruvu kwenda maeneo mengine ya jiji lini watapatiwa maji ya uhakika?

**36. Mheshimiwa Spika**, kwa ushahidi wa uhakika uliotolewa na taasisi ya shahidi wa maji kuhusu uchafuzi wa maji kwenye Mto Ngerengere ambao unamwaga maji yake kwenye Mto Ruvu, ambao ni chanzo kikuu cha maji yanayotumiwa na wakati wa Mkoa wa Dar es Salaam na hivyo kuhatarisha maisha ya maelfu ya wakazi wa jiji la Dar es salaam, Kibaha na Bagamoyo.

**37. Mheshimiwa Spika**, Mto Ngerengere unapokea maji taka kutoka kwenye ukanda wa viwanda wa Morogoro pamoja na mfumo mzima wa maji taka ya mji wa Morogoro (**Morogoro Industrial complex and Morogoro Urban Water Supply and Sewerage Authority-MORUWASA**).

**38. Mheshimiwa Spika**, maji taka yanayoingia kwenye mto huo kutoka kwenye viwanda vya nguo na viwanda vya ngozi hayafai kabisa kutumika kwa matumizi ya nyumbani na kwa matumizi ya kilimo kutokana na kuwa na viwango vya juu vya kemikali hatarishi kwa viumbe hai.

**39. Mheshimiwa Spika**, kutokana na kutokuwa na chanzo mbadala cha maji kwa wakazi zaidi ya 5000 waishio kwenye maeneo ya Kipera, Kingolwira, Bomba la Zambia na Sanga Sanga wanalazimika kutumia maji ya mto huo kwa matumizi ya nyumbani na mashambani hivyo hivyo bila kutiwa dawa. Jambo hilo linahatarisha usalama wa afya zao. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli kuhusiana na uchafuzi huo wa chanzo kikuu cha maji kwa mamilioni ya wakazi wa Dar Es Salaam sambamba na wale wa jamii tajwa hapo juu.

## 6.0 MIRADI YA MAJI YA KIDUNDA, KIMBIJI

40. **Mheshimiwa Spika**, ukiangalia Randama ya Wizara inaonesha kuwa mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ili ukamilike unahitaji kiasi cha dola za Kimarekani milioni 215. Kwa mwaka 2018/19 mradi wa Bwawa la Kidunda uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 3 lakini haikutoka hata shilingi na mwaka 2019/20 zimeombwa tena shilingi bilioni 3, na kwa mradi wa Mpera na Kimbiji mwaka 2018/19 ziliidhinishwa shilingi 14,109,999,000.00 lakini hazikutoka hata shilingi, mwaka 2019/20 zimeombwa tena shilingi bilioni 3. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Serikali haina uhakika na nini hasa inataka kifanyike katika huo Mradi wa Mpera na Kimbiji kwani tofauti ya maombi ya mwaka jana na mwaka huu ni kubwa sana pia kwa kuangalia hali halisi ya thamani ya shilingi kwa dola ya Kimarekani. Hii inapelekea kushindwa kufanya tathmini ya thamani ya fedha iliyotumika na kazi iliyofanyika.

41. **Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo tumetangulia kusema, kuwa hakuna huduma ya bure na hivyo ukiangalia mwongozo wa biashara kwa mradi huo ni dhahiri inajulikana wanufaikaji ni wangapi na kwa muda gani uwekezaji huo utakuwa umerejesha fedha hizo. Kwa mantiki hiyo basi kushindwa kumalizia mradi huo ambao kwa sasa umeishachukua takriban miaka zaidi ya minane (8) na wakati huo huo thamani ya shilingi yetu dhidi ya dola inazidi kuporomoka.

42. **Mheshimiwa Spika**, mtazamo huo wa Serikali maana yake ni kwamba miradi mingi ya huduma za jamii hazitakuja kukamilika kwa miaka ya karibuni hadi watu wenye muono wa kibiashara watakapo kuwa kwenye madaraka.

43. **Mheshimiwa Spika**, ukiangalia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/19 (Randama) uk. wa 44 hadi uk. wa 49 kuna miradi ya maji inayofanyiwa usanifu na mingine inayoendelea au mingine iliyokamilika (*Mradi wa Same - Wanga - Korogwe, Maji Mkoa wa Kigoma, Mradi wa Maji wa Ntomoko, Maradi wa Chiwambo, Mradi wa Ukarabati na*

**ujenzi wa Mabwawa, Mradi wa Maji wa Lukululu n.k.)** lakini mingi haifanyi kazi na imetumia fedha nyngi na mingine inailazimu Wizara itoe maelekezo kuwa miradi mingine isitekelezwe na Halmashauri kutokana na sababu zao na hivyo mamlaka za maji za mikoa zihuishwe katika utekelezaji wake. Lakini hoja ya msingi ni je ikishatekelezwa ni mamlaka ipi itakuwa inaiendesha miradi hiyo? Hapa ndipo kutupia mpira kunapoanzia, kwani waendeshaji watasema haikujengwa kwa kiwango kinachohitaji na visingizo vingine kama hivyo.

**44. Mheshimiwa Spika,** tatizo sio uwezo mdogo wa Halmashauri,tatizo linaanza Serikali Kuu ambao ndio waratibu, wasimamizi na walipaji. Hapa lipo tatizo la msingi la kutokuwa na vipaumbele vinavyogusa moja kwa moja maisha ya watanzania na maeneo yenye mchango mkubwa na wa haraka kwa maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Wimbo wa Serikali inayodhamiria kujenga uchumi wa Viwanda utaendelea kuimbwa bila mafanikio ikiwa mwelekeo huu hautabadilika na kuwekeza kwenye miradi yenye kuchochea maendeleo halisi ya uchumi wetu kama kwenye maji.

**45. Mheshimiwa Spika,** tumesema maji ni uhai, ni umeme, ni kilimo cha uhakika,ni chakula ni mifugo, ni usafi na mazingira yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kufahamu hivi mradi kama wa Kidunda wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 215 unalinganishwa na nini hasa? Hivyo ilikuwa sahihi kuwekeza katika ununuzi wa Ndege za ATCL zaidi ya mara mbili ya fedha zilizotakiwa kukamilisha Bwawa la Kidunda litakalotoa ajira zaidi ya ATCL, kwani litatoa maji kwa ajili ya umwagiliaji, hususan kilimo cha miwa, viwandani,litainua uvuvi, litavutia watalii n.k Kwa muktadha huo Kambi Rasmi inahitaji maelezo ya Serikali kwanini hadi sasa mradi huo haupatiwi fedha ili ukamilike.

**46. Mheshimiwa Spika,** katika ujenzi wa miradi mikubwa Serikali inaweza kuingia katika ubia na Sekta binafsi na miradi kutekelezwa kwa utaratibu wa Kujenga mradi na kuuendesha na baadae kuurudisha Serikali (Build Operate and Transfer-BOT). Utaratibu huu kwa mazingira yetu ambayo Serikali

imeshindwa kupata mikopo ya masharti nafuu-(concessional/ soft loans) ndio utaratibu utakaokuwa suluhisho katika miradi ya maendeleo. Na katika hili mjenzi wa mradi kwa njia ya ubia naye ndiye atakuwa muendeshaji hadi fedha zao zilizowekwa kwa mujibu wa mkataba zitakaporudi na faida ndipo mradi utaendeshwa na mbia mwenza Serikali au wakala wake

**47. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa hili inasisitiza mikataba kuwa wazi na yenye tija baina ya wabia watakao husika katika utekelezaji na usimamizi wa miradi hiyo.

#### **7.0 UZALISHAJI NA MAHITAJI YA MAJI MIJINI (Upatikanaji wa maji mijini)**

**48. Mheshimiwa Spika**, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, aliyoitao hapa Bungeni mwezi Mei, 2018 uk. wa 8 aya ya 16 imetoa takwimu ya kukamilika kwa baadhi ya miradi ya maji kwa kipindi cha mwezi Machi 2017 hadi Machi 2018, ikionesha ongezeko la maji dhidi ya mahitaji kwa maeneo ya mijini. Hivyo imetulazimu kuchambua takwimu hizo kama ifuatavyo ili kuonesha hali halisi ya upatikaji wa maji kwa maeneo ya mijini kulingana na takwimu zilizotolewa na Waziri

	Uzalishaji-(ita kwa millioni kwa siku)	Mahitaji-(ita kwa millioni kwa siku)	% ya Upungufu
Miji Mikuu ya Mikoa	404	646	37.4
Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo	100.6	277.8	63.7
Miradi ya Maji ya Kitaifa	67.2	125.6	46.5
Dar na Miji ya Kibaha na Bagamoyo	504	544	7.35
<b>Wastani wa upungufu wa uzalishaji kwa siku kwa mijini</b>		<b>38.74</b>	
<b>Upatikanaji wa maji mijini</b>		<b>61.3</b>	

**49. Mheshimiwa Spika**, kutokana na takwimu hizo ni kuwa upatikanaji huo ni pale miradi inapokuwa imekabidhiwa kwa kuanza kutumika, lakini kutokana na mambo mbalimbali yaliyo ndani na nje ya uwezo wetu miradi hiyo inalazimika kufanyakazi chini ya kiwango au kusimamisha kabisa kufanya

kazi. Hivyo tatizo la Upatikanaji wa maji kuzidi kuwa kubwa zaidi na takwimu ya 61.7% kushuka chini sana kutokana na ukweli kwamba ongezeko la watu kwa mwaka (Population growth rate), kwa makadirio ya mwaka 2017 ilikuwa ni asilimia 2.75. Changamoto ya ubora wa maji (water quality); Usafi na uhakika wa upatikanaji wa maji. Aidha, upotevu wa maji kutokana na uharibifu wa miundombinu na uchakavu wa mabomba ni moja ya sababu dhahiri za kutilia shaka takwimu zinazoelezwa. Mfano DSM inaelezwa kuwa zaidi ya 49% ya maji hupotea njia, lakini kinachothesabiwa ni maji yanayotoka kwenye chanzo kuingia kwenye mitambo ya bomba.

## **8.0 UPOTEVU WA MAJI**

**50. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri alioitoa hapa Bungeni mwezi Mei, 2018 uk wa 19 aya ya 19 changamoto kwa mamlaka zinazotoa huduma za maji ni upotevu wa maji. Takwimu zinaonesha kuwa upotevu wa maji kwa Jiji la Dar, Kibaha na Bagamoyo ni asilimia 49, Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ni asilimia 39, Miji Mikuu ya mikoa ni asilimia 32. Sababu zilizotolewa kuhusiana na upotevu wa maji Rejea Randama ya Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/20 - uk. 47 na 48 kubwa ni uchakavu wa miundombinu ya mifumo ya usambazaji wa maji.

**51. Mheshimiwa Spika**, kwa mahesabu hayo ni kwamba upatikanaji wa maji halisi kwa Jiji la Dar pamoja na Kibaha na Bagamoyo ni sawa na asilimia uzalishaji ukitoa asilimia ya upotevu. Hivyo kwa Jiji la Dar-es-Salaam sawa na upatikanaji wa maji halisi ni kwa asilimia 51 hapa ni kwa wale tu ambao tayari wako kwenye mtandao wa mabomba ya maji. Vivyo hivyo kwa miji mikuu ya mikoa, wilaya na miji midogo hali ni mbaya zaidi. Kwani ukichukulia asilimia ya upungufu kulingana na mahitaji halisi ya maji ambayo imeoneshwa kwenye jedwali hapo juu na utoe pia asilimia ya upotevu hali inazidi kuwa mbaya zaidi.

**52. Mheshimiwa Spika**, kwa hesabu za kawaida ni kuwa kwa wilaya na miji midogo asilimia ya upungufu kulingana

na mahitaji halisi ni 63.7% na upatikanaji ni 36.3% wakati Hotuba ya Waziri kwa mwaka 2018/19 inasema upotevu ni 39%. Hii maana yake ni kuwa Wilaya na Miji Midogo mingi, haina kabisa uhakika wa upatikanji wa maji.

**53. Mheshimiwa Spika**, lengo lililowekwa na ilani ya CCM iliyoingiza madarakani Serikali ya awamu ya tano ya Rais Magufuli ni kuwa hadi 2020 Dar iwe na upatikanaji wa maji kwa asilimia 95 na miji mingine iwe ni asilimia 90. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je, kwa mwendo huu wa hali halisi ya maji tutafikia malengo?

#### **9.0 MFUKO WA MAJI**

**54. Mheshimiwa Spika**, mfuko wa maji unachangiwa kwa makato ya watumiaji wa bidhaa ya mafuta ya petrol kwa shillingi 50 kwa kila lita moja ili kuwa endelevu. Taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2018/19 inaonesha kuwa mfuko umepata jumla ya shillingi billioni 93.661 sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mapato ya mwaka wa fedha 2018/19.

**55. Mheshimiwa Spika**, lengo lilikuwa ni kumtua mama ndoo ya maji lakini kwa makusanyo hayo maana yake kuna tatizo sehemu fulani kwa nini mapato hayakukamilika angalau kwa asilimia 90? Lakini makato hayo hayawezhi kuwa ya milele bila kuwepo kwa ukomo kuwa mfuko unaweza kujidesha wenyewe, kama ni hivyo huo sio mfuko bali ni kitu kingine. Kwa dhana ya uendelevu ni lazima upatikanaji wa fedha zinazokuwa zimepangwa zifiki angalau asilimia 75 na kufikia asilimia 100, sasa makusanyo ya asilimia 59 na chini yake maana yake makato yataendelea kwa miongo kadhaa ijayo na watumiaji wa mafuta wataendelea kupata shida.

**56. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa kutokukamilika kwa lengo angalau kwa asilimia 90 ni kutokana na msinyao wa uchumi unaoendelea kuikumba nchi yetu, jambo linalopelekea matumizi ya mafuta hasa petroli na dizeli kushuka.

**57. Mheshimiwa Spika**, kwa dhana hiyo ya mfuko, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia mfuko huo kuingia katika ubia na Sekta binafsi kuendesha miradi mikubwa ya maji kama vile miradi ya umwagiliaji, miradi ya marambo kwa ajili ya ufugaji na miradi ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Kwa njia hii ni dhahiri mfuko utazidi kuwa endelevu na hivyo kupunguza kilio cha kila siku kuwa Serikali haina fedha. Ni ukweli kuwa maji ni huduma lakini vile vile ni biashara pia tena kubwa; suala hapa ni Serikali kuacha undumila kuwili na kufanya kazi Sera ya PPP kwa vitendo kwa maeneo yenye uhitaji mkubwa wa maji ya shughuli za kibiashara kama kilimo cha umwagiliaji na mifugo.

**58. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisisitiza uhusishwaji wa Sekta binafsi katika hatua zote za utoaji wa huduma za msingi hasa miradi ya maji, kwa kutokana na historia ya matumizi ya Serikali Inaonesha kuwa sekta ya maji imetumia fedha nyingi sana lakini upatikanaji wa maji hauakisi thamani halisi ya fedha zilizowekezwa.

**59. Mheshimiwa Spika**, ukiangalia Randama uk. wa 50 Serikali kwa kushauriwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DFID) wamebuni mpango wa kuimarishe uendelevu wa Huduma ya Maji Vijiji-Mfumo wa Malipo kwa Matokeo. Hii ni kutokana na miradi mingi kutokuwa endelevu na hivyo kuwa changamoto kubwa sana kwa Serikali.

**60. Mheshimiwa Spika**, jambo hili kwa kiasi kikubwa ni kutohusisha sekta binafsi na hivyo kukosekana kwa dhana nzima ya umiliki wa miradi hiyo, fedha za mikopo au ufadhilli zinaonekana kutokuwa na mwenyewe (*Kasumba ya Mali ya umma haina mwenyewe*) kwa kuanzia na hatua za mwanzo kabisa za usanifu na utekelezaji wa miradi na inapofikia hatua ya uendeshaji ndipo balaa la ufujaji wa fedha linapogundulika. Tunatakiwa kuondoa kwanza kasumba hiyo kwa watendaji kwa kupitia umiliki na uendeshaji wa Sekta binafsi kwa miradi ya maji.

**61. Mheshimiwa Spika**, kuundwa kwa Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs) kuhusu uendeshaji na

matengenezo ya miradi ya maji vijijini, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa suala hili halitoweza kutoa suluhisho la tatizo lillipo katika miradi hiyo, kwani watumiaji hawana umiliki wowote kwa maana ya uchangiaji wakati mradi unaanza na kutekelezwa.

**62. Mheshimiwa Spika**, kuondokana na tatizo hili ni vema watumiaji wa maji wakashirikishwa toka mwanzo, mawazo na matamano yao yakazingatiwa ili kuleta dhana ya ushirikishwaji kamili sio hila ya kubambikiwa miradi yenye matatizo toka siku ya kwanza ya kukabidhiwa.

#### **10.0 UTAFUTAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAJI**

**63. Mheshimiwa Spika**, ukurasa wa 53 wa Randama ya mwaka 2018/19 ulionesha kuwa mbali na kupatikana na ahadi za dola za Kimarekani billioni 1.93 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya Pili ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, pia Serikali ilikamilisha majadiliano kwa ajili ya mikopo ya masharti nafuu yenye jumla ya dola za Kimarekani milioni 829.7.

**64. Mheshimiwa Spika**, Randama ya Wizara Fungu 49 kwa mwaka wa fedha 2019/20 uk. 40 na 41 inaonesha kuwa fedha ambazo zimeshatafutwa kwa ajili ya miradi maji katika miji mbalimbali ni **Euro milioni 313** kwa **exchange rate** ya Euro 1 shilingi 2,605.09 kama ilivyotolewa na BOT 15 Aprili 2019 ni sawa na **shilingi bilioni 815.4 au** (*815,393,170,000.00*) hizo kutoka Benki ya KFW ya Ujerumanii pamoja na Green Climate Fund. Kiasi cha **Euro milioni 70 sawa na shilingi bilioni 182.4 au** (*182,356,300,000.00*) Aidha, **USD milioni 500** kutoka Serikali ya India, ambazo ni sawa na **shilingi trilioni 1.12 au** (*1,115,050,000,000.00*)

**65. Mheshimiwa Spika**, jumla ya fedha hizi kwa mahesabu yetu ni **shilingi trilioni 2.12 au** (*2,117,024,970,000.00*); hizi ni fedha nyingi sana zinahitaji uangalizi wa karibu kwa kushirikisha wadau wakubwa katika miradi hiyo ambayo ni wananchi katika mchakato mzima wa kufuatilia na kuona thamani ya fedha hizo inapatikana.

**66. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kama ilivyosema katika Hotuba yetu ya Utumishi na Utawala Bora kwamba, tatizo kubwa la nchi yetu ni kukosekana kwa **mifumo imara ya Ufuatiliaji na tathmini** katika ufuatiliaji wa miradi ya maji vijijini kuna mfumo wa kidigitali uliotumia fedha nyingi katika uwekezaji wake wa **WATER MAPPING SYSTEM** lakini wahandisi wa maji hawatoi taarifa zenyе uhalisia juu ya utendaji kazi wa miradi yote. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina ni kwanini Serikali inakosa takwimu za uhakikia kuhusiana na upatikanaji wa maji hapa nchini?

**67. Mheshimiwa Spika**, kuna mfumo mwingine wa EWURA ambao kila mwaka mamlaka hii hutoa taarifa za utendaji za Mamlaka za Maji kwenye Miji na Miji Midogo, lakini kwa bahati mbaya watanaotakiwa kuchukua hatua wanakuwa ni sehemu ya utendaji mbovu wa mamlaka hizo.

**68. Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa tangu mwaka 2006- WSDP-I ilipoanza jumla ya miradi 1810 ilipangwa kutekelezwa, lakini hadi sasa ni miradi 1493 ndiyo imekamilika na miradi 366 inaendelea kujengwa. Aidha, vituo vya kuchotea maji 123,888 vilijengwa lakini vinavyofanya kazi ni vituo 85,286 na vituo 38,602 havifanyikazi kabisa sawa na asilimia 31, Mheshimiwa Spika, huu ni udhaifu mkubwa sana ambao ni lazima utafutiwe ufumbuzi wa haraka.

**69. Mheshimiwa Spika**, katika miradi hiyo yote ni kuwa fedha zilikwishatolewa lakini matokeo yake wananchi wanaendelea kukosa maji. Kambi Rasmi ya Upinzani inaelewa kuwa hata hiyo miradi ambayo Serikali inasema kuwa imekamilika kwa ajili ya matumizi ya wananchi, uwezekano mkubwa ni kuwa iko pale lakini wananchi hawanufaiki nayo na hata ile inayofanyakazi bado mingine siyo kwa asilimia 100.

**70. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kwamba licha ya jitihada hizo za kutafuta mikopo lakini bado tunatatizo la uendelevu wa miradi, kama tulivyo shauri ni muda mwafaka sasa PPP itakayohusisha BOT ndilo

litakalokuwa suluhisho la uendelevu wa miradi ya maji (kwa kilimo, matumizi ya nyumbani, mifugo na viwandani).

**11.0 UWEKEZAJI MDOGO NA USIOAMINIKA KATIKA MIUNDOMBINU KWA AJILI YA SEKTA NYINGINE ZINAZOTUMIA MAJI.**

**71.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ina kiwango cha juu kabisa cha uwezo wa kuhifadhi maji asilia Barani Afrika, lakini hakuna jithada za makusudi na makini za kuwekeza katika eneo hili bali tunabaki kutegemea kudra za Mwenyezi Mungu.

**72.** *Mheshimiwa Spika*, mbali na uwekezaji mdogo katika kilimo cha umwagililaji mahitaji ya maji kulingana na ongezeko na kupanuka kwa makazi ya watu yanazidi kuwa makubwa lakini rasilimali watu na fedha ni kidogo mno kukabiliana na mahitaji. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni vyema kuwekeza vya kutosha katika kuhakikisha miradi yote ambayo imeishaanza inamalizika kikamilifu na kwa wakati.

**12.0 KIWANGO KIDOGO CHA URATIBU WA KISEKTA NA UWEZO WA KITAASISI.**

**73.** *Mheshimiwa Spika*, Sekta hii bado inakabiliwa na tazito la uratibu duni wa mipango na maendeleo miongoni na baina ya sekta. Utengano huu unasababisha kushughulikia kwa mtazamo finyu maji kama suala la kisekta (yaani usambazaji wa huduma ya maji, usafi na utupaji wa maji taka) badala ya kushughulikia maji kama kipaumbele kikubwa na kugharimia maendeleo na usimamizi wake kama kitovu cha mafanikio kwa sekta kadhaa kuu za uchumi. Jambo hili ni muhimu katika kufanikisha nguzo za ukuaji wa uchumi za Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini Tanzania (MKUKUTA) kukuza kipato binafsi, ubora wa maisha, na utawala bora.

**13.0 MAPITIO YA BAJETI KWA MIRADI MAENDELEO YA MAJI KUANZIA 2015/16 HADII 2018/19**

**74.** *Mheshimiwa Spika*, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu 49 na Fungu 05

iliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilioni 565.9** au 565,862,426,195. Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **bilioni 512.5** au 512,235,736,000 kati ya fedha hizo shilingi **bilioni 27** au 26,966,326,000 ni fedha za matumizi ya kawaida (fedha hizi zinajumuisha mishahara shilingi **bilioni 18** au 17,960,716,000 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 9 au **9,005,610,000**). Na kiasi cha **shilingi bilioni 485.3** au 485,269,410,000 zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

75. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili 2019, Fungu 49 lilikuwa limepokea fedha za maendeleo **shilingi bilioni 137** au **136,900,281,752** tu **kati ya shilingi bilioni 485.3** au 485,269,410,000 zilitengwa ambazo ni sawa na asilimia 28 ya bajeti yote ya maendeleo.

76. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Fungu 49 likildhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 938.3** au **938,246,195,000**. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 913.8** au **913,836,029,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

77. **Mheshimiwa Spika**, lakini hadi mwaka huo wa 2016 / 17 unamalizika Wizara Fungu 49 ilipokea fedha za **maendeleo jumla ya shilingi bilioni 231** au 230,997,934,672. tu sawa na asilimia **25.7** ya bajeti yote ya maendeleo.

78. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18 fungu 49 liliidhinishiwa na Bunge fedha za maendeleoz jumla ya **shilingi bilioni 624** au 623,606,748,000. Lakini hadi mwezi Machi 2018 fedha za maendeleo zilitokuwa zimepokelewa ni **shilingi bilioni 135.2** au 135,191,256,566 tu, sawa na asilimia 22 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo kwa Wizara ya Maji-fungu 49.

79. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huu wa fedha 2018/ 19 Bunge linaombwa kuidhinisha fedha za miradi ya maendeleo yenye jumla ya **shilingi bilioni 673.2** au 673,214,033,677 kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 443.2** au 443,214,034,677.00 sawa na asilimia 66 zilikuwa ni fedha za

ndani na **shilingi bilioni 230** au 229,999,999,000.00 sawa na asilimia 34 zilikuwa ni fedha za nje.

**80.** **Mheshimiwa Spika**, hadi Mwezi February 2019 jumla ya shilingi **bilion 100.1** au 100,068,574,321.92 sawa na asilimia 15 ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 95.3** au 95,335,378,365.39 sawa na asilimia 22 ya fedha za ndani. Fedha za nje zilizotolewa ni **shilingi bilioni 4.7** au 4,733,195,956.53 tu sawa na asilimia 2.06 ya fedha za nje. Takwimu hizi zinaonesha kuwa fedha za maendeleo zinazotolewa zinakuwa zikipungua kila mwaka hii ni dhahiri kuwa maji sio kipaumbele kwa Serikali ya CCM.

**81.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2019/20 Wizara inaomba fedha za maendeleo jumla ya **shilingi bilioni 610.5** au 610,469,888,530.00 kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 349.45** au 349,449,000,000.00 ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 261.021** au 261,020,888,530 ni fedha za nje. Bajeti ya maendeleo ni pungufu kulinganisha na ile ya mwaka 2018/19 kwa **shilingi bilioni 62.7** au 62,744,145,147.00 sawa na asilimia 9.32.

**82.** **Mheshimiwa Spika**, ukiangalia miradi ambayo imekosa fedha na iliyopatiwa fedha ni dhahiri kwamba tunachokipanga na kukipitisha hapa Bungeni, kinakuwa sio kinachopatiwa fedha; mfano mradi wa maji toka Ziwa Viktoria kwenda Kahama-Shinyanga-Tabora ultengewa shilingi bilioni 1 lakini hadi mwezi Machi 2018 hakuna hata shilingi iliyokuwa imetolewa. Mradi wa Masasi-Nachingwea hakuna fedha yoyote iliyotolewa, Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda zilitengwa shilingi bilioni 10 lakini hakuna fedha iliyotolewa. Mradi wa kuboresha upatikanaji wa maji katika miji ya Same na Mwanga shilingi bilioni 12 lakini hadi Machi hakuna fedha iliyotolewa na Hazina. Mradi wa kupanua na kukarabati miradi ya maji vijiji ambayo inaendelea ya shilingi bilioni 20.7 hakuna fedha zilizotolewa hadi Machi, 2018 (Rejea Jedwali Na. 5 uk.14 hadi 16 wa Randama, Fungu 49).

**83. Mheshimiwa Spika**, ukiangalia Randama ya mwaka 2018/19 uk. 15,16 & 17 utaona miradi mikubwa ya kitaifa Mradi wa Maji Makao Makuu ya Mikoa Mipyä, Mradi wa Masasi Nachingwea, Mradi wa Ziwa Viktoria, Kahama/Shinyanga na Tabora, Huduma za Maji Jijii la Dar-es-Salaam, Mradi wa maji Bwawa la Kidunda, Mradi wa maji Mpera na Kimbiji yote hiyo haikupewa hata shilingi. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni utaratibu wa Serikali sasa kuomba Bunge lipitishe fedha lakini haitoi fedha kama zilivyoombwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi husika. Jambo hili linazidisha madeni kwa Serikali kwani mara nying fedha hizo zinakuwa ni za mikopo ya kibiashara ya ndani au ya nje.

**84. Mheshimiwa Spika**, hapa kuna miradi ambayo toka imeanza kuandikwa kwenye vitabu vya bajeti ni zaidi ya miaka 7 sasa na bado haloneshi kama inamalizika, kama mradi wa bwawa la kidunda na Mpera na Kimbiji. Madhara yake ni kwamba gharama zinazidi kuongezeka kila kukicha kutokana na ukweli kwamba thamani ya shilingi yetu dhidi ya Dola ya Kimarekani inazidi kuperomoka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni muda mwafaka sasa kwa Serikali kabla ya kuanzisha miradi mipya tumalize miradi iliyopo tayari, kinyume cha hapo ni kuendelea kupoteza fedha za walipa kodi. (Matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi).

**85. Mheshimiwa Spika, Mradi wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 6.66 Kuchelewa Ukamilishaji**, Tarehe 25 Mei 2015 MWAUWASA iliingia mkataba na Kampuni ya M/s Jassie & Company Limited wa Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Safi na Majitaka katika Mji wa Geita wenye thamani ya Shilingi bilioni 6.66. Mradi huu ulipangwa kuanza mwezi Juni 2015 na kumalizika ndani ya siku 360. Hata hivyo, hadi mwezi Novemba 2017, mradi ulikuwa haujakamilika na mkandarasi ameshaondoka eneo la kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa hizi ni fedha za walipa kodi na matumizi kama haya yanapofanyika wahuksika wanahamishwa toka eneo moja kwenda eneo lingine. Katibu Mkuu wa Wakurugenzi wa Wizara wapo ofisini wanazunguka kwenye viti vyao tu.

#### **14.0     HUDUMA YA MAJI TAKA**

**86.**     **Mheshimiwa Spika**, utoaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka mijini bado ni tatizo kubwa sana, hii ni kutokana na uwekezaji mdogo katika utoaji wa huduma hii. Takwimu zinaonesha kuwa ni miji 11 tu ndiyo yenye mifumo ya uondoaji wa maji taka, na ni asilimia 20 tu ya wakazi wa mijini ndio waliounganishwa na mtandao wa majitaka.

**87.**     **Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo tumekuwa tunashauri kwamba ni muda mwafaka haya maji taka yasafishwe na kuingizwa upya kwenye mfumo wa matumizi (recycling). Na tulitoa mfano wa Singapore kama nchi inayotumia vizuri rasilimali ya maji.

**88.**     **Mheshimiwa Spika**, zipo mamlaka zimeanza utaratibu huu japokuwa kwa kiwango kidogo sana kama MUWASA. Ni vema miradi yote mikubwa inayojengwa sasa kuzingatia hoja hii kwa lazima kabisa toka hatua ya usanifu. Ipo miradi mikubwa sana inayoendelea mfano mradi wa Arusha, Same, Monduli, Tabora, Songea n.k. ni vema Mheshimiwa Waziri akalieleza Bunge hili kama jambo hili limezingatiwa.

**89.**     **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanza kufikiria au kukaribisha wawekezaji wa kuweza **ku-recycle majitaka** ili hapo baadaye tuweze kuwa salama kwani viashiria vya upungufu wa maji viko wazi kabisa na jambo hilo halihitaji kubishaniwa au kufanyiwa tafiti.

**90.**     **Mheshimiwa Spika**, kuna watu wanajiaminisha kuwa tuna maziwa makubwa hapa kwetu na hivyo maji sio tatizo, lakini wafahamu kwamba uwekezaji wa kuyatoa maji hayo kwenye hayo maziwa na kuyaleta kwenye miji mingi na gharama ya kufunga mitambo ya kusafisha maji hayo ni vitu viwili ambavyo uwezi kulinganisha.

#### **15.0     UJENZI WA MAOFISI**

**91.**     **Mheshimiwa Spika**, ukiangalia Randama ya mwaka 2018/19 uk.51 kifungu cha 3.4.2.4 ukarabati na ujenzi wa

majengo ya Wizara. Hili kwa kweli linatusumbua kwani, ujenzi wa Maji House Dar es Dar es Salaam jengo lenye ghorofa 13 na pale pale kuna ujenzi wa Makao Makuu ya Wizara yatakuwa ni Dodoma. Jengo la Dar es Salaa, litakuwa ni kwa ajili ya watu gani? Hizi zote ni fedha ambazo zingetakiwa ziingie katika utoaji wa huduma. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa majengo bado ni mengi kwa watendaji kufanya kazi na sio jambo la haraka kiasi cha kupelekea miradi ya maji kukosa fedha za kumalizia miradi hiyo. Kwa muktadha huo ni vyema jengo hilo likauzwa kama zilivyouzwa nyumba za Serikali miaka hiyo, ili fedha ziingizwe kuhakikisha upatikanaji wa maji mijini na vijiji.

**92. Mheshimiwa Spika**, sasa hivi utendaji katika Serikali unaunganishwa katika Mtandao Mkuu wa Utumishi, na pia malipo yote kwa huduma zinazotolewa na Serikali zinakuwa kwenye mfumo wa e-payment uliopo Hazina au TRA. Kwa muktadha huo inakuwaje taasisi za kutoa huduma kwa wananchi zinaweza kutumia mamilioni ya shilingi kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi badala ya fedha hizo kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi? Mfano mzuri ni MWAUASA ambao wametumia takriban bilioni 1 kwa ujenzi wa Ofisi wakati wakazi wa Mji wa Mwanza wanapata shida ya maji, na wakati huo maji yamejaa Ziwa Viktoria. Rejea taarifa ya CAG 2016/17

#### **16.0 HITIMISHO**

**93. Mheshimiwa Spika**, maji ni muhimu kwa uhai wa binadamu na viumbe vingine na kwa hiyo, yanatakiwa kusimamiwa vizuri, pia maji ni hitaji muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na hiyo wananchi wanayo haki ya kupata maji safi na salama.

**94. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba magonjwa yatokanayo na maji machafu yanababisha vifo vingi kuliko vile vitokanavyo na vita na machafuko mengine ya kijamii duniani, kwa muktadha huo tutajikita katika uhifadhi endelevu wa vyanzo vya maji, na hili litafanyika kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

**95.** **Mheshimiwa Spika**, tutahakikisha ubia imara kati ya sekta ya umma na binafsi katika kuwekeza kwenye miradi ya maji kwa mfumo wa anzisha, endesha na hamisha umiliki (Build Operate and transfer). Mfumo huu utatoa hakikisho la upatikanaji wa maji ya kutosha kwa matumizi ya majumbani, viwandani, wakulima, wanyama wafugwao na wale wa porini.

**96.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Devotha Mathew Ninja (Mb)

Kny: **MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
WIZARA YA MAJI**

02 Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devatha Ninja, ahsante kwa kuwasilisha taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza moja kwa moja na mjadala wa jumla. Tutaanza na Mheshimiwa Balozi Adadi na baadaye Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kupata nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana na ni tatizo kubwa sana mpaka sasa hivi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya. Pia nawapongeza Mkurugenzi wa Tanga-UWASA pamoja na *engineer* wa Muheza, Eng. Bakari na Eng. Elikana ambao wanafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba maji kwenye Jimbo la Muheza yanapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, sisi Muheza tuna mradi, ukiacha mradi mkubwa lakini uko mradi ambao

unatoa maji kutoka Tanga (Pongwe) na kuyaleta Mjini Muheza ili kuondoa tatizo la maji Muheza. Mradi huu ulitegemewa umalizike tangu Mei 2018 lakini mpaka sasa hivi mradi huo bado unaendelea kujengwa na uko kwenye asilimia 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa inafanyika lakini mradi huu ambao tunautegemea ulikuwa kwenye *Quick-Wins* ili kupunguza tatizo pale Mjini Muheza. Sasa hivi kama nilivyo sema imebaki kitu kidogo sana ni asilimia 30 ili maji haya yaweze kutiririka pale Muheza ingawa haitakidhi sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo limebaki ni kufumua mabomba yaliyochakaa pale Mjini Muheza na kuweka mapya. Suala hili limesitishwa kidogo ili tusubiri mradi mkubwa wa maji wa kutoka India wa Dola milioni 500. Nimeongea na Waziri na nasisitiza sana kwamba waruhusu sasa hivi ili mabomba yale yaanze kufumuliwa kwa sababu tenki ambalo lilikuwa linachelewesha limekwishatengenezwa na limekaribia kumalizika. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu mmefika kule na mmeona kazi kubwa ambayo imefanyika ya kutoa tenki kubwa Pongwe na mabomba yameshalazwa. Nashukuru sana hivi karibuni mmetoa fedha kwa wakandarasi na sasa hivi mabomba ya chuma yanalazwa kupelekwa kwenye chanzo kikubwa cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi maji hayawezi kwenda kwa sababu bado hiyo sehemu ndogo ambayo imebaki ifumuliwe. Nimeona kwenye bajeti mmepanga karibu shilingi milioni 700, Mheshimiwa Waziri naomba uruhusu, wakati tunasubiri mradi mkubwa, mabomba ya Muheza Mjini yaanze kufumuliwa ili mkandarasi aanze kazi hiyo na maji yaanze kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nashukuru sana kwamba tumepewa fedha kwa ajili ya maji vijijini, karibu shilingi bilioni moja na zaidi. Ipo miradi mingi sana pale ambayo imebuniwa, kwa kweli nawashukuru sana ma-

engineer wa maji pale Muheza ambapo tumebuni na mmekwisharuhusu tutangaze zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi, kuangalia uwezekano wa kuanza kujenga Miradi ya Kwemdimu, Zaneti na Tongwe. Hii miradi ni maji ambayo yanachirizika kutoka milimani yaweze kusafishwa na kusambazwa kwa wananchi kule vijiji.

Kwa hiyo, nashukuru sana isipokuwa nashauri tupunguze urasimu wa kutoa vibali uliopo pale Wizarani. Baada ya kutangaza basi mruhusu moja kwa moja ili wapatikane wakandarasi na watie saini badala ya tena irudi Wizarani kuomba kibali kingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo nataka kuongelea ni mradi huu wa India wa Dola milioni 500. Najua Mheshimiwa Waziri unatupa taarifa, maendeleo yanavyokwenda kila mara lakini mradi huu ni muhilmu sana na una-cover miji karibu 29 hapa nchini. Mradi huu ukikamilika utapunguza sana tatizo la maji hapa nchini. Pamoja na kwamba suala hili lipo kwenye mchakato lakini unachukua muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Waziri aangalie uwezekano wa kuona huu mchakato utafupishwa namna gani, umekuwa ni mrefu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba uweke jitihada sana kwenye suala hili kwa sababu watu wengi tumeliongelea kwenye majukwa ya kisiasa kwamba mradi unakuja mpaka sasa hivi tunashindwa kueleza kwamba mradi unakuja namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni kama walivyosema Kamati kuhusu tozo ya maji ya shilingi 50. Suala hili limepigiwa kelele sana, miaka mitatu sasa na Kamati imependekeza hapa kwamba tozo ya shilingi 50 inatakiwa iongezwe ili ifikie shilingi 100. Hii ni kutokana na fedha ambazo zinapatikana kwa sababu fedha ambazo zinalipa wakandarasi sasa hivi inaonekana zote zimetoka kwenye Mfuko wa Maji wa Taifa. Mfuko huu umesaidia sana kuonekana kwamba Wizara haina fedha. Kutokana na Mfuko huu kuwa *ring fenced*, imesaidia sana kulipa malipo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini fedha hizi hazitoshi, wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri umetembelea miradi mbalimbali hapa nchini na umeona kabisa wakandarasi wengine wamesimama kutokana na kutokulipwa fedha. Kwa hiyo, ni vizuri kilio cha Wabunge ambacho wengi tangu miaka hiyo tumekuwa tunasema tuongeze shilingi 50 ili tozo hii ya mafuta iweze kuwa shilingi 100 ili iweze kusaidia kidogo kupunguza tatizo kubwa la maji. Naamini kabisa kwamba tutakapoongeza fedha hizo basi inaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa kuweza kufikia lengo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni Uanzishwaji wa Mamlaka ya Maji Vijiji. Wazo hili ni zuri sana na tunategemea linaweza likasaidia sana kupunguza tatizo la maji kwenye vijiji vyetu. Hata hivyo, ni vizuri tuangalie tumeipangia kiasi gani na tutapata wapi fedha za kuanzisha Mamlaka hii kwa ajili ya kutatua matatizo ya maji vijiji? Tumeanzisha *TARURA* lakini fedha ambazo zinakwenda *TARURA* ni ndogo sana. Kwa hiyo, ni vizuri sana kuangalia uwezekano wa kupeleka fedha ili Mamlaka hii itakapoanza basi ianze kwa bidii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Adadi. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Ally Keissy na Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare wajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii. Kwanza niishukuru sana Serikali, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu. Profesa Mbarawa nakuamini sana na nakuheshimu sana. Katibu Mkuu wa Wizara hii namheshimu sana na namwamini sana kwa sababu ya utendaji kazi wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitazungumzia Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria peke yake. Tarehe 5 Februari, 2016, niliuliza swali, lilikuwa linasema hivi: "Je, ni lini mradi wa ujenzi wa bomba la maji ya Ziwa Victoria kutoka Magu, Sumve, Malya utaanza?" Tarehe 5 hiyo, Serikali ikasema: "Kazi ya

upimaji pamoja na usanifu itakamilika Aprili, 2016 na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2016/2017 baada ya usanifu kukamilika". Kwa maana hiyo, usanifu umeshakamilika, mradi huu ulitakiwa uanze mwaka wa fedha 2016/2017. Cha kushangaza, kama nilivyosema, Profesa Mbarawa nakuheshimu sana, Katibu Mkuu, nakuheshimu sana na hasa tunaposimama sisi Wabunge wakongwe humu ndani na huwa hatupendi kusimama na kuanza kulaumu lakini hii inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi, kwenye kitabu chako hiki, ukurasa wa 155, umetenga shilingi milioni 200. Unasema, shilingi milioni 200 kwa ajili ya kujenga mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi Mji wa Malampaka, Sumve na Malya. Naijuliza, kwa mtu mwenye akili yake timamu kabisa, maji unayatoa Ziwa Victoria mpaka Malampaka kwa shillingi milioni 200? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha huwezi ukasema ni za usanifu ni za ujenzi. Sasa shilingi milioni 200 unajenga choo au unajenga mtandao wa mabomba kutoka Mwanza, Ihelele, Magu, Sumve, Malya, Malampaka kwa shilingi milioni 200? Mheshimiwa Waziri, *with due respect*, hebu tuangalie sasa mambo haya mengine jamani haya, hivi hawa wataalam wetu hawa wanatusaidia au hawatusaidii? Unatenga shilingi milioni 200, usanifu umeshakamilika, *no doubts*, sasa hizi shilingi milioni 200 Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa, Katibu Mkuu, Dkt. Mkumbo ni za nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, niombe sana kwa kweli mliangalie suala hili. Hata kama ungekuwa ni wewe leo, Waziri na Waziri mwingine tu, kwa hali kama hii, hivi unaweza ukasimama ukasema naunga mkono hoja, naunga mkono bajeti, kwa milioni 200 zinakwenda kufanya nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wataalamu wako mradi huu ni wa siku nyingi muuangalie. Ukitazama miradi mingine iliyoanza na imekamilika, huu ukaachwa, Maswa, Itilima, Bariadi, Busega

imeshakamilika na Magu uko njiani kwenda kukamilika. Huu sasa mmeweka kama kisiwa, Jimbo la Sumve na Malampaka, tumewakosea nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ahadi hii siyo ya leo. Alikuja Rais wa Awamu ya Nne, pale Ngudu, Waziri Mheshimiwa Maghembe alikuwepo na akaambiwa kwamba mradi huu tunataka ukamilike mwaka 2015 lakini haukukamilika. Akaja Waziri Mheshimiwa Lwenge, mradi haukukamilika, akaja Mheshimiwa Kamwelwe na nimekaa naye na nimekwenda mpaka ofisini kwake anasema mradi huu utaanzia Fela - Sumve - Malya - Malampaka, kwenye kitabu hiki mnakuja kutenga shilingi milioni 200!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, hivi mnataka Mbunge kama mimi mzoefu humu ndani nisimame na kupiga kelele kila siku humu ndani? Hata ile heshima tu, Mheshimiwa Mbarawa nakuheshimu sana lakini tutazame basi suala hili. Ni bora kabisa msingetenga hata senti tano, ndiyo maana nauliza hizi shilingi milioni 200 mmezitenga ni kwa ajili ya nini? Kwa sababu siyo za usanifu maana ulishakamilika siku nydingi na maeneo ya kuweka matenki yameshaainishwa, wataalamu wenu wamekwenda kule wakasema tenki litakaa hapa na mtirikio utakuwa hivi, mradi huu utapitiwa na vijiji zaidi ya 40 mpaka Malampaka, kazi imeshafanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake aje na majibu ya mradi huu. Kwa sababu majibu haya ambayo anasema kazi ya upimaji tayari, ujenzi wa mradi utatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2016/2017, haya ni majibu ya Serikali, lingekuwa ni swalil la nyongeza ingekuwa suala lingine. Swalil la nyongeza unaweza ukalibabaisha lakini jibu hili ninyi wenywewe mmeandika kwa maana ya kwamba utafiti mmeshafanya na majibu ya wataalam mmeshaletewa na ndiyo maana mkasema mradi huu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo siyo majibu yangu, ni majibu ya Serikali. Majibu haya pia yalitolewa humu Bungeni.

Wananchi wote wa Jimbo la Sumve, Wilaya ya Kwimba na Malampaka waliskia majibu haya ya Serikali na wakashangilia, leo ni miaka minne mradi hata kuanza bado leo tunakuja kutenga shilingi milioni 200! Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, tafadhalii sana, wataalamu tafadhalini sana, mradi huu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano lakinii na ahadi ya Mawaziri humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana, utakapokuja kusimama kuhitimisha Mheshimiwa Waziri, uniambie mradi huu utakamilika lini. Pamoja na kazi nzuri sana unayofanya, basi mradi huu nao uingizwe kwa mwaka huu. Donyoadonyoa kila sehemu mnakoweza ili upate angalau shilingi bilioni 2 au 2.5 ili mradi huu uanze kwa mwaka huu wa fedha. Kwa sababu haiwezekani nitakapotoka hapa nakwenda kule jlimboni, tumeshawaambia siku nyingi mradi huu unaanza, nikienda kule nawaambia nini hawa wananchi wa Jimbo la Sumve? Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Profesa Mbarawa nawaambia nini kwamba huu mradi ni kiini macho, mbona hautekelezwi, leo tunatenga shilingi milioni 200?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuwa upande mwingine huko labda ningesema lakini niiombe sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali yangu sikuvi, kama nilivyosema kwamba nawaheshimu sana Mawaziri na wataalamu, mradi huu naomba upangiwe utaratibu wa kuanza kwenye mwaka huu wa fedha 2019/2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, lakinii niseme kwa sababu nawaamini, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndassa, tunaendelea na Mheshimiwa Ally Keissy baadaye Mheshimiwa Rwakatare ajiandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa naunga mkono hoja Wizara

ya Maji hii, kwa kuwa Mheshimiwa Prof. Mbarawa, Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu, Naibu Katibu wanafanya kazi ambayo sikutegemea. Mheshimiwa Prof. Mbarawa anafanya kazi kama vile Mhandisi anapita mpaka anachimba mifereji yeye mwenyewe kwa mkono wake, sijaona Waziri anafanya kazi kama Prosefa kwa vitendo. Lakini tatizo wanaomuangusha ni wafanyakazi wake, watendaji wake, namwambia ukweli awe mkali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua mfano Namanyere, nimezungumza sana kuhusu Namanyere mpaka sasa Namanyere wamepata maji asilimia 15, hata huo mradi uliokuja Mheshimiwa Profesa Mbarawa huo mradi wa sasa Namanyere wapata asilimia 46 katika Mji wa Namanyere ambayo siyo kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kawaida mijini lazima wapate maji asilimia 86 mpaka 85, lakini pamoja na huo mradi mpya Namanyere wamepewa Mkandarasi watapa maji asilimia 46. Kwenye kitabu chako hiki ukurasa 146, umeandika imetengwa shilingi milioni 300 kwa ajili ya kupeleka umeme kwa ajili ya mradi wa Bwawa la Mfili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme umeshafika na transfoma ipo angalia wasikupige changa la macho pae tulipohitaji ni mtambo wa umeme mashine, *pump* ya umeme kwenye Bwawa la Mfili.

Nakuomba vilevile Mheshimiwa Waziri Mkandarasi aliyepewa bwawa la Mfili na mtaalam anayeshiriki kumpa lile Bwawa la Mfili kawatapishe pesa mara moja. Haiwezekani ile bwawa thamani yake ifike milioni 900, wakati ukipiga hesabu za haraka haraka lile bwawa haifiki hata milioni 300, haiwezekani lazima ufanye jitihada kwa uwezo wako ninavyokuamini lazima mkandarasi apanue lile bwawa au atapike zile hela moja, hamna kuonea huruma! Wamezidi kuchakachua kwenye mabwawa haya mabwawa ya maji wamezidi nchi nzima nilikuambia unda tume ufuatilie mabwawa ya nchi nzima kuna uchafuaji wa hali ya juu, miradi

ya maji wageuza kama ndiyo vichaka vyakubia pesa katika nchi hii haiwezekani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza Bunge la Awamu ya Nne hapa wanaandika kabisa Ofisini wamekaa Ofisini anaandika neno kodisha gari kutoka Namanyere kwenda Dar es Salam kwa shilingi milioni 14 wakati gari milioni tatu, nimepakia mabomba ya shilingi milioni 98, Mheshimiwa nilidai, hakuna mabomba waliyopakia wala hakuna gari iliyokuja Namanyere. Anakaa Ofisini anakula hela kijanja kijanja, wafuatilie wote, Wakandarasi wameshirikiana na Maofisa wako kuiba hela za miradi ya maji, unda tume, kagua mradi kwa mradi ninavyokuamini upitie nchi nzima watapike pesa mara moja. Hakuna huruma kuwachekeea chekeea, wengine wamejenga maghorofa, wengine wamenunua majumba kwa ajili ya miradi ya maji katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ninao, maana yake walitaka kunihonga na mimi nikawakatalia, shahidi na Mbunge wa Chembu Ndugu Nkamia walikuja mpaka Bungeni hapa, nikawaambia mimi sihongeki wananchi wangu wamejipanga foleni kunichagua niwatetee, leo Namanyere hawana maji, mnipe pesa wananchi waangamie, kupata maji kwa ajili ya utamaa tamaa, wako kwa majina, hakuna kufichika, Mradi wa Maji Kirando kabla hujakuwa Waziri walikula shilingi milioni 201 Kirando hakuna kitu kilichotengenezwa. Walijenga vizimba 18 na wakanunua *pump* moja kwa shilingi milioni 200 waliandika *certificate* za uongo hela wanachukua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimwambia Waziri aliyeondoka mbele ya bwawa na RASambaye leo ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, anafahamu alikuwa RAS Sumbawanga; tukamwambia usiwalipe hawa pesa iliyobaki shilingi milioni 300 kwa sababu hili Bwawa la Mfili lazima likaguliwe, lakini walilipwa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huyo Mkandarasi kama yupo hajafa atapike zile hela, akapanue Bwawa la Mfili... (*Makofii*)

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipe taarifa..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakajoka taarifa.

## TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namsikia nataka kumpa taarifa Mhehsimiwa Mjomba wangu Keissy pale, anasema kwamba fedha zote hizo anazozitaja zimeliwa na wakandarasi, zimeliwa na watu ambaao ni watendaji wa Serikali kwenye Jimbo lake la Nkasi. Lakini namshangaa sana kwa sababu mimi najua kabisa Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana ya kumaliza mafisadi nchini, sasa hizo hela wanakulaje wakati mafisadi tumeshawamaliza kabisa katika nchi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mjomba wangu amekwenda vibaya, hivi mafisadi wamekwisha, juzi walitaka kuiba hata za ndege hapa juzi, wewe huna habari, kupaka rangi ya ndege tukasema shilingi milioni 300 wamekwisha mafisadi! Hata humu Bungeni wako mafisadi watakwsa wapi mafisadi. Mafisadi watakwsa labda mwisho wa dunia ndiyo wataisha mafisadi, nani kakuambia, mjomba uwe macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji kadhaa katika Jimbo la Nkasi Kaskazini ukianzia Masoro, Kata nzima ya Mkwamba kule Riele, Itindi, Tambaruka, Swaila hawana hata visima vya maji, Kakoma, Lunyalahakuna hata visima wananchi wanahangaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakuomba ndugu yangu hata angalau kisima kimoja kimoja katika vijiji vyangu hawana kabisa maji; maji ni uhai nakuelewa kwa sababu

unatenda kazi, unafanya kazi, unakemea uovu, nimekuona kwa macho yangu sasa jitahidi kuwabana kabisa fukua makaburi, wameiba miaka ya nyuma mjomba wangu, labda kwako Tunduma kama hawajaiba, wameiba sana hawa watu wa maji bila kuwaonea huruma wameiba sana; walikuwa wanapeana kijomba kijomba *tender* kama ufahamu wewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapewa *tender* ana-*raise certificate* kazi haifanyaki hamna kazi, Namanyere kwa ushahidi kabisa wewe uliona wapi mjomba kazi itoke gari Dar es Salam mpaka Namanyere unapajua Namanyere, gari fuso shilingi milioni 12 uliona wapi wewe! Ni kwenda Lubumbashi na kurudi! Nilidai risiti ya hiyo gari haikuonekana kwa nini tusifukue makaburi mnaogopa kitu gani? Ushahidi upo, mabomba sikuona nimekwenda kwenye *Full Council* nadai mimi risiti kwa yule mtu wa maji haoneshi. Gari liko wapi, nioshe gari, nipe namba ya gari haoneshi, nikaenda TAKUKURU hamna kitu jamani, tufanyaje nchi hii, tumsaidie Rais.

Mheshimiwa Profesa Mbarawa ninakuamini unda tume pitia mabwawa yote nchi nzima, miradi ya maji nchi nzima utakuta ufisadi wa hali ya juu. Tunashida ya maji kweli Serikali inaleta pesa, lakini wapi hakuna chochote, hakuna chochote, mfano najua Namanyere, uende Namanyere wewe mwenyewe unafahamu Mheshimiwa Waziri, juzi uliunda tume, wakaja Namanyere mpaka Kirando ulikuwa mradi wa shilingi bilioni 7.4 baada ya kuleta wakandarasi wapya na watu wa tume, mradi umegundulika bilioni 4.6 wewe mwenyewe shahidi. Kabla hujakuwa Waziri ule mradi ulikuwa umeshaibiwa hela, ulikuwa umeshaibiwa shilingi bilioni 7.4, ulipokuja Waziri ukataa nikakushawishi wewe ukakataa ukasema huu mradi haiwezekani tutume watu wa kwenda kule. Tumegundua ule mradi ni shilingi bilioni 4.6 tumeokoa shilingi bilioni tatu, Mheshimiwa sasa tutasema namna gani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawambia Waziri yuko Waziri mmoja nikimtaja itakuwa aibu, akanambia utajuaje

haya mambo Mheshimiwa Keissy, nikamwambia nitakushtaki kwa Mheshimiwa Rais wewe nyamaza kimya, akanyamaza kimya, naweza kumtaja. (*Makof*)

**WABUNGE FULANI:** Mtajeee!.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Anajijua, alinitisha humu Bungeni, Waziri mmoja alinitisha Bungeni wewe usiingilie mambo ya utaalamu, unajuaje utaalamu nikamwambia mzee hata kipofu atajua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Prof. Mbarawa nakuamini, unda tume pita kila kijiji, pita kila mkoa siyo kama Waziri wengine unamletea taarifa anakwambia unajuaje, kwani mimi ni sanamu nisikose kujua, nikose kujua mimi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumtishia nitakupeleka kwa Mheshimiwa Rais akatetemeka, unakuwa Waziri tukikwambia wewe unasema Mbunge utajuaje unashirikiana na mafisadi haifai kuwa hata Waziri wewe, bora utumbuliwe tu. (*Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Mtajeee!

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, huku nyuma. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## TAARIFA

**MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Keissy angetutajua tu na sisi tumjui bwana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Keissy naomba uendeleee.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea tutamtaja hata Mheshimiwa Rais akiniita faragha nitamtaja, si anasikia Mheshimiwa Rais nitamtaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu hii miradi ya maji tumsifu Mheshimiwa Prof. Mbarawa maana yake anafanya kazi kwa vitendo, Mheshimiwa Aweso anafanya kazi kwa vitendo na wasaidizi wake wanafanya kazi kwa vitendo, naomba muendelee na msikubali makadirio wanawaleta ya uongo uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashauri angalia *certificate* wanazoleta lazima mzipitie, siyo wanaandika *certificate* mnazipitia haraka haraka mnalipa hela, wakati mwininge ni hewa, ni unafiki ulikwenda Mheshimiwa Waziri ulikuja kule Mradi wa Kata ya Isale tangu umeondoka mpaka leo kama siyo ....*DC, DC* ndiyo amekuwa kama mkandarasi wa Nkasi anahamasisha wananchi wachimbe mtaro ili walipe yule mkandarasi, ye ye hafanyi kazi yoyote, angalieni *certificate* hizi na nimeshukuru kwa sasa nasikia sheria imebadilika mkimpa mtu mkandarasi kwanza afanye asilimia 30 ya kazi ndio alipwe pesa, hiyo ndiyo sheria nzuri, sio mnaanza kumlipa hela mkandarasi ajaanza chochote hayuko kwenye *site* anakula pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nikuombe Mheshimiwa Waziri nakuambia ukweli Mradi wa Maji Kirando alikula makandarasi shilingi millioni 201 lazima azitapike, amejenga tu vizimba 18 na kila kizimba kimetumia mifuko mitano ya *cement* na aliyekula hela za mradi wa Bwawa la Mfili lazima atapike huyo mkandarasi lazima maana yake ye ye ndio aliyemshawishi yule mtu akaandika pesa kama waligawana sisi hatujui nataka kujua kazi yetu ya Namanyere, wana Namanyere wana shida ya maji hawapati maji chini ya asilimia 16 mzee, ahsante naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Keissy tunaendelea na Mheshimiwa Rwakatare baadaye Mheshimiwa Joseph Mhagama ajiandae.

**MHE. DKT. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, awali ya yote ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema ye ye ambaye ametupa zawadi ya uhai,

ametupa zawadi ya afya, ametupa zawadi ya maji, ametupa zawadi ya ulinzi, na hakika tunasafiri na kurudi kwa sababu ya ulinzi wake. Mungu wetu ni mwema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tena kuchukua nafasi hii niweze kumuweka kila mmoja wetu hapa mikononi mwa Mungu aweze kuwatetea nakuwalinda kwenye Majimbo yenu kazi zenu ziweze kwenda salama.

**WABUNGE FULANI:** Ameen!

**MHE. DKT. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE:** Lakini zaidi ya yote tuombe maombi rasmi kwa ajili ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, hakika kabisa tumepata chuma, tumepata jembe, lakini tumepata baba yeye hakika ana upendo, ana huruma, anafanya kila kitu ili mradi kuhakikisha Watanzania tukoa sawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba apate kibali kwa watu wote wanaume, wanawake jina lake liwe sukari midomoni mwa watu, jina lake liwe chumvi na ulinzi wa Mungu uwe juu yake kwa jina la Yesu. (*Makof!*)

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**MHE. DKT. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua pia nafasi hii niweze kumkumbuka Mheshimiwa Dkt. Reginald Mengi mfanyakia shara mashughuli pia tukikumbuka katika bajeti yetu ya maji yeye ndio aliyeanzisha maji ya chupa Kilimanjaro, yeye ameanzisha ITV mambo mengi tu amefanya, ana huruma anakula na watu wenye shida, watu walemovu, kwa hivyo amefanya kazi nzuri Mungu aiweke roho yake mahali peponi.

**WABUNGE FULANI:** Ameen!

**MHE. DKT. MCH. GETRUDE P. RWAKATARE:** Tunaomba pia kwa ajili ya faraja katika familia yake, tunaomba kuwe siku zote na amani Mungu atende na hakika msiba huu uishe salama kwa Utukufu wa Bwana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwisha kusema hayo ningependa niweze kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mbarawa kwa ajili ya kazi nzuri na timu yako mnayoifanya katika Wizara hii ya Maji. Kwa kweli tunaona mabadiliko makubwa na pia tunaona kwamba mko wasikivu katika mambo ambayo tunawashauri mnafanya na tunaona kwa kweli hata kule kwetu Kilombero kuna mabadiliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijikite kwenye maji safi na salama hakika kabisa mnajua maji ni kila kitu na lengo letu ni kumtua mwanamke ndoo ili aweze kupumzika maji yafike nyumbani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano natoka Mkoa wa Morogoro kuna Mito 177 hiyo mito ni ya kudumu sio ile mito ya kukauka, pia katika Wilaya ya Kilombero ambako natoka pia kuna mito 38 ya kudumu na sio mito ile ya kukauka, tukijumlisha tuna mito mingi. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba watu wengi hawajafikiwa maji safi na salama inabidi wakachote mtoni, inabidi wakatafute ni shida. Lakini nilikuwa naomba katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri tunaomba utuhurumia watu wa Kilombero ya kwamba uweze kuangalia kwa maana maji yapo Mungu ametupa neema tatizo kubwa ni miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ni mibovu ni mizee ya siku nyngi na vilevile watu wengi wameongezeka zamani Kilombero tulikuwa watu 300,000 siku hizi tunakaribia milioni moja kwa sababu watu wengi wanahamia kwa ajili ya kilimo na kwa ajili ya kufuata maji. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri iangalie Kilombero kwa hali ya huruma kabisa tumevumilia miaka mingi. Nakumbuka ya kwamba miundombinu ile ilikuwa kama Ifakara Mjini ilikuwa ni ya watu 7000 enzi hizo sasa hivi wako watu wengi zaidi ya 300,000 yaani Mji wa Ifakara peke yake. Kwa hivi tunaomba kwa kweli mtusaidie ili na sisi tuweze kupata maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumependa pia kumpongeza Waziri ya kwamba hakika kwa utendaji wake

bora na timu yake tumeona ya kwamba sasa hivi kipindupindu ni kama kinatokomea vile kwa maana kwa kweli hatusikii tena magonjwa ya kipindupindu na hiyo ni kwa sababu maji yapo watu wanapata maji ya kutosha, watu wanapata maji na ndio maana unakuta magonjwa yale nyemelezi ya siku nyingi sasa hivi yamepungua. Kwa hivi tunasema ahsante kwa kazi nzuri mnayoifanya muendelee mbele ila zingatia Kilombero iipe kipaumbele cha peke yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tena nichukue nafasi hii nikiangalia kwamba sisi tunasema Kilombero ni ghalia chakula au Morogoro ni ghalia chakula lakini pamoja na kwamba Mungu ametubariki na mito 177 kimkoa, mito 38 Kilombero lakini ulimaji wa kilimo cha umwagiliaji ni percent 2.7 tu, maji yapo tatizo lile lile ni miundombinu mtusaidie kwa sababu sisi hatuna shida kama mmeweza kuchota maji kutoka kwenye maziwa mkawapelekea watu ni rahisi zaidi kama watu wana mito kila kitu kipo ni miundombinu tu kuwapelekea watu. Tena hii inakuwa ni kama ulinzi wa vyanzo vya maji kwa sababu kama watu watapata maji ya kutosha wana haja gani kuharibu vyanzo vya maji wale ndio wanakuwa walinzi wetu. Kwa hivyo tujitahidi kutoa maji ya kutosha ili watu wale wasiwe waharibifu wa vyanzo vya maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu nilikuwa napongeza Serikali kwa ajili ya mradi mkubwa wa *Stigler's Gorge* kwa kweli ni mradi mzuri hakika kabisa utatupa umeme wa kutosha na hata ziada lakini ninavyoona kwa uharibifu wa bonde la Kilombero itakuwa ni ngumu ule mradi kuweza kwenda smoothly kwa sababu watu wengi wamevamia vyanzo vya maji. Kwa hivi dawa ni ile ile tufanye juu chini kwa uwezo wote kama ikiwezekana tukisambaza maji kila mahari watu waweze kupata maji ya kutosha kwa matumizi yao, kwa matumizi labda ya wanyama wao hakika tutaweza kuufanya ule mradi wa *Stigler's Gorge* uweze kumalizika vizuri na hakika utakuwa Baraka kwa Tanzania nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ningependa pia kuwapongeza kwa ajili ya sehemu ambazo hazina maji naona mnasaidia kuweka visima lakini taitizo kubwa ni uangalizi *management* ndio inapungua kwa hivi tunaomba muimarishe kwenye upande wa *management* kwa sababu watu wengi wanakuwa wanaharibu ile miundombinu kwa hivi mwisho unakuta maji hayawafikii watu sawasawa kwa sababu wengine wanachukua njiani, wengine wanafanya hivi tuangalie pia *management* yetu katika wizara yetu ili hakika maji tunayowapelekea watu yawafikie na yaliwafikia ni ulinzi na kama ulinzi pia na hapo tunaweza kuwa tuna *save* pesa badala ya kupoteza pesa. Kwa maneno haya machache ningependa kuunga mkono hoja mia kwa mia na Mungu awabariki. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Rwakatare Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Mhagama baadaye Mheshimiwa Joseph Selasini ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu sana Wizara ya Maji, na nianze kwa kumshukuru sana kuishukuru sana Serikali hususani Mheshimiwa Prof. Mbarawa Makame pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa ushirikiano mkubwa sana ambao mmetupa wana Madaba kuhakikisha miradi yetu ya maji inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Mheshimiwa Jumaa Aweso mmekuja wenyewe mmetembelea miradi mbalimbali ya maji Madaba, mmeshirikiana na wananchi wa Lilondo kuhakikisha kwamba miradi yao ya jamii kuititia vikundi inafanikiwa kwa kuchangia pesa ninyi wenyewe, pia kwa kuwatia moyo ninawashukuruni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru miradi mingine ambayo inaendelea iliyokamilika Madaba ya maji na hii ambayo imetengewa bajeti ya zaidi ya bilioni moja kwa ajili

ya kuendelea kuitekeleza. Siku ya leo nilitamani sana nitume muda mrefu kuishauri Serikali juu ya mambo kadhaa ambayo ninadhani kama hayatachukuliwa umaanani Wizara hii itawaangusha watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza naomba tulijue kwamba kama vitu ambavyo vinambeba Mheshimiwa Rais ni uzalendo wake na upendo wake kwa watanzania. Amejitoa kwa hali na mali kufa na kupona Watanzania wapate unafuu katika Nyanja zote, amekusudia kwa kufa, kupona kuhakikisha wakina Mama tunawatua ndoo vichwani ili kuhakikisha hawapati tena usumbu wa maji. Lakini Watumishi ndani ya Wizara ya Maji ni mzigo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kusema na hili limesemwa na Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwenye ukurasa wa 108 wa hotuba yake. Amesema: "moja katika changamoto katika Wizara hii ni uwezo mdogo katika utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji" na kama ningepata fursa ya kurekebisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ningeandika kama ifuatavyo: "Dhamira ndogo ya Watumishi katika idara inayohusiana na masuala ya maji kutekeleza na kusimamia miradi vizuri". (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa nyingi zimetengwa kwenda kwenye miradi, sisi Madaba pia tumetengewa na Mheshimiwa Waziri anahangaika sana kuhakikisha tunafanikiwa, lakini *procedure* ndogo tu ya kupata vibali vyta kutekeleza miradi iliyotengewa fedha inachukua karne nzima. Mwaka mzima Mtumishi wa Madaba anaandika barua Wizarani, anasubiri majibu ya kibali cha kutekeleza mradi. Mradi umetengewa fedha, tupo ndani ya bajeti, mradi hauchukuliwi umaanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Waziri, watu kama hawa awaondoe, wanamchafua, wanaichafua Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Inawezekanaje wewe umeandikiwa barua Mwezi wa nane, Mtumishi umeipokea kutoka kwa mtaalam mwenzako, hata ku-*acknowledge* kwamba umeipata hiyo

barua na hata baada ya kukumbushwa, inakaa miezi sita, saba mpaka Mbunge anakwenda kwa Waziri, Waziri anaafuatlia ile barua, tutafika kweli na Awamu hii ya Tano? Inasikitisha sana kuona kasi ya Mheshimiwa Rais, kasi ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Naibu Waziri wake inaangushwa na watu wadogo, watu walio katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumebadilika sana, Watanzania tumeakisi falsafa, tumeiishi falsafa ya Mheshimiwa Rais ya "hapa kazi tu", wananchi wanahangaika kila siku, wanapambana kuhakikisha kwamba tunaitekeleza lakini bado baadhi ya watumishi wa umma wanaishi maisha yale yale ya *business as usual*. Yamesemwa haya na Mheshimiwa Adadi humu humu ndani, yamesemwa na Mheshimiwa *senator* hapa, yamesemwa na Mheshimiwa Keissy na mimi nayasema na naamini Wabunge wengine watayasema, wanaotuangusha naomba Mheshimiwa Waziri wa Maji akafanye nao kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto ya *certificate*, siyo Madaba peke yake, sehemu nydingi tunalalamika sana, Wakandarasi wametekeleza wajibu wao, walipwe ili kazi ziende, lakini nalo hilo linamhitaji Mbunge aende mguu kwa mguu mpaka Wizarani, hawa watumishi wana kazi gani?. Hili kwa kweli limenisikitisha na nimeungana na Wabunge wenzangu kulisema na naamini Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo sisi tunamwamini na tunamtegemea, atakapopitisha Bajeti yake ambayo tutaiunga mkono, aende akasafishe huko chini wanatuangusha sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na michakato hii, vijiji saba vya Wilaya ya Madaba vimeendelea na utaratibu wa usanifu wa mradi. Mradi wa Vijiji Saba unakwenda kunufaisha wananchi 25,000. Mradi huu ngazi ya Halmashauri walishamaliza usanifu wa awali kabisa na wameomba kwa Mheshimiwa Waziri na amewakubalia, amewapa kibali lakini wameomba pia kwake kibali alichowapa ni kwa ajili ya kuweka maji ya muda

mfupi kwa kutumia visima virefu. Tunamshukuru na tunaamini utaanza kutekelezwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo walilonalo ni kwamba wanashindwa kufanya usanifu wa kina kwa sababu zaidi ya miezi sita sasa wanasubiri majibu ya Wizara, waletewe wataalam kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina na pengine hili lingekuwa limeshafanyika leo tungeweza kuisoma Bajeti ya eneo hilo. Mheshimiwa Waziri tunamwomba sana, tunamwamini, tunamtegemea na tunaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhagama. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Selasini, baadaye Mheshimiwa Sonia Magogo ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi na kabla sijaanza kuchangia hoja hii, naomba nichukue nafasi kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani niweze kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Reginald Abraham Mengi, Wafanyakazi wote wa Makampuni ya IPP, Wanahabari wote Nchini na Afrika Mashairiki, Jumuiya ya Wafanyakabiashara wa Tanzania, Watanzania wote na wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kifo hiki cha ghafla cha ndugu Mengi ambaye alikuwa mtu mkarimu, alisaidia Watanzania wengi, aliajiri wengi, alikuwa Baba mwenye huruma kwa watu wote hasa walemovu na aliwasaidia Watanzania kuwajengea ari ya kujitegemea. Tutakumbuka kitabu chake kile cha "*I can, I will, I must*" kimewasaidia Watanzania wengi sana kuwa na *courage* na moyo wa kufanya biashara. Kwa hiyo huu ni msiba mkubwa unatusikitisha wote, naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, niseme tu kwamba Wizara hii ni Wizara nyeti, ni Wizara ambayo inategemewa na Watanzania lakini inategemewa na sekta zote hapa nchini; inategemewa na Kilimo, Afya, Viwanda

na kila kitu. Kwa hiyo ni Wizara ambayo inahitaji ushauri mzuri na inahitaji msaada wa kutosha kwa kweli badala ya kulaumu tu. Kabla sijatoa ushauri, niseme tu kwamba Jimbo langu ya Rombo lina shida kubwa sana ya maji na utashangaa Rombo ndiko ambako Mlima Kilimanjaro upo. Zamani kulikuwa na mito mingi ikitoka pale mlimani na kugawa maji katika maeneo mengi ya Mkoa wa Kilimanjaro, lakini sasa nadhani Rombo ni Wilaya inayoongoza kwa uhaba wa maji pale mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niseme tu kwamba naishukuru Wizara, tuna mradi pale katika Vijiji vya Shimbi Mashariki, Ngareni na Ngoyoni ambavyo kwa jumla tulikuwa tunahitaji bilioni 1.33 ili kukamilisha ile miradi lakini Wizara imeshatupatia shilingi milioni 717.7 na sasa hivi tunaomba Wizara itukamilishie shilingi milioni 617 ili miradi hii ambayo ni ya siku nyingi lanze kufanya kazi. Ni matumaini yangu kwamba Wizara itatekeleza kwa sababu niliongea na Naibu Waziri, nimeongea na Katibu Mkuu kwa kweli ni watu ambao ni wasikivu, wanapenda kushirikiana, kwa hiyo nadhani kwamba hili lilatekelezwa, naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ni vyema Serikali pamoja hata na wananchi wangu wa Rombo kufahamu kwamba changamoto ya maji Rombo ukubwa wake unatokana na kwamba hakujawahi kuwa na uwekezaji mkubwa wa maji katika Wilaya ya Rombo kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita. Kwa hivyo miundombinu na vyanzo vya maji vilivyopo kwa miaka 20 iliyopita havijawahi kuboreshwa. Hata hivyo, kwa sasa ninayo furaha kwamba Serikali imeridhia kuboresha huduma hiyo ya maji kwa vijiji 41 vya ukanda wa chini ambavyo ndiyo nina shida kubwa sana ya maji. Kuna usanifu umeshafanyika kutoka chanzo cha maji cha Ziwa Chala ambacho chanzo kile kilikuwa kidogo Wakenya wanasumbuasumbua lakini sasa hivi wameshakubali na Serikali imeshaanza usanifu, kwa hiyo nawaomba Warombo wenzangu wawe watulivu, kazi hiyo inafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna chanzo kingine cha Mto Njoro kule Tarakea vilevile Wizara kwa kutumia wataalam

wake na wataalam wa kule Halmashauri wameshaanza uwezekano wa kupata maji katika chanzo kile na chanzo kingine cha Kinyasini, Mto Uwashi na Mbushi vyote hivyo katika Mwaka huu wa Fedha huenda kazi ikafanyika na nimeongea na Katibu Mkuu kwamba tayari fedha ambazo zimeshatengwa bilioni 10 huenda zikapatikana kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, tulishasema mara nyingi hapa Bungeni kwamba tunayo shida kubwa sana na Jumuiya ya maji inayosambaza maji kule Rombo. Hii Jumuiya inaitwa *Kiliwater*. Utashangaa mwezi uliopita, mimi binafsi nimepokea bili ya maji Sh.58,000 na kule nyumbani nimeacha watu wawili tu ndiyo wanaotumia maji, lakini imeingia bili ya Sh.58,000. Nimejaribu kulalamika wakaniambia iko sawasawa, haya ndiyo malalamiko ya wananchi kwamba hata maji kidogo yaliyopo yanagawanywa vibaya na wale wanaotaka wafungiwe maji, hawafungiwi kwa sababu ambazo wala henzieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwanzo wakati Mzee Lwenge akiwa Waziri tulilalamika na tukaomba kwa sababu Halmashauri iliweka azimio kwamba tuombe tuanzishiwe Mamlaka ya Maji katika Halmashauri ya Rombo baada ya kuindoa hii Halmashauri na ombi hili lilikubalika sasa kama litatekelezwa au kama tutaanzisha ile Mamlaka ya Maji ile ya Kitaifa ambayo itasimamia maji kwa ujumla, lakini kwa wakati huu wa mpito ile Jumuiya inayogawa maji pale, ifanywe mikakati ya kuiangalia ili isiendelee kuumiza wananchi, wakifanya hivyo watakuwa wamewasaidia sana watu wa Rombo .

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo lingine ambalo nataka kusema, suala la maji ni kubwa na kama tusipokuwa makini suala hili linaweza likaja kusababisha hata vita ya tatu ya dunia kwa sababu vyanzo vingi vya maji vinakauka nchini na hata duniani kwa ujumla. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali; kwanza tufanye mkakati wa kuanzisha mabwawa maalum ya kuhifadhi haya maji ya mvua ambayo yanapotea hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukivuna haya maji ya mvua yanaweza kutusaidia. Nilisema tena katika mchango wangu mwaka uliopita; ukiangalia hapa Kongwa mpaka Kibaigwa maji mengi yanamwagika hovyo kutoke Kiteto huko na nchi kama zile za Senegal, Siera Leone huko walianzisha kitu kinaitwa “*man-made lakes*”, wakachimba, wakakinga yale maji na sasa hivi wanayatumia, hiyo itatusaidia. Vilevile tuanze utaratibu wa kugawana pia hata maji haya tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tuanzishe utaratibu wa makusudi kwa baadhi ya maeneo hata mjini kufanya *recycling* ya maji haya tunayotumia tunasema machafu, tunayatupa, kwa sababu haya maji yanaweza yakatusaidia kwa matumizi mbalimbali; kwa matumizi ya wanyama, yanaweza yakatusaidia kwa matumizi ya umwagiliaji na matumizi mengine hata matumizi ya majumbani ukiondoa matumizi ya chakula na kadhalika. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba, inawezekana tumerdhika kwamba maji tunayo, mito ipo na kadhalika, lakini tunakokwenda maji yanapungua Kitifa na Kimataifa, kwa hiyo Wizara ifanye mikakati ya namna ya kuhifadhi haya maji yaliyopo ili yaweze kutumika sawasawa. Pia watunze na haya mabwawa kwa sababu kuna mabwawa mengine yanapotea. Angalia kwa mfano, Ziwa hili la Babati; Ziwa la Babati sasa hivi linajifukia kwa sababu ya uchafu. Angalia Ziwa Jipe; na lenyewe linajifukia kwa sababu ya uchafu kwa sababu tusipofanya bidii wenyewe kile alichotupa Mwenyezi Mungu kinapotea

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni huizi *certificates*; ni kweli zinachelewa na zikichelewa zinapandisha gharama kwenye ile miradi na ni kweli vilevile kuna ufisadi kwenye hii miradi na ni ukweli vilevile kwamba baadhi ya Watumishi katika mamlaka zetu na kadhalika bado hawajaenda na kasi ambayo inazungumzwa. Sasa nifikie mahali niseme, kwa nini tuna mamlaka halafu tunalalamika? Yaani kwa nini tunalalamika kuhusu Watumishi wa Halmashauri sisi Bunge? Yaani tunakaa hapa Bungeni tunamjadili Injinia wa Maji wa Halmashauri fulani, hivi hii inawezekana kweli? Kwa hiyo, niseme kwamba labda pengine sisi tumekosea mahali fulani.

Niishauri Wizara hao wanaolalamikiwa wachukue hatua ili Wizara iendelee na kazi yake nzuri ambayo inafanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Tunaendelea na Mheshimiwa Sonia, baadaye Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa John Kadutu ajiandae.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Pamoja na hotuba ya Mheshimiwa Waziri kugusia baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Tanga kuwemo katika miradi ambayo inaendelea kutekelezwa lakini ningeiomba Wizara iiangale miradi hii kwa jicho la tofauti. Nasema hivi kwa sababu miradi mingi ya maji Mkoani Tanga imechukua muda mrefu sana kukamilika na imezua sintofahamu kwa wananchi, hawajui ni kwa nini miradi hii imekuwa ni ya muda mrefu lakini haikamiliki na kuendelea kuacha changamoto ya maji ikiwakabili Wananchi hawa wa Mkoa wa Tanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano wa mradi wa maji wa *HTM*; huu mradi umechukua muda mrefu sana na umesababisha tatizo kubwa sana la maji kwa wananchi wa Wilaya ya Handeni. Wilaya ya Handeni tatizo la maji limekuwa kama ni historia sasa na kila siku wanapewa ahadi juu ya huu mradi kwamba kuna mradi wa maji, kuna mradi wa maji lakini huu mradi umekuwa haukamiliki na wananchi wanaendelea kuteseka sana na maji. Hivyo, niiombe Serikali iangalie kwa jicho la tofauti ni nini kinazuia huu mradi usikamilike na wananchi wale waweze kupata maji kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga tuna vyanzo vingi vya maji na sioni ni kwa nini tunakuwa na tatizo kubwa sana la maji kiasi hiki. Hivyo Serikali iangalie vile vyanzo ambavyo tunavyo kuweza kuwasaidia wananchi hawa wa Mkoa wa Tanga kuondokana na hili tatizo la maji. Sisi sote

tunafahamu umuhimu wa maji katika maisha ya mwanadamu na Mkoa wetu wa Tanga shughuli zetu nyingi sana zimetawaliwa na viwanda na kilimo, lakini tunapokuwa na uhaba wa maji tayari kwetu hili linakuwa ni tatizo kubwa sana. Huwezi kuendesha viwanda kwa ufanisi kama huna maji ya kutosha, huwezi kuendesha shughuli za kilimo kwa ufanisi kama huna maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Sera ya Elimu bure ambayo inatolewa na Serikali. Hii sera ya elimu bure itakuwa haimfikii hasa mtoto wa kike vile ipasavyo kwa maana watoto hawa muda mwingi ndiyo wanatumika kwenda kusaka maji. Ule muda ambao wangeweza kuutumia kwenye masomo unakuta wanatumia kwenda kutafuta maji na katika harakati hizo za kutafuta maji ndiyo unakuta watoto wengi wanapata mimba za utotoni na maradhi mengine ambayo hayatibiki. Wakati huo huo kuna kipindl ambacho mtoto wa kike anakuwa kwenye hedhi na shule nyingi hazina maji. Unakuta mtoto ile hali inampelekea asiende shule kwa kuogopa kwamba nikienda shule nitajisitiri viperi nitakapokuwa katika hali hii. Hivyo Serikali iwasaidie watoto hawa kama tumeamua kuwapa elimu bure basi ikamilike pia, tuangalie na vichocheo ambavyo nivapelekea hii elimu iweze kuwafikia kwa ufanisi ikiwemo suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwenye miundombinu ya maji; miundombinu yetu ya maji hajakaa vizuri na hii inapelekeea wananchi wengi kulalamikia suala la bili ambazo haziko *realistic* kutokana na kile ambacho wanakitumia. Mabomba mengi yanavuja na unaweza ukamwita fundi labda ukapiga simu ili upate msaada, lakini hupati ule msaada kwa wakati, hivyo kupelekeea kupata bili ambayo pengine ilikuwa siyo tatizo lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hii *system* ambayo inanipa utata ya kwamba maji yanapovuja mbele ya mita inakuwa ni juu ya ofisi lakini inapovuja nyuma ya mita inakuwa ni juu ya mteja. Hili ni tatizo kwa sababu kama miundombinu yenu haiko sahihi ni lazima maji yatavuja. Pia tungeweza kuzuia pale mwanzo wakati yule mteja anaweka ile *system*

yake ya maji kukawa na watu ambao wanakuaja kukagua kabla hamjamwekea maji ili kuona kama ameweke vitu vyake kwa usahihi ambapo itapelekeea mwananchi huyu asipate bili zinazosababishwa na uvujaji wa maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine naomba pia Serikali iangalie umuhimu wa kutoa elimu juu ya matumizi ya vyanzo vya maji kwa wananchi. Wananchi wengi hawana uelewa juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na kupelekea vyanzo vingi kukauka na uharibifu wa vyanzo hivi vya maji. Hivyo, niiombe Serikali kuliko kuangalia zaidi kwenye kuwapa adhabu hawa wananchi waangalie zaidi kuwaelimisha kuwasababisha wawe mabalozi wazuri kwa utunzaji wa vile vyanzo vya maji ambavyo vinawazunguka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia nizungumzie mfumo wa *prepaid*. Mfumo huu kama ungeweza kusisitizwa nchi nzima na ukatolewa elimu kila mtu akaufahamu vizuri ungeweza kusaidia kupunguza haya malalamiko ya bili za wateja. Hivyo, niiombe pia Serikali iangalie umuhimu wa kuhakikisha hii huduma ya *prepaid* inaenea nchi nzima na kila mwananchi anaelewa matumizi yake ipasavyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sonia. (*Makof!*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Nape Nnauye na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ajiandae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kuwapongeza kwa kazi nzuri sana ambayo Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji Wizarani wanafanya. Tunawaona wanajitahidi, wanakimbia, wanafanya kazi,

wanabeba maji vichwani, wanafanya kazi nzuri, nawapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuongelea eneo la uboreshaji wa Mamlaka mbalimbali za Usimamizi wa Maji. Imefanyika kazi kubwa sana na mfano mzuri ni pale Dar es Salaam (*DAWASCO*), nadhani kuna maboresho na uimarishaji mkubwa wa Mamlaka ile kiasi kwamba kelele ambazo tulikuwa tukizisikia sana Dar es Salaam zimepungua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni vizuri tupongeze na kutambua kazi ya Bodi inayoongozwa na Gen. Mwamnyange pia na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hii Ndugu Luhemeja. Nadhani wanafanya kazi nzuri sana. Kwa muda sasa zile kelele ambazo tulikuwa tukizisikia zimepungua, wanajituma, tunawaona mtaani wanafanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya maboresho na marekebisho yaliyofanyika kwa Mamlaka ya Dar es Salaam yafanyike na mikoani na kasi iende hiyohiyo kwa Mamlaka zingine. Nadhani itatusaidia sana kwa sababu moja ya eneo kubwa lenye changamoto ni usimamizi. Kwa hiyo, Mamlaka hizi zikiboreshwu wakaiga mfano wa hii Bodi ya Gen. Mwamnyange na mwenzake Ndugu Luhemeja nadhani watakuwa wamefanya kazi nzuri na tutayaona mabadiliko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli napongeza kazi nzuri iliyofanyika Dar es Salaam na sasa ihamishiwe mikoani. Nadhani ni vizuri uimarishaji huu ukaenda pia kwenye Mamlaka zile ndogo za kule chini kabisa na zile Jumuiya za Usimamizi tusiwaachie wananchi peke yake. Usimamizi uwe wa wananchi lakini pengine tupeleke utaalam fulani pale ili kusaidia usimamizi uwe bora zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka ni Mfuko wa Maji. Mwaka 2018/2019 takwimu za upolekaji wa fedha kwenye miradi ya maji kutoka kwenye Mfuko wa Maji zimepelekwa asilimia 67, napongeza, lakini kutoka

kwenye vyanzo vya ndani vingine tumepeleka asilimia 17. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba kama isingekuwa Mfuko Wizara hii mngekuwa hamjafanya chochote kwa sababu ingekuwa asilimia 17 peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu mfululizo hoja ya kuongeza fedha ili zikaongezeke kwenye Mfuko huu zimekuwa zikija hapa Bungeni. Hoja yangu hapa nachoshangaa huku kutoona kwa Serikali kunakuja kwa sababu gani? Ni kwamba ninyi mkishawaza ndiyo *final*, hapa tunakuja kufanya nini kama kwa miaka mitatu tunasema hela iongezwe na haiongezwi na Serikali inaendelea na msimamo wake? Tunaletwa kufanya nini hapa, shilingi 50 tu inashindakana kuongezwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwetu sisi umeme ni bora kuliko maji kwa sababu *REA* tunapeleka shilingi 100 na mambo yanakwenda vizuri na tunaipongeza sana Serikali lakini kwenye jambo ambalo linagusa maisha ya kila mtu hata maskini wa mwisho, hivi tunachoogopa ni nini? Tunachong'ang'ana nacho ni nini? Kwa nini tunataka tulifanye Bunge lioneokane halina maana kwa miaka mitatu mfululizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani safari hii Waheshimiwa Wabunge tusikubali. Tumesema na tumebembeleza vya kutosha, safari hii tuweke mguu chini fedha iongezwe, si sawa hivi tunavyoenda. Mimi nimeona hapa tunabembelezana inakuja tunajibishana ooh sijui *inflation* sijui nini si sawa. Kwa sababu tatizo hili ni kubwa na takwimu zimeonesha bila huu Mfuko miradi yote ingesimama, sasa tusiendelee na kiburi hiki maana kinaumiza wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona humu kuna miradi kwa mfano kuna fedha zile wa Wahindi dola milioni 500, hizi fedha zina miradi *specific* sisi wananchi wa vijiji hizi fedha hazitafika kwa baadhi ya maeneo yetu. Ukombozi wetu peke yake ni huu Mfuko wa Maji.

## TAARIFA

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu kwa Serikali na kwa Bunge...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape, tusikilize taarifa kidogo.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema kaka yangu Mheshimiwa Nape Nnauye naungana naye kwa silimia 100 siyo tu lazima tupate fedha kutoka kwenye chanzo anachokisema cha mafuta lakini ku-*compliment* anachokisema Mheshimiwa kaka Nape tunaweza tukapata fedha za kuwasaldia Watanzania hata kutoka kwenye mawasiliano ya simu. Mheshimiwa kaka Nape unachokisema nina ku-*compliment* safari hii bila kuongeza fedha Wabunge hatutokubali kwa lengo la kuwasaidia watu wetu kwenye sekta ya maji. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa yake na namshukuru kwa kuniunga mkono. Ni kweli Serikali tukibaki na kisingizo kwamba kwenye mafuta kutaleta *inflation* hivi chanzo ni mafuta peke yake, je, kwenye simu au data? Hoja yetu hapa ni kwamba huu Mfuko uongezewe chanzo cha fedha, basi. Mnatoa wapi msiende kujificha kwenye mafuta peke yake, Serikali inaweza kufikiria nje ya boksi tukaenda kwenye vyanzo vingine. (*Makofii*)

Hoja yetu ni kwamba bajeti ya maji safari hii tunaipitisha hapa kama mnakuja na mpango wa kuongeza fedha vinginevyo mtatuona Waheshimiwa Wabunge wabaya. Kwa hiyo, zile siku za mashauriano zikatumike vizuri na Serikali wekeni *commitment* hapa kwamba mnakwenda kushauriana, nendeni mkabane kwenye vyanzo vingine huu

Mfuko tuuon gezee fedha tuone maji yanatiririka vijijini.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tatizo kubwa hili la maji linahitaji mikono ya wadau wengi tulete nguvu ya pamoja. Tilitunga sheria hapa ya Kudhibiti Rasilimali ya Maji ya mwaka 2009. Sheria hii ilianzisha pia mabonde, yako mabonde ya usimamizi wa maji ni kama tisa (9) kama sikosei. Huku kuna kanuni zimetungwa za kusimamia, lengo ni jema lakini zimeweka tozo mbalimbali za watumiaji wa maji haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanatumia maji kwa *domestic use*, mtu anachimba kisima nyumbani kwake kwanza anatakiwa apewe kibali na anatakiwa akilipie halafu kila mwaka anatakiwa alipe tozo kwa ajili ya kutumia kile kisima. Mimi nasema tukiwatoza watumiaji wa maji ambao wanakwenda kutumia kiblashara sina matatizo nalo lakini hawa ambao ni mtu binafsi ameamua kusaidia watu kwenye eneo lake amechimba kisima kwa fedha zake, ameweka *infrastructure* kwa fedha zake halafu bado tunaenda kumtoza, *actually*, nilidhani Serikali badala ya kumtoza ilitakiwa kumlipa kwa sababu anaisadia kusambaza huduma ya maji kwenye eneo lake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana mnasimamia na kutekeleza kwa sababu ni suala la kisheria. Ushauri wangu kama ni sheria leteni hapa tufute kwa sababu ni sheria ambayo haina maana badala ya ku-*encourage* watu wachimbe visima zaidi, kwangu pale Mtama Makao Makuu ya Jimbo kuna watu zaidi ya 50 wamechimba visima halafu unajua kilichotokea nyuma pale walikuwa wanafumbia macho kidogo hivi kwa hiyo watu wanachimba wanaendelea, sasa hivi kwa sababu ya hii dhana ya kukusanya zaidi wameenda kukusanya mpaka madeni ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamkuta mtu ana kisima anaambiwa alipe Sh.700,000 leo, mwanakijiji wa kawaida amechimba kisima kwa hela zake, unachofanya ni kumwambia huyu afunge na akifunga hasara ya nani? Kwa

sababu maji yakikosekana hapa mwisho wa siku Serikali itabidi mpeleke fedha za kutibu watu waliouguwa kwa sababu ya kupata maji machafu, sasa mnachokipata ni kipi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu Serikali kwanza wekeni *commitment* halafu jipangeni leteni kama ni sheria hiyo tubadilishe, kama ni kanuni nendeni mkakae mzibadilishe. Mimi nashauri wale wanaofanya biashara tena siyo ile biashara ya kuuziana mtaani pale, mtu amechimba kisima anawauzia wenzake pale shilingi tano na yeze mnafanya ni mfanyabiashara, huyu ni mtoa huduma tu. Kuna watu wanafanya biashara, wanaotaka kuzalisha umeme tozeni kodi mnayotaka, wanaozalisha maji yale ya kuuza ya chupa tozeni kodi mnayotaka, wale wanaofanya umwagiliaji mkubwa tozeni lakini watumiaji wa kawaida, nimechimba kisima nyumbani kwangu nataka nijihudumie mwenyewe na majirani zangu, nadhani tuklendelea kutoza si sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa malizia.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja nikiamini kwamba Serikali itakuja na *commitment* ya kutosha juu ya hoja nilizoziveka hapa. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nape, tunaendelea na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa naunga mkono hoja ni hoja ni nzuri. Mheshimiwa Waziri umeeleza vizuri sana wewe na Mheshimiwa Naibu Waziri na timu yako nzima ya Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na mimi niendelee tu kusema kwamba naunga mkono hii shilingi 50 ambayo ni hoja au ushauri wa Kamati na imeelezwa hapa. Sasa itatoka wapi, inaweza ikatoka kwenye mawasiliano au kwenye mafuta. Hivi mtu anayejaza mafuta kwenye gari lake au mtu anayetumia simu akaona kabisa shilingi 50 hii nailipia kwenye maji, inamuumua kweli? Ni suala la Serikali kuamua tu, ninyi amueni mambo yaishe, wanaojaza mafuta kwenye magari yao au watumiaji wa simu watalipa tena wanalipa wakiwa na furaha kwelikweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo llingine hii ni utekelezaji wetu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Maana yake tunakwenda kukamilisha ahadi tulioiweka kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hili ni jambo jema sana Mheshimiwa Waziri wa Maji lichukue ukalifanyie kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Ziwa Victoria ambaao unatoka Solwa ambaao Mheshimiwa Waziri ameutaja hapo unaokwenda Tabora. Mradi huu umetoka kwenye Jimbo langu unakwenda mpaka Nzega baadaye unakwenda Igunga na maeneo mengine. Ni mradi mkubwa sana, gharama yake nafikiri kwenye dola milioni 270. Ni mradi uliosanifiwa vizuri sana unakwenda kutibu tatizo la maji kwenye zaidi ya vijiji 50 katika Jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una uzuri wake sana na niishukuru sana Serikali tena kwa asilimia zote na nimshukuru Mheshimiwa Rais na wewe pia Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, kuna kata ambazo mmeziruka kwa maana ya kwamba ama mmeruka katika upembuzi yakinifu ama mmeziruka kwa maana ya kwamba vijiji viro nje ya kilometra 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri anisikie, athari yake ni kwamba Kata hizo tano ni Bukene, Usule, Nsalala na Usanda maana yake ni kwamba mradi ukipita wanaona wenzao wanatumia maji na wao wamerukwa matokeo yake ni kwamba watakwenda

kuhujumu mradi. Sasa hapo tutakwenda Waheshimiwa Wabunge kwenda kuongea nao acheni tunafanyia kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, una Katibu Mkuu Profesa mzuri sana, tuma timu hata kama vile vijiji viko nje ya kilometra 12 kwenye Kata hizi hasa Usule, Bukene, Nsalala na Usanda zikafanyiwa upembuzi ziingizwe. Hivi kweli mainjinia ambao tunao kweli katika Tanzania hii wanashindwa kwenda kufanya usanifu hata hivyo vijiji ambavyo viko nje ya kilometra 12 na wenyewe wakapata maji? Mimi sidhani na gharama siyo kubwa hivyo ili mradi ukipita upite moja kwa moja na mambo hayo yawe yamekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana Tinde mmelingiza ilikuwa imerukwa. Mheshimiwa Aweso nakushukuru sana, Mheshimiwa Waziri tuliongea hayo mambo sasa hivi umetupa kibali Tinde vijiji vyake vyote vinapata maji ya Ziwa Victoria. Jana nimepata taarifa kwa maana ya kwamba tulikuwa tunahangaika kijiji kimoja cha Weleza kinapata maji sasa hii kimoja kimoja hapana, tufanye kwa pamoja mambo yote yaishe kwa pamoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Solwa litakuwa ni mfano, hata *National Housing* wanavyojenga nyumba wanajenga nyumba moja wanasema hii ni ya mfano anapokuja mteja anaitizama ili aweze kuvutika kununua nyumba. Jimbo la Solwa mradi huu ukiisha nakwenda kuwa na vijiji zaidi ya 86 vyenye maji ya Ziwa Victoria na ni Jimbo la kwanza kabisa naweza ku-*declare* tumefika asilimia 85. Kwa hiyo, ni jambo jema sana, niishukuru sana Serikali yangu pamoja na Mheshimiwa Rais wetu. Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Mwakitolyo na Mwasekagi wa mwaka 2017. Mradi huu uko asilimia 85, tuna fedha kidogo sana imebaki bilioni 150, *tume-raise certificate* kwa ajili ya shilingi bilioni 63 ili zile kazi ndogo ndogo zikamilike. Sasa hivi wanatumia maji lakini kuna kazi

ndogondogo za kumalizia ili mradi huu uishe moja kwa moja katika eneo la Mwakitolyo na Mwasekagi kwenye Kata ya Solwa. Naomba sana hili mlifanyie kazi, Katibu Mkuu unanisikiliza, tulipe hii billioni 63 mkandarasi akamalize kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mwakitolyo kwa kipekee kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri nikushukuru sana na Mungu akubariki sana na kama una mke mmoja akupe wa pili, wa tatu na wa nne. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Mwakitolyo, huu mradi wa maji ni wa shilingi 1,400,000,000, ilikuwa fedha zake zimelipwa na mradi haukuweza kufanya kazi. Umekuja pale, ukaongea na Katibu Mkuu kwa simu na wananchi wanakusikia. Katibu Mkuu akajibu vizuri, nafahamu kazi iko vizuri, Tume imeenda na mpaka sasa mmeshachukua hatua. Ombi langu nataka sana uende haraka kwa maana najua kuna usanifu na *design* mpya inafanyika itengwe fedha ili wananchi wale wa Mwakitolyo ni wengi, pale kuna wachimbaji wadogo wadogo wengi sana, ni mji unaokuwa haraka sana, una fedha watu wanajenga nyumba za kisasa kabisa, nafikiri umeshanisikia suala hili utalifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Keissy masuala ya mabwawa kuna changamoto makubwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Ya pili, malizia sentensi yako.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, duh, naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa na Mheshimiwa Mboni Mhita ajiandae.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya Maji. Kwanza nitangulize shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Waziri na kwa timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nitumie fursa hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa sababu kati ya watu amba wameguswa na kujaribu kutatua tatizo la maji nchini ni pamoja na Wilaya yangu ya Longido baada ya ule mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Simba kwenye Nyanda za juu za Mlima Kilimanjaro kufikisha yale maji Longido na watu wamefurahia na maji yale kwa kweli yamekuwa ukombozi maana kiangazi ambacho kimekuwa kinaendelea kilipelekea watu wanunue maji mpaka Sh. 1,500 kwa ndoo kutoka katika vyanzo mmbalimbali. Tunaishukuru sana Serikali kwa hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mawazo mazuri yaliyojitekeza katika hotuba hii na nimeona mambo mengi mazuri yanayofanyika, mimi kwanza niwaunge mkono Waheshimiwa Wabunge wanaosema kwamba tuweke miguuu chini leo mpaka Wizara ya Maji watenge fedha za kutosha kuhakikisha kwamba maji yanamfikia kila Mtanzania ili azma yetu ya kumtua mama ndoo kichwani iweze kutimizwa kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa sababu hii fedha ya Mfuko wa Maji ambayo asilimia 70 imepatikana ikaenda kwenye maji na asilimia 17 tu ndio imepatikana kwenye vyanzo vingine, imeonesha kwamba kumbe tungetenga fedha nyangi zaidi kwa vyanzo mbalimbali vya Serikali tungeweza kufikia malengo. Ninaiomba Serikali izingatie suala hili la kuongeza hiyo tozo kwenye mafuta ifike shilingi 100, lakini pia ikamue *percent* fulani katika kila aina ya tozo inayotozwa kwa huduma mbalimbali katika vyanzo

mbalimbali ambavyo Serikali inatoza kodi katika nchi hii. Iwe ni katika Sekta ya Utalii, iwe ni katika Sekta ya madini; sekta zote ambazo Serikali huchukua tozo wekeni *percent* kidogo iende kwenye kuboresha Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tuzingatie kwamba sasa hivi tuna *RUWASA*, sasa *RUWASA* kama ni taasisi iliyoundwa ya kuhakikisha kwamba kuna wataalam wa kutosha, kuna vifaa vyta kutosha, watapataje kuendesha kwa ufanisi kama hawana fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba kwanza kodi zinazokera, za kuumiza hizi tasisi za maji, ziondolewe, kama mitambo ya maji ifutiwe kodi, vifaa vyta kuchimba mabwawa vifutiwe kodi na kila namna ifanyike ili kuhakikisha kwamba tunauinua huu mfuko ili tumtoe mama ndoo kichwani na kweli tuflikishe huu uhai ambao tunasema maji ni uhai kwa kila Mtanzania. Tukipata maji safi na salama katika nchi hii miradi mingine yote ya maendeleo itawezekana. Afya ya watu itaboreka, muda wa kuwekeza kwenye shughuli nytingine za uchumi utaimarika maana muda mwingu hypotea katika kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hiyo hoja na kutoa dukuduku langu la kutamani Wizara iongeze bajeti yake, naomba nijielekeze katika masuala mahususi ambayo yamejitokeza katika hii hotuba, na imegusa miradi ambayo inagusa sana maisha ya wananchi wa Jimbo langu la Longido. Katika ukurasa wa 119 kuna kiambatisho namba 2 kinachoongelea kiwango cha maji katika maziwa, mito mabwawa na vyanzo mbalimbali vyta maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mto unaitwa Mto Ngarenanyuki, huu mto unatiririsha maji kutoka *Arusha National Park* unapitia Arumeru unakuja mpaka Longido, Kijiji cha Ngereiyani. Maji yake yana *fluoride* nytingi, sio mazuri kwa binadamu, lakini yanafaa sana kwa kilimo cha nyanya. Wakulima wengi wamegundua kwamba hayo maji yanaotesha nyanya ya ubora wa kimataifa, nyanya zinazuwa

kila mahali nchi hii, Dar es Salaam, mpaka nchi za nje, Mombasa na zinakwenda mpaka Nchi za Uarabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kwa matumizi holela ya huo mto mifereji imepasuliwa kila mahali, nyanda za mto zimeharibiwa, huo mto unakwenda kupoteza hadhi yake na mazingira yanaharibika na maji hayafiki tena kwenye nyanda za chini, wananchi wa Ngereiyani hawapati tena yale maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali pia iweke usanifu wapime kiwango cha hayo maji na ikiwezekana wajenge matenki maji yapitie kwenye matenki ndiyo kutoka kwenye mabomba yaende kwenye mashamba ya wakulima wadogo wadogo ili tuhifadhi mto na watu wengi waweze kufikiwa na hayo maji, tuboreshe kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa sababu maji ya Mto Simba yanakwenda kusuluuhisha tatizo la maji kwa wakazi ambao kwa sasa hivi, hii awamu ikikamilika ni watu kama 18,000 tu wa Kata ya Longido na Kata ya Engikaret na kwa sababu tumetengewa bilioni 2.9 na ninaishukuru Serikali sana kwa sababu ya usambazaji wa hayo maji. Basi huu mradi utakapokuwa umesambaza hayo maji yakatimiza ahadi ya viongozi wakuu wa Serikali akiwepo Rais ya kupeleka hayo maji mpaka Namanga, Kimokowa na kusambaza kule Kiserian, tutakuwa tumetatua kero ya maji kwa wananchi wasiopungua 30,000 wa Longido, lakini bado kuna watu zaidi ya 100,000 ambao hawana chanzo cha uhakika cha maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kusema katika Bunge hili kwamba maji ya mafuriko ya mwaka jana yalitupasulia mabwawa ambayo ndiyo yalikuwa yanategemewa na jamii ya wafugaji katika wilaya yangu. Kuna mabwawa yamefukiwa kabisa, kuna mabwawa yamepasiuka, nilitegemea kwenye bajeti hii kwenye ile miradi mingine ambayo Waziri ametaja katika hotuba yake, kuona kuna miradi mingine ya maji ukiacha haya maji ya mito; ningetegemea mabwawa yale yaliyopasuka na yaliyojaa

udongo yangetengewa bajeti maana sisi mabwawa hayohayo ndiyo maji ya binadamu ndiyo hayohayo ya mifugo; Bwawa na Kimokowa, Bwawa la Tinga Lesing'ita, Bwawa la Sinoniki, Bwawa la kule Muriatata na mabwawa mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuna ahadi za Serikali za kuchimba pia mabwawa mengine ambayo yatafaa kwa hata umwagiliaji pale katika Kata ya Tingatinga. Kuna ahadi ya Serikali ya kuchimba bwawa la umwagiliaji ili haya maji yanayotiririka ya msimu wa mvua kutoka Kilimajaro yatekwe wananchi wa Tingatinga waweze kuendesha kilimo cha umwagiliaji na maji hayohayo yatafaa kwa mifugo na watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kule Wosiwosi, mwisho wa Wilaya hii ya Longido katika Ukanda unaopakana na Kenya na Wilaya ya Ngorongoro kuna Kijiji kinachoitwa Wosiwosi, wao maji ya kunywa binadamu hakuna kabisa mpaka wanakwenda Kenya kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba pia bwawa na nilitegemea bwawa hilo lingewekwa kwenye ile miradi mingine ili wananchi wa Longido amba wako mbali na haya maji ya Mto Simba waweze nao kufarrijika na kuona kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inawajali kwa suala la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru baadhi ya wadau amba wametuunga mkono katika kutatua kero za maji Longido; tuna Shirika la Maisha Bora, wamekuwa wakitusaidia katika miradi ya kuchimba visima virefu katika Kata ya Matale; kuna taasisi ya kiwindaji inaitwa *Kilombero Safaris* wakishirikiana na Shirika linaitwa *World Self International*, wamekuwa wakitusaidia kupima maeneo mbalimbali kubainisha maeneo yenye maji ya chini pamoja na wengineo kama *Friends for African Development*, marafiki zetu kutoka Chuo Kikuu kimoja cha Marekani amba wametuchimbia visima vitatu. Naomba Serikali itambue juhudzi zao na iendelee kututengea fedha za kuchimba visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ninapenda kuchangia ni suala la umuhimu wa kuvuna maji ya mvua katika nchi yetu. Maji ya mvua yakivunwa, na sheria ipitishwe – maana kabla sijawa Mbunge ilishatengeneza sheria lakini sidhani kama inafanyiwa kazi – na iwekwe kwamba ni kampeni ya kitaifa; kila kaya wahimizwe wawe na mfumo wa kuvuna maji ya mvua, iwe ni sehemu ya *requirement* katika kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa nyumba za makazi ya watu na taasisi mbalimbali nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya mvua yatauondolea kero ya maji kwa asilimia kubwa. Inaponyesha hata katika maeneo kame maji mengi yanapotea kwa sababu hatuvuni maji ya mvua na nimeenda katika nchi zingine, kama Jimbo la California kule Marekani, wao hawana mto wowote lakini maji yote ya mvua yanavunwa na wanalimia mpaka wanauzu mazao ya matunda nchi za nje; kwa nini sisi Tanzania wenye maji mengi ya mvua ambayo yanafurika kila wakati inaponyesaha, hata katika maeneo kame tusiige huo mfano tukahimiza uvunaji wa maji ya mvua katika mabonde, tuhimize uvunaji wa maji ya mvua katika nyumba zetu za bati kila kaya ihmizwe iwe na mfumo na wataalam wa Serikali wasimamie hiyo kama kampeni mahususi katika shule, katika hospitali, katika taasisi za dini na nyumba za makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu, nipende pia kutumia fursa hii kuishukuru Serikali kwa sababu sisi katika Wilaya ya Longido ambayo ni wilaya ya wafugaji kwa asilimia 95, na ni wilaya ya uhifadhi pia wa mazingira ya wanyamapori kwa asilimia hiyo hiyo 95, tumeendelea kuona mkono wa Serikali kuititia kile chakula tulichopewa wakati wa ukame. Wananchi wa Longido wamefarikika na wamesema kila wakati ukisimama Bungeni mshukuru Rais kwa sababu tulipolia njaa kwa sababu ya ukame tulipewa chakula, tulitengewa chakula tani 10,000 za mahindi na tani 1,000 ndiyo zinazoendelea kuwalisha watu katika mwezi huu wote tunavyoangalia hali ya hewa itakavyokuwa. Na tumshukuru Mungu mvua imenyesha lakini haitoshelezi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho, Mheshimiwa Mbuni Mhita.

**MHE. MBONI M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba awali ya yote nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu pamoja na watendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niendelee kutoa kilio cha wananchi wa Wilaya ya Handeni, niendelee kutoa kilio cha wananchi akina mama wa Handeni Vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya maji Handeni imegeuka kuwa janga la kiwilaya. Nasema janga kwa sababu ukosefu wa maji katika Wilaya ya Handeni pamoja na Jimbo la Handeni Vijijini umezuka sasa na kusababisha changamoto mbalimbali ambazo sasa zimeanza kuingia katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa maji Handeni umechangia kwa kiasi kikubwa kusababisha milipuko ya magonjwa. Historia ya kupatikana Ugonjwa wa Kipindipindu Handeni ni kwa sababu ya ukosefu wa maji katika Wilaya ya Handeni ambayo sasa hiyo imeingia kwenye Sekta ya Afya. Lakini wakati huohuo, ndoa za akina mama Wilaya ya Handeni zinalegalega, akina mama wanaamka alfajiri saa kumi kwenda kutafuta maji, na haina *guarantee* kwamba wakirudi wanarudi na maji. Wakati mwingine wanatoka saa kumi wakirejea ni saa saba au saa nane za mchana na wakati huo hawajarudi na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe utajionea, uaminifu kwenye zile ndoa unapungua, ndoa

nyingine zinalegalega, na akina mama wengine wamekosa ndoa zao kwa sababu ya changamoto ya maji. Hilo ni tatizo la kijamii sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtagundua kwamba watoto wa kike Mkao wa Tanga tumekuwa tukishika mkia kwenye ufaulu, sasa hapo tumeingia kwenye elimu. Kwa sababu mabinti hao badala ya kutumia muda huo kwenda kujisomea wanatumia kwenda kusaka maji. Wakati wenzao wa wilaya na mikoa mingine wakitumia muda huo kujisomea, sisi mabinti wa Handeni Vijiji tunatumia muda huo kwenda kusaka maji, hali kadhalika mtajionea kwamba *comparison* ya ufaulu utatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huohuo, muda ambao akina mama wanaamka kwenda kusaka maji ndiyo muda ambao na wanyama wakali pia wanatoka kwenda kusaka maji. Sasa hebu tuangalie mwanamama *in a very vulnerable situation* anakutana na mnyama mkali, wengine wamedhurika na wengine wamepoteza maisha kabisa, hilo ni tatizo la kiusalama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo kubwa kabisa ni kurudi nyuma kiuchumi. Wakati ambao wenzetu wa wilaya na mikoa mingine wanajijenga kuanzisha miradi ya akina mama na kutumia mikopo mbalimbali sisi akina mama wa Wilaya ya Handeni na Jimbo la Handeni Vijiji tunatumia kwenda kusaka maji. Ni ukweli usiofichika kwamba hata ukituangalia hatuwezi kulinga na akina mama wa mikoa mingine, hatuwezi kulingana na akina mama wa wilaya nyingine kiuchumi kwa sababu muda ambao wenzetu wanatumia fursa za Serikali za kutengeneza vikundi, za kuanzisha miradi, sisi tumejitiwika ndoo tunasaka maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike? Naomba nitoe maoni yangu; kwanza niishukuru sana Serikali ilitupatia bilioni mbili ili kuweza kukarabati Mradi wa HTM ambao kwa kirefu ni *Handeni Trunk Main*. Lakini mradi huu ulianza mwaka 1974 ukiwa na *lifespan* au uhai wa miundombinu wa miaka 20, nikiwa na maana kwamba mwaka 1994 ile miundombinu

itakuwa imechoka. Sasa wenyewe tufanye hesabu kuanzia mwaka 1994 mpaka 2004 mpaka 2014 mpaka 2019, miaka mmingi imekwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashukuru Mungu Serikali imetuweka kwenye mpango lakini naomba sasa pendeleko langu liwe Serikali iharakishe ukarabati wa miundombinu ya *HTM* ili akina mama wa Handeni ambao wamekuwa sasa wamezoea kuisikia hii ahadi, imekuwa kama ni ahadi sugu, angalau waone utekelezaji wa kuonekana. Naamini kwamba Serikali ina mipango mizuri lakini bado iko kwenye *paperwork* Wizarani, hatujaanza kuona *implementation* katika Wilaya yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendeleko langu la pili, naomba Serikali iridhie sasa Mji wa Mkata ambao ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Handeni *Vijiji*, itegemee vyanzo tofauti vya maji. Pale kunategemewa *HTM*, kunategemewa visima, lakini tunategemea *CHALIWASA* ambao ni mradi wa Chalinze, ambao tunashukuru Mungu mpaka sasa hivi ile miundombinu imefika Manga, na Manga ni kijiji ambacho kiko ndani ya Kata ya Mkata. Kwa lugha nyingine ni kwamba Serikali ikiridhia basi miundombinu ile inaweza ikasogea mpaka Mkata Mjini na kata ile ikawa ina sources mbalimbali za kuweza kujipatia maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu ni Serikali ifuatilie ubadhirifu mkubwa ambao umefanya kwenye mabwawa ya Manga, Mkata na Kwandugwa, pamepotea zaidi ya bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Mungu kwamba Waziri alifika, Naibu Waziri amefika na amejionea. Tulifanya ziara na Mheshimiwa Waziri, na tukafanya ziara na Mheshimiwa Naibu Waziri, kaka yangu, Mheshimiwa Aweso alifika mpaka eneo na alijionea na siku hiyo baadhi ya wakandarasi pale walishikiliwa. Lakini kushikiliwa kwa wale bado hakuaokoa hali ya changamoto ya pale Handeni, Handeni *Vijiji* na Kata nzima ya Mkata. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisitumie muda naona kengele ya pili imelia, kwa hiyo naomba Serikali ichukue hatua kali. Baba yangu, Mheshimiwa Keissy alisema fedha zile zitapikwe, bilioni moja ni nyingi sana kupotea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja. Nashukuru sana, ahsante sana kwa kuniskiliza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mboni, nawashukuru wote kwa michango yenu mizuri ya leo hii ambayo mmetumia kwa lugha ya staha, ya Kibunge, Mungu awajalie muendelee hivyo hivyo.

Baada ya kusema hayo, kabla sijasitisha Shughuli za Bunge, natoa tangazo; kuna mtu ambaye ameshahau ufunguo wake, nafikiri wa gari, uko kwenye *key holder* ya Toyota, kwa hiyo yejote ambaye amesahau mahali ufunguo wake, ulikuwa nyuma pale kwa Mheshimiwa Taska, basi aje kuwaona makatibu hapa ili aweze kupatiwa ufunguo wake.

Baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 07.00 Mchana, Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, majadiliano yanaendelea na tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, baadaye Mheshimiwa Suleiman Kakoso ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukupongeza wewe na pia kwa kuwapongeza Mawaziri; Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na Mheshimiwa Aweso kwa kazi

nzuri wanayoifanya. Kusema ukweli wanahangaika sana, wanafanya kazi sana, miradi ya maji imeongezeka, maji yameongezeka, lakini tatizo moja bado watu wanahitaji maji. Ninavyoongea sasa hivi, ni asilimia 64.8 ya wananchi wamefikiwa vijiji na asilimia 80 mijini wamefikiwa na maji. Kwa hiyo, watu bado wanahitaji maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikileta mfano mmojawapo kwa Mkoa wangu wa Morogoro, ambao ni mkoa uliojaliwa ambaao una mito mingi sana, lakini mpaka sasa hivi sehemu nyingi za Mkoa wa Morogoro wana matatizo ya maji. Kwa mfano, nikija kwenye Mji mdogo wa Gairo, Malinyi, Vijiji vya Morogoro Vijiji, Mvomero pamoja na Kilosa bado wana matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa maji ambaao ni wa Manispaa Morogoro ni tatizo mpaka sasa hivi kwani umechukua muda mrefu. Ni kweli naamini Serikali inajitahidi na imesema kuwa kuna *Euro* milioni 70 ambayo itafadhiliwa itasaidia pamoja Serikali pamoja na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), lakini tatizo ni kuwa mpaka sasa hivi umechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wanajua tatizo la Morogoro na tatizo la manispaa, nilishaongea na Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge wameongea naye na amekiri kuwa kweli ni tatizo. Naomba atuambie tufanyeje Mkoa wa Morogoro hususan manispaa ili upungufu wa maji uweze kwisha na wananchi waweze kupata maji. Ninavyoongea hivi, Kola A, Kola B na Mkundi hawapati maji kabisa na wale Kata zinazopata maji hazipati maji ya kutosha, wanapata maji pungufu. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atujibu tufanyaje kama kuna uwezekano wa kuona tufanyeje ili waweze kupata maji waweze kuchukua hatua hiyo tukiwa tunasubiri huo mradi mkubwa unaoshirikisha Bwawa la Mindu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka mitatu sasa hivi imepita tunajadili kuhusu kuongeza tozo ya maji kutoka Sh.50

kwa lita mpaka Sh.100 lakini mpaka sasa hivi bado utekelezaji ndio tatizo. Humu Bungeni tulishapitisha, lakini tatizo ni utekelezaji, sjui kwa nini; Mheshimiwa Waziri naomba atujibu. Naamini kuwa kama tungakuwa tumeongeza hiyo tozo au tumechukua njia nyingine ya kuongeza huo Mfuko wa Maji wa Taifa tungakuwa tumeweza kupata maji mengi ya kutosha na hasa maji huko vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inathibitishwa kuwa mwaka huu Aprili, fedha zilizotolewa kwa miradi ya maendeleo asilimia 67 zilitoka kwenye Mfuko wa Maji na asilimia 17 tu zimetoka kwenye vyano vingine vya maji. Naomba waweze kutueleza tutafanyaje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Ujenzi wa Bwawa la Kidunda tangu nimeingia humu Bungeni nasikia ujenzi wa Bwawa la Kidunda, ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Naomba kujua ingawaje na leo wameweka ujenzi wa Bwawa la Kidunda, lakini inaonekana kuwa bado hakuna hela na bado hakuna mfadhili. Kupanga ni kuchagua, naomba tuone tufanyaje kwani kwenye Bwawa la Kidunda linasaidia sana kuongeza maji kwenye Mto Ruvu; Ruvu Chini na Ruvu Juu pamoja na *megawatt* 20 za umeme pamoja na maji ya umwagililaji. Kwa hiyo, nafikiri na barabara ya kutoka Ngerengere kwenda mpaka Kidunda. Naomba na yenye we iweze kupewa kipaumbele hili jambo la Kidunda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Wakala wa Maji Vijijini yaani huyu ni mfadhili mkubwa sana. Naishukuru na kipongeza Serikali kwa kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini, ila ninachoshauri ikisimamiwa vizuri na ikapewa hela ya kutosha, naamini kuwa itafanya kazi nzuri na maji yataweza kuongezeka Vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kutunza vyano vya maji, nikiongelea Morogoro, vyano vya maji vingi vimeharibika. Tulikuwa na Misitu ya Uluguru, maji zamani na ninyi mnajua ilikuwa inaimbwaa kuwa maji yatiririka milimani Morogoro lakini sasa hivi nenda hakuna maji yanayotiririka;

vyanzo vimeharibika, mito inakauka, mito inakuwepo wakati wa mvua. Kwa hiyo, hii ni kama kokote kule, kwa hiyo naomba katika vyanzo nya maji waendelee kutoa elimu tuone wakisaidiana pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu kutunza vyanzo nya maji. Vyanzo nya maji sera zipo, naomba sera zitiliwe mkazo kusudi tuweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa uvunaji maji. Miongozo na sera zilishatolewa kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi lakini sera hazitekelezwi. Naomba kwa kusaidiana na Wizara zingine, hii nasema nina uhakika nayo kuwa zilishatolewa, kwa hiyo naomba sana waweze kutekeleza na kusimamia hizi sera na miongozo kusudi uvunaji wa maji hasa kuititia kwenye mapaa ya majumba kwenye taasisi na nyumba ya mtu mmoja mmoja iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kulipia maji kabla ya kutumia (*prepaid*). *Prepaid* ni mfumo mzuri, huu mfumo hausumbui, kwenye ziara zetu tumekutana nao Arusha na Kishapu, watu hawasumbuliwi. Kwa hiyo, nashauri kuwa kwa kusaidiana na TAMISEMI na Wizara zingine, huu mfumo wa *prepaid* uweze kutumika kusudi watu waweze kutopata matatizo wakati wa kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya maji huchukua muda mrefu kukamilika kwa sababu fedha zinazotolewa hazitoshi, tumeona mpaka Aprili ni asilimia 51 tu imetolewa. Kwa hiyo, nashauri kuwa hela zote ambazo zitapitishwa za maendeleo ziweze kutolewa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naamini ananisikia kusudi tuweze kupata maji, maji ni muhimu, maji ni uhai; naomba sana fedha itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Chalinze ni wa muda mrefu ambao huu Mradi wa Maji Chalinze Awamu ya Tatu umesimama, mkandarasi alishindwa na mpaka sasa hivi bado hajatafuta mkandarasi mwингine. Mheshimiwa Waziri wa Maji afanye juhudhi sana ili tuweze kupata mkandarasi mwингine kwani huu mradi wa Chalinze unasaidia hata Vijiji nya Morogoro ikiwemo Kidugalo,

Ngerengere pamoja na vijiji vingine vya Chalinze. Mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo naomba utiliwe mkazo kusudi ziweze kutolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ukusanyaji wa maduhuli, imejitahidi kukusanya maduhuli kwa sababu kufikia hadi Machi imekusanya asilimia 81. Kwa hiyo, naamini kuwa ikijitahidi kukusanya maduhuli hata miradi mingine itaweza kuendelea kuwa mizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naipongeza Serikali kwa miradi mikubwa yote inayotekelawa ikiwemo mradi wa *Lake Victoria* ambao unaleta maji mpaka Tabora, Uyui, Shinyanga na mahali popote. Wanafanya vizuri ila naomba wajitahidi wananchi bado tunahitaji maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, tunaendelea na Mheshimiwa Suleiman Kakoso, Mheshimiwa Emmanuel Papian ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kupata nafasi ya kuchangia kwenye bajeti muhimu ya Wizara ya Maji. Awali ya yote, niipongeza Serikali kwa jithada kubwa ambazo inazifanya hasa kwenye miradi ya maji. Jimboni kwangu ipo miradi ya maji ambayo ilishaanza kutekelezwa; nina mradi wa Kijiji cha Kabungu ambao una thamani ya shilingi milioni 600, mradi wa Kijiji cha Kamjela wenye thamani ya shilingi milioni 800 na mradi wa Kata ya Mwese wenye vijiji vitatu ambao una thamani ya shilingi bilioni moja na milioni mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ikikamilika itawasaidia sana wananchi wa maeneo husika ambao wanategemea kutatua kero ya maji. Niiombe sana Serikali iharakishe kupeleka fedha kwa ajili ya kumalizia hii miradi. Fedha zitakapokuwa zimeenda, tunategemea kero ya maji ambayo ipo kwenye hivi vijiji itakuwa imetoweka na

kuwafanya wananchi waweze kuzalisha na kufanya shughuli zao za maendeleo bila kuwa na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vijiji 18 ambavyo vilichimbiwa visima. Vijiji hivi vinategemea mradi huo ambao ulikuwa na thamani ya shilingi milioni 400 uweze kutatua tatizo kubwa kwenye maeneo husika ya hivyo vijiji, mpaka sasa bado vijiji hivyo havijakamilishiwa hiyo miradi ya visima. Niombe sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana akisaidiwa na Naibu wake watoe msukumo mkubwa ili hivyo vijiji viweze kukamilika, miradi hii itawasaidia sana wananchi. Akinamama wengi kipindi cha kiangazi hawafanyi kazi nyingine, kazi kubwa ni ya kwenda kutafuta maji yalipo. Kwa hiyo, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kusaidia kwenye maeneo haya ili vijiji hivi viweze kukamilisha na kazi ilishafanyika, wametumia fedha nydingi lakini bado kile kilichokuwa kimekusudiwa hakijatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mmradi wa Kijiji cha Ngomalusambo. Mradi huu fedha zilizopelekwa zimeliwa, mradi ulikamilika lakini haujatoa hata tone la maji. Niombe sana Mheshimiwa Waziri afike kwenye eneo hili akajionee, aangalie tatizo lilitopo kwenye eneo la Kijiji hiki cha Ngomalusambo. Mradi ulipokamilika wananchi walifurahi wakitegemea watapata maji ya kutosha, lakini toka ulipokuwa umekabidhiwa kwenye kijiji husika, mradi huu umebakii kuwa pambo, haujaonesha matunda yake. Naamini watendaji waliosimamia ule mradi hawakuutendea haki na ni vyema wakawafuatilia ili waangalie zile fedha zilizotumika zaidi ya milioni 200 hazikufanya kazi ya aina yoyote na tija haipo. Naomba hili Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mradi wa Kijiji cha Karema; Mradi wa Maji wa Karema ni mradi ambao tulitegemea kwamba ungekuwa umetatua kero ya wananchi kwenye eneo la Kata ya Karema. Kwa bahati mbaya sana mradi huu toka umekamilika umekuwa na shida kubwa sana ya kutoa huduma ya maji. Niombe sana Serikali

iende ikachunguze ule mradi ili tuangalie ni kitu gani kinachosababisha mradi usitoe maji kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama chanzo cha maji kinaonekana hakifai, Mji wa Karema upo jirani sana na Ziwa Tanganyika; tutaona kitu cha ajabu sana kama maji hayatapatikana kwenye maeneo hayo. Niombe Mheshimiwa Waziri najua anaufahamu mradi huu, waufanyie uhakiki na watume wataalam waende wakafanye kazi ili tutoe tatizo lile la maji ambalo lipo kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utakapokuwa umefanyiwa ukarabati na ukakamilika, utakuwa umetatua kero kubwa sana. Wananchi wengi wa ukanda wa ziwa huwa wanapata mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu kwa sababu ya kutumia maji ya ziwani. Kwa hiyo, tunaomba muufuatilie huu mradi ili uweze kutoa suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mradi mkubwa wa maji unaotarajiwu kufanywa na Serikali wa kutoa maji Ziwa Tanganyika kuyapeleka Makao Makuu ya Mkoa wa Katavi, Mpanda Mjini. Mradi huu ni muhimu sana kwa wakazi wa Mkoa wa Katavi na utasaidia karibu maeneo yote. Nauzungumzia mimi kwa sababu mradi huu upo Jimboni kwangu na utakapokuwa umekamilika, utawanufaisha wananchi wa vijiji takribani 10 ambaao watapitiwa na ule mradi. Niombe sana Wizara iharakishe mchakato wa mpango wa kupeleka maji kwenye Mkoa wa Katavi, ule utakaotoa maji kutoka Ziwa Tanganyika ili uende kutatua kero ya Manispaa ya Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mpanda una matatizo makubwa sana ya maji, mji umekua lakini bado unahitaji sana huduma ya maji. Chanzo pekee cha maji kilichopo hakitoshelezi kupeleka maji kwenye maeneo husika. Kwa hiyo, tunaomba mradi huu ujengwe haraka na unapojengwa upewe kipaumbele kwenye maeneo ambayo yatapita kwenye mradi, Kijiji cha Kapalamsenga tunategemea kabisa nacho kitapata huduma ya maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Itetemya, Kijiji cha Kasekese, Kijiji cha Kaseganyama, Kijiji cha Sibwesa, Kijiji cha Mkungwi, Kijiji cha Ikata, Kijiji cha Kabungu na vinginevyo ambavyo vitapitiwa kwenye Jimbo la Mheshimiwa Kapufi, Mpanda Mjini viweze kunufaika na mradi huu. Ni vyema Serikali ikausukuma huu mradi ili uweze kufanya kazi kwa wakati na tuna mategemeo sana na Waziri husika na msaidizi wake kwamba wataufanya kazi wakishirikiana na timu yao ya wataalam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo Viji 16 kwenye Jimbo langu; Viji vya eneo la Mishamu. Viji hivi vilikuwa na visima vya maji, ni eneo liliokuwa la wakimbizi na *UNilichimba* visima vingi kwenye maeneo hayo. Bahati mbaya, miradi hii ni ya muda mrefu na nimekuwa nikiiomba Wizara kila siku iweze kuwasaidia wananchi wa maeneo yale kuvifanya ukarabati vile visima ili viweze kutoa huduma ya maji. Ni mategemeo yangu kwamba Wizara ni sikivu, mtaenda kuangalia changamoto zilizopo kwenye viji hivi vya Mishamo viro 16 ili waweze kuwasaidia na waweze kutoa huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunaipongeza Serikali kwa jitihada ambazo wamezifanya na zaidi tunawapongeza Mawaziri kwa kazi kubwa sana wanayoifanya. Naamini Waziri husika amefika kwenye miradi ambayo nimeitaja, tunaomba akalfanyie kazi, awape fedha wakandarasi waweze kukamilisha ile miradi ili iweze kutoa huduma husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kakoso. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa John Kadutu ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nawapongeza Mawaziri ambao wametuletea bajeti hii ambayo inakidhi matarajio ya maeneo mengi kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nongoose Kamati ambayo na yenye imesoma taarifa yake na kuainisha baadhi ya mambo ambayo na sisi tuliyajadili na tukaona kwamba yanafaa kuingia kwenye bajeti hii ya 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa namna ambavyo imejithahidi kulipa wakandarasi. Mpango wa kulipa wakandarasi unaonekana sasa uko kwenye utaratibu ambao unakwenda vizuri, wakandarasi wengi wanalipwa kwenye maeneo mengi, zaidi ya shilingi bilioni 84 zimetamkwa kwamba zinakwenda kulipa wakandarasi ili waweze kurudi site.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara iweze kukaa na kuandika barua kwa wakandarasi wote nchini ambao wana miradi vijijini wawe wameripoti kwenye maeneo yao ya kazi kwa sababu wengine wamelipwa na hawajaripoti. Matokeo yake ni kwamba watalipwa watapotea na hiso pesa na mwisho wa siku miradi ya maji haitakamilika. Ili tuweze kudhibiti hali hii tunaomba Wizara iwaandikie barua wawe wameripoti kwa wakati na waweze kufanya kazi na sisi tutarudisha mrejesho kwamba hawa watu sasa watakapo-*raise certificates* nydingine wawe wame-*qualify* kwenye kupewa pesa zao nydingine ambazo zitakuwa zinabaki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naomba Serikali itusaidie juu ya jambo kuongeza shilingi 50 kwenye maji. Hii shilingi 50 tunayoiomba tumeona kwamba ni njia pekee ya kutatua migogoro ya maji nchini mwetu kwenye maeneo mengi. Niombe sasa Serikali ilione hili na Bunge zima tukubaliane kwamba hii shilingi 50 ya maji itakapokuwa shilingi 100 inaonekana miradi mingi vijijini itaweza kukamilika kwa wakati. Kuna miradi mingi na visima vya maji vimesimama, tunadhani kwamba hii shilingi 100 inaweza kusaidia ku-*push* miradi mengi ya maji vijijini ikaweza kukamilika kwa wakati kabla ya 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii iende sambamba na vichoteo vya mifugo. Unapotengeneza mradi wa maji

unaweza kuweka na kichoteo cha mifugo kwa hiyo maji hayohayo binadamu watatumia upande mmoja na upande mwingine mifugo inapata maji. Kwa hiyo, kwenye vijiji vyetu pale ambapo wakulima na wafugaji wetu wapo wote wata-enjoy mradi uleule ambao uwezo wa pampu ni huohuo, matenki ni yaleyale, ni kiasi cha kuweka tu mbauti kwa ajili ya mifugo na yenye we ikapata maji ili kupunguza adha ya wanayoipata wafugaji na kusumbuana kwa kwenda kwenye maeneo mengine au kufanya *double projects* kwenye maeneo wakati sisi tunahitaji pesa ziweze kusaidia maeneo mengi wakati hatuna pesa za kutosha. Kwa hiyo, nadhani hiyo programu inapokuwepo basi kwenye miradi ya maendeleo mikubwa kuwepo na programu ya kutengeneza mbauti kwa ajili ya mifugo halafu miradi yote iende sambamba, binadamu atumie maji lakini na mifugo yetu iweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze kwa Bwawa la Dongo. Muda mrefu tumeahidiwa Bwawa la Dongo kwamba linakwenda kujengwa, mwaka jana kwenye bajeti lilikuwepo na mwaka huu lime-*appear* tena. Naomba nisaidieni hili bwawa lijengwe, programu ianze, wekeni *fund* kwa sababu tuna shida kubwa sana katika Vijiji vya Rogoiti, Laiseri, Dongo na vijiji vingi ambapo kanda ile yote ni kame lakini vijiji hivyo vinakwenda mpaka upande wa Dodoma kwa maana ya upande wa Kongwa; vijiji hivyo vinakwenda mpaka upande wa Gairo, Morogoro. Bwawa hilo ni *potential* kwenye kanda hiyo wa sababu litasaidia maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti yenu mnaainisha vijiji 19 lakini ni zaidi ya tarafa nne zitakazohudumiwa na bwawa hilo. Zaidi ya vijiji hamsini vitapata maji kutokana na bwawa hilo kwa sababu unaweza kuendelea kufanya *extentions* kwa kuunga mabomba kwa sababu litakuwa ni bwawa kubwa sana na litatosheleza maeneo hayo. Tunataka tuombe sasa Serikali ichukue *initiative* ianze kujenga hili bwawa angalau basi miaka miwili, mitatu inayokuja basi bwawa liwe limekamilika ili Gairo, Kiteto

na Kongwa wapate maji tuweze kupunguza adha ya maji kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wetu wa Kibaya muda mrefu ni wa ukame lakini maji tunayo chini. Tunaomba Serikali itusaidie jambo moja, tunaomba *DDC* waje watumie maji kwa sababu tunayo, watuchimbie na yaungwe kwenye *tanks* ambazo sasa hivi zinajengwa ili tuweze kutosheleza ule Mji wa Kibaya kwa maji tuwe tumpunguza adha ya maji kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunayo maeneo kame kwa mfano Kata za Makame, Ndido, Rorela, ni maeneo ya wafugaji lakini maeneo yale hayana shida kubwa sana ya maji kwa maana ya maji chini ya ardhi, maji chini ya ardhi yapo, tunachotafuta sisi ni wataalam wa kuweza kuja kuchimba yale maji kwa wakati, mita ni zaidi ya 100, 150 unapata maji. Kwa hiyo, tulitaka *surveyors* na *team work* ya Wizara ije kufanya ile *survey*, ijiridhishe halafu inaweza kutuchimbia kwa awamu angalau na sisi wananchi wetu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo lingine moja la miradi ya maji ambayo haikamiliki na mmeona Rais kila wakati anapotembea analalamikiwa maji, tumekuwa na wakandarasi ambao hawamalizi kazi kwa wakati. Naomba kuishauri Serikali, kama kweli Wizara ya Maji mko *serious* kumaliza huu mgogoro, tuumalize hivi, wakandarasi wote kwenye kila wilaya ambayo Rais anakanyaga wawe pale waeleze miradi ya maji wamefanya lini, wamemaliza lini, miradi inatoa maji au haitoi, waachane na Rais palepale. Waende kwenye *site* Rais anapofanya ziara akiuliza miradi ya maji wao wasimame washike *microphone* waeleze, maji yapo, hayapo aachane nao hukohuko magereza ili tupunguze utapeli wa wakandarasi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakandarasi wengi inaonekana kwamba ni kifo cha pesa kwa sababu unapotandaza bomba chini kwenye ardhi anakuja anakwambia mimi bomba niliweka, haya, uthibitisho

mtachimbuu mita 300, 400, mtachimbuu kilometra? Sasa kuna uongo na udanganyifu mwingu, anaweza kuwadanganya kwamba aliweka bomba kumbe hakuweka. Sasa mimi naomba ili tumalize ubadhirifu wa pesa za Serikali kwenye miradi ya maji, kila Rais anapokanyaga waende, waseme maji yapo au hayapo waachanie magereza Rais aendelee na safari zake uone kama miradi ya maji kwa wananchi haitapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ndiyo ushauri wangu kwa Serikali, sasa hivi tuamue. Miradi inayoendelea kwenye Wilaya yangu mkandarasi kama hajatoa maji hajapokelewa mimi na yeye tutamalizana mtasikia. Ninyi mmewalea sana na mmesababisha uharibifu mwingu wa maisha ya binadamu na upotevu wa pesa nydingi za Serikali kwenye miradi mingi ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mradi wa Matui, Naibu Waziri tulikubaliana kwamba uje Kiteto ukaishia Simanjiro. Njoo Matui uangalie mradi wa shilingi milioni 600 zimeteketea, hakuna maji, watu wanakimbizana, kichoteo ni kimoja, maji hayapatikani. Sasa uje tuamulie pale Matui, tusiache kuzungumza suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki miradi viporo Kiteto, sitaki migogoro, miradi ambayo imeanzishwa kwa sasa hivi ninalsimamia na inatoa maji, ile ya nyuma njoo tumalizane kulekule ueleze wananchi imepotelea wapi, imefia wapi, umeamua nini. Njoo wewe na wakandarasi nikukabidhi wananchi uwahutubie uwaambie kwamba wanapata lini maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba aniahidi ni lini tunakwenda Kiteto, mambo mengine yamekwisha. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa fursa ya kuchangia jioni hii juu ya jambo muhimu sana kuliko mambo mengine, maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema maneno yangu, Mheshimiwa Waziri, Profesa, pamoja na mdogo wagu Mheshimiwa Aweso, mimi sina matatizo na ninyi bali Serikali. Kwa sababu hapa ndani wakati mwengine Wabunge tunazungumza inaweza ikaonekana kama tuna matatizo na Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema maji ni uhai. Mawaziri mnisikilize vizuri, maji ni uhai. Waheshimiwa Wabunge, hebu tujaribu wiki yote moja hii tule bila kunywa maji tuone itakuwaje, hapo ndio tutakapoju maji ni uhai. Sasa ukishakuona ndugu na jamaa zako wanakutenga na maji, hawa wana mawasiliano na Mwenyezi Mungu afungue lango la mbinguni ili wewe uende kule maana yake hawataki upate maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Ulyankulu tumetengwa na nitaendelea kusema mpaka siku ya mwisho. Alikuja Makamu wa Rais, unajua wanasiasa unaweza ukaanza kusema lolote, mtu mmoja akasema Ulyankulu ni mbali kwa hiyo maji yasiende, ajabu kabisa hii. Sasa kutoka Tabora kwenda Ulyankulu yaani kuingia kwenye Kijiji cha Kadutu kilometa 60...

**MBUNGE FULANI:** Ni mbali sana.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Ni mbali hiyo? Kutoka Tabora kwenda Urambo kwa Mheshimiwa Mama Sitta ni kilometa 94; kutoka Tabora mpaka Kaliua ni kilometa 120, hapo ni karibu sana; kutoka Kahama kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kishimba pamoja na Mheshimiwa Kwandikwa kuingia kwenye Jimbo langu la Ulyankulu ni kilometa 80, bado watu wanasema Ulyankulu ni mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna miradi miwili, mradi wa kwanza unatoa maji Ziwa Victoria, hawataki ufile Ulyankulu. Kwa sababu maji Kahama yapo yangeweza kuletwa Ulyankulu watu wakatulia, Tabora yatafika lakini hata maandishi tu ya kupeleka maji Ulyankulu hayapo. Tuna mradi wa maji Malagarasi, hapo sasa nadhani ndipo

hatutaelewana, maji ya Malagarasi yanatoka Ulyankulu lakini mradi huu umeandikwa maji yatakwenda Kaliua na Urambo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tulikuwa tunakutana Kaliua na Profesa akija kwenye ujenzi. Kuna picha moja ya Chuck Norris walikuwa na kamanda mwingine hivi wakapotezana kwenye ile filamu. Siku ya mwisho kamanda yule anamwambia Chuck Norris *we meet again*, sasa Mheshimiwa Profesa tumekutana tena. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa alikuwa anakuja nakupokea Kaliua nikawkambia Ulyankulu mpaka uwe na dhamira ya kwenda Ulyankulu, sasa maji mimi sina. Sasa huu mradi wa Malagarasi maji yanatoka Mto Igombe Ulyankulu, sasa niwaambie tu, kama hamtatupatia maji watu wa Ulyankulu tunakwenda kuziba mto halafu mje mniweke ndani mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila jambo Ulyankulu inatengwa. Sijui na kwenye maji mtasema wakimbizi. Jamani hebu kuweni na huruma wakati mwingine. Hatupendi kusema Mheshimiwa Profesa, hebu tupeni maji muone, tutatulia. Maji yanawezekana, kilometra hizo nimesema lakini kama nilivyosema, mtu anasimama kwa Makamu wa Rais unadanganya yaani ili kuhakikisha tu watu wa Ulyankulu hatupati maji. Mheshimiwa Profesa na Naibu wako fanyeni mnaloweza tupate maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tutatengwa kwa kila jambo? Tuna mradi wa bwawa pale Kijiji cha Ichemba, wameshakuja wametembeatembea sijui ndiyo upembuzi, lakini wamekwenda moja kwa moja hatujui itakuwaje, wananchi bado wana tataruki kwa sababu hawajajua mradi ule utapita kwenye mashamba gani ya watu. Kwa hiyo, hatuna shida nyingine zaidi, kama kila huduma ya Serikali hailetwi Ulyankulu mimi siwezi kujua, sijui tatizo ni Kadutu, sijui kama kweli ni wakimbizi au ni nini, hata maji? Hivi mtu anaweza kuja nyumbani kwako akakuomba maji kikombe

kimoja, utamnyima? Huwezi kumnyima, tupeni basi maji.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hamtaki kutupa tawala za mikoa tupeni maji tu tutaishi. Kama hamtupi maji hatuwezi kuishi. Maana ninyi mna mawasiliano na Mwenyezi Mungu, tutaona sasa nani mwenye mawasiliano na Mwenyezi Mungu na lango halitafunguliwa, hatutakufa sisi, tutakuwepo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nilisema *last week* na kama alivyosema Mheshimiwa Ndassa, tunakuwa na hoja mahsusini moja, tusipende kuchanganya na mimi sijapenda kuchanganya. Bahati nzuri wataalam wako hapa nyuma yangu, wajue tu tutaleta vagi hata wenyewe hawatakanyaga huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa John Kadutu, tunaendelea na Mheshimiwa Lucia Mlowe.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lucia Mlowe na Mheshimiwa Maftaha ajilandeae.

**MHE. LUCIA M. MLLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya. Pili, naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu nikianza na fedha za maendeleo kwenda kidogo. Nikiangalia mwaka 2015/2016, fedha za maendeleo zilizokwenda ni asilimia 28; mwaka 2016/

2017 zilikwenda asilimia 25 na mwaka 2017/2018 zilikwenda asilimia 22. Ukiangalia huo mtiririko unaona kabisa Wizara hii inazidi kwenda chini na kwamba wananchi watazidi kupata matatizo siku hadi siku badala ya kwenda juu inakwenda chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kwenye ripoti ya CAGinaonesha kwamba fedha zilizokwenda kwenye Bodi ya Mabonde ya Maji ambapo zilipangiwa kwenda shilingi bilioni 49.5 kwa mwaka 2016/2017 lakini zilikwenda shilingi bilioni 6.6 tu, sawa na asilimia 13 tu. Fedha ambazo hazikwenda ni shilingi bilioni 42.9, sawa na asilimia 87. Tukiangalia mwaka uliofuata wa 2017/2018 kati ya shilingi bilioni 38.4 zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilikwenda shilingi bilioni 7.2 tu, sawa na asilimia 19 ya bajeti yote ya mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, je, Serikali ina dhamira kweli ya kumtua mama ndoo kichwani? Kwa sababu tumekuwa tukiimba kwamba Serikali inataka kumtua mama anayetaabika ndoo lakini kwa mtiririko huu tutafika kweli? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia upotevu wa maji, ni mkubwa sana ambao umesababisha hasara ya shilingi bilioni 47.18. Ukiangalia mikoa 15 yenye upotevu wa maji ambayo imeoneshwa kwenye ripoti ya CAG, tukianza na Mkoa wa Njombe ambao inaonesha hapa kiasi cha upotevu wa maji kisichokubalika shilingi milioni 196.2. Tukija Mwanza ni shilingi milioni 677.52 na mikoa mingine imedorodheshwa hapa ambayo jumla yake inakuja shilingi bilioni 47.18. Wakati huo huo tunaongelea juu ya uhaba wa maji. Upande mwingine tunaona upotevu wa maji upande mwingine tunaona uhaba wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweke mfumo ambao utasaidia kupunguza upotevu huu wa maji. Niishauri Serikali wale wanaokwenda kusoma mita za maji basi wawe na wajibu wa kuhakikisha wanaangalia mabomba au miundombinu ambayo inatoa maji ambayo

inavujisha maji kwa sababu kuna upotevu mkubwa sana wa maji, nikianza hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakaa kisasa nimeshawasilisha hii hata mwaka jana kwamba kuna mabomba yana tiririsha maji na nimeenda kuripoti mara nydingi huko kwenye mamlaka ya maji *DUWASA* juu ya upotevu wa maji huu, lakini ukija siku inayofuata unaona maji bado yanaendelea kutiririsha, sasa kama hapa Dodoma ipo hivi hayo maeneo mengine inakuwaje? Kwa hiyo niombe Serikali ifuatilie suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni suala la wateja kutokuwa na mita za maji kuna wateja wengi ambao hawana mita za maji matokeo yake, unakuta bill zinakadiriwa juu na mtu anaendelea kutoa bili hizi maana hajawi sasa nitoe mfano halisi mimi wazazi wangu walkuwa kila mwaka wanatozwa pesa nydingi sana mwaka huu nikashtuka nikasema haiwezekani hizi bili ni kubwa sana nikaenda kufuatilia, nikakuta hawana mita nikawauliza watu mamlaka ya maji kwanini hamjawawekea mita hawakuwa na chakuwaeleza, kwa hiyo niombe Wizara ifuatilie suala hili kuhakikisha wateja wote wanapata mita za maji, kusudi watu walipe hela kwa uhalali wasizidishiwe na wala isiwe chini zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uhaba wa maji kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malizia kengele ya pili hiyo.

**MHE. LUCIA M. MLLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niombe Wizara ifuatilie suala hili kwa sababu kuna maeneo ambayo tulikuwa tukiimba kila siku hapa kwamba tunaomba maji kwa mfano kuna kijiji cha Itengelu huko Wanging'ombe huko nyuma walikuwa wanamaji mengi tu kwenye bomba mpaka mabomba toka mabomba yamekufa sasa hivi wanahangaika hawa wananchi wanachota maji machafu kwa kilometra nydingi naomba Wizara ifuatilie suala hili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucia, Mheshimiwa Maftaha baadaye Mheshimiwa Hussen Amar ajilandaye

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya njema niweze kuzungumza machache yanayohusu maji hasa katika jimbo langu la Mtwara mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya tano kwa kuwa na maji mengi ardhini leo hii, ni jambo la ajabu sana mpaka leo tunazungumza suala la maji, maji, maji, Tanzania kwamba tuna maji wakati ukichimba hata chini ya Bunge ndani yake huko kuna maji mengi kabisa maji baridi kabisa.

Mhrdhimies Mwenyekiti, kwa miaka mitatu hivi sasa kuna miradi mingi tumekuwa tunalzungumza miradi ya maji ya maji kwa mfano; mradi wa kwanza ambao ni mradi mkubwa sana tulielezwa ndani ya Bunge mwaka 2016 kwamba Serikali inataka kujenga Mradi mkubwa wa maji ambao utatatua kero ya maji katika majimbo ya Mtwara mjini, Jimbo la Mtwara vijijini na Jimbo la Nanyamba na huu mradi ni mradi wa kutoa maji mto Ruvuma kule Kitaya wenye gharama shilingi bilioni 200, mpaka leo huu mradi aujahanza na tulielezwa wakati ule kwamba huu mradi ni fedha za kutoka Benki ya Watu wa India Exim Benki ni mkopo lakini mpaka leo hatuelewe huu mradi umefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kila mwaka unawekwa kwenye bajeti, kila mwaka unaelezwa kwenye vitabu vya bajeti kwamba kuna mradi mkubwa wa kuboresha majiji ikiwemo mji wa Mtwara, Mtwara Mjini lakini pia wilaya zile zingine ambazo nimeweza kuzitaja. Sasa tulikuwa tunaomba sana kwamba wakati huu mwaka huu ni mwaka wa nne sasa tunaenda tunahitaji miradi hii mikubwa iweze kutekeleza fedha zake ziweze kuletwa kwa ajili ya kuweza wananchi wetu kuondokana na tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine tulikuwa na mradi wa maji pale Mtwara mwaka jana zilipelekwa bilioni

tano kasoro hivi huu mradi, ni mradi wa kutoa maji kutoka kule Kata ya Jangwani eneo la Lwelu na lengo lake ni kusambaza maji maeneo yale ambako mtandao wa Bomba haujafika. Sasa huu mradi nataka kumueleza Mheshimiwa Waziri hapa kwa sababu, Waziri hakuwepo wakati huu mradi tunaanza lakini Naibu Waziri alikuwe kwamba huu mradi wale wahusika wa maeneo yale ambapo visima vimechimbwa na tunashukuru kwamba tulifanya *pump test* maeneo yale maji yakapatikana mengi sana pale Lwelu, lakini kuna maeneo ambapo lile bomba limeweza kuitishwa lile bomba limepita mule wale wananchi wa maeneo yale mashamba yale hawajapewa hata senti tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepigiwa simu sana wananchi wa maeneo yale wamenijia nyumbani zaidi ya mara kumi mara ngapi wakakaa wananiambia kwamba Mheshimiwa Mbunge tunataka utufikishie kilio chetu kwamba tunahitaji maji kweli wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini, lakini huu mradi wa bilioni tano inakuwaje kwamba Serikali imeleta huu mradi wamechukuwa mashamba ya watu wamechimba visima wamepitisha bomba lakini hawajapewa hata senti tano wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakaniambia Mheshimiwa Mbunge utufikishie kwa Mheshimiwa Waziri na nikaongea na Mheshimiwa Prof. Mbalawa nikamueleza Mheshimiwa Waziri tunakufahamu kwa utendaji wako mzuri ukiwa kwenye Wizara ile ya Mawasiliano ulikuwa unafanya kazi nzuri sana nilikueleza suala hili kwamba wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ambapo huu mradi umepita hawajapewa hata senti tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujuwa naomba kuuliza hivi ni kweli kwamba wananchi wakipelekewa mradi eti kwa sababu wanashida ya maji hawa watu hawapewi fidia japo mashamba yao yamechukuliwa maeneo yale yamechukuliwa siyo kweli Mheshimiwa Waziri tunaomba Mheshimiwa Waziri ule mradi wa Lwelu ambapo unaenda kupeleka maji kwenye maeneo ya Kiolo maeneo ya Mbalawa chini kule, Magomeni,

Chipuputa, Mitembo na maeneo yote ya Jimbo la Mtwara mjini hawa wananchi lile pomba lilipita wananchi walipwe fidia yao kwa sababu ni haki kulipwa fidia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa ninaomba kuzungumza siku nyingi tuna pitia taarifa kwamba Serikali imedhamiria kuondoa tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam na nizungumze tu kwamba sisi Wabunge wote ni wadau wa mji wa Dar es Salaam na sisi Wabunge la Kusini hasa hasa ni wadau wa maeneo ya Mbagala, maeneo yale ya Chamazi kule ndiko tunakoishi tukifika Dar es Salaam. Sasa haya maeneo yanatatizo la maji sana na kila mwaka inawekwa kwenye mpango kwamba tuna visima yya borehole ambayo vinachimbwa kule kibiji na maeneo mengi lakini inazungumzwa tu kila mwaka kuna visima visima. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mtandao wa maji haujengwi kupelekwa maeneo ya Rangi Tatu, kupeleka maeneo ya Chamazi, kupeleka maeneo ya Mbagala kiujuimla wake tunahitaji watu wale wa Dar es Salaam wapate kweli maji kwa sababu pale Kimbiji kuna maji mengi sana sana huu ni mwaka wa tatu tunapitia taarifa kwamba visima vimeandaliiwa, visima vitapeleka maji lakini utekelezaji haupo Mheshimiwa Waziri tunaomba kwamba maeneo haya yapelekewe maji safari hii, hii miradi isiwe kizungumkutu kwamba inazungumzwa inatajwa inatajwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa naomba kuzungumza hapa ni mradi wa Makonde, huu mradi ulijengwa na wakoloni mwaka 1953 na wananchi wa Wilaya ya Tandahimba, Jimbo la Nanyamba, Newala Kiujuimla wake, wanashida ya maji sana, sana, pale Mtwara na huu mradi ndiyo suluhisho lakini kila mwaka inazungumzwa fedha zinazopelekwa ni fedha chache kila mwaka inaelezwa hapa kwamba tumetenga fedha kwa ajili ya kurekebisha mtandao maji yapo pale Makonde yapo mengi sana, lakini tatizo ni serikali kupeleka fedha ili yale Mabomba ili yaweze kurekebishwa na mashine iweze kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunaambiwa mashine iliamishwa kwenye mradi huu miaka hiyo ya nyuma iliamishwa mashine na kupeleka maeneo mengine sasa naomba kujuwa sisi wananchi wa kule wananchi wa Mtwara hatupaswi kutumia mashine ile ili tuweze kupata maji kwa hiyo, tunaomba Serikali kwa sababu Serikali ndiyo yenyewe ilifanya *blunder* ya kuondoa mashine ya mradi wa Makonde watenge fedha za kutosha ili wananchi wa Tandahimba, Newala, Nanyamba na Mtwara Vijijini wapate maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mfumo wa maji taka kwamba kumekuwa na baadhi tu ya mijii hapa Tanzania ndipo huu mfumo umeweza kurekebishwa au umeweza kutengenezwa. Lakini maeneo mengi ya mijini Tanzania huu mfumo wa maji taka ni mfumo muhimu sana kwa sababu, mfumo wenyewe wa watu wanavyoenda kuchimba vyoo vyao vile halafu hali inakuwa ni mbaya vikijaa inakuwa hali mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi hawana fedha ya kukodi maboga kila siku kwenda kuondoa maji taka tunaomba sasa Serikali kuanzia Mji wa Mtwara Mjini hakuna kabisa huo mkakati yaani Serikali haituelezi. Nimekuwa nauliza kila mwaka hapa kwamba kwanini Serikali haiweki mfumo wa maji taka katika Mji wa Mtwara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi pale Mtwara Mjini tuko karibu na bahari sana gharama yake inakuwa ni ndogo na tunavyojuwa mfumo wa maji taka kwenye maeneo yenyeye vyazo maji vikubwa kama Bahari ya Hindi mifumo inaelekea huko baharini, kwahiyo tunaomba Serikali safari hii itenye kiasi cha fedha Mheshimiwa Waziri unanisikia Mheshimiwa Naibu Waziri unapiga kazi sana tunakusikia tunaomba mfumo wa maji taka Jimbo la Mtwara Mjini kwa sababu sisi tumekuwa tukipata shida sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba kuzungumza ni hili suala la wakala, wa wachimbaji wa visima wa ujenzi wa mabwawa. Mheshimiwa

Waziri amezungumza vizuri sana hapa kwamba kuna huyu wakala, lakini jambo la ajabu huyu wakala ukitaka kuchimba kisima chochote kile hata ukiwa wewe ni Mbunge ukaenda ukawaeleza kwamba tunahitaji kuchimba kisima gharama wanazokupa ni kubwa sana na wananchi wa kawaida wanakuwa hawawezi kuwa-*ford*, kchukua hizi gari ambazo ni wakala wa Serikali gharama zake zimekuwa ni kumbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati fulani nilikuwa natafuta maji Mtwara Mjini nikaenda kuwaeleza hawa mawakala lakini gharama walizonipa ilikuwa ni kubwa sana hata kama ni Mbunge niliweza, yaani sikuweza kuwa-*ford* zile gharama kwa hiyo watu wa kawaida, inakuwa ni hatari zaidi. Kwa hiyo, naomba kwa sababu lengo la Serikali ni kuwasaidia wananchi wa Tanzania, wananchi wa vijijini waweze kupata maji maeneo ambako hakuna vyanzo vya maji, lakini hizi gari za wakala zinaweza zikachimba visima virefu na visima vifupi gharama ziwe nafuu ili wananchi waweze kuwa-*ford*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Maftaha. Tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Hamad, baadaye Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa afya njema. Lakini pia napenda nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri niwponceze pia watendaji wote wa Wizara ya Maji. Pia nipende kuiponceza Serikali kwa kututengea pesa katika bajeti hii nimeona ukurasa 123 tumeweza kutengewa karibu 900,066,000.8. Lakini pia nipende kuishukuru Serikali kwa kuwalipa wakandarasi wetu zaidi ya bilioni 1.7 na sasa hivi tayari wapo kazini naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo cha ajabu ni kwamba Serikali ilitutengea mradi huu mkubwa wa

kutoka Nyamtukuza kwenda Bukwimba mradi huu ultengewa zaidi ya bilioni 15. Mpaka sasa hivi zimeshatoka takribani bilioni nane lakini cha ajabu kazi inavyoenda mpaka sasa hivi ninavyoongea hakuna hata tone moja ambalo linatoka la maji na mradi huu unagusa vijiji vinane, vijiji hivi ikiwa ni kutoka kule Nyamtukuza kwenye chanzo cha maji, panaitwa Nyamtukuza kupita Kakola, Kitongo, Ikangala, Kalumwa, Izunya, Kayenze na Bukwimba lakini mpaka leo hii hata tone moja la maji halijatoka.,.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pamoja na kutoa fedha zaidi ya bilioni nane ebu jaribuni kufuatilia mkaangalie huu mradi, huu mradi tangu mwaka 2010 naupigia kelele tangu 2010 mpaka leo hii mradi huu haujatoa hata maji kidogo. Bahati nzuri hata Mheshimiwa Mbalawa kipindi kile alikuwa Waziri wa Maji nimeenda naye mpaka kwenye chanzo cha maji. Waziri Mkuu amefika kule kwenye chanzo cha maji, eeh! Ndiyo kipindi kile alichokuwa waziri maji tumeshawahi kwenda naye, Mheshimiwa Eng. Kamwele tumekwenda naye mpaka kule na baadhi ya viongozi mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha ajabu kuna mdudu gani ambaye anasababisha maji yasitoke nakuomba Mheshimiwa Waziri kwenye Bunge hili kabla ya kuhisha twende pamoja ukaone tatizo ni nini kwa sababu wananchi wa Nyangwale wanashida kubwa sana ya maji, mradi huu bilioni nane hata tone la maji halijatoa kwanini. Kwa hiyo, naungana kabisa na Wabunge wenzangu kwamba ufuatilaji unakuwa ni mdogo, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba utakapokuja hapa uniambie ni lini mimi na wewe tuondoke twende tukaangalie huu mradi tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze Serikali kwa mradi wa pamoja na Bulyang'ulu Acacia mradi huu ambaو umegharimu takribani bilioni 13 naishukuru sana Serikali kwamba tayari imeshatenga fedha na wakandarasi wapo kazini mradi huu unatoka kwenye bomba kuu linalokwenda Kahama kwenda Irugi. Nimepata takribani vijiji saba ambavyo vitapitiwa na mradi huo kwa kweli

naipongeza Serikali mradi huo utakapokamiliaka basi baadhi ya vijiji hivyo saba ambavyo nimevitaja vinaweza kupata maji, ambavyo ni vijiji vya lyugwa, Tarumwa, Mwamakiriga, Izunya, Kavita pamoja na Lushimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia hili suala kwa uchungu sana ni kwanini kwa sababu kila ninaposimama miaka yote nazungumzia huu mradi wa Nyamtukuza, leo nazungumza taratibu sana mnielewe, sitaki kuzungumza kwa kasi na kwa haraka nizungumze taratibu mnisikilize vizuri, naomba Waziri twende pamoja tukaangalie mradi huu nini ambacho kinakwamisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimeona kwenye kitabu chako Serikali kwamba Serikali ya Oman na Serikali ya Tanzania wamekubaliana kuchimba visima mia moja, katika visima hivi ambavyo vitachimbwa kwenye shule za msingi na sekondari na Wilaya ya Nyang'hwale naomba basi niangaliwe angalau sekondari nne ambazo zinashida sana maji kama vile Nyang'hwale sekondari, Msalala Sekondari, Bukwimba Sekondari, Mwingiro Sekondari naomba angalau nipate visima vinne hivi ambavyo tunachangiwa na Serikali ya Oman. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bwawa moja kubwa sana ambalo lipokule Kata ya Shabaka kijiji cha Nyamgongwa, bwawa lile lilikuwa kubwa sana na lilikuwa linanufaisha zaidi ya kata tano bwawa limeshaaribika takribani miaka thelathini na tano miundombinu yake imearibika lakini manufaa makubwa yalikuwa yanapatikana kwenye lile bwawa. Wananchi wengi walikuwa wakilima bustani walikuwa wakivua samaki, walikuwa wakilima kwa kumwagilia na manufaa mengine mbalimbali yalikuwa yanapatikana kwenye hilo bwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa ninaomba basi itengwe pesa kwa ajili ya kwenda kulitengenezea miundombinu bwawa lile liweze kuwasaidia wananchi, wananchi waweze kupata maji na kujipatia mapato, lakini pia mifugo kuweza kupata maji. Kwa hiyo, naomba katika

bajeti hii angalau itengwe hiyo pesa kwa ajili ya hilo bwawa la Shabaka kijiji kimoja kinaitwa Nyamgongwa ambako amezaliwa ndugu yetu nimemsikia yuko hapa anaitwa Luhemeja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia baada ya kuyasema haya kuna kisima kirefu ambacho kimechimbwa katika Kata ya Nyangwale, Kijiji cha Nyang'hwale kisima kina miaka kumi na moja, miundombinu pale ilishakamilika Jengo lipo pump ipo, lakini cha ajabu maji mpaka sasa hivi hajaanza kusukumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu sana kufuatilia halmashauri wanasema wao hawana fedha kuna upungufu kidogo. Nilikuwa naiomba Serikali ikaiuangalie huo mradi ukamilishwe ili huo mradi uweze kusaidi kupunguza tatizo la maji katika Kata ya Nyang'hwale lakini pia vijiji vingine ambavyo viro pale jirani kwa sababu ni kisima kirefu na kinamaji mengi sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mchango wangu ni huo hauna maneno mengi kikubwa nakuomba tu ukautembelee mradi wangu wa Nyang'hwale ili uweze ku-pump hiyo hela na kuangalia tatizo nini ili sasa na mimi wananchi wangu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein tunaendelea Daimu Mpakate halafu Mheshimiwa Julius Kalanga ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi jioni hii kuchangia hoja ya Wizara ya Maji. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama, lakini nitakuwa sina fadhilila niwashukuru wadau walionisaidia Jimbo la Tunduru Kusini kwa kuwataja kuchimba vya maji, nikianzia na *Help for Under Reserved Community* ambao wamechimba visima 74 vya maji virefu kwa gharama ya kila kisima shilingi 650,000 kitu ambacho ni kikubwa kwetu gharama ya visima vinaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niwashukuru Kanisa la Anglicana, Dayosisi ya Masasi, kwa kupertia Mradi wa CHIP wao wamechimba visima virefu vyta maji 24 ambavyo vinawasaidia wananchi wangu kuweza kupata maji salama. Tatu, nawashukuru Taasisi za Kidini za Firdaus na Istiqama wao wamechimba visima 60 kwenye Jimbo langu bure bila hata senti tano. Kwa hiyo nawashukuru sana wamesaidia kuondoa kero ya maji kwa asilimia kubwa katika maeneo yangu. Kwa hiyo ukiangalia katika Jimbo langu, hawa wadau wamechimba visima zaidi ya 200 ambavyo vimesaidia kupunguza kero ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda moja kwa moja kwenye hoja, naomba nimshukuru sana Waziri. Waziri pekee aliyekanyaga kwenye Jimbo langu, kaenda kwenye Mradi wa Mtina na kwenye mradi wa Mbesa. Mradi wa Mtina alitoa maagizo, mradi ule unaendelea vizuri kidogo, lakini kuna matatizo mawili, matatu ambayo yametokana na kutokuelewana kati ya Mkandarasi na Mhandisi wa Maji. Katika mchoro wa ule mradi ulionesha kwamba watatumia *solar panel* 16 na kutumia *battery* 32. Ushauri wa Mkandarasi alishauri kwamba tutoe *battery* 32, wanunue panel 16 jumla ziwe 32 ambazo zitakuwa na uwezo sawa na kuwa na *battery* 32 ili waweze kusukuma maji. Matokeo yake Mhandisi alivyokataa imeonekana maji hayapandi ipasavyo kwa hiyo wakati wa kifuku kama sasa wananchi wale hawapati maji. Kwa hiyo tunaomba Wizara iingilie kati ili yule Mkandarasi aruhusiwe kununua *panel* zingine 16 ili maji yaweze kupatikana kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Waziri alivyokuja Mbesa alitoa ahadi ya kuchimba kisima kirefu kimoja, kile kisima mpaka leo hakijachimbwa. Naomba sana afuatilie ile ahadi yake iweze kutekelezeka wananchi wa Mbesa pamoja na kuwa watu wengi sana lakini wana shida kubwa ya maji. Maji Mbesa ni tatizo kubwa sana, Waziri mwenyewe amefika, Mradi ule wa Benki ya Dunia mpaka leo maji hayafiki kwenye lile tenki kubwa, limekuwa ni tatizo kubwa sana. Hata *feasibility study* iliyo fanyika maji yanaishia kwenye tenki na pesa kwa ajili ya kugawanya maji kwenye vijiji bado

haijaweza kupatikana. Kwa hiyo naomba Waziri afuatilie ile ahadi yake bado haijatekelezwa na wananchi wanaendelea kupata shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni suala la wafanyakazi wa Idara ya Maji, kwa upande wa Tunduru ina shida kubwa sana. Mwaka jana mwaka wa fedha 2017/2018, tulipata fedha kwa ajili ya kukarabati visima vya *DANIDA*. Vile visima vya *DANIDA* vingi vimejengwa miaka ya 80 na 90 na ndivyo vinavyowasaidia karibu maeneo mengi ya Jimbo la Tunduru Kusini, lakini kutokana na ongezeko la watu vile visima vimeshindwa kutosheleza mahitaji ya watu na vimezeeka. Mwaka jana tulipata fedha kwa ajili ya kukarabati visima 25, kwa milioni tatu kila kisima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya tatizo la wataalam mpaka leo vile visima vyote, walinunua vifaa lakini havifanyi kazi. Vifaa vimenunuliwa, wamekwenda kuvifunga, naamini kutokana na ujuzi na namna fulani ilivyofanyika vile visima mpaka leo havitoi maji pesa imeondoka. Kwa hiyo tuna tatizo kubwa la watumishi katika idara yetu hasa Mhandisi nina mashaka naye kwa sababu miradi mingi ameshindwa kuisimamia. Hata hawa wahisani niliokuwa nawashukuru walikuwa na mkataba na halmashauri kwa ajili ya kusimamia, watoe gari, watoe mafuta, watoe mfanyakazi, lakini wameshindwa kufanya hivyo, tumekaa vikao mara chungu nzima, lakini imeshindikana. Mpaka leo bado anaendelea kufanya kazi halmashauri kwa upande wa Idara ya Maji wameshindwa kusimamia. Kwa hiyo naomba kwa kuwa Idara ya Maji sasa iko chini ya Mheshimiwa Waziri, awasiliane na huyu Mhandisi, kwa kweli ni kero, ni shida, ameshindwa kusimamia kutekeleza miradi ya maji katika Jimbo la Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda sana kuliongelea ni suala la maji kwa vile vijiji vilivyopo kandokando ya Mto Ruvuma. Kuna vijiji takriban 10, kuna Vijiji vya Amani, Mkalachani, Misechela, Liwanga, Mkapunda na Makande, vyote hivi vipo pembezeni mwa Mto

Ruvuma, lakini hawa watu wana shida kubwa sana ya maji, maji yako kilomita nne, tatu, tano. Kwa hiyo hawana visima vya maji, wanategemea kuchota maji mtoni, mara nydingi watu wanapata shida sana wanakumbana na mamba kule watoto wanakwenda na maji, wanakuwa na maji kutokana na shida ya maji. Naomba kama Serikali yetu inajali watu wetu kama tunavyozungumza kila siku basi tuanzishe mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwa ajili ya hivi vijiji vilivyopo pembezoni mwa Mto Ruvuma ili hili kero ya maji iweze kuondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, sio kwa umuhimu, naomba kwenye vile vijiji vilivyokuwa kwenye miradi ya Benki ya Dunia kwa mfano Mchoteka na Namasakata. Vile vijiji vilioneckana havina vyanzo vizuri vya maji kulingana na utafiti, lakini ukweli vyanzo viro. Tunaomba basi ule mradi urudi tena ili vile vijiji viweze kupata maji ya kutosha kwa sababu Mchoteka peke yake ina vijiji vine, umati ulioko pale ni zaidi ya watu 8,000, wanategemea visima vinne tu ambavyo kila kijiji ina kisima kimoja. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tulikuwa na nia nzuri ya kuweka Mradi pale wa Benki ya Dunia, lakini utafiti ulifanywa shaghalabaghala, haukuweza kutosheleza mahitaji yale, naamini kuna andiko lilipelekwa Ofisini kwa Mheshimiwa Waziri tangu 2017 kutokana na utafiti ulifanyika na Mhandisi wa Maji aliyekuwepo kipindi kile, lakini mpaka leo lile andiko halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na andiko hilo kuna andiko la Namasakata, nacho Namasakata ni kijiji kikubwa sana, nacho tulikuwa na andiko ambalo thamani yake ilikuwa ni milioni 180 tu ambavyo ingeweza kusaidia kupata maji ya uhakika kutokana na utafiti ambao ulifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa kuna mradi wa Amani. Naishukuru sana Serikali ule mradi umeweza kusaidia vijiji vitatu, lakini maji yale ni mengi, mabomba yanapasuka kila siku nilipeleka Ofisini kwa Mheshimiwa Waziri andiko la kuongezea vijiji vitatu ili kuweza kuondoa tatizo hili la kupasuka mabomba kila siku kutokana

na presha kubwa ya chanzo cha maji ambayo yanakuwa supplied katika mradi ule. Lile andiko liko ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, lina thamani ya milioni 300 tu ambalo lingeweza kusaidia kuondoa hilo tatizo la kupasuka mabomba yale kila siku ili kuweza kuwahudumia wananchi wengine wa Misechela, pamoja na Liwanga ambao wanateseka na wanashida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daimu. Mheshimiwa Julius Kalanga, baadaye Mheshimiwa Jitu Son ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwanza nimshukuru mwenyezi mungu, kwa kuendelea kutupa afya njema na kutufikisha katika siku ya leo. Nitumie nafasi hii pia kuishukuru sana Wizara ya Maji kwa jinsi ambavyo wameshughulika na matatizo ya Watanzania. Mnyonge mnyongeni lakini ukweli Wizara ya Maji chini ya uongozi wa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wao wanajitahidi sana kuhangaika na miradi ya maji pamoja na changamoto nydingi ambazo wamekutana nayo katika miradi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Bunge hili likakumbuka kwamba matatizo mengi yaliyoko Wizara ya Maji, hawa waliopo sasa wameyarithi, matatizo haya yalikuwepo huko nyuma, lakini Wizara kwa kweli wanajitahidi kuhakikisha kwamba tatizo la ubadhirifu wa miradi ya maji linaondoka. Tunawapongeza, kwa kweli si rahisi sana kukubali kwa sababu kule Jimboni kwangu kuna tatizo lakini kazi wanafanya tunawatia moyo waendelee kufanya kazi vizuri. Tunampongeza sana Profesa kwa jinsi ambavyo anawasaidia kutimiza majukumu yao na uzuri ni kwamba hawakai ofisini kila siku tunawaona huko na huko wakikimbia kuangalia matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu kama Bunge ni kuwasaidia Wizara kutafuta fedha na kuzipata kwa ajili ya kutekeleza miradi yetu. Kama Bunge hili hatutashauri namna ya kupata fedha, tutakuwa tunalalamika habari ya maji lakini hatutatatu tatizo, ndio maana naungana na walioomba kwamba tunawasaidia Wizara wafanye kila namna katika chanzo chochote wapate shilingi hamsini kwa ajili ya kuboresha Mfuko wa Maji. Hii ni faida kwao na lawama hizi za Wabunge za matatizo ya maji wataepukana nazo, kama watakubali ushauri wetu kwamba tukubali kutafuta chanzo chochote, sio lazima kwenye mafuta, mahali popote watakapoona inafaa tupate fedha kwa ajili ya kuboresha Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila Mbunge akisimama hapa anapongeza Wizara ya Nishati lakini ni kwa sababu wao wamepata chanzo cha uhakika cha fedha, ndio maana tunaona *REA* inapeleka umeme vijijini na watu wote wanapongeza. Kwa nini Wizara hii nao wasipate vivu wa kutafuta namna ya kupata hiyo shilingi hamsini ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya miradi hii ya maji. Kwa hiyo, naomba ile shilingi hamsini waone kwamba ni nia njema ambayo inaweza ikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili niwashukuru kwa kutoa kibali cha miradi miwili Monduli. Mradi wa Meserani na Mradi ule wa Nanja. Nampongeza Naibu Waziri alikuja Monduli alituahidi na sasa nimepata taarifa kwamba wamepata *approval* kwa hiyo miradi hiyo miwili inaweza kuanza wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, ukiangalia katika Wizara ya TAMISEMI wamefanikiwa sana katika miradi yao ya ujenzi wa vituo vya afya na wamefanikiwa kwasababu wametumia *Force Account* na kipindi hiki tunao wasomi wengi, ma-engineer wa maji walioko vijijini ambao hawana ajira. Kwa nini tusiwe na mradi wa kutumia *Force Account* katika miradi mingi ya maji ili kule kijijini tuokoe fedha tunazopeleka kwa Wakandarasi, fedha kidogo tunazopata tununue vifaa

wataalam wetu wazalendo walioko vijiji ni watasimamia miradi hiyo. Kwanza utakuwa umewapa ajira, lakini vilevile umeokoa fedha nyangi ambazo zingeenda kuwa faida ya Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule chini wananchi wanaweza wakachimba mitaro, wananchi wanaweza wakafanya kazi ndogongogo, halafu tukapata miradi mizuri kwa bei nafuu, kwa nini tusitumie mfumo huu wanaotumia TAMISEMI kujenga vituo vya afya, kutekeleza miradi ya maji kuliko kupeleka fedha *billions of money* kwa Wakandarasi ambao wame-prove failure na kila siku tunasumbuana nao kwa kuchelewesha miradi. Ni kwa nini Wizara wapokee lawama hiyo, tupeleke miradi hiyo kwa wananchi, kwanza itafanya *ownership*, wananchi watamiliki miradi yao na tutaokoa fedha nyangi kwa sababu wananchi watafanya kazi nyangi na hawa vijana wetu wanaomaliza Vyuo Vikuu, watatoa taaluma *technical* katika miradi hiyo na tutaokoa fedha nyangi. Kwa hiyo naomba, Waziri walione hilo, tutafute miradi ya *pilot* tuanze ili tufanye namna ya kuokoa fedha zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, naomba nishauri pia katika eneo hili la maji, miradi mingi ya maji hakuna mradi ambao uko chini ya milioni 800, 700 lakini ukiangalia watu wengi wanalamika unamaliza mradi leo, ukija kesho mradi huo hautoi maji. Mradi unakamilika leo kisima kesho hakitoi maji na kama kinatoa maji kinatoa kwa kiwango cha chini. Hivi ni taaluma gani inayofanya tathmini ya kujua hapa maji yapo na ni chanzo cha uhakika ambapo baada ya miezi miwili, mitatu mradi kukamilika, miradi haitoi maji.

Kwa hiyo ni muhimu tukafanya tathmini ya miradi yote nchi nzima kufahamu ni miradi mingapi inatoa maji na mingapi haitoi, kwa sababu takwimu za wataalam kwamba asilimia 80 mjini wanapata maji si kweli, miradi mingi imekamilika lakini haitoi maji, maana yake wananchi wa maeneo hayo hawapati maji. Tufanye *review* ya miradi ili tuwe na takwimu sahihi ya kiwango gani cha Watanzania wanaopata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya hasa katika majimbo ya vijiji na naomba Serikali itambue kila siku naona miradi mikubwa ya wafadhili inafanyika mijini, sisi watu wa vijiji ambao uwezo wa kupata maji hata iwe mita 400 wametuweka wapi. Hii si sawa, wafadhili wanatoa fedha mijini kwa sababu wana *interest*, sisi ambao tuko vijiji nani mwenye *interest* na sisi ambao hata sisi hiyo mita 400 wanayozungumza kuchota maji, sasa tunafuata maji kilomita tano na wakati mwingine hatupati maji hayo. Kwa hiyo tutazame kwa jicho la huruma majimbo ya vijiji, hali ya wananchi wetu ni mbaya sana na ndio walipakodi na ndio watu wetu waaminifu wakati wa uchaguzi, lakini tumewaacha nyuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukatambua kama wafadhili wanatusaidia mijini, Serikali ijielekeze kusaidia majimbo ya vijiji angalau sisi tukipata maji ndani ya kilomita moja bado ni faida, achana na hao wa mjini wanaosema mita 400, mita 400 ni ndani ya kiwanja chako sisi tunafuata kilomita 10 na bado maji yenewe hatuyapati. Kwa hiyo, Wizara itusaidie ni kwa namna gani ambavyo tunaweza kutatua changamoto hii, kwa kweli hali ya maji katika maeneo yetu ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niombe jambo moja, nimekuwa nikisikia visima vya *DDC* kila siku, mimi sijawahi kupata hata kimoja, walau leo ikimpendeza Mheshimiwa Waziri wanipe hata vine, hii si sawa. Mwaka juzi niliona, mwaka jana nimeona, mwaka huu naona lakini kwangu siaona hata kimoja na sisi tuna maeneo machache yenye maji, wanipe vijiji vizima vinne kule Mswakinini kule Makuyuni, nitaondolewa kwenye tatizo la maji, lakini kila siku wanagawa *DDC* mimi wameniweka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alikuja Monduli akasema hatanipita nami nimesema nikisimama mahali popote, akiniambaia niombe jambo moja, wanisaidie kutatua tatizo la kero ya maji katika Jimbo la Monduli. Wakinisaidia hayo, hayo mengine naweza nikasubiri, lakini nimewaomba hili moja tu la maji, kuhakikisha tunatatua tatizo

la maji katika Jimbo letu. Juzi nilikuwa na Katibu Mkuu, akasema Majimbo mawili ambayo yana kero kubwa ya maji Arusha ni Ngorongoro na Monduli, basi watuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu hiki naona tu Majimbo mengine Longido, wapi, watutaje basi na sisi ili na sisi tujisikie kuwa ni sehemu ya mafanikio ya mradi na ya Wizara yetu. Naomba kwa unyenyekevu watuangalie kwa jicho la huruma, hali ya maji kwenye Jimbo la Monduli ni mbaya sana na mabwawa mengine mengi yamepasuka, tulikuwa na mabwawa 51, leo yanayofanya kazi hayafiki kumi, tutapata wapi sisi maji?

Naiomba Wizara itusaidie, kwa kweli ninaomba nione huruma yao wakati wa kuhitimisha bajeti, wanatuongezea shilingi ngapi na wanatusaidia nini visima vingapi ili kuondokana na kero ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimekuwa nikienda sana pale Wizarani, pale Wizarani inaonekana watumishi wengi wanakaimu, kwa nini tusiwape nafasi hiyo kama wanatosha ili waweze kufanya kazi? Tusipende tu kuwalaumu, lakini pale ambapo ni stahiki zao wawape idara, wawape nafasi wanazokaimu ili waweze kufanya kazi vizuri, wanakaimu kule wilayani, wanakaimu Makao Makuu, wawathibitishe kama wanatosha ili tuweze kupima katika utumishi wao, hatuvezi kuwapima kama hatujawapa majukumu kamili ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabisa naomba wakati wa mwaka wa fedha unaokuja, tunatamani Wizara ituambie tatizo la maji katika maeneo mbalimbali ambayo hatuna vyanzo vyya uhakika vyya maji kwa nini Serikali isitengeneze utaratibu hata wa uvunaji wa maji ya mvua kwenye maeneo yale ili wananchi wetu waweze kupata maji na waondokane na tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kalanga. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni, baadaye Mheshimiwa Dua William Nkurua ajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya kuchangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa kazi nzuri inayofanya, vile vile niwapongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake ya wataalam wote kwa kazi nzuri wanayofanya. Pia niishukuru Serikali kwa kukubali kuanzishwa kwa Wakala wa Maji *RUWASA* yaani chombo ambacho kitakuja kusaidia na kuondoa kero zote ya maji, tunaamini hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kwenye *RUWASA* ni kuwa na chanzo cha uhakika cha mapato ambapo itakuwa inatekeleza miradi. Huku kote tulikuwa tunalalamika kwamba miradi inasimamiwa vibaya, miradi imesanifiwa vibaya naamini *RUWASA* wakianza, wataanza na wataalam walibobea wataalam wazuri na kutakuwa na usimamizi mzuri. Kwa hiyo *RUWASA* tunaamini itakuwa sawa na *REA* kwa upande wa maji. *REA* imepata mafanikio makubwa kutokana na usimamizi mzuri, lakini pia upatikanaji wa fedha wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, leo hii tumepata Sh.50 ambayo tulitenga kama Bunge kwa ajili ya kwenda kwenye Mfuko wa Maji. Kwa sehemu kubwa bilioni 106 ambayo ni sawa na asilimia 67 ya fedha iliyotakiwa kwenda ya bilioni 158 ndiyo fedha ya Mfuko wa Maji. Fedha ya bajeti ya kawaida ni bilioni 333, bilioni 443 ni asilimia 17 tu iliyendo yaani bilioni 43 ndiyo zimeenda. Sasa ukizijumlisha zile zote mbili ya Mfuko wa Maji iliyendo na bajeti ya kawaida iliyendo, bado hajafikia fedha zote ingekuwa imepatikana asilimia 100 ya Mfuko wa Maji ambayo ni *ring fenced*. Sasa tunapoomba iongezwe shilingi 50 iwe shilingi 100 au tutafute na vyanzo vingine iwe ni kwa kutokana na mitandao yaani kutokana na *DART* au *EWURA* au vyanzo vingine zikipatikana

bilioni 150 nyingine ya ziada itakuwa tunapata karibu bilioni 300 na ndiyo fedha zote zilizoenda leo kwenye miradi yote ya maji ya fedha ya ndani, ya nje yote jumla imeenda bilioni 343 ambayo ni asilimia 51 tu ya fedha iliyotengwa kwa ujumla wake. Kwa hiyo sehemu kubwa ya hii fedha ni huu Mfuko wa Maji lakini pia Mfuko wa Maji unapeleka maji mijini pamoja na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni vizuri tukaboresha Mfuko huu ukapatiwa, tusiogope kuweka hata hiyo ya mafuta watu ambao wanasema italeta *inflation*. Kipindi hicho bei ya mafuta imeshuka mpaka Sh.1,400, hakuna nauli iliyoshuka, hakuna bidhaa iliyoshuka wala hakuna kodi ya ziada, walikusanya kutoka kwa wafanyabiashara waliopata *super profit* kutokana na hiyo bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mfuko huu wa Maji unapeleka maji mijini na pamoja na vijijini. Ni vizuri tukaboresha mfuko huu, tusiogope kuweka tozo kwenye mafuta ambapo watu wanasema italeta *inflation*. Kipindi bei ya mafuta yameshuka mpaka 1,400 hakuna nauli au bidhaa iliyoshuka bei wala hakuna kodi ya ziada mlkusanya kutoka kwa wafanyabiashara waliopata *super profit* kutokana na bei hiyo. Sisi kama Wabunge tutawaelimisha Watanzania kwamba tumefanya hivyo ili wapate maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu sana ni suala la uvunaji wa maji ya mvua na mito ili tuweze kuyatumia vizuri. Kwenye hilo la uvunaji wa maji tulishapitisha sheria kwamba majengo yote yanayojengwa mijini na sehemu nyingine kama huna mfumo wa kuvuna maji basi usipewe kibali cha kujenga. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia huko tunapopoteza maji mengi kwenye mito na maji ya mvua, Serikali iondoe kodi kwenye mitambo ya kuchimba maji na kutengeza mabwawa. Siyo lazima kila kitu kifanywe na Serikali mitambo ikiwa ya bei nafuu wananchi wa kawaida (*private sector*) itawasaidia kujenga mabwawa kwa bei nafuu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaposema tumtue mwanamke ndoo kichwani ni vizuri Serikali ikaondoa pia kodi kwenye *solar pumps*. Leo hii miradi mingi ya maji ambayo inatumia *diesel* au umeme, wananchi vijiji ni wanashindwa kulipa bili tungetumia *solar pumps*. *Solar pumps* ukileta leo ina kodi lakini *solar pump* hiyo hiyo ukileta kwa njia ya irrigation haina kodi, ni *controversial*. Anayetaka kuleta *pumps* kwa ajili ya umwagiliaji haina kodi ila ukileta kwa ajili ya matumizi ya kawaida ina kodi. Ni vizuri Serikali ikaweka msimamo ikaondoa kodi jumla ili hata yule mwananchi wa kijiji *pump* hiyo imsukumie maji mita 400 sawa na yule wa mjini inawezekana ikidhamiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hizi mashine za kuchuja maji (*water purifiers*? Mkiondoa kodi kwenye *water purifiers* bajeti ina maana tunayotumia zaidi ya shilingi bilioni 45 ya kutibu magonjwa ambayo yanatokana na maji hiyo pesa tungeweza kuitumia kupata maji safi na salama, ni bora kukinga kuliko kutibu. Kwa hiyo, tungeweza huku kuondoa kodi ndiyo utapoteza kidogo lakini ile shilingi bilioni 45 unayopeleka kwenye afya utaweza kuiokoa na wengi wanaopata shida hiyo ni watu wanoishi vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye mitambo ya kuchimba maji, nchi zote za Afrika Mashariki hazina kodi isipokuwa Tanzania. Kwa wale wakandarasi wakubwa ambaao wanaleta vifaa vya kuchimba maji pamoja na *Drilling and Dam Construction Agency* wote wanapata msamaha wa kodi lakini mwananchi wa kawaida akitaka kuleta mashine yake moja hata kama ni mtumba bado anatozwa kodi ndiyo maana gharama za uchimbaji maji zimekuwa kubwa na uvunaji wa maji umekuwa mgumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo Wakala wa Maji katika maeneo mbalimbali katika wilaya ambazo zina Bodii ni vema tungeziunganisha. Kwa mfano, Bodii moja inaweza kuhudumia wilaya tatu, nne hata mkoaa mmoja kwa sababu ndiyo tutapata ufanisi kuliko kila kata na tarafa kuwa na Bodii yake ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukajipanga na naamini tukijipanga vizuri haya yote ambayo tunayazungumza tutafanikiwa. Maeneo mengi ambapo mashine zinatumia *diesel* au umeme tufunge *solar* na hasa katika taasisi mbalimbali za Serikali. Tukiweza mifumo hiyo gharama ya uendeshaji itakuwa ndogo na pia upatikanaji wa maji ni mwingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haya maji tusipoyavuna ndiyo yanakwenda kuharibu miundombinu ya barabara na reli. Tukiweza kuvuna maji hayo na tukayatumia vizuri tutapata maji ya kunywa, ya umwagiliaji na mabwawa ya kufugia samaki na pia tutaweza kuzalisha zaidi hata maji ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tunalopata uzalishaji wetu unakuwa mdogo hata upande wa umwagiliaji kutokana na kwamba hatuna vifaa vya kuchimbia mabwawa haya. Ondoeni hiyo kodi kidogo wenye kustahili kupata msamaha tayari wanapata ni hao wachache wachache ndiyo hawapati. Kwa hiyo, mngeruhusu hata kwa *private sector* pia maana itaweza kusaidiana na Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tozo mbalimbali ambazo zinachajija na Mabonde kwa watu ambao wanatumia maji. Ni vizuri tukaangalia zile chaji katika Mabonde yote bei zifanane. Ni vizuri tukawezesha haya Mabonde zikasaidia upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwininge ambao naomba Serikali izingatie, leo hii kwa sehemu kubwa tumeanza kutumia maji ya ardhini lakini hatujawekeza hata shilingi moja wala hatuna asilimia hata moja ambayo inaenda kwenye kutunza vyanzo vya maji na maeneo ya *catchment* (vidaka maji) ambavyo *vita-recharge aquifer* za kule chini. *Tusipo-recharge* zile *aquifer* baada ya muda hata hivi visima ambavyo leo tunapata maji kwa mita 80 mpaka 100 tutakuja kujikuta tunatafuta maji kwa mita 200 au 300 ambapo hatutakuwa na uwezo wa kutoa hayo maji huko

chini. Kwa hiyo, suala la mazingira nashauri Serikali kwenye kila mradi ambao tunaanzisha angalau asilimia moja ya fedha yote mradi iende kwenye kutunza mazingira, kuboresha vyanzo vya maji na vidaka maji (*catchment area*) ili tuweze ku-recharge aquifer za huko chini ili tuweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali ni moja ingeangalia bajeti tunayotumia upande wa afya kutibu magonjwa yatokanayo na ukosefu wa maji lakini vifo vinavyotokea kwa kutumia maji machafu na ambayo siyo salama, hayo tungeweza kuepuka kama tutaondoa baadhi ya kodi. Najua Serikali inasita kuondoa hizi kodi kwenye *water purifier* kwa sababu tutakosa kodi kwenye viwanda zinavyouza maji ya chupa lakini ni vizuri tukose kodi hiyo afya ya Watanzania iwe salama haswa huko vijiji ambapo sehemu kubwa tunakosa maji. Tukiboresha huduma za maji, umeme kama inavyoenda sasa hivi na miundombinu huko vijiji hakuna mtu yuko tayari kukaa mjini kwani maisha ya vijiji ni mazuri. Tukiboresha huko vijiji watu hawatarundikana mijini na kukosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kuboresha huduma mbalimbali huko vijiji na maji ni uhai na maji ndiyo maisha, kwa hiyo, kilimo mifugo, uvuvi haya yote tunaweza tukafanikiwa kama Wizara hii ya maji itashirikiana na kuratibu masuala mbalimbali ya namna ya kuboresha miundombinu ya maji kwa njia zote, iwe ni uvunaji wa maji na kusimamia. Pia Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha zikae pamoja ili kuangalia na kuondoa baadhi ya hizi kodi ambazo zitakuwa ni chache sana.

Mimi naamini kwa *data* ambazo tunazo ni kodi kidogo sana ambazo tutapoteza kutoptana na msamaha tutakaotoa ambapo *multiply effect* yake hii mitambo yote ikiletwa kwa bei nafuu watu wengi sana watachimba maji wenywewe na itaisaidia Serikali maana siyo lazima kila kitu kifanywe na Serikali. Kwa hiyo, dhana nzima ya *PPP* (*Public Private Partnership*) tutakuwa tumeifikia kama *private sector* na Serikali watashirikiana kufanya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji kama ilivyo Babati MJINI ndiyo hivyo hivyo ilivyo katika wilaya zote Tanzania. Hakuna sehemu yenyewe nafuu, iwe mjini au vijijini kote kuna tatizo la kubwa la maji. Hakuna mahali hata huko mijini unawenza kufungua bomba la maji ukanywa yale maji bila uhakika kama ni safi au salama kwa sababu upatikanaji wa maji ni jambo moja lakini maji safi na salama ni jambo lingine. Kwa hiyo, ni muhimu tupunguze bajeti ya kwenye matibabu turudishe huku kwenye maji hata namna ya kutibu maji ili Watanzania wapate maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika Serikali hii ni sikivu huu ushauri ambaao tumeutoa kwa muda wote huu mtauzingatia vizuri na haswa hii ya kuongeza bajeti ya Mfuko wa Maji ili iweze kufika agalau shilingi bilioni 350 maana pesa yote iliyoenda kwa ujumla wake ni shilingi bilioni 343. Kwa hiyo, ingekuwa tumeongeza mwaka jana au mwaka juzi badala ya shilingi 50 iwe 100 ungekuta pesa yote asilimia mia moja ingetokana na huo Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tujue hii miradi mingine, iwe ni mradi wa zile fedha za Exim Bank ya India au fedha nyiningine tunayopata kutoka kwa wafadhili mbalimbali halengi Watanzania wote bali inaenda kwenye *specific project*. Kama ni miradi ya miji 28, kama ni ule Mradi wa Ziwa Victoria yaani ni miradi ambayo imetengwa na imechaguliwa, je, sisi ambaao hatuko kwenye hiyo miradi tunapata wapi hiyo bajeti na ukiangalia ni shilingi bilioni 41 tu ndiyo imeenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima muweke utofauti kati maji mjini na maji vijijini. *Percent* kubwa ya Watanzania wanakaa vijijini, kwa hiyo, asilimia kubwa ya fedha inatakiwa kwenda vijijini. Ni sawa na hii ya *TANROADS* na *TARURA* ilivyowekwa kwamba asilimia 70 ni ya *TANROADS* na asilimia 30 ni *TARURA*, hapa pia kwenye huu Mfuko wa Maji asilimia 20 ndiyo iende mjini na asilimia 80 iende kuwasaidia Watanzania wanaoishi vijijini kwa sababu huko ndiko kwenye shida kubwa ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tutumie *E-water*. Mfumo wa *E-water* itasaidia maji kupotea na ni eneo ambapo Serikali itaweza kukusanya mapato yake kabla. Hata kama ni zile Kamati za Maji zinazosimamia gharama ya usimamizi wa maji inakuwa ndogo, Serikali itaendelea kupata unafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuendelee kuboresha vyuo vyetu ambavyo vinafundisha hawa wataalam wa maji na naamini kabisa *RUWASA* ndiyo itakuja kuwa mkombozi wa sekta ya maji Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Tunaendelea na Mheshimiwa Dua Nkurua na Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Tunza Malapo wajiandae.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya kutoa mchango wangu katika eneo hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa ushauri au mchango wowote, nitumie fursa hii kuwashukuru sana viongozi wa nchi, hii hasa Jemedari wetu Rais wetu mpwendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na viongozi hasa Waziri wa Maji, Naibu na watendaji wote wa Wizara ya Maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuizungumzia Nanyumbu kwa sababu tuna shida kubwa sana ya maji kwenye Wilaya yetu ya Nanyumbu. Nanyumbu tunaposema hatuna maji tafsiri yake ni kwamba hata maji ya kuokota ni shida. Kuna watu kijiografia tumekaa sehemu mbaya hata maji ya kuokota hayapatikani. Katika vijiji vya Nanyumbu tunapofika mwezi Juni maji yanakuwa ya shida sio ya bomba wala siyo hayo mnayosema maji bora sisi ya kuokota yanakuwa shida, tunapata sana shida ya maji hata ya kuokota, hata oga yetu inakuwa ya shida. Waziri

ninapomwambia Nanyumbu kuna shida ajue kwamba hata maji ya kuoga ni shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa mkakati wake wa kuondoa shida ya maji katika mji wetu wa Mangaka ambapo ndipo Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu. Pale Mangaka tuliiomba Serikali itupatiate maji kutoka chanzo kikubwa cha maji cha Mto Ruvuma, nashukuru Serikali ilifanya upembuzi yakinifu lakini baada kukamilisha ripoti Serikali ikabaini kwamba gharama ya kutoa maji kutoka Mto Ruvuma mpaka Mangaka ambapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ni kubwa sana na ikaja na utaratibu wa kuyatoa maji kutoka Mbwinji kuleta Mangaka. Mimi kama Mbunge naishukuru sana Serikali kwa wazo hili zuri na naona jitihada ya Waziri namna ambavyo anakamilisha mchakato huu ili maji yaweze kupatikana pale Mangaka Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida na hilo lakini ombi langu la kwanza. Naomba Mchakato huu uende kwa spidi nzuri Mheshimiwa Waziri, muda hautusubiri, 2020 ni kesho na mimi wananchi wangu walitaka maji. Natamani sana wakati wa kipindi changu maji hayo yaanze kufanyiwa kazi. Mheshimiwa Prof. Mbarawa nakuamini na nina mategemeo makubwa kwamba suala hili utalikamilisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kutoka Mbwinji kuja Nanyumbu sheria inasema kilomita 12 kutoka kwenye bomba kuu vijiji vyake vitapata maji. Naomba suala hili lizingatiwe katika kulishughulikia tatizo la maji pale Mangaka kwa sababu tuna vijiji vingi sana kutoka kule mpakani mwa Masasi na Nanyumbu mpaka kufika Mangaka. Kwa hiyo kama sheria itazingatiwa vijiji vingi vya Mangaka, vya Wilaya ya Nanyumbu vitakuwa vimepata maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushukuru hilo ambalo nina matumaini makubwa muda si mrefu mradi utaanza, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba kuna baadhi ya maeneo, ingawa tuna shida kubwa sana ya

maji lakini tumetofautiana kutokana na eneo na eneo. Kuna Kata za Mnanje na Maratani, kata hizi zina shida kubwa sana ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Juni Mheshimiwa Waziri ukija Maratani hutaoga kwa sababu kuna shida kubwa sana ya maji, vyanzo vyote vya maji vinakauka. Pia ukija kwenye Kijiji cha Michiga ni kikubwa sana na kina watu wengi sana lakini hakina maji hasa inapofika mwezi Juni na kuendelea. Kwa hiyo, naomba sana katika mipango ya baadaye na mimi nitakaa na Waziri nitatoa mapendekezo ya maeneo ambayo tunatakiwa tupeleke miradi kwa haraka kabla ya vijiji vingine kutokana umuhimu na shida ya eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji haya yakifika Mangaka tulikuwa na matumaini makubwa sana ya kutoka Mangaka mpaka Masuguru ambako kulikuwa na chanzo cha Mto Ruvuma wangepata maji yale ya kwanza. Kwa mabadiliko haya vijiji hivi ni kama wamekumbwa na butwaa. Nitakaa na wewe tupendekeze namna ya kuweza kushughulika na vijiji hivi ili tuondoe tatizo kubwa la maji katika vijiji hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kwanza twendeni tukachimbe mabwawa, tunayaacha maji yanakwenda mtoni na baharini. Bahati nzuri bado maji ya mvua yanapatikana lakini tunashindwa kuyadhibiti ili wananchi wetu waweze kupata haya maji. Kwa hiyo, nashauri sana Serikali iwekeze kwenye uchimbaji wa mabwawa aidha ya umwagiliaji lakini pia ya upatikanaji wa maji ya kunywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maliasili kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Maige yupo hapa aliahidi kusaidia maji kwenye Kijiji cha Masuguru na Kijiji cha Chinika aliahidi kutoa shilingi milioni 6. Mpaka leo nashindwa kukaa vizuri hapa Bungeni, wananchi wanankumbusha pesa ile, pesa ile ilitolewa ahadi na Serikali ya Awamu ya Nne. Mimi nataka iende pesa *cash*, Halmashauri itaongezea

tutachimba visima, ahadi hii ni ya Serikali inatutia aibu sana. Serikali ya Awamu ya Nne aliahidi Mheshimiwa Ezekiel Maige na bahati nzuri nilikuwepo pale wakati ahadi inatolewa. Naomba sana unisaidie Mheshimiwa Waziri wa Maji kuikumbusha Wizara ya Maliasili wasisahau deni hilo wananchi wanakumbuka. Kama ninyi mmesahau lakini wananchi hawajasahau. Naomba sana ulitilie mkazo suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri, kutoka Mto Ruvuma mpaka walau Makao Makuu ya Tarafa ya Nanyumbu, Tarafa yenye ya Nanyumbu si mbali sana. Makao Makuu ya Wilaya ya Mangaka tunategemea maji kutoka Mbwinji lakini tuna uwezo pia wa kuanzisha mradi mdogo kutoka Mto Ruvuma mpaka kwenye Kijiji cha Nanyumbu ambako ni Tarafani pia tukaweza kusaidia kutoa maji kusaidia vijiji ambavyo vimezunguka ile Tarafa ya Nanyumbu. Tukifanya hivyo, nina hakika sana Wilaya ya Nanyumbu itakuwa imepata maji ya kutosha na hatimaye kero ya maji itakuwa haipo. Vijiji vingine sisi kama Wilaya tumejipanga namna ya kuweza kusaidia kwa sababu Halmashauri ina mtambo wa kuchimba visima virefu, basi tunaendelea kupunguza baadhi ya vijiji ambavyo vina shida ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, sisi Nanyumbu tuna pesa ya kuchimba mabwawa mawili, moja kwenye Kijiji cha Maratani na lingine kwenye Kijiji cha Namasogo. Taratibu zote kama Nanyumbu tumekamilisha ni ngazi ya Wizara inatuchelewesha na mvua zimeanza kuisha na ni vizuri mabwawa yakachimbwa kipindi ambacho mvua hainyeshi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja hapa hebu nipe matumaini na wananchi wasikie, hizi pesa utazipeleka lini maana mkandarasi ameshapatikana, tunataka tu utoe *go-ahead* kazi ianze ili wananchi wa Kata ya Maratani na Namasogo wapate maji kama ambavyo Serikali ilikuwa imeahidi kushughulikia tatizo lao la maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye ushauri sasa kwa sababu nimeweza kuyapunguza machache

yanahusu Nanyumbu. Watu wengi sana wanaongelea hapa kuongeza nguvu ya Mfuko wa Maji. Mheshimiwa Waziri hayo unayokwama nayo hufanyi makusudi, huna fedha, lakini chanzo kikuu ambacho tumekiona hapa ni ile shilingi 50 ya kwanza, Wabunge wanapendekeza tuongeze, kuna ugumu gani Serikali kutusikiliza sisi Wabunge? Sisi tumechaguliwa msituone hivi, tumeaminika. Kama kuna hofu tutawaambia wananchi wetu kwamba hakuna kitu cha bure duniani ni lazima tufunge mikanda. Mimi naomba sana Serikali kubalini mawazo ya Wabunge, twendeni tuongeze shilingi 50 kwenye mafuta ili Mfuko wa Maji utune. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti iliyopita ya 2018/2019 mpaka leo una asilimia 51 tu ya pesa, tunajifunza nini hapo? Ni kwamba uwezo wetu wa kupambana na hii kitu bado ni mdogo lazima tuongeze nguvu. Nitashangaa sana ukija hapa Mheshimiwa Waziri usikubaliane na mawazo yetu, nitakushangaa kweli. Una muda, kaa na wenzako ambaao mnakaa nao huko na ambaao wana hofu, Wabunge ambaao ni wawakilishi tumekubali tutakwenda kuwaeleza wananchi, sisi ndiyo tunakaa nao wale ninyi hofu ya nini? Serikali, sikieni hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vyanzo vingi mbali ya mafuta kuna simu. Mtu mmoja alisema hapa, hivi mtu akiona kwamba umenunua vocha ya Sh.1,000 akaona Sh.20 imeeda kwenye maji wananchi watakasirika, vingapi tunachangia wananchi wasikasirike? Maji ni shida kubwa kwa wananchi wetu tena wanyonge hawa ndiyo zaidi.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa, muda wako umeisha. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri mawazo yangu yamesikika vizuri, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Komu na Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa wajiandae.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nakushukuru kunipa nafasi kuchangia hii Wizara, ambayo kwa kweli ni Wizara nyeti, ni Wizara muhimu sana, ni Wizara ambayo kwa kweli inasimamia uhai wetu. Maana yake hali ya maji, isipokuwa nzuri hatuwezi kuwa na Kilimo kizuri, hatuwezi kuwa na hali nzuri ya hewa, hatuwezi kuwa na mazingira mazuri na kwa kweli hatuwezi kuendelea. Kwa hiyo, ni jambo la muhimu sana sana kuzungumza haya mambo ya maji na kuyazungumza katika hali ya umakini wa hali ya juu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba nimemiskiliza Waziri vizuri, nimesikiliza Kamati na bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa hiyo nafahamu vizuri, niseme kwa kweli, kwamba bado hatujawa *serious* vya kutosha katika kuwekeza katika maji, kwa sababu ukiangalia tu kitakwimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi asilimia 51 ambazo tunazzungumza, tunazungumza bilioni 106 ambazo ni fedha zinatokana na ule mfuko wa maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika fedha za ndani, za vyanzo vingine ambazo ni bilioni 284, tumetoa bilioni 48 tu sawa na asilimia saba. Sasa ni vizuri Wabunge wakaelewa, na mtu mwengine yoyote anayeona kwamba tuna tatizo kubwa la maji, akaelewa kwamba hatuko *serious* kiasi hicho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama tumetenga pesa, halafu tunatoa asilimia saba, tunataka tufanye maendeleo ambapo viwanda vyetu vinategemea maji. Chakula chetu kinategemea maji, mazingira yetu yanategemea maji, hali ya hewa inategemea maji, halafu tunatoa asilimia saba *we are not serious*. Kwa hiyo nafikiri tuna tatizo hapa la vipaumbele vyetu, kupanga ni kuchagua najua

kuna matatizo makubwa mengi, ambayo tunataka kufanya, lakini tunalinganisha maji na nini? Katika nchi hii? Ni kwa nini hatuwekezi kwenye maji vya kutosha? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana, kwamba Waziri akija hapa na kwenye ukurasa wa 22 wa kitabu chetu hiki cha Kambi Rasmi ya Upinzani, tumesema fedha ya nje imetoka asilimia nne, ni kwa sababu randama inasema hivyo. Kwa hiyo, na Waziri akija hapa tumuombe, hizo bilioni 188 za nje, hata kwenye Kamati, kwa kweli hazikuletwaka wakati huo. Kwa hiyo, aje atuambie zimetoka wapi? Na zimekwenda kufanya nini kwenye hiyo miradi ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo na mbaya zaidi, leo pamoja na kwamba changamoto za maji zimeongezeka, lakini bajeti ya maji inapungua. Mwaka jana kwenye hii bajeti tunayoimaliza sasa hivi, tulikuwa na bilioni 673 kwa ajili ya maendeleo, safari hii ni bilioni 610 zaidi ya asilimia nane *drop* kwa hiyo unaweza ukaona, kwamba ni tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu zenyewe za Waziri hapo, inaonyesha kwamba nchi yetu sasa hivi iko kweye *red line*, kwenda kwenye nchi ambazo zina uhaba mkubwa wa maji duniani. Kwa sababu kiwango cha chini, ni meta za ujazo, 1,700 kwa mtu mmoja kwa mwaka. Leo sisi tuko kwenye 1,952 ukilinganisha na mwaka wa 1962 tulivyopata uhuru, tulikuwa 7,000 na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kuona ni namna gani, tunaenda kwenye *danger zone* kwa hiyo nilikuwa naomba sana, kwamba tuendelee kufanya jitihada. Sasa watu wamezungumza hapa, kwamba miradi inaenda kwa kusuasua na Serikali inachangia sana, wakati tunafanya ziara, tulikuta miradi haitekelezwi kwa sababu unakuta mahali ambapo kuna mradi unatekelezwa, mradi mkubwa mzuri unaohitajika sana lakini unaambiwa kwamba vifaa viko bandarini toka mwezi wa kumi na mbili mpaka mwezi huo

wa nne ambapo tulikuwa tunapita kwenye hizo ziara havijatoka, kwa sababu msamaha wa kodi haujatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini waliosaini Mkataba na wakasema kwamba kutakuwepo na msamaha wa kodi ni Serikali yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali saa nyingine inajishika mashati, tunaomba wafanye *coordination* na Mheshimiwa Jenista yuko hapa, awaratibu hao watu wake, ili tusije tukakutana kutana na hivyo vitu vya aina hiyo kwa sababu *implication* zake ni kubwa, miradi inachelewa na gharama zinapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana, hilo lizingatiwe, niende Moshi, kule kwenye Halmashauri ya Moshi, tunaambiwa kwamba hali yetu ya maji ni nzuri, nataka ni sema hali si nzuri, kwa sababu hiki kinachosemwa ni pamoja na miradi ambayo ilijengwa miaka ya sabini wakati wa Lucy Lameck wanasema bado inafanya kazi. Ukienda kule kwenye Kata kadhaa, Kata ya Kimochi, ukienda kule *old* Moshi, ukienda kule uru, (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo vyanzo vyenyewe vya maji vilishakauka. Kuna mito ambayo ndiyo ilikuwa ina kuwa *source* ya maji ilishakauka, kuna chemchem nyingine hazipo tena, mabomba yamechakaa, kwa hiyo, niombe sana, kwamba kama alivyozungumza, Mbunge mmoja hapa ifanyike *review* tuweze kujua hali halisi ya upatikanaji wa maji ukoje na tusipofanya hivyo tunajivuna leo kwamba tuna bajeti kubwa ya afya ni kwa sababu watu wanaugua sana, na magonjwa mengine yanasa babilisha na kutokuwa na maji salama. (*Makofi*)

**MHE. JOHN W. HECHE:** *Sixty percent ya ...*

**MHE. ANTONY C. KOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Moshi, kuna, na nitoe pongezi sana kwa Mamlaka ya maji pale Moshi, inaitwa MUWASA, inafanya kazi nzuri. Lakini

niwaombe sana Wizara, kwamba kuna madeni makubwa wanadai, Majeshi yetu, Chuo cha Polisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanadai Magereza zaidi ya bilioni mbili, walipwe hizi fedha. Ili waweze kufanya huu ukarabati ninao uzungumza, waweze kupanua maeneo mengine kupeleka maji. Tunao mradi mmoja sasa hivi ambao unatekelezwa kule, Kata ya mabogini, tunahitajia kama bilioni 1.8. Waziri ameshaniahidi kwamba wanapeleka hizo hela. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, hizo fedha ziende na tusingekuwa na tatizo kiasi hicho kama hizi fedha zetu ambazo Mamlaka yetu imeshatoa *service* kwa Serikali yenu halafu hamlipi? Kwa hiyo niwaombe sana kwamba mpeleke hizi fedha ili hiyo miradi iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Kamati imeshauri, Kamati yetu ya Kilimo, Mifugo na Maji imeshauri kwamba ni usanifu wa miradi inavyofanyika iwe *comprehensive* iwe inazingatia mambo yote ya muhimu kuwepo na *provision* kwa ajili ya maji taka. Kuwepo na *provision* kwa ajili ya fidia, kuwepo na *provision* kule maji yanakopita. Wale, hata kama haijengwi sasa hivi, lakini *designing* izingatie hilo. Ili kule maji yanakopita, kwa mfano tumeenda kule Arusha, kuna mradi ambao unatoka Jimbo la Siha kilomita 64 kwenda Jimbo la Longido, hapo katikati kuna watu wana uhitaji mkubwa wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hakukuwepo na *provision* yoyote kwa ajili ya kuwapa maji kwa ajili ya mifugo, na kwa ajili ya matumizi ya binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba huu mradi utakuwa hatarini siku zote, lakini ukienda pale Arusha Mjini kuna mradi mkubwa unatekelezwa, lakini ukienda kuangalia ni namna gani, *design* imezingatia *land acquisition* na kule mabomba ya maji taka yatakapopita unaona bado kwamba watu wana jikanyaga kanyaga. Ndiyo maana unakuta kwamba miradi mingi inaanza, lakini kwenye *process* unaambiwa kwamba usanifu ulikosewa na sasa mradi umepanda kutoka bilioni fulani mpaka bilioni

fulani, sasa ili tuondokane na hilo nafikiri ushauri wa Kamati uzingatiwe. Lingine ambalo tulilliona ni Kampuni moja kupewa miradi mingi kwa wakati mmoja, na matokeo yake, kunakuwepo na visingizio mbalimbali katika kuitimisha hiyo miradi na hili tatizo tulilliona pale Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo tuwaombe sana Mheshimiwa Waziri na watu wake, wafuatilie mambo kama hayo na wahakikishe kwamba hayajirudii. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Komu. Tunaendelea na Mheshimiwa Tunza Malapo, baadaye Mheshimiwa Godfrey Mgimwa ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea jioni ya leo, nina mambo machache tu, la kwanza nilichojifunza kwenye hii Wizara ya Maji, kuna matatizo makubwa mawili, tatizo la kwanza ni kutopewa fedha za kutosha kulingana na bajeti yao. Tatizo la pili, hata hizo pesa kidogo wanazopewa bado hawazitumii vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa maana ipi, ukiangalia tunapotembea na Kamati kwenye halmashauri nydingi unakuta miradi mingi ya maji inasuasua, usanifu mbovu sijui *pressure* ya maji ndogo, *DP* hazitoi maji, mtu, mfano tumeenda Mkoa wa Kagera zimejengwa DP kumi na saba, lakini tisa hazitoi maji, unajiuliza?. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu si wasomi? Wamesoma wanajua kufanya usanifu kwa nini haya mambo yanatokea? Lakini nilichojifunza ni kwamba watu hawako *serious* katika kufanya hizi shughuli hata hicho kidogo wanachokipata basi hawakitumii vizuri achilia kwamba nayo Serikali pia haiko *serious* kutoa pesa za kutosha, ili kuleta maji ya kutosha katika Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufanuzi kuhusu ile miradi ya vijiji kumi kila wilaya ambayo ilikuwa inafanya kupitia mikopo ya Benki ya Dunia, miradi mingi

haifanyi vizuri, kwa hiyo, nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie kama Tume aliunda imeona nini na inatatua vipi changamoto hii. Kwa sababu kama ni pesa za mkopo tutakuja kuzilipa kwa hiyo tulitaraji watu wafaidike na kuna tabia imezoleka. Wakijua Kamati inapita, basi maji watayafungua, ama Kiongozi anapita, maji wanayafungua. Kiongozi akiondoka anaondoka na maji yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni tabia mbaya watu wa maji, Wizara ya Maji, hiyo ni tabia mbaya, tunatamani tuone wananchi wetu wanapata maji siku zote, hatutaki mambo ya geresha, kwamba tu kwa sababu leo Rais anakuja basi maji yanatoka. Kwa sababu leo Kamati ya Bunge inakuja basi maji yanatoka. Hilo ni tatizo tumeliona na ninao mfano dhahiri tumeenda kule Karagwe na wakatuambia kwamba haya maji, mmekuja nayo ninyi na mtaondoka nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate ufanuzi kuhusu mradi wa maji kutoa maji Mto Ruvuma kuleta Mtwara mjini ambao ulikuwa ufaidishe vijiji 26 katika Jimbo la Mtwara Vijijini, naomba tu nipata ufanuzi kwanza ule mradi bado upo ama haupo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nikisoma katika hiki kitabu cha kwako Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 150 umesema kwamba Serikali itagharamikia imetenga bilioni moja, lakini mwanzoni tuliamiwa ule mradi utatekelezwa kutokana na mkopo kutoka Benki ya *Exim* ya China, *which is which?* Huu mradi bado upo, ama haupo? Na kama haupo ni kwa nini? Na kama upo utatekelezwa lini? Tangu nimeingia Bunge hili Kila nikisimama lazima niuongelee huu mradi lakini umekuwa unasuasua hatujui hatima yetu. Naomba tupatiwe ufanuzi wa kutosha ili kusudi sisi watu wa Mtwara tujue huu mradi kama upo ama kama haupo mtuambie. Si oleo mnatzungusha, Benki ya China, kesho Serikali tunataka tujue hatima yake ni nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 112 kwenye Hotuba ya Waziri, Mamlaka nyngi za maji zinadai

Taasisi za Serikali, deni limefika bilioni 21.84 na Mamlaka zile tunajua zinajиidesha zenyewe. Sasa nataka kujua kauli Waziri zile Taasisi za Serikali zinapewa pesa kwa ajili ya kulipia huduma zinazotumia ikiwemo na maji, kwa nini hazilipi kwenye hizi Mamlaka za Maji, na hizi Mamlaka za Maji zinajиidesha zenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zina mambo mengi ya kufanya, hizi pesa zinazodaiwa ni nydingi nataka kujua Mkakati wa makusudi kabisa wa kuwaweka hadharani watu hawa ambao hawataki kulipa maji kwa sababu sisi wananchi wa kawaida kwa mfano kule Mtwara, ukishatumbia maji, yakafika deni 30,000 wanakuja kukata maji. Kwa nini kwenye hizi Taasisi tunaacha mpaka madeni yanakua, kama Serikali haitoi pesa basi mtuambie, na sio kuzunguka zunguka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nipate ufanuzi ukiangalia ukurasa wa 90 katika hotuba ya Waziri, kuna ule mradi wa maji katika Miji ya Mtwara na Babati, ukisoma pale umeongea tu kwa ujumla kwamba usanifu unaendelea mradi utafanya kazi, usanifu utakapo kamiliika. Nataka njue hili suala liko siku nydingi, linaongeleta ni lini, usanifu unakamiliika na lini mradi unaanza kufanya kazi huu mradi katika hii Miji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio mambo ya jumla ya kutuambia kwamba ukikamiliika hamna *deadline*, hamna kipindi maalum umesema umemaliza hilo halikubaliki kabisa, tunaomba tupatiwe kwa sababu tunahitaji huduma hiyo ya maji. Miundombinu yetu pale Mtwara ni chakavu haitoshelezi, kulingana na watu ambao wapo kwa kipindi hiki. Miundombinu ile ni tangu enzi za Mkoloni, kwa hiyo sasa hivi tunapata shida za maji ingawa maji tunayo lakini kwa sababu miundombinu ni mibovu ni michache haiwezi kukidhi haja ya wananchi ambao wapo katika Mkoa wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo machache, ukifungua, naomba tu niulize swali moja, ukifungua kwenye hotuba yako ukurasa wa 134, kuna kampeni za maji na usafi wa mazingira chini ya mafungu

mengine, lakini ukisoma pale, unakuta fedha zote ni fedha za nje. Sasa tunaenda kufanya kampeni za maji, na usafi wa mazingira, lakini fedha zote tunategemea kutoka nje, maana yake ni nini? Serikali hajatenga fedha za ndani kugharamia hii kampeni. Na tunajua mambo ya maji na usafi wa mazingira ni jambo nyeti, kwa nini Serikali inategemea zaidi pesa kutoka nje. Naomba nipatiwe majibu ya suala hilo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kengele ya pili imelia.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. (*Makoff*)

**MWENYEKITI:** Haya, tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na baadaye Mheshimiwa Gekul ajiandae.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi, kwanza niishukuru sana Wizara ya Maji nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, nimshukuru sana Naibu Waziri, nimshukuru sana, Katibu Mkuu kwa nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya maji katika Majimbo yetu na katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda sana kuanza na mambo matatu ya muhimu sana, jambo la kwanza nitaenda kwenye mapendekezo ya Kamati, mapendekezo ya Kamati yako mengi, lakini nitazungumza mapendekezo matatu ambayo ningependa sana Wizara iweze kuyasisitiza na kuyaangalia kwa jicho la kipekee, ili tuweze kutatua tatizo la maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza katika ukurasa wa 18, katika ripoti ya Kamati, imeelezea na imeshangazwa na kushuka kwa kiwango cha bajeti cha asilimia 9 katika kipindi cha bajeti cha mwaka 2019/2020 ukilinganisha na 2018/2019. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikiwa kama tuna malengo mazuri ya kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya maji, naungana na Kamati kuuliza swalii hili, hivi kwa nini kama tuna malengo ya kutatua tatizo la maji katika nchi yetu ya Tanzania bajeti ipungue kwa asilimia 9? Lakini jambo la pili ninaenda tena kwenye ukurasa wa 19 ambapo unasema inazungumzia masuala mazima ya mfuko wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mwaka uliopita tulizungumza na miaka mitatu sasa mfululizo tumekuwa tukiendelea kuishauri Serikali kuongeza tozo kutoka shilingi 50 mpaka shilingi 100. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kipindi cha miaka mitatu yote, bado hakuna lolote ambalo limefanyika, na kwa kweli kwa sisi Wabunge ambaao hasa tunatoka kule vijijini. Tunajua adha ya maji, changamoto kubwa ambayo ipo vijijini ni suala zima la maji, ukienda kule hawaongelei kitu kingine zaidi ya maji, na hata sisi ambaao tuko mjini huku wakati tukiwa Dodoma, kitu kikubwa ni maji. Sio kitu kingine, ni maji, utaenda mjini maji, utaenda vijijini maji, sehemu yoyote utakayoenda Tanzania hapa, tatizo ni maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachouliza hivi ni kwa nini Serikali inashindwa kusikiliza na kuamua tu sasa tufanye utaratibu wa kuwa na shilingi 100 badala ya shilingi 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nadhani peke yake itaweza kutatua changamoto hii kubwa sana, kwa sababu kwa asilimia kubwa mfuko wa maji, umechangia kwa asilimia 67 ambaao unalipa pamoja na mengineyo unalipa wakandarasi, na unasaidia kuendelea kuwa na vyanzo mbalimbali vyaa maji. Kwa hiyo, ikiwa kama tutaongeza shilingi 50 kwenda 100 basi nadhani changamoto ya maji tunaweza tukaipunguza kwa kiasi kikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia ukilinganisha kati ya vyanzo vyaa mapato ya ndani na hii tozo,

utaona kwamba asilimia kubwa ya vyanzo nya ndani havikidhi mahitaji na ndipo hapo utakapoona kwamba asilimia saba ya vyanzo nya ndani nya mapato ndivyo vilivyokidhi mahitaji, lakini kwa asilimia kubwa, asilimia 67 imetokana na changamoto ambayo tumejaribu kuweka tozo ya shilingi 50. Nilikuwa nadhani ni wakati sasa umefika 2019 tuweze kuweka mguu chini, tuweze kuishauri Serikali na Serikali isikilize maoni yetu kama Wabunge kwa sababu tunatoka vijijini tunajua changamoto na tatizo kubwa kule vijijini ni maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine au kitu kingine cha tatu ambacho ningependa kushauri kupitia ripoti ya bajeti ni kwamba kuna maeneo ambayo yameonekana fedha ambazo zinatolewa na Wizara ya Fedha kwenda kwenye maji zinaenda kwa kususua. Ningependa kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha zinaenda kwa wakati. Vilevile maeneo mengine madogo madogo kwa mfano kuna misamaha ya kodi kwenye vifaa nya maji, vifaa pia kuchelewa pale bandarini ambapo vyote vimeelezwa kwenye ripoti ya Kamati. Ningependa sana kuendelea kuishauri Serikali kuangalia mambo haya matatu. Pia tunaweza tukaangalia katika yale mapendekezo mengine ya Kamati, lakini kwangu nadhani kwamba haya matatu ni ya msingi sana kuhakikisha kwamba tunatatuwa changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kitu kimoja kwamba Naibu Waziri amefika pale Jimboni kwangu, kuna mradi mkubwa sana ambao unaendelea kwa zaidi ya miaka mitano ambao umekwama, Mradi wa Isupilo, Itengulinyi, Magunga ambao kwa kadri ya nafasi ambayo nimeipata nimekuwa nikiongea na Waziri, amejitahidi kufanya kazi yake, amekuja jimboni kuangalia changamoto hii, amejaribu kutatua, lakini bado changamoto iko pale pale. Wananchi wangu sasa hivi wameshachoka, toka mwaka 2014 wameongea kitu hicho hicho na wamenituma niendelee kuongea kuhusu mradi huu, mradi ambao umegharimu jumla ya shilingi bilioni 2.2, umelipwa bilioni 1.2 lakini mradi umekufa. Sasa hebu tuangalie tunapoteza au hatupotezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea tu kuwasihii viongozi wa Wizara, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwamba tuangalie namna ambayo tunaweza tukalisaidia Jimbo la Kalenga, tukasaidia Mkoa wa Iringa, tukasaidia namna ambavyo tunaweza tukapata maji katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru pia Wizara kwa kutusaidia zile milioni 49 katika Mradi wa Nyamlenge ambaao Mheshimiwa Naibu Waziri alitusaidia na Mheshimiwa Waziri analifahamu hili, nilikwenda kwake nimeongea, ametusaidia kuweza kuziweka zile milioni 49 kwa ajili ya ku-*design* Mradi wa Nyamlenge ambaao kwa namna moja au nyiningine utasaidia kutatua changamoto katika vijiji 16 katika Jimbo la Kalenga. Naendelea kuishukuru Serikali na kuendelea kuipongeza Serikali kwa sababu nina imani na Mheshimiwa Mbarawa, nina imani na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini vilevile Katibu Mkuu na Wizara yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme tu shukrani kwa baadhi ya taasisi ambazo zimeendelea kulisaidia Jimbo la Kalenga kupata maji. Niseme *WARID/wametusaidia* sana ambaao ni wa Marekani, *USAID* wametusaidia pia kwa kiasi kikubwa lakini pia Makanisa ya Anglikana na baadhi ya Makanisa mengine wameendelea kutusaidia katika kuhakikisha kwamba tunapata maji katika Jimbo la Kalenga. Zaidi ya yote niendelee kusisitiza zaidi na zaidi Mheshimiwa Mbarawa alikuja jimboni wiki tatu zilizopita, tukaongea kuhusu Mradi wa Kalenga- Tanangozi na akanisaidia na akasema kwamba niandike andiko ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya mradi huu. Maandiko nimeshaandika nitamsaidia kuyafikisha katika meza yake aweze kututatulia tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote, pale Kanisani kwetu sisi tuna wimbo huwa tunasema usinipite Mwokozi, usinipite Mwokozi, kwa hiyo nami leo nasema Mheshimiwa Mbarawa asinipite katika bajeti hii, aje Kalenga atusaidie kupata maji. Mungu ambariki, Wizara yake ibarikiwe na namshukuru sana, naamini kabisa kwamba 2019/2020 atatatua tatizo la maji katika Jimbo la Kalenga. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Godfrey Mgimwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweke mawazo yangu katika Wizara hii ya Maji lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa nafasi hii maana ni kwa neema yake tu tutimize wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu na Katibu Mkuu na timu yake kwa jinsi ambavyo wanachapa kazi hongera sana. Nafahamu wanapambana sana, Wizara hii kila mmoja anatamani atendewe haki kwenye eneo lake na kila siku wako *site*. Pia niwashukuru wanatutembelea huko majimboni, Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Babati, akafika Imbilili kwenye mradi ambaao umekuwa ukisumbua muda mrefu sana, lakini naona sasa kuna mwanga na mambo yanaendelea. Niwapongeze mno kwa kuwa wanapambana usiku na mchana ili wananchi wa Tanzania wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie Mradi huu wa Maji katika Mji wa Mtwara na Babati, ukurasa wa 90 kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Naomba tu watusaidie wawe wakweli, watuambie wapi wamekwama kwa sababu wameandika Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa mradi na ujenzi wa mradi utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu huo. Sasa naomba nifahamu usanifu unafanyikia wapi Dodoma, Dar es Salaam au Babati na Mtwara. Kama ni Babati na Mtwara nafikiri warudi kwa wataalam wao wawaambie tu ukweli, huyu mtu wanayemsema Mtaalam Mshauri amefika, hayuko *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachofahamu Mradi huu wa *Kfw* kati ya Serikali yetu na wenzetu wa Ujeruman ni mradi wa mwaka wa kumi na moja sasa ambaao ungetusaidia kilomita 45 *coverage* pale tukapata maji, lakini ukatusaidia

kujenga vyoo katika maeneo ya *stand*, masoko na maeneo mengine katika shule zetu. Maeneo mengine wameshatekeleza, Mheshimiwa Makamu wa Rais alikuja Babati tukaomba pia na hili, tukaomba kwa Mheshimiwa Waziri aliyeпитa na aliyeƿo sasa na Naibu Waziri wakatuambia tatizo Wizara ya Fedha ndio hawajasaini huu mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tu nisikitike kuwa Mheshimiwa Waziri leo anatuambia Mtaalam Mshauri yupo *site* Babati huko akiendelea na usanifu, nafikiri hizi taarifa zao waziangalie upya kwa nia njema tu, kwa sababu ni mradi wa miaka kumi na moja sasa. Sasa ni vizuri wakatuambia kwa sababu utatusaidia sana pale Babati Mjini na sijapoteza imani na Mheshimiwa Waziri, lakini natamani tuwe wakweli, kama tumekwama mahali tuambizane, hilo tu. Kwa huu mradi wakate mzizi wa fitina, wasituambie mkataba haujasainiwa, Mtaalam Mshauri yuko *site*, wakati hayuko *site*, naomba kwa hili watuambie ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niwapongeze walifika katika Kaya ya Sigino upande wa Imbilili. Usiposhukuru kwa kidogo pia maana yake utakosa kikubwa, wametulipia *certificate* za Mradi wa Malangi na Mradi wa Haraa na unaendelea vizuri. Pia nimewapatia *certificate* ya Imbilili ambako wamefika, kwa kweli niwaombe wanafahamu ni viongozi wangapi wamefika pale, sitaki kuwataja, nawaomba watulipe hizo fedha za *certificate* ya Imbilili milioni mia mbili kama na arobaini ili ule mradi uende kwa sababu mradi ule ume-expire mara tatu, 2017 yule mkandarasi aliyeko *site* mkataba wake uli-expire. Mwaka 2018 tukaongezea tena ule mkataba uka-expire na mwaka 2019 ume-expire tena, lakini sasa anaendelea *site* kwa sababu fedha hazitoki na maeneo mengine pia anafanya miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, ninachoomba katika zile bilioni 40 walizosema zimesalia basi watulipe na ule mradi kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, ndio kijiji pekee kati ya vijiji vinne kwenye kata nzima ambako mradi ndio umeanza kidogo. Kwenye Kata ya Sigino Mheshimiwa Waziri wa Maji alifika baba yangu ambaye sasa yuko kwenye Wizara ya Ujenzi, akafika pale, akaongea na wale wananchi, akawaambia Kata ya Sigino tunawapatia maji umekuwa ni wimbo wa miaka yote. Naibu Waziri amefika ameona kata nzima ule mradi haujafika, naombeni Kata ya Sigino ndio mradi wetu wa kwanza Halmashauri ya Mji wa Babati hatuna mradi mwingine ni wa Kata ya *Sigino*, Kijiji cha Singu, Kijiji cha Sigino, Dagailoi na hicho cha Imbilili milioni 230 wakitulipa sisi hatuna ugomvi na wao, watupatie hizo fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau naomba nishukuru sana pia kwa kitendo walichotufanya watu wa Babati na Watanzania kwa kipindi hiki, wamefuta *service charge* kwenye billi zetu za maji, billi za mwezi wa Nne zimekuja, wananchi wa Babati walikuwa wanalia kuhusu Sh.2,500 kwa kila bili, kwa kweli nawapongeza na hii kauli ni ya wananchi wa Babati, wameondoa hiyo *service charge*, hongera sana. Sasa wanapopiga hatua mbele Mheshimiwa Waziri ni vizuri wakatuletea sasa *prepaid meters*, hizo wakitupatia kwanza zitatusaidia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hayatapotea pia zile bili za maji ambazo zilikuwa hazikusanywi zitakusanyika sasa kirahisi, nawaomba *wa-roll out* mapema Waheshimiwa Mawaziri wetu, wameshafuta hilo wananchi wa Babati wamefurahi sana kwa sababu ilikuwa kila mkutano nikienda wanasesma mama tunakuomba *service charge* iondolewe, wameiondoa hatuna cha kuwalipa tunawashukuru, lakini sasa watuletee *prepaid meters* tasa idia sana maji yasipotee na watu walipe bili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika Mji wetu wa Babati bili za maji imependekezwa na *EWURA* na mchakato kutoka chini kwamba ipandishwe kutoka *unit* moja kwa Sh.1,190 hadi Sh.2,000. Hivi *imagine* ongezeko la Sh.1000 niwaombe sana watu wa *EWURA* wasije wakathubutu kupokea hayo maombi ya kupandisha bili za maji katika Mji

wa Babati kwa sababu hata hizo za sasa tu wanaona watumiaji wa maji sio wengi ni kwa sababu pia hizi bili ni kubwa kwa *units* tano mpaka 10 haitoshi kwa matumizi ya nyumbani, lakini *units* 10 na kuendelea wakaongeza kutoka Sh.1,100 mpaka Sh.2,000 Mtanzania wa Babati hawezи kumudu hiyo bili. Kwa hiyo chondechonde watu wa *EWURA* wasije na watu wa maji wakapandisha hizo bili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni suala la usimamizi wa maji. Mheshimiwa Waziri amesema ana upungufu wa watumishi 3000, hao watumishi 3000 katika Wizara yake ambapo alitakiwa awe na watumishi 10,000, sasa una 6,000 lakini hiyo inashuka mpaka kwenye halmashauri zetu. Mimi nishauri kama hawa watumishi ni pungufu fedha za maji wanazotutengea waache mamlaka zisimamie kwa sababu hao ma-*engineer* wa maji wameshindwa kusimamia miradi ya maji katika halmashauri zetu. Utakuta usanifu mbovu, maeneo ambako mabomba ya chuma yanatakiwa yawepo kwenye makorongo wanaweka ya plastiki, tatizo ni kubwa kwenye mji wetu sisi miradi mingi ya halmashauri tumekuwa tukikabidhi *BAWASA* kwa sababu mradi unatekelezwa na halmashauri ukipelekwa kwa wananchi wau-test haufai hata kidogo. Mradi wa Managhat jana tumetoka kulipa, juzi kwenye kikao cha Kamati ya Fedha imebidi tutoe milioni 10 kwa ajili ya ku-*repair* ule Mradi wa Managa kukabidhi kwa *BAWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mradi wa Nakwa milioni 800, umechakachuliwa ilibidi tulipe zaidi ya milioni 26 ndio *BAWASA* waupokee, kwa nini tupoteze fedha. Nashauri hivi, ni vizuri fedha wakatuletea halmashauri lakini wataalamu *Experties* wakasimamia watu wa *BAWASA* maana halmashauri zetu wameshindwa kusimamia hii miradi, inasababisha miradi inakuwa mibovu, kunakuwa na uchakachuzi mwingi, mwisho wa siku wananchi wanakosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo niwatakie kila la heri, wanipatie fedha za Kata ya Sigino, *certificate* zetu

watulipe, nawashukuru kwa kufuta service charge, tupo pamoja. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Gekul. Tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond, baadaye Mheshimiwa Mwita Getere ajiandae.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hii nafasi na naungana na waliozungumza asubuhi na maombi aliyotoa jirani yangu Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare kumwombea ndugu Reginald Mengi apumzike mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa jioni ya leo na ndio mchango wangu wa kwanza kwenye bajeti na nilikuwa naisubiri sana hii Wizara ya Maji kwa sababu nikiwa kama mwakilishi wa wanawake maji ni kila kitu kwa mwanamke yejote. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Makame Mbarawa, Naibu Waziri mwanangu Mheshimiwa Aweso, timu yote ya wanamaji maana yake wao wanafamilia ya maji kutoka wizarani mpaka mikoani, niwapongeze kwa juhudhi zao kwa kipindi chote kuhakikisha kwamba maji yanapatikana. Kipekee niwapongeze wanawake wote, wanawake wa Tanzania wasiochoka kuhakikisha maji yanapatikana, kulea familia zao, kutunza familia zao, wakiwemo wa mjini na vijiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Mungu ni mwema naye leo ametupa uhai tukaweza kuzungumza haya mambo hapa nami nimrudishie sifa na utukufu Mwenyezi Mungu nikiamini kwamba atatupatia maji mengi zaidi Tanzania. Niseme kwamba ni vyema basi kama tunaamini hivyo na tumeipokea hii ripoti nzuri maana yake hii ripoti kwa kweli inatiririka kama kitabu cha hadithi, niseme kwamba hakuna litakaloshindikana kwenye ripoti hii ila tu Serikali nayo isikie na ili nisikose muda wa kukamilisha azma yangu naomba kuunga mkono hotuba hii kwa aslimia mia moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani ni mwaka wa nne sasa toka nimeingia kwenye Bunge hili la Kumi na Moja, nimewakuta Wabunge waliokuwa wametangulia wanazungumzia Sh.50 nyingine ya maji ambazo zimekuwa *ring fence* ambazo zimefanya kazi kubwa na leo kwa hiari yao wenye we wanaomba tena Sh.50 ziongezwe, labda chanzo cha mafuta ni kigumu sana kwamba vitu vitapanda bei, lakini Wabunge sisi ndio wawakilishi tumekuja na chanzo kingine tumesema kwamba basi ikatwe kwenye *bundle* za simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiari yashinda utumwa, kwa hiari yao na watajua namna ya kuongea na wawakilishi ili kila mtu apate maji safi na salama ambayo ni haki yake. Mungu alitupa maji tunafurahi kabisa. Nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri toka ule ukurasa wa 12 mpaka wa 22 ambapo ukurasa huo wa 12 anazungumzia uslmamizi na uendeshaji wa rasilimali za maji, akizungumzia mabonde ya maji, vyanzo mbalimbali na *management* ya maji, lakini sikuona msisitizo kwenye maji yanayotoka angani. Tanzania inaelekea kupata athari kubwa kwa ajili ya tabia nchi na zikianza mvua zinaanza kwa kasi kama zile za juzi zilizoharibu miundombinu ya barabara au watu walishindwa kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niulize tu wasomi wetu wako wapi? Hayo maji yanayotiririka na kupotea ardhini na kurudi tena baharini wamejipanga vipi kuhakikisha tunayakinga. Hivi majuzi Wabunge wote walikwenda kule kwenye mji mpya Ihumwa, sijui yale majengo kama yana makinga maji, mimi nilibahatika pia kwenda na Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama na tukahoji hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaalamu wa *ku-reserve rain water* ni mdogo sana. Miaka hiyo nikisoma Kifungilo tulikuwa na *rain water* na ndio maji safi na salama. Sasa wamejipanga vipi pale Ihumwa kuwa na maji mengi maana yake zikija mvua za Dodoma ni nyingi sana kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia sasa eneo ambalo mimi nashiriki kama Diwani ambapo ni kule Siha. Siha

kuna shida ya maji, pia tambarare yote ya Kilimanjaro, wengi waliniambia wewe unachangia nini na Kilimanjaro maji bwerere. Nataka niwaambie hivi kuna maeneo ambayo hayajaona maji safi na salama ikiwepo Same, Mwanga, Rombo na huko Siha, maji safi na salama ni shida. Alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye namshukuru sana aliona wote walikuwa wanamwomba maji safi na salama naye alisema jambo hili ataliwekea mkazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Mamlaka za Maji zina mafanikio makubwa na *best practice* zinaonekana, *successful cases* zimeonekana ikiwemo Mamlaka ya Maji MUWSA inayoongozwa na Joyce Msiru binti aliyekubuhu kabisa katika nyanja ya maji na anaipeleka vizuri. Sio hayo tu Dodoma yenye hatuna shida ya maji na Dar es Salaam pia niwapongeze sana Wakurugenzi hao na wale wengine. Siha kuna shida moja tu MUWSA ilipopelekwa kwenda kusimamia sasa *management* maana yake shida ni *management* na mpaka sasa hivi kwa kipindi kifupi sana tumeata Siha bilioni 4.3, naishukuru Serikali. Hata hivyo, ile bilioni ya kwanza bilioni 1.8 ya mwaka 2016 iliyojenga yale matenki ni kama imepotea maana yake yale matenki sasa hayatoi maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu ambaye nimempongeza sana awali katika ile timu, waone sasa kwamba hawa wenzetu wa MUWSA watakafopika kule Hai wasisikilize hiyo ya kwamba haitawezekana, maana yake zimetokea tuhuma nyingi, hapa sio mahali pake lakini waendelee kusimamia ili maji hayo yaweze sasa kutumika kwa wingi na kusambazwa katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiomba fomu ya kuomba maji kule Siha ni Sh.345,000 ambapo MUWSA ni Sh.20,000 tu. Sasa nashindwa kuelewa kwa nini wale wananchi wanashindwa kukubali, labda hapa pamepungua elimu. Nawaomba sana MUWSA itoe elimu na Katibu Mkuu asimamie jambo hili kwa sababu wanaoteseka ni wale wanawake wa kule mbali. (*Makof*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## TAARIFA

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally, muda wako umemalizika. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, niwapongeze Maprofesa wawili, Profesa Katibu, Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Aweso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui nianze wapi kwa sababu kuna vitu vingine niliwaza wakati hawa watu wameteuliwa, nikamwona Profesa Kitila, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Mheshimiwa Aweso wote wajanja. Kwa lugha ya kilaini kabisa na ya kitaalam na ya watu wale waliosoma wanasesma, *is software siyo hardware. (Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuja kutazama mambo yanavyokwenda, hivi kweli kwenye Wizara ya Maji ambako kuna wataalam leo wanapotuambia kwamba kufika Aprili katika nchi yetu kuna watu asilimia 64.08 wamepata maji vijiji, kweli? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Uongo mtupu.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa lugha nyingine maana yake ni kwamba katika vijiji 1,000, *at least* vijiji 650 vina maji safi na salama na vijiji 350 ndiyo havina maji safi na salama. Kwa hao watu ambaao tuko nao hapo ofisini kwa nini tunakariri vitu ambavyo havipo? Hivi Wabunge walioko hapa sasa wakisimama leo kila mta aseme kijijini kwake kuna nini, kuna haja hiyo kweli jamani? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Hakuna maji.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunapewa takwimu ambazo hazipo? Kwa hiyo, wakati fulani vitu vingine vinachanganya kidogo. Kwa nini watu ambao tunawaamini wanaotumia kompyuta siyo maneno ya zamani, kompyuta halafu tunapewa takwimu siyo sahihi? Leo *REA* wanaweza kukuambia Bunda kuna vijiji 15 havina umeme na vijiji 20 vina umeme. Leo maji wanaweza kutuambia kila mkoa, wilaya, halmashauri, Jimbo la Mbunge lina vijiji vingapi vina maji, takwimu ikaja hapa. Jamani nyie bado vijana tupeni maji hakuna lugha nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema wazi hapa, katika kitabu hiki kuna changamoto zimetolewa. Changamoto ya kwanza nzito sana iliyotolewa ni ukosefu wa fedha za kutekeleza miradi ya maji, ndiyo iko humu jamani. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli amepita kila mkoa anawaambia viongozi sisi *sometimes* hatusaidii matatizo ya wananchi. Sasa leo Wabunge tunasema tunataka kusaidia mambo ya maji yaende, shida iko wapi sasa? Tunataka maji sasa yaende, tunataka aidha fedha shilingi 50 inatoka wapi lakini Kamati ya bajeti ikae ituletee, kwamba jamani eeh ili twende huko fedha ni hii hapa, nchi yetu wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nani aliyechagua watu wachafu wakae vijijini halafu watu wasafi wakae mjini? Watu wanasema watu wamesongamana sana mjini, nani anayekaa kwenye uchafu huko vijijini, sisi wasafi tuko huku ndani. Mimi kijijini kwangu dampo ambalo ng'ombe na mbuzi wanakunywa maji ndiyo binadamu naye anakunywa yaani kila kitu kinakunywa mle ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki ni kipindi cha kuamua tu kwamba tunataka kusaidia nchi yetu iende, tupeni maji, tutafutie fedha. Mmetuletea wenyewe hapa, mmesema kikwazo ni fedha na sisi Wabunge tunasema fedha iko hapa, sasa shida iko wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi mnafanya kazi nzuri lakini ndiyo hivyo sasa mmesema matatizo ni haya na sisi

tunataka kuyasema. Mheshimiwa Waziri alipokuja Mheshimiwa Rais tarehe 09/9/2018, alipofika pale Nyamswa alikusimamisha Mheshimiwa Prof. Mbarawa kukuambia matatizo ya Jimbo la Bunda na mimi nilimwambia Mheshimiwa Rais matatizo yaliyopo na bahati nzuri nishukuru Wizara yako imetuma wataalam, wametembelea vijiji 30, wameleta mchanganuo lakini toka asubuhi nikasema labda miwani sina, nimenunu miwani nimetazama humu ndani sikuona hata kitu kimoja. Mheshimiwa Rais kasema, Waziri maliza matatizo, Waziri katuma wataalam wakaenda kufanya tathmini, wataalam wamekuja sioni Jimbo la Bunda hapa, sioni Bunda *DC* kuna nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kwamba wakati fulani labda mtakuwa mmesahau lakini najua mtalikumbuka mtaniwekea hivyo vijiji ambavyo vina Kata za Unyali, Bungeta, Mihingo, Kitare, Salama, Nyamswa na ya Nyamang'uta. Wataalam walitembelea kote huko, nadhani mtaniambia kuna kitu gani kimetembea hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza vizuri na naendelea kuzungumza vizuri kwamba nyie ni *software*, haiwezekana tukakariri gharama kubwa za kuendesha maji, gharama ni kubwa kuliko kawaida, kubwa sana. Leo mradi mmoja shilingi bilioni 20, shilingi bilioni 3, shilingi bilioni 4, tumefanya majoribio ya kujenga Hospitali za Wilaya na vituo vya afya kwa kutumia *Force Account*, gharama ni ndogo sana. Ninyi kwa nini msikae mkasema tufanye kama Malawi, tutandaze bomba kutoka Ziwa Victoria lipite barabarani tu, kila kituo, kila kijiji mnaweka toleo, barabarani tu. Vijiji vingine vilivyoko huko porini vitakuja kuchota maji pale kwa sababu vitakuwa na uhakika wa maji. Bomba lipite liende, inakuwa maajabu leo Bunda kilometra 15 kwenda kilometra 15 nyingine kutoka Ziwanı hakuna maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnafanya wananchi wanakuwa watu wa ajabu. Hivi kama tunasema tunahurumia wananchi hawa, wanaendaje kupiga kura wakati wote hawana maji? Saa 12 akina mama ndiyo wanapiga kura, hawaendi kupiga kura maji hayapo, tupeni maji tuache

maneno jamani, tupeni maji. Tumechoka tupeni maji, haiwezekani. Mheshimiwa Aweso bado kijana mdogo unaweza ukatoa maji, tupeni maji. Kwa hiyo, nisema gharama za uendeshaji wa maji ni kubwa mno, tutumie akili tutengeneze namna ya kuwa na gharama ndogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimewaaambia pale Bunda, kama mnaweza kunipa shilingi bilioni 10, nipeni mimi nipeleke maji nakotaka. Wataalam wa MUWASA wako pale, tutengeneze gharama. Tumeshatengeneza bomba, kiasi gani, wachimbaji ni wanakijiji wenyewe, ufundi unakuwepo tunaweka maji, kila mahali patakuwa na maji. Kama hiyo RUWASA hatuwezi kuiwekea mazingira mazuri itakuwa na hela kutokea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala llingine ambalo liko hapa, haiwezekani tukasema tunatafuta fedha, haiwezekani Mawaziri mkahangaika, haiwezekani Mheshimiwa Rais akahangaika mpaka anaomba misaada ya fedha kutoka nje, halafu watu wanaitwa sijui watumiaji maji, *MUWASA*, *DUWASA*, wanakula fedha. Tumeona kwenye ripoti ya *CAG* maeneo yote haya ya maji hasa ya majiji wamekula fedha. Tusisubiri ripoti kwamba *PACna LAACwafanye* kazi, hapana. Tukiona kuna chokochoko mahali, watu wanakula fedha za maji wakamateni waondoeni kwenye nafasi, mnasubiri Kamati za nini? Hatuwezi kukusanya fedha halafu watu wengine wanakula. Kwa hiyo, naomba tuangalie tunakwendaje kwenye suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili sasa nitaongea kwa upole, polepole tu msikie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni karne sijui ya ngapi, sijui ni 21 au 22 sielewi.

**MBUNGE FULANI:** Hiyo ndiyo polepole?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Hiyo ndiyo polepole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekanaje leo eti mtu anakuja pale hodi, hodi, nani? Mimi mpima mita, jamani! Anakuja kuangalia bili apelke ofisini. Kwa nini tusiwekewe mita mtu alipie maji kadri anavyotumia, kuna shida gani? Hili nalo mpaka Mheshimiwa Rais aje aseme ndiyo mfanye? Kwa nini watu wanatumia *bill* kwa ajili ya kula fedha? Kwa nini wanaletea watu bili kwa maji ambayo hawajatumia? Kwa nini tusitumie mita kila mtu anakunywa analipa, shida iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie hili tena polepole ili muelewe vizuri. Mheshimiwa Waziri, Naibu Mheshimiwa Aweso, Katibu Mkuu katika jambo ambalo hatuwezi kufanya mchezo wa kuigiza au wa kupiga siasa ni suala la maji, watu wana hali mbaya sana. Wakati fulani naenda kijijini nasema huu Ubunge wa nini sasa, si bora nitoke tu. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ni vizuri mkafanya kazi ya kutusaidia kupata maji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake umeisha, Mheshimiwa Getere muda wako umemalizika.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimwambie tu Mheshimiwa Getere labda si kwenye

Jimbo lake lakini hizi mita zipo kila mahali na zimeanza kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Tuendelee na Mheshimiwa Allan Kiula baadaye Mheshimiwa Mattar ajiandae.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niseme maneno machache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja. Pili, nitoe pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima kwa jinsi wanavyofanya kazi, wanafanya kazi vizuri. Tunaelewa kwamba wameikuta Wizara ina changamoto mbalimbali lakini wanaendelea kupambana nazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulikumbusha, tulipoingia Bungeni baada ya muda kidogo tuliwekewa fomu kwenye maboksi yetu pale tukaambiwa tuandike miradi yenyе matatizo. Sasa kwangu iko miradi yenyе matatizo na niliandika na hajachukuliwa hatua. Juzi alipokuja Mheshimiwa Makamu wa Rais, tulikuwa na Naibu Waziri, mradi wa Nyahau ulileta shida kidogo lakini Mbunge alikwishawasilisha. Mimi niliomba miradi yangu hiyo yote ifanyiwe *audit* na nilikuwa na maana yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka miradi ya Iguguno, Kikonda, Kidarafa na Mtamba ifanyiwe *audit* kwa sababu *design* na kilichojengwa siyo chenyewe. Tulikwenda na Waziri aliyeondoka mwananchi wa kawaida anasema tuliamiwiwa ma-*tank* mawili na visima vya kuchotea maji kadhaa. Kwa hiyo, mwananchi wa kawaida anazo data, mainjinia wetu kwa nini hizo data hawazifanyii kazi. Bado nasisitiza tunaomba miradi hiyo ifanyiwe *audit* lakini pia hiyo *liability* nimeshaihamishia Wizarani kwamba nimesema ziko changamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, Waziri alipofika Kidarafa na Kikonda aliahidi *solar*. Mheshimiwa Waziri

nilizungumza, nafikiri jambo hilo linafanyiwa kazi maana kuendesha miradi hiyo kwa kutumia *diese*/ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu nimesoma, ukurasa wa 167 kuna shilingi milioni 90 zimetengwa naomba ule mradi usome Lelembo. Kwa heshima kubwa Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Waziri naomba mradi huu usomeke Lelembo. Nikisema kwa heshima kubwa nina maana yangu na nina maana kubwa sana na ikibidi tuma wataalam wako wachunguze kwa nini nimesema hivyo na jambo hili nimezungumza na Mkurugenzi.

Kwa hiyo, tumekubaliana pasomeke Lelembo, mradi ule uende ukakamiliike na huu ni mradi mmojawapo yapo majenereta mapya kabisa pale yanaoza, naomba mkayachukue muondoke nayo, maana siyahitaji lakini najua watu wengine watahitaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu malipo ya wakandarasi. *Certificate* za wakandarasi hazijalipwa miradi wa Nduguti, Kinyangiri na Ipuli, tunaomba waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na mradi wa visima 10, kihistoria tuna viji 70 lakini viji ambavyo vina maji havifiki 10 isipokuwa ule mradi wa viji 10 ungefanya viji 20 viwe na maji. Tunaomba hiyo miradi basi itengewe fedha kidogo kidogo lakini pia tunaomba usimamizi, jicho la karibu muweze kuona utekelezaji wake unakwenda vipi. Hizi fedha mnazoweka huko na siasa za kwenye Halmashauri huko unakuta fedha zinakuwa *diverted* zinakwenda kufanya miradi mingine tena. Kwa hiyo, tuna miradi lakini inaanzishwa mingine, kwa hiyo, tunaomba jambo hilo liweze kuangaliwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa miradi. Wilaya nyingi mpya zina changamoto ya magari, tunaomba hata gari bovu sisi tutatengeneza. Yaani gari lile bovu kabisa lilioko Wizarani nyie mtupe, mimi niondoke nalo Bunge likiisha, halafu tutakwenda kulitengeneza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo lingine ambalo tulikuwa tukizungumza la vyanzo vya maji. Yako maji mengi wamezungumza Wabunge wengine ambayo yanatiririka. Kwenye Bonde lile la Msingi maji yanatiririka mpaka Nyahaa kule. Niliwahi kuuliza swali hapa la msingi kwamba utafiti unafanyika, hakuna namna ya kukinga yale maji? Kwa sababu sisi hatuna ile mito inayotiririka kwa mwaka mzima ili tuweze kupata maji, sasa hilo bonde likifanyiwa tathmini tunaweza tukapata maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwenye visima vilevile 10 tunaomba mtume *auditor*, visima vimechimbwa, watu wamelipwa wameondoka vingine havina maji na fedha ya Serikali imeshakwenda. Hilo ni jambo la muhimu sana la kuweza kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wamezungumzia suala la *Force Account*. Ni muhimu sana tukaangalia kama kuna uwezekano tukaenda kwa *approach* hiyo tunaweza tukaokoa fedha nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tulianzisha Mfuko wa Maji, wamezungumza Wabunge wengi, lazima tukubaliane kwamba unahitaji fedha na kama unahitaji fedha tunafanya nini. Sasa tukubaliane kama Bunge hapa, tuangalie chanzo mahali popote pale, fedha ya Mfuko ya Maji iende, kile kiwango tuklongeze ili tuwe na fedha nydingi kwenye Mfuko wa Maji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na fedha nydingi kwenye Mfuko wa Maji hizo fedha basi na zenyewe zionekane vijijini. Wamesema wenzangu hapa mijini wana miradi mingi ya wafadhili lakini vijijini watu wanahitaji maji. Kauli kubwa hapa watu wanayozungumza, kila mtu anazungumza suala la maji. Leo sijazungumzia asilimia ya upatikanaji wa maji vijijini kwa sababu wenzangu wameshazungumza. Tufikie mahali tuwe na takwimu sahihi ya upatikanaji wa maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii fupi. Ahsante. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Allan, tunaendelea na Mheshimiwa Mattar dakika tano.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ahsante kwa kunipa nafasi lakini la pili nikushukuru sana. La tatu niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri wanazozifanya ambazo zinaleta matumaini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuzungumza na la kwanza ni kuhusu miradi ya maji vijijini. Baadhi ya miradi ya maji wanatumia majenereta ambapo ni kuwapa mzigo mkubwa wapiga kura wetu. Niombe sana Serikali iweze kufikiria kutumia *solar system* kwa sababu upatikanaji wa maji unaweza kuwa rahisi zaidi kuliko kutumia majenereta. Kwa hiyo, nikuombe sana Waziri uweze kwenda mbali zaidi kwenye *solar system* ili kuwapunguzia mzigo wa gharama wananchi wetu. Unapotumia *solar system* hata Serikali inaweza ikawa imepunguza mzigo mkubwa katika matumizi ya maji na hili ndilo tunalolitaka kwa wananchi wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, fedha za kwenda kwenye miradi ya maji bado ni tatizo kubwa na halijapatiwa ufumbuzi. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri ujue ni miradi gani ni muhimu uikamilishe kuliko kukusanya miradi mingi ambayo haimaliziki. Tunaziumiza fedha za Serikali kisha baadaye ile miradi haifanyi kazi, ina maana hakuna faida ambayo ninyi mnaipata na wananchi hawapati faida kutoka kwa Serikali yao. Kwa hiyo, nikuombe sana, Mheshimiwa Waziri unafanya kazi vizuri lakini kuwe na miradi maalum ambapo kwa fedha ambazo tunaweza tukapata basi tunaweza kuitekeleza na kuisha. Tukifanya jambo hili tunaweza tukafanya kazi nzuri na wananchi wetu wakapata mafanikio mazuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni shilingi 50 kuongezwa kwenye Mfuko wa Maji. Ninyi Serikali mnaweza mkatafuta chanzo chochote lakini shilingi 50 hii kwenda kwenye Mfuko wa Maji ni jambo la lazima kwa sasa ili

tuwasaidie wananchi wetu. Ili tuweze kupata kile ambacho tulichokusudia ni lazima tuongeze shilingi 50, ikiwa ni kwenye mafuta, simu au mahali pengine popote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tumwambie sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha hili suala la shilingi 50 ndiyo mwarobaini wa matatizo ya maji. Ukiangalia mtiririko wote wa fedha basi fedha inayotoka na inayokwenda kwenye miradi ya maji na inayotoka kwenye Mfuko wa Maji tu peke yake, ukiangalia fedha ya Serikali iliyokwenda ni ndogo sana. Ni kwa nini Mheshimiwa Waziri msiveze kuwakubalia Wabunge hawa, ndiyo wananchi, hiki kishilingi 50 kikienda kwenye Mfuko wa Maji tukatatua matatizo ya maji, nia yetu sisi ni safi, tunakushaurini vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Fedha huwezi kupokea huu ushauri wa Wabunge? Sisi tunakushangaa sana na tunaona mambo ya ajabu sana. Kubaliana na ushauri wa Wabunge, ukikubaliana na ushauri wa Wabunge maana yake umekubaliana na ushauri wa wananchi wote, sisi ndiyo wenyewe wananchi. Nikueleze tu Mheshimiwa Waziri na Serikali suala la shilingi 50 safari hii halina mbadala. Tunawaomba sana muweze kufanya kazi vizuri. Mkipewa shilingi 50, naamini tatizo la maji tutakuwa tumeliondoa kwa asilimia kubwa kwenye nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nilzungumzie sana, Mamlaka za Maji zinadai sana, Serikali yetu inadaiwa. Ukiangalia tathmini za Mamlaka zote za Maji zinadai Serikali yetu. Tuombe sana Serikali ikubaliane na kulipa madeni haya ili iwaachie hizi Mamlaka ziweze kujiendesha wao wenyewe, zina uwezo kujiendesha lakini bado madeni makubwa yako Serikalini. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uweze kulipokea hili na uweze kutoa fedha kuzilipa hizi Mamlaka za Maji ziweze kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mattar. Huyo ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo. Niwashukuru wote kwa michango yenu ambayo mmetoa kwa hekima nzuri sana na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake naamini wameyapokea na yatafanyiwa kazi inavyostahiki.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 3 Mei, 2019 saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 3 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*